*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA SABA

### Kikao cha Tatu – Tarehe 6 Aprili, 2017

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Tukae Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Mkutano wa Saba na Kikao chetu hiki ni Kikao cha Tatu. Katibu.

**NDG. CHARLES MLOKA – KATIBU MEZANI:**

### HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE WALEMAVU:**

Taarifa za Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na Nyongeza zake yaliyochapishwa tangu Mkutano wa Bunge uliopita kama ifuatavyo:

(i) Toleo Na. 4 la tarehe 27/01/2017
(ii) Toleo Na. 5 la tarehe 03/02/2017
(iii) Toleo Na. 6 la tarehe 10/02/2017
(iv) Toleo Na. 7 la tarehe 17/02/2017
(v) Toleo Na. 8 la tarehe 24/02/2017
(vi) Tolea Na. 9 la tarehe 03/03/2017
(vii) Toleo Na. 10 la tarehe 10/03/2017

(viii) Toleo Na. 11 la tarehe 17/03/2017
(ix) Toleo Na. 12 la tarehe 24/03/2017

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE KATIBA NA SHERIA):**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2016/2017 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu maoni ya Kamati hiyo juu ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa mwaka wa fedha 2016/2017 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kemi, ni upande huu mwingine.

**MHE. KEMILEMBE J. LWOTA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE MASUALA YA UKIMWI):**

Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Tume ya Uratibu na Udhibiti UKIMWI) kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumzi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**MHE. CECIL D. MWAMBE (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU OFISI YA WAZIRI MKUU):**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Ofisi ya Waziri Mkuu juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**SPIKA:** Ahsante sana. Katibu.

**NDG. CHARLES MLOKA – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, leo ni siku ya Alhamisi ambayo ni tarehe 6 Aprili, 2017 naomba kuwaarifu kwamba hakutakuwa na kipindi cha maswali kwa Waziri Mkuu kama mnavyoona katika *Order Paper* zenu za leo. Baada ya kipindi cha maswali kukamilika Mheshimiwa Waziri Mkuu, mara moja atatakiwa kuwepo hapa ili aweze kuwasilisha hotuba ya bajeti ya ofisi yake kwa mwaka wa fedha 2017/2018, hivyo tunampa nafasi ya kujiandaa kwa ajili ya shughuli hiyo ambayo itaanza muda si mrefu ujao.

Tunaendelea na maswali, tunaanza na Ofisi ya Rais TAMISEMI. Swali la kwanza Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi.

Na. 19

**Ujenzi wa Madaraja ya Shaurimoyo, Nakalolo na Miesi**

**MHE. JEROME D. BWANAUSI** Aliuliza:-

Serikali iliahidi kujenga madaraja ya Shaurimoyo, Nakalolo na Miesi.

Je, ni lini madaraja hayo yatajengwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** Alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi, Mbunge wa Lulindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Masasi kwa msaada wa Wakala wa Barabara *(TANROADS)*

imekamilisha usanifu wa madaraja yanayohitajika kujengwa katika mito ya Mpindimbi - Shaurimoyo - Nakanyimbi mpaka Nakalolo. Gharama za awali za ujenzi wa madaraja hayo zimebainika kuwa ni shilingi bilioni tatu. Kutokana na ufinyu wa bajeti ya Halmashauri, Wakala wa Barabara *(TANROADS)* imekubali kutenga fedha hizo chini ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano katika bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018 kwa ajili ya kuanza kazi ya ujenzi.

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri. Kwa kuwa Naibu Waziri anayeshughulika na barabara yupo, je, anaweza akalithibitishia Bunge hili kwamba fedha hizi *TANROADS* wameshazitenga kweli kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii?

Swali langu la pili, je, ni lini madaraja haya yatajengwa, kwa sababu wananchi hawa wa maeneo ya Miesi, Kata za Mkundi na Mpindimbi kwa miaka minne sasa wanapata tatizo kubwa sana baada ya madaraja haya yaliyokuwepo kuzolewa na mafuriko, je, ni lini baada ya bajeti kazi itaanza?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Mbunge sana kwa harakati zake kubwa na kazi kubwa anayofanya katika Jimbo lake kuhakikisha wananchi wake wanapata huduma za maendeleo. Kama tulivyosema, kutokana na kazi hiyo nzuri ambayo ameifanya ndiyo maana sasa, kwa sababu barabara ile ilikuwa chini ya barabara ya Halmashauri lakini kutokana na msukumo mkubwa ndiyo maana *TANROADS* imeamua kufanya *assessment* ya barabara ile na kukubali kwamba madaraja haya yataweza kujengwa.

Nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge hilo ondoa hofu kwa sababu kwanza imeshafanyika hiyo tathmini na kuona kwamba shilingi bilioni tatu na ofisi ya ujenzi naamini katika harakati za hii bajeti ambayo itakuja hapa tutaona katika jedwali hilo ambalo linaeleza kwa sababu tathmini wameshaifanya tayari.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, suala la ni lini barabara hii itajengwa. Barabara hii itajengwa mara baada ya kutengwa kwa bajeti, kwa hiyo, naomba nikuondoe hofu Mheshimiwa Dismas kwa sababu wananchi wa eneo lile wana umuhimu mkubwa wa barabara hii ambayo ni barabara ya kimkakati kwa suala zima la uchumi wa korosho katika maeneo haya, naomba ondoa hofu. Serikali iko tayari kuhakikisha kwamba itafanya kila liwezekanalo kuhakikisha wananchi wa Lulindi wanapata huduma ya ujenzi wa barabara.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi niulize swali dogo la nyongeza. Matatizo yaliyoko huko Lulindi yapo katika Jimbo la Manyoni Magharibi, kuna barabara kutoka Idodyandole kwenda Ipangamasasi, kuna tawi la Mto Kizigo imekuwa ni korofi sana na kwa nguvu ya Halmashauri hatuwezi kujenga;

Je, Mheshimiwa Waziri anaweza akatuahidi angalau kwa maneno kwamba Serikali kupitia *TANROADS* itatusaidia katika kipande hicho kidogo cha daraja?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, naomba tupewe muda mfupi tu, hatutahitaji muda mrefu tutakuja kutoa taarifa ya barabara ambazo tunapendekeza zipandishwe hadhi na nyingine zikasimishwe kwa *TANROADS.*

Naomba tu nitoe tahadhari, inaonekana maombi ni mengi sana na tukipeleka barabara nyingi sana *TANROADS* uwezo wao kwa sababu kifedha haiongezeki sana kulinganisha na mzigo tunaowapa, tusije tukaishia nazo zikawa za *sub standard* kwa sababu kazi ni kubwa na uwezo ni mdogo.

Kwa hiyo, nilitaka tu nitoe tahadhari hiyo lakini tutakuja kutoa taarifa hivi karibuni ni zipi zitapandishwa hadhi na zipi zitakasimiwa kwa *TANROADS.*

Mheshimiwa Spika, naomba tupewe muda kidogo.

Na. 20

## Uzaji wa Majani Mabichi ya Chai

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA** Aliuliza:-

Wakulima wa chai wa Wilaya ya Rungwe wanauza majani ya chai kati ya shilingi 230 hadi 240 kwa kilo, wakati wakulima wa Njombe wanauza majani ya chai kwa shilingi 500 kwa kilo huku kukiwa na Bodi moja na ni nchi moja.

Je, kwa nini wakulima wa chai Wilaya ya Rungwe wanalazimishwa kuuza majani mabichi ya chai kwa bei ndogo kuliko wakulima wa chai wa Wilaya za Njombe na Lushoto?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** Alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, bei dira ya majani mabichi ya chai hupangwa katika mkutano mkuu wa wadau wa chai ambao ni wa kisheria na hufanyika kila mwaka kabla ya msimu kuanza. Kwa mfano, mkutano wa wadau wa msimu 2016/2017 uliofanyika Njombe wadau walikubaliana bei dira kuwa shilingi 230.

Hata hivyo, kulingana na kifungu cha 49(2) katika kanuni za zao la chai za mwaka 2010, wakulima kupitia vyama vyao wamepewa uwezo wa kujadiliana bei na wenye viwanda ambayo itakuwa zaidi ya bei dira. Kutokana na makubaliano na wakulima Kampuni ya Chai ya Mufindi wanaomiliki viwanda vya Kibena, Luponde, Ikanga na Itona waliwalipa wakulima shilingi 250.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa bei dira hupangwa na kukubaliwa na wadau wote, tofauti ya bei kati ya eneo moja

na lingine hutokana na majadiliano kati ya wakulima na wenye viwanda kama ilivyoainishwa kwenye kanuni za zao la chai. Majadiliano hayo ndiyo yaliyopelekea wakulima wa Wilaya za Mufindi na Njombe kulipwa shilingi 250 kwa kilo wakati wale wa Lushoto, Muheza, Korogwe na Kagera wanalipwa shilingi 230 ambayo ni bei elekezi.

Kwa upande wa Wilaya ya Rungwe, bei ni kati ya shilingi 240 na 250 ambayo ni juu ya bei elekezi. Tofauti ya bei kwa maeneo hayo inatokana na malipo ya pili, kwa mfano katika mwaka 2015/2016 Kampuni ya Unilever inayomiliki viwanda vya Kibwele, Kilima na Lugoda, imelipa malipo ya pili kati ya shilingi 80 hadi 200 kwa kilo kutegemeana na ubora wa majani ya chai na hivyo kufanya malipo ya jumla kuwa kati ya shilingi 330hadi 400.

Mheshimiwa Spika, kiwanda cha *Wakulima Tea Company* cha Rungwe hulipa malipo ya kwanza shilingi 240 na ya pili shilingi 29 na kufanya jumla kuwa shilingi 259. Katika mwaka 2016/2017 Kiwanda cha Kibwele kinachomilikiwa na Unilever kinatoa malipo ya pili ya shilingi tatu na jumla kuwa shilingi 253 na Viwanda vya Kilima na Lugoda malipo yatakuwa kati ya shilingi 100 na 200 ingawa vinamilikiwa na kampuni hiyo hiyo. Kiwanda cha Dindira kilichopo Lushoto malipo ya kwanza yatakuwa shilingi 230 na ya pili shilingi saba na jumla kuwa shilingi 237.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, jibu la Mheshimiwa Waziri halijaniridhisha. Bodi ya Chai Rungwe imeweka wanunuzi wa chai wa aina mbili, wako *WATCO* na *Mohamed Enterprises. Mohamed Enterprises* amekuwa akinunua chai ya wakulima kwa bei nzuri na *WATCO* ikawa inanunua chai kwa bei ya chini, lakini cha kushangaza Serikali ikaamua kumwambia *Mohamed Enterprises* aombe kibali upya, mpaka sasa tunaongea *Mohamed Enterprises* hana kibali cha kununua chai ya wakulima na hii inapelekea wakulima kuuza kwa bei inayotaka Serikali ambayo ni ya chini.

Swali langu la kwanza, Serikali iko tayari kuvunja Bodi

hiyo ili tuweze kupata watu tunaowaamini watakaotetea wakulima wa chai wa Rungwe? *(Makofi)*

Swali langu la pili; Serikali iko tayari na Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuongozana na mimi kwenda kuonana na wakulima wa chai na kusikiliza kero za wakulima wa chai wanavyoteseka kwa muda mrefu?

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, Kilimo, Mifugo na Uvuvi, pamoja na msisitizo wa swali la pili la kuambatana na Mheshimiwa kwenda kule pia. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze na hilo la pili, nitakuwa tayari kuandamana naye muda wowote kuanzia sasa kwenda kusikiliza kero za wakulima wa chai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali la nyongeza la kwanza, kama nilivyoeleza bei ya chai hupangwa kwenye mkutano wa wadau ambayo kawaida inakuwa ni bei ambayo tunasema ni bei dira. Maana yake ni bei ambayo hairuhusiwi mtu yeyote kumlipa mkulima chini ya hapo, lakini Kanuni za zao la chai zinaruhusu majadiliano yafanyike kati ya mkulima na mnunuzi, maana yake wanaweza wakakubaliana bei kuwa juu ilimradi isije ikawa chini ya kile ambacho kimewekwa kama bei dira.

Kwa hiyo, tofauti anayoiona Mheshimiwa Mbunge kuhusu wanachotoa *WATCO* na *Mohamed Enterprises* inatokana na majadiliano yale ya ziada ambayo kanuni inaruhusu.

Mheshimiwa Spika, vilevile ningependa kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba tofauti ya bei hutokana na ukweli kwamba kunakuwa na tofauti ya ubora wa chai moja kutoka mkulima mmoja hadi mwingine, kwa hiyo mara nyingine kuna makampuni yanaamua kulipa kitu tunachoita *bonus* au malipo ya ziada kutokana na ubora

wa chai, ndiyo maana tunaendelea kuwashauri wakulima wetu wajaribu kulima chai kwa viwango vinavyotakiwa ili kuwa na ubora ambao utawafanya wapate bei nzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuvunja Bodi ya Chai kwa sababu hiyo, katika hali kama hii inakuwa ni vigumu kusema kwamba wao wanahusika moja kwa moja, kama nilivyosema kama Mheshimiwa Mbunge haridhiki na majibu ambayo nimeyatoa niko tayari kukutana naye ili niendelee kumuelewesha zaidi, pia kuandamana naye kwenda kwa wakulima wa chai.

**SPIKA:** Ahsante sana, swali la nyongeza niyatoe hapo tuanze na Mwenyekiti wa *PAC,* halafu tutamalizia kwa Mheshimiwa pale maswali mawili ya nyongeza. Mwenyekiti wa *PAC*

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Kwa vile tatizo la Rungwe ni sawasawa na tatizo linalowapata wakulima wa tangawizi wa Jimbo la Same Mashariki na kwa vile wakulima hao walipata tatizo kubwa tangu walivyosaidiwa na *SIDO* mpaka leo kiwanda hakifanyi kazi na wameshauriwa kwamba waunde Kampuni na *LAPF* wamekuwa tayari kusaidia kuingia katika Kampuni hiyo.

Je, Wizara inawezaje kuwasaidia hawa wakulima ili wasije wakaingia tena katika tatizo walilolipata ambalo mpaka leo kiwanda hakijaweza kufanya kazi? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo yanayohusu zao la tangawizi, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, Serikali au Wizara iko tayari kukutana na Mheshimiwa Mbunge pamoja na wakulima wa tangawizi ili kuangalia namna gani bora wanaweza wakatumia hicho kiwanda kwa manufaa yao na hivyo kuondokana na matatizo ambayo yameshatokea huko nyuma.

**SPIKA:** Mheshimiwa unaweza ukaendelea tafadhali.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa vile viwanda vya chai vipo Mufindi na katika majibu ya Waziri ameeleza vizuri sana viwanda vya Unilever na *Mufindi Tea Company* na ni kweli kabisa kwamba wakulima wa Mufindi wanapata shida sana kuhusiana na bei ya chai na makampuni makubwa yanakopesha wakulima mbolea halafu wanakatwa kwenye bei ile ya chai mwisho wa siku wale wakulima hawapati kitu chochote.

Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa wakulima wadogowadogo wale wa Mufindi Serikali ikasimamia wakajenga kiwanda chao, badala ya kuuza majani mabichi waweze kuuza majani makavu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba kuuza majani ghafi husababisha bei kuwa ndogo na ndiyo maana Serikali ya Awamu ya Tano inaweka jitihada katika uchumi wa viwanda. Tunaamini kwamba tutakapojenga viwanda vingi maana yake wakulima wetu watakuwa na faida zaidi.

Kwa hiyo, Wizara iko tayari kushirikiana na wakulima wa Mufindi na wakulima wa chai wa maeneo mengine ili kuendelea kuongeza viwanda vya chai tuweze kufanya uchakataji badala ya wakulima kuendelea kuuza chai ghafi. Nakubaliana nae kwamba ni kitu na Wizara itafuatilia.

**SPIKA:** Swali linalofuata Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini uliza swali lako.

Na. 21

**Kampuni ya Chai ya Maruku**

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA** Aliuliza:-

Kampuni ya Chai ya Maruku imekuwa sugu kwa kutowalipa wakulima wanaoiuzia chai pamoja na kutowalipa wafanyakazi wake wenyewe.

Je, ni kwa nini Serikali haichukui hatua ya kuwasaidia wakulima na wafanyakazi hao ili kupata haki yao?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** Alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ucheleweshwaji wa malipo ya wakulima na wafanyakazi katika kiwanda cha Chai cha Maruku yalianza Septemba, 2011. Hali hiyo ilitokana na uwezo mdogo wa kifedha wa *Kagera Tea Company Limited* iliyowekwa na *Spearshield Africa Company Limited* inayomiliki Kiwanda cha Chai cha Maruku kwa asilimia 75 kusimamia uendeshaji wake ikiwemo ununuzi majani mabichi ya chai kutoka kwa wakulima wadogo. Wakulima hawa wanamiliki asilimia 25 walizopewa na Serikali kufuatia kiwanda hicho kubinafsishwa kwa *Spearshield Africa Company Limited* kutoka kwa Mamlaka ya Chai Tanzania waliokuwa wanamiliki kiwanda hicho. Mkataba wa mauziano ulisainiwa terehe 25 Septemba, 2001. Sababu nyingine ni tija ndogo ya majani ya chai ikilinganishwa na gharama za uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, ili kunusuru wakulima na wafanyakazi wa kiwanda hicho, Serikali kupitia uongozi wa Mkoa wa Kagera, Bodi ya Chai ya Tanzania na Wakala wa Wakulima Wadogo wa Chai Tanzania, kwa nyakati tofauti wamekutana na mwekezaji huyo kumuelekeza atekeleze wajibu wake wa kulipa wakulima na wafanyakazi. Kufuatia

hiyo mikutano, mwekezaji ametafuta fedha na kulipa madeni mbalimbali ikiwemo malipo ya wakulima na wafanyakazi. Mpaka sasa ameshalipa wakulima wadogo malimbikizo yote ya nyuma hadi mwezi Oktoba, 2016 na ameahidi kulipa madeni ya Novemba na Disemba, 2016 ndani ya mwezi Januari, 2017.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rweikiza swali la nyongeza.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza siyo kweli kwamba amelipa madeni hadi Oktoba mwaka jana. Madai ninayo bado yapo mengi yana zaidi ya mwaka mmoja, miaka miwili sasa nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, inakuaje Serikali inampa mtu kiwanda kwa mikataba na kwa utaratibu unaokubalika anashindwa kutimiza wajibu wake ambao ni pamoja na kulipa bei za wakulima na mishahara ya watumishi Serikali inamuangalia tu mwekezaji huyo, anasema hapa ameahidi ambapo siyo kweli kama nilivyosema na Serikali inamuangalia tu huyu inasema ameahidi halafu inamuachia?

Swali la pili, wakulima hawa ambao hawalipwi hela yao ya chai ndiyo wakulima hawa ambao wanalima kahawa. Tumesema humu mara nyingi kahawa ina bei hafifu. Wizara ni hiyo hiyo ya kilimo imeagizwa na Mheshimiwa Rais iondoe kodi kwenye zao la kahawa, kodi ziko nyingi karibu 30. Kwa nini mpaka leo kodi hazijaondolewa na wakulima hawa wanazidi kuumia, kwenye chai wanaumia na kwenye kahawa wanaumia? Ahsante sana.*(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Naibu Waziri, Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Ole Nasha.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu kama ni kweli au siyo kweli kwamba tayari haya malipo yamefanyika, mimi nipo tayari kukaa na Mheshimiwa Mbunge ili tufananishe taarifa

tulizonazo, kwa sababu kwa ripoti ambayo ninayo na ambayo ni ya Serikali inaonesha kwamba kuna malipo yamefanyika lakini niko tayari kukutana nae, tujadili tuone taarifa sahihi ni ipi.

Mheshimiwa Spika, vilevile mazingira ya kampuni ambayo anazungumzia ni magumu kidogo kwa sababu wakulima wenyewe ni wamiliki vilevile wa hisa kwenye kampuni ile kwa hiyo ilipobinafsishwa na Serikali wakulima wa chai vilevile nao waliweza kupata asilimia fulani. Pamoja na changamoto ambazo zimekuwepo bado wakulima nao vilevile ni wamiliki wa kiwanda kwa kiasi kikubwa, lakini kama nilivyosema Serikali imekuwa ikiendelea kuwasiliana na kiwanda ili kuondoa hizo changamoto ambazo zimetokea.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la pili, ni kweli kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema kwamba kumekuwepo na manung'uniko ya haki kabisa kuhusu tozo na kodi nyingi ambazo zimepitiliza katika zao la kahawa na mazao mengine. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba siku tutakaposoma hotuba yetu kwa ajili ya mwaka ujao wa fedha awepo maana yake tutaziondoa tozo mwaka huu mpaka nyingine mtatuomba tuzirudishe.*(Makofi)*

**SPIKA:** Tubakize maswali haya Kagera huko huko, Mheshimiwa Rwamlaza na Mheshimiwa Gashaza, Mheshimiwa endelea.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kushangaza na kusikitisha kwa sababu wafanyakazi mimi nina malalamiko yao, nina *document* nitaweza kumletea Mheshimiwa Waziri hawajalipwa wale wafanyakazi na wengine wamefikia mahali pa kustaafu hawajapata hata pesa zao. Kile kiwanda kimebaki kubadilishwa na wasimamizi mara kwa mara kwa ajili ya kutaka kuwadhulumu wafanyakazi pamoja na wakulima. Ni lini Waziri utakwenda pale kuhakikisha wewe mwenyewe kwamba wafanyakazi wameshalipwa?

Mheshimiwa Spika, nina uhakika hawajalipwa hata senti tano.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwishasema kwa Mheshimiwa Rweikiza, niko tayari kukutana na Waheshimiwa Wabunge ili tufananishe taarifa tulizonazo. Taarifa sisi tuliyonayo ni kwamba tayari kuna malipo ambayo yamefanyika siyo yote sawa, lakini niko tayari kama nilivyosema kukutana nae ili tuangalie kwamba nani ana taarifa sahihi na vilevile Wizarani au Serikalini kama kuna Afisa ambaye ameniletea mimi taarifa za uongo atachukuliwa hatua.

**SPIKA:** Mheshimiwa Gashaza.

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nianze kwa kupongeza Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa ushirikiano wanaonipa kuhakikisha kwamba tunapata zao jipya Tanzania, zao linaloitwa *stevia* kupitia Jimbo langu la Ngara.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi tayari wameshatoa kibali cha kuingiza mbegu ya zao la *stevier* zao ambalo ni sukari ambayo ni *anti-diabetes, anti-pressure* lakini zao ambalo ni zao la kuinua kipato cha Watanzania. Pamoja na kutoa kibali hicho kwa sababu ni zao geni tunahitaji kufanya utafiti kwanza na tayari Wizara imeelekeza Kituo cha Utafiti Maruku ambacho kiko Mkoa wa Kagera kushirikiana na Kampuni ya *East African Stevier and Agro-Investment* kufanya utafiti wa zao hilo lakini tatizo ni fedha za kufanyia utafiti. Je, Wizara ya kilimo, Mifugo na Uvuvi wako tayari kutenga pesa ili kuwezesha kituo cha utafiti Maruku kushirikiana na Kampuni ya *East Africa Stevier* kutoa pesa ili kuweza kufanya utafiti huu na hatimae zao hilo liweze kuanzishwa katika nchi yetu ya Tanzania na kuleta mabadiliko ya uchumi?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri William Tate Ole Nasha.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Gashaza kwa jitihada na ubunifu ambao ameufanya Jimboni kwake katika kutafuta mazao ambayo yana tija kwa wakulima. Kimsingi tumekuwa tukishirikiana naye kama Wizara ili kuangalia namna ya kuleta nchini zao la *stevier* ambalo huko maeneo mengine linakolimwa lina tija kubwa sana. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kama ambavyo tayari tumeshashirikiana naye katika hatua za kusajili hilo zao, Wizara iko tayari vilevile kushirikiana naye na wananchi wake katika kufanya utafiti katika kituo chetu cha Maruku ili zao hilo liweze kuanza kulimwa nchini na Wizara iko tayari kutenga bajeti ya kawaida ya utafiti kwa kituo hicho ili utafiti huo uweze kufanyika.

**SPIKA:** Tunaendela Waheshimiwa Wabunge na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Swali litaulizwa na Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabla ya kuuliza swali hili kwanza naomba ku-*declare interest* kama mimi ni mfanyabiashara. Jambo la pili niwapongeze watendaji wa bandari kama *Port Manager* na wachukuzi wa bandari kwa kufanya kazi katika mazingira magumu ikiwemo tope na umeme ambao ni hatari. Baada ya maelezo haya naomba Serikali itoe majibu kwa wananchi na wafanyabiashara.

Na. 22

## Wafanyabiashara wa Zanzibar Kulipishwa Fedha nyingi katika Bandari ya Dar es Salaam

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB** Aliuliza:-

Kumekuwepo na malalamiko makubwa kwa wafanyabiashara wa Zanzibar wanaotumia Bandari ya Dar

es Salaam kwa meli za Zanzibar zinapovuka Malindi hulipishwa fedha nyingi na mizigo kupimwa kwa *CBM* tofauti na ilivyokuwa kabla; huku baadhi ya wafanyabiashara wengine wanachajiwa kwa tani ambapo ni nafuu kutokana na hali halisi ya mizigo yenyewe.

(a) Je, ni sawa kwa vyakula *(local goods)* kama vile viazi mbatata, dagaa, mahindi, dawa zinazopelekwa hospitalini, vitunguu kuchajiwa kwa *CBM;* na je, ni kweli kunasaidia wafanyabiashara au kuwakandamiza kiuchumi hasa ikizingatiwa kuwa bidhaa zenyewe ni vyakula?

(b) Je, nia ya Serikali ni kuwakwamua wananchi kiuchumi au kuwakandamiza hasa ikizingatiwa kuwa baadhi yao ni wafanyabiashara wadogo wadogo?

(c) Je, ni sababu gani za msingi kwa bandari hiyo kuchukua fedha wakati huduma nyingine hawazipati kwa miaka yote?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Injinia Ngonyani.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, Mbunge kutoka Baraza la Wawakilishi lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Tozo zote bandarini huzingatia uzito yaani *tonnage* au ujazo wa shehena *(CBM)* kwa mujibu wa kitabu cha Tozo cha Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari *(TPA).* Viwango vya tozo vilivyopo vimelenga katika kuwasaidia wafanyabiashara kupata huduma bora na pia kuhakikisha kuwa bandari inajiendesha na gharama za uendeshaji zinarudishwa *(cost recovery).* Aidha, hufanyika mashauriano ya wadau kabla ya viwango vilivyopo kuridhiwa.

(b) Serikali siku zote imekuwa na nia njema ya kuwakwamua wananchi kiuchumi kwa kuweka mazingira

mazuri kwa wananchi kufanya biashara kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za utoaji huduma za bandari.

Aidha, Serikali kupitia mamlaka ya usimamizi wa bandari imenunua vifaa vya ukaguzi wa mizigo, vifaa vya kuhudumia shehena na kuboresha maeneo ya kupumzikia abiria. Serikali itaendelea kuboresha huduma za bandari na kuangalia tozo ambazo ni stahiki kwa wadau wa bandari.

(c) Sababu za msingi kwa *TPA* kutoza tozo kisheria ni kurejesha gharama za utoaji wa huduma za bandari ili kufanya huduma hizo kuwa endelevu na kuendelea kuwekeza katika mifumo ya usimamizi ambayo itaongeza ufanisi na hatimaye kupunguza gharama za utoaji wa huduma za bandari.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jaku swali la nyongeza.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, ningeomba tu Mawaziri na Naibu Mawaziri wakafanye utafiti kwanza wa kina kabla ya kujibu maswali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu aliyojibu Naibu Waziri, haoni wakati umefika sasa ukiona kuwa mizigo iliyokuwa inapimwa kwa tani hapo mwanzo na hivi sasa kuchanganywa na *CBM* haoni ipo haja kwa hivi sasa mzigo wote ule ukapimwa kwa tani badala ya *CBM* ukizingatia Wazanzibari wanategemea chakula sana kutoka Tanzania Bara kwa ndugu zetu wa damu na vilevile biashara kubwa iliyopo kati ya Zanzibar na Tanzania Bara ndiyo uchumi mkubwa wa Zanzibar ukiacha zao la Karafuu kuzaa mwaka hadi mwaka?

Swali la pili, Mheshimiwa Naibu Waziri utakuwa tayari kufuatana na mimi mguu kwa mguu na tarehe unipe ili *Hansard* zikae sawa kwenda kuona kama alivyofanya Waziri aliyepita Mheshimiwa George Harrison Mwakyembe na akaona matatizo yaliyopo pale na mengine akayapatia ufumbuzi lakini kwa bahati mbaya akaondoka Wizara ile, ikiwemo umeme uliopo pale ni hatari chini, mabonde ya

mpunga yaliyopo pale hivi sasa bila kukusudia baada ya bandari na wakati wenye meli wanalipa gharama zile.

Je, ni lini tutafuatana mimi na wewe ili kwenda kuona kadhia zilizopo pale ikiwemo na Kampuni ya Hisab kushindwa kufanya majukumu yake?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Jaku, majibu ya maswali haya Mheshimiwa Waziri, Injinia Ngonyani.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, hivi vyote viwili ni vipimo vinavyotumika kutegemeana na aina ya mzigo ulivyopakiwa, ni lazima vyote hivi viwili vitumike *the Cubic Bank Metres* pamoja na *tonnage.* Kutaka itume *tonnage* peke yake kuna aina ya mizigo itatoa hali siyo nzuri kwa *TPA* namna ya kui-*handle* kutokana na namna ilivyopakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo kutokana na swali lake la pili na ukijua wazi kwamba Waziri wangu ni mdau mkubwa wa bandari zote za kule Zanzibar nitaomba niwasiliane nae tukubaliane yeye au mimi na tukishakubaliana nitakupangia tarehe, tutakupigia siku ya kwenda huko Zanzibar kulishughulikia hili.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Hairuhusiwi taarifa kwa wakati huu. Mheshimiwa Maryam Msabaha na Mheshimiwa Ally Keissy.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Watanzania wengi wanategemea bandari na kumekuwa na ukiritimba wa kutozwa kodi mara kwa mara wafanyabiashara sasa hivi wanakwepa bandari zetu, je, Serikali ina mikakati gani

kuweka utaratibu mzuri wa utozaji kodi katika mizigo ya wafanyabiashara ili biashara zipate kupita katika bandari zetu?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Injinia Ngonyani.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika swali langu la msingi kwamba upangaji wa bei na hiki kitabu ambacho kinatumika na watu wa *TPA* wakati kinaandaliwa kabla hakijapitishwa huwa kinashirikisha wadau wa bandari. Labda tu nimhakikishie kwamba tutakapofika muda wa ku-*review* hizi *rates* tutahakikisha wadau tunawashirikisha tena, inawezekana *dynamics* zimebadilika kwamba mazingira ya wakati bei hizi zinapangwa ni tofauti na mazingira ya sasa. Tutamshirikisha na nitaomba sana *comments* zako na wadau waziweke ili tupate kitabu kipya ambacho kitazingatia hayo ambayo wewe umeyasema na Mheshimiwa aliyeuliza swali la msingi ameyasema.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Keissy, swali la mwisho la nyongeza.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Katika kijiji cha Kirando mwambao wa Ziwa Tanganyika, *TPA* wameweka mtu wao kutoza ushuru mzigo wowote unaotoka pale katika kijiji cha Kirando wakati *TPA* hawajaweka huduma yoyote. Hamna kibanda, hamna hata choo, hamna chochote walichoweka lakini kila mwananchi anayesafirisha mzigo kwenda Kabwe, kwenda Mwandakerenge, kwenda Mvuna anatozwa ushuru na watu wa *TPA.*

Mheshimiwa Spika, je hiyo ni halali?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo kuhusu bandari ya Kirando. Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, kuna huduma nyingi za bandari na mojawapo ni kuwa na vyoo, sehemu ya kupumzikia lakini kuna huduma zile za kutoa mzigo kutoka kwenye maji na kuupeleka kwenye nchi kavu. Ile huduma ina gharama, inahitaji kulipiwa. Kwa hiyo, wale ambao wanapata hiyo huduma hata kama hizi huduma zingine hazijakamilika kwa vyovyote vile watatakiwa walipie ili ku-*recover* zile gharama wanazotumia watu wa bandari.

Mheshimiwa Spika, labda tu hoja yake ni kwamba tuboreshe hii bandari ya Kirando ili huduma zote za bandari ikiwa ni pamoja na uwepo wa vyoo na huduma zingine eneo la kupumzikia abiria tuzijenge. Hilo nimelipokea, tutalifanyia kazi.

**SPIKA:** Swali la mwisho kwa siku ya leo linaulizwa kwa Wizara ya Maliasili na Utalii na Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya Mbunge wa Kaliua.

Na. 23

**Kuilinda Hadhi ya Hifadhi ya Ngorongoro**

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA** Aliuliza:-

Hifadhi ya Ngorongoro *(NCAA)* ni hifadhi ya kipekee hapa nchini, Afrika na dunia kwa ujumla; hifadhi hii ina vivutio vya kipekee pamoja na kuwa na matumizi mseto *(multiple land use)* ambapo wanyama na mifugo inachungwa pamoja; kutokana na upekee huo hifadhi hii imetambuliwa na kuwekwa kwenye maajabu saba ya dunia chini ya Shirika la Uhifadhi Dunia *(UNESCO).*

Je, Serikali ina mpango gani endelevu wa kuhakikisha hadhi ya hifadhi hii inabaki kwenye ubora wake kwa ajili ya vizazi vya leo na vijavyo na pia kwa uchumi wa Taifa letu?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** Alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mbunge wa Kaliua, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa eneo la hifadhi la Ngorongoro ni muhimu na lina hadhi ya kipekee inayotokana na wingi na ubora wa vivutio vyake ambavyo vinatambulika Kitaifa na Kimataifa. Vivutio hivyo ni pamoja na matumizi mseto ya eneo, uwepo wa viumbe hai walioko hatarini kutoweka duniani na umuhimu wa kihistoria uliothibitishwa na tafiti mbalimbali kuwa binadamu wa kwanza aliishi katika eneo hilo takriban miaka milioni 3.6 iliyopita. Aidha, kutokana na sifa hizo Shirika la Umoja wa Mataifa la *UNESCO* kupitia orodha yake ya maeneo ya urithi wa dunia (*World Heritage Sites)* imelipatia eneo hilo hadhi ya kimataifa, ambapo tangu mwaka 1979 limekuwa moja ya maeneo ya Urithi wa Dunia kwa kigezi cha thamani ya maliasili iliyomo *(The Integrity for natural value).*

Mheshimiwa Spika, pamoja na sifa zilizotajwa hapo juu, kuanzia Februari, 2010 eneo hili limepewa hadhi nyingine kwa kigezo cha eneo la rasilimali mseto za maliasili, malikale na utamaduni yaani *the mixed heritage value* hivyo basi kwa kutambua upekee huo kwa Taifa, Serikali imejipanga kuhakikisha kuwa eneo hili linabaki katika viwango bora vya uhifadhi kwa kuchukua hatua zifuatazo:-

(a) Kudhibiti ongezeko la idadi ya watu na mifugo ndani ya eneo la hifadhi, zoezi ambalo litaanza rasmi tarehe 12 Aprili, 2017 na kukamilika mwezi Juni, 2017. Aidha, wadau mbalimbali watashirikishwa katika zoezi hili ikiwemo mamlaka za Mkoa na mamlaka ya Wilaya, Taasisi ya Taifa ya Takwimu, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa na TAMISEMI.

(b) Kuendelea kuimarisha ulinzi wa wanyamapori na maeneo yote muhimu kwa shughuli za utalii kama vile *crater* na kutoruhusu shughuli za kibinadamu katika maeneo hayo.

(c) Kufanya mapitio ya sheria iliyoanzisha Mamlaka

ya Hifadhi na kuiboresha ili iendane na hali halisi ya sasa. Zoezi hili liko katika hatua za awali na linatarajiwa kukamilika katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sakaya, swali la nyongeza.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ni kwa nini Serikali inaruhusu na kutoa vibali kujengwa kwa hoteli za kitalii kuzunguka *rim* ya *Ngorongoro Crater* hali inayoharibu mandhari ya Ngorongoro lakini pia ni vyanzo vya maji kwa ajili ya hifadhi hii?

Swali la pili, wakati Ngorongoro inaanzishwa mwaka 1959 ilikuwa na wakazi 8,000 lakini kwa takwimu za mwaka 2013 hifadhi hii ina wakazi elfu 87.7 kwa hivyo leo tunavyozungumza ni zaidi ya laki moja. Lakini kuongezeka kwa watu maana yake ni kuongezeka kwa mifugo lakini pia kuongezeka kwa mahitaji na huduma mbalimbali.

Naomba Serikali iliambie Bunge, wakati Hifadhi inaanzishwa, *master plan* ya *Ngorongoro Crater* inasemaje juu ya uwepo wa idadi gani ya watu ambao wanaweza kuhudumiwa kikamilifu wakapata huduma zote, lakini pia hadhi ya hifadhi ikaendelea kubaki kama ambavyo tunategemea? Ahsante sana.*(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Maliasili na Utalii, Injinia Ramo Makani.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Magdalena Sakaya kwa kuwa kwanza yeye ni Mhifadhi kitaaluma lakini pia amekuwa miongoni mwa Wajumbe wa Kamati ya Maliasili na Utalii ambao wamekuwa katika mstari wa mbele kuishauri Serikali kuhusiana na masuala ya maliasili na utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la kwanza ni kweli ukienda Ngorongoro leo utakuta kuna hoteli zimejengwa kandokando ya *crater* kwenye eneo linaloitwa *rim* ya *crater.* Lakini uwepo wa hoteli hizi ni ambao umetokana na mabadiliko mbalimbali tangu sheria ilipokuwa imeandikwa kwa mara ya kwanza mwaka 1952. Sheria hii ilifanyiwa marekebisho ya kwanza mwaka 1963 lakini baadae sheria hiyo ilifanyiwa marejeo mwaka 2002. Katika vipindi hivyo mabadiliko mbalimbali yametokea, sasa tangu amri ilivyotolewa kutokana na sheria kwamba sasa hakuna kuanzisha hoteli kandokando ya *crater* na hasa kwenye eneo la *rim* hakuna hoteli nyingine yoyote imeanzishwa katika kipindi hicho. Nyingi zilizopo ni zile ambazo zilianzishwa katika kipindi cha nyuma.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali lake la pili ni kweli kwamba mwaka 1959 wakati sheria hii inapitishwa kulikuwa na takribani watu 8,000 katika eneo la hifadhi na kwamba ni ukweli ulio wazi takwimu zinaonesha mwaka 2013 tayari idadi ya watu ilifikia 87,851. Ukifanya hesabu ni kama vile ongezeko la wakaazi 1500 takriban kwa kila mwaka. Hili ni ongezeko linaloashiria kwamba leo tukifanya takwimu kweli tunaweza kupata wakaazi wanaokaribia laki moja, hii ni idadi kubwa sana na ni tishio  kwa shughuli za hifadhi katika eneo hili la Hifadhi la Ngorongoro.

Mheshimiwa Spika, hatua ambazo Serikai inafanya kama nilivyojibu kwenye swali la msingi ni uwepo wa sheria peke yake utakaoweza kutoa mwongozo na mwelekeo namna gani tunaweza kukabiliana na changamoto za hifadhi katika eneo la Ngorongoro. Sasa sheria iliyopo ina mapungufu ni kweli na ndiyo maana nimesema katika jibu la msingi kwamba katika kipindi cha muda mfupi ujao mchakato wa kufanya marekebisho ya sheria ili iendane na matakwa ya sasa ya uhifadhi katika eneo linalohusika utaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe Waheshimiwa Wabunge, mara Serikali itakapoleta sheria hii mbele ya Bunge hili baada ya kukamilisha michakato ya awali, wote tuwe

na *spirit* ya kutaka uhifadhi uimarishwe katika eneo la Ngorongoro ili tuweze kupata faida zote za urithi na kiuchumi na faida nyingine zote zinazotokana na uhifadhi kupitia utalii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Shally Raymond na Mheshimiwa Pauline Gekul maswali ya mwisho ya nyongeza.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hadhi ya Hifadhi ya Ngorongoro inafanana kabisa na hadhi ya Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro, mlima ambao ni mrefu sana, mlima ambao unaingiza kipato kikubwa kwenye utalii, mlima ambao ni wa pekee wenye theluji katika nchi za *tropic.*

Je, Serikali sasa ina mpango gani kuhakikisha kwamba wanaozunguka mlima ule wanaweza kuwekwa katika hali ambayo wataendelea kuutunza ili ile theluji isije ikayeyuka yote na ule mlima ukabakia katika ubora wake?

**SPIKA:** Majibu kwa kifupi Mheshimiwa Naibu Waziri Maliasili na Utalii, hifadhi ya Mlima Kilimanjaro.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwanza ni kweli kwa maana ya sifa za uhifadhi, lakini pia faida za kiuchumi zile za Ngorongoro zinafanana kwa karibu sana na za hifadhi ya Mlima Kilimanjaro. Sasa kuhusu swali lake nini Serikali itafanya ili kuweza kuboresha zaidi shughuli za uhifadhi kwa faida za kiuchumi Kitaifa lakini pia kwa faida ya jamii inayoishi kwenye maeneo haya ya Hifadhi ya Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba kwanza Serikali inatambua umuhimu wa ushiriki wa wananchi katika shughuli za uhifadhi na kwa kweli tunatoa wito kwa wananchi wanaoishi katika eneo hili la Mlima Kilimanjaro waweze kuendelea kushirikiana na Serikali katika kuhakikisha kwamba uhifadhi unaimarishwa katika eneo la Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, jitihada za Serikali ni kuendelea kusimamia sheria iliyopo lakini pia tunakaribisha maoni kutoka kwa wananchi wanaoishi kwenye eneo hilo hata wengine waweze kutusaidia ili kuweza kupata maoni ya wananchi yatakayotuwezesha kuboresha zaidi shughuli za uhifadhi katika eneo la Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa gharama kubwa ambazo Hifadhi ya Ngorongoro inatumia ni pamoja na kumtunza faru Fausta ambaye chakula chake kwa mwezi ni shilingi milioni zaidi ya 64. Naomba kufahamu, Serikali ina mpango gani juu ya faru huyu Fausta ambaye analigharimu Taifa au hifadhi ile kwa fedha nyingi sana kwa mwezi na hata kwa mwaka?

**SPIKA:** Mheshimiwa Pauline unaulizia kuhusu faru Fausta, lakini huulizii kuhusu faru Ndugai. Mheshimiwa Waziri majibu. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Gekul kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli yuko faru Fausta pale Ngorongoro na amewekwa kwenye *cage* kwa sababu amekuwa mzee sana na amekuwa ananyemelewa na magonjwa aina mbalimbali na lengo ni kuhakikisha kwamba maisha yake yanaendelea utafiti na takwimu ambazo zinakusanywa kwa ajili ya faru huyu zinaendelea, kwa sababu wanyama hawa ni wachache sana nchini hivi sasa na kila takwimu ambayo tunakusanya na kuilinganisha na maisha halisi ya wale ambao wako kwenye pori ni muhimu kwa maisha ya wale wengine ambao wanaishi humo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kufanya kazi hii kuna gharama, lakini hizi ndiyo gharama halisi za uhifadhi.

Namuomba Mheshimiwa Mbunge aendelee kutuamini kwamba tunafanya jambo hili kwa nia njema na kwamba takwimu zinazopatikana zinathamani halisi kwa ajili ya uhifadhi wa wanyama hawa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati wa maswali umeisha.

Waheshimiwa Wabunge, wengine walifikiri nafanya utani, ni kweli Ngorongoro yuko faru anaitwa faru Ndugai. Mlimuona eeh? Eeh yupo, Mheshimiwa Waziri huyo faru akipotea kama faru John itakuwa patashika hapa ndani. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, ni matangazo mafupi na baada ya shughuli hizi fupi basi tutaendelea na hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nitaomba muendelee kuwepo ili tumsikilize Mheshimiwa Waziri Mkuu na huo ndiyo utakuwa mwanzo wa *marathon* yetu ya bajeti kama ilivyo ada huwa tunaanza na Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mkumbuke tu kwamba safari hii Wizara ya TAMISEMI haipo kwa Waziri Mkuu iko kule Ofisi ya Rais, kwa hiyo, baadae wakati wa uchangiaji msije mkajisahau maana baada tu ya Waziri Mkuu itafuata sasa Ofisi ya Rais ambako TAMISEMI ipo.

Wageni walioko katika jukwaa la Spika ni pamoja na Dkt. Hamisi Mwinyimvua, Katibu Mkuu, Sera na Uratibu, ahsante na karibu sana. Ndugu Erick Shitindi, Katibu Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu. Karibu sana. *(Makofi)*

Wengine ni Ndugu Maimuna Tarishi, Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu na Bunge. Huyu ndiye Katibu Mkuu anayeshughulika na mambo yetu ya Bunge katika Ofisi ya Waziri Mkuu. Wameambatana na Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu.

Pia wapo wageni mbalimbali upande wangu wa pili wa jukwaa, tunawakaribisheni sana wote. Kipekee tunao

wageni wanafunzi wa Shule ya Msingi ya *St. Ann's* kutoka Morogoro Mjini, wapo 60 na walimu watano naomba msimame pale mlipo, karibuni sana wanangu, karibuni sana hapa Bungeni tumefurahi sana kuwaona. Mmetoka Morogoro kuja kujifunza na mtapata mafunzo mbalimbali ambayo yameandaliwa na Ofisi yetu ya Bunge, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine ni kwamba leo siku ya Alhamisi tarehe 6 Aprili, 2017 mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge hapa saa saba kamili mchana mnaombwa wote kuhudhuria ibada itakayoongozwa na Mtumishi Mwalimu Mwakasege ambaye atakuwa pamoja nasi katika ibada hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, wote wa madhehebu mbalimbali mnaalikwa kuhudhuria, baadaye kidogo nitawatangazia kwamba ibada hiyo itafanyika katika eneo gani la Bunge. Tunajaribu kutafuta eneo ambalo ni *more spacious*.

Waheshimiwa Wabunge, jana mchana baada tu ya shughuli za Bunge saa saba, palitokea ajali nje tu ya geti letu hapa ya mwendesha pikipiki ambaye baada ya askari kuzuia magari yasimame kuwawezesha Wabunge wanaopita kwa miguu kwenda upande wa pili walikoegesha magari waweze kupita, magari yote yakawa yametii yamesimama, lakini akatokeza mtu mmoja anayeendesha pikipiki nadhani ni bodaboda, yeye akawa anakuja wangu wangu wakati watu tayari wameshajaza barabara ile kupita. Kutoka huko anakotoka akiwa anaendesha kama mwendawazimu akamvamia Mbunge mwenzetu ambaye anaitwa Mheshimiwa Aida Khenani na alianguka chini akagonga kichwa chini na akaumia vibaya sana.

Kwa jinsi hiyo, tukampeleka Hospitali yetu ya Mkoa pale wakashauri kwamba anahitaji matibabu ya haraka sana Muhimbili, na jana ile ile kupitia Bima zetu za Afya za Mfuko wa *NHIF* tukaomba watuletee ndege, kwenye majira ya saa kumi na nusu baadhi ya Wabunge walituwakilisha wakawa pale uwanjani na mimi mwenyewe nilienda pale

tukamsafirirsha mwenzetu. Kwa hiyo, amepelekwa Muhimbili bado hatujapata mrejesho wa anaendelea vipi kule. Kwa hiyo naomba katika dua zenu na sala zenu mumkumbuke mwenzetu Mheshimiwa Aida Khenani, kwa kweli alikuwa ameumia sana. Inasemekana huyo mwendesha pikipiki mwenyewe alivunjika mguu.

Kwa hiyo, nawaomba askari pale nje waimarishe usimamizi wao na uangalizi wao wa barabara, lakini pia tunakuomba Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi iko haja kubwa ya kuweka matuta, katika maeneo yanayopakana na Bunge ya barabara hii kuu kwa vile hivi sasa magari yameongezeka sana na kwa kweli kuna tatizo kubwa sana Wabunge wanapotoka na kuingia humu Bungeni. Tujaribu kuangalia namna gani ya kusaidia katika jambo hilo. *(Makofi)*

Kabla sijaendelea tuna dakika chache ambazo naweza nikapokea miongozo miwili, mitatu.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**SPIKA:** Haya Katibu nitajie majina.

Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, Mheshimiwa Kangi Lugola, Mheshimiwa Mlinga, Mheshimiwa Jaku Hashim, Mheshimiwa Joseph Mhagama, wanatosha hao twende hivi hivi mlivyojiandikisha. Joseph Mbilinyi kifupi sana naomba muda wa leo ni mdogo tuna mambo mengi sana.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

Naomba Mwongozo kupitia Kanuni ya 68(7) jambo lililotokea mapema Bungeni, majadiliano yanayoendelea miongoni mwa Wabunge walio wengi kuhusiana na tukio lililotokea jana saa moja usiku ambapo watu wenye silaha wakiwa kwenye gari aina ya Noah walivamia studio za *Tongwe Records* Oyesterbay Dar es Salaam, wameteka watu watatu akiwemo msanii maarufu Roma Mkatoliki na wote hawajulikani walipo mpaka sasa. Pia kwenye studio hiyo

watu hao wenye silaha wameondoka na *computer*, *camera* na vifaa vingine vya studio. Sababu za kuvamiwa studio hiyo zinafanana na sababu za kukamatwa kwa Msanii Nay wa Mitego ambaye kimsingi Rais alitengua kukamatwa kwake.

Mheshimiwa Spika, naomba kupata Mwongozo ni nani anayetoa amri za mambo haya, bunduki kuwa nje nje kwenye Taifa hili. Mara *Clouds Media* wamevamiwa na bunduki, mara Waziri Nape ametolewa bastola *where are we taking this country?*

Naomba Mwongozo wako ili Serikali sasa ichukue wajibu wake kulinda mali za raia badala ya kutumia *mercenaries* kwa sababu hawana *uniform*, hawajitambulishi, hawaambii watu kwamba wanawakamata kwa sababu gani, na ndiyo maana tunasema watu wametekwa. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mimi naamini Serikali imesikia katika hili, Serikali tu ifuatilie kuweza kujua jambo hili kwa sababu ni vigumu kwa Spika kutoa Mwongozo ndiyo nasikia kutoka kwako. Kwa hiyo, ndiyo Mwongozo wangu kwamba Serikali ilifuatilie jambo hili *(Makofi)*

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwakajoka atafuatiwa na Mheshimiwa Waitara.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mwongozo wangu unaelekea kwenye jibu la msingi la Mheshimiwa Waziri alipokuwa akijibu swali la Mheshimiwa Gekul kuhusiana na faru Fausta.

Majibu ya Mheshimiwa Waziri anasema kwamba faru Fausta yupo, kama swali lilivyokuwa likielekezwa kwake na anatumia gharama ya shilingi milioni 64 kwa mwezi. Tafsiri yake ni kwamba kwa mwaka anatumia karibuni shilingi milioni 768 na sifa yake kubwa ya kutumia fedha hizi, na ni kwa nini wanamgharamia, faru huyu ni mzee sana.

Mheshimiwa Spika, shilingi milioni 64 kwa mwezi na milioni 768 kwa mwaka ni fedha nyingi sana ambazo zingeweza kuhudumia shughuli mbalimbali za Kitaifa.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba mwongozo wako kwamba ni namna gani fedha hizi zinaweza zikaokolewa na kwa sababu faru huyu ni mzee na inaonekana kwamba hawezi kuingiza faida yoyote kwenye Taifa hili ni namna gani Serikali inaweza ikachukua nafasi ya kuziokoa fedha hizi na ikiwezekana aachiwe aendelee kula kama ambavyo inatakiwa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana huo ni ushauri kwa Serikali naomba wala hamna haja ya kujibu Mheshimiwa Waziri wa Maliasili naomba muuchukue na kuufanyia kazi kama mtaona ni jambo ambalo lina tija na kamati husika na ninyi muendelee kufatilia na kuishauri Wizara namna bora zaidi ya kushughulika na huyu Dada Fausta.

Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naomba Mwongozo wako katika mambo mawili. Jambo la kwanza...

**SPIKA:** Jambo moja Mheshimiwa kwa sababu ya muda.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, *okay* basi nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, hapa Bungeni leo wamekuja wageni sikuwaalika mimi ni wananchi wa kawaida tu lakini wametokea Dar es Salaam, na wengine kutoka Jimbo la Ukonga. Wameniita hapo nje wakasema ni muhimu Serikali kupitia mwongozo wako itoe maelekezo, tamko au utaratibu kwamba kuna suala linaendelea kubwa katika Taifa hili la njaa. Dar es Salaam kwa mfano sasa hivi tunavyozungumza unga kiroba kilo 25 ulikuwa unauzwa shilingi 22,000 sasa imefikia mpaka shilingi 48,000 mpaka

shilingi 40,000 kwa sasa tunavyozungumza. Vilevile hata wale wafugaji wadogo wa kawaida kwangu kule wanafuga kuku wa kienyeji na wa kisasa, debe sasa hivi inauzwa shilingi 6000, gunia shilingi 30,000 kutoka shilingi 20,000 ya mwanzo.

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba inaonekana watu wengi siku hizi wanashinda njaa kwa sababu ya hali ngumu ya maisha. Sasa Serikali inasema chakula kipo na huu mzunguko wa fedha haupo.

Sasa naomba Mwongozo wako, ili Mheshimiwa Waziri Mkuu na Serikali watoe tamko la kuachia mahindi yaingie mtaani ili wananchi wetu wapate unafuu wa ununuzi wa chakula wasife njaa kwa kuuziwa kwa bei nafuu zaidi kwa watu ambao wana hali ya chini. Huo ndiyo Mwongozo wangu naomba usaidie. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waitara, pia suala hilo Serikali imesikia kupitia hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu tutakapokuwa tunaijadili, watakapokuwa wanahitimisha wanaweza wakaligusia na kama hawajagusia Ofisi ya Waziri Mkuu, basi Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi wapo kwa vyovyote vile wakati wa bajeti yao watalifafanua jambo hili la chakula kwa Watanzania.

Mheshimiwa Kangi Lugola.

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo chini ya Kanuni ya 68(7). Hadi hivi sasa ninavyozungumza na kuomba Mwongozo wako, kupitia vyombo vya habari mbalimbali na ikiwemo mitandao ya kijamii ambayo simu yangu hii niliyoishika hapa na kukuonesha kuna *clip* ambayo inazunguka kwa Watanzania ambayo inatokana na maudhui yaliyofanyika kwenye uchaguzi wa kuwachagua Watanzania kutuwakilisha kwenye Bunge la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, maudhui hayo yanatokana na matusi makubwa ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni Mheshimiwa Freeman Mbowe akilitukana Bunge lako Tukufu,

akitukana Chama cha Mapinduzi ambapo maana yake Chama cha Mapinduzi Kiongozi wake Mkuu ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utakumbuka na Bunge lako Tukufu uchaguzi huu ambao tuliufanya hapa Bungeni, ni uchaguzi ambao ulikuwa wa kidemokrasia, ni uchaguzi ambao tuligawiwa vitabu vya kupigia kura ambavyo vilikuwa na orodha ya majina ya Watanzania waliokuwa wanagombea nafasi hizi kupitia vyama vyao vya uwakilishi ndani ya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kilichotokea baada ya kuonekana kwamba Chama cha Demokrasia na Maendeleo wagombea wake wawili wameshindwa, wamekataliwa kwa kura za kidemokrasia na Bunge lako, Mheshimiwa Freeman Mbowe ameamua kutukana Bunge hili kwamba ni wajinga, wapuuzi na hawana maana yoyote.

Mheshimiwa Spika, Mwongozo ninaouomba hivi ni ruhusa kwa kiongozi wa chama ambaye Wabunge wake wameshindwa kihalali, ni ruhusa kulitukana Bunge hili na kulinajisi miongoni mwa Watanzania na kumtukana Rais ambaye anaongoza Chama cha Mapinduzi ilihali kuonesha demokrasia kuna Wabunge zaidi ya 50 wa CCM ambao waliwapigia kura CHADEMA kuonesha misingi ya demokrasia CCM iliyokomaa ni halali kulitukana Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naendelea tena kusema kwa mara nyingine safari hii tuko hapa kwa muda mrefu. Tuko hapa takribani miezi mitatu, kila mnachofanya hapa tumeimarisha sana hapa Bungeni, tunamuona kila mmoja wenu kwa tabia zenu na mwenendo wenu. Nimeshasema sana na tuko tayari kwenda *extra mile* kuleta *displine* ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Narudia tena mnapozungumza ninyi, wenzenu wanawasikiliza, wanapozungumza wenzenu kazi yenu ni

kuzomea, kila mmoja tunampata hilo nataka kuwahakikishieni. Tutachukua hatua, tutachukua hatua, tutachukua hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mlinga.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mwongozo wangu naomba kupitia Kanuni ya 68(7) nikiwa naongezea kutoka kwa Mbunge aliyepita.

Mheshimiwa Spika, juzi ulifanyika uchaguzi. Uchaguzi huo ulikuwa kwa ajili ya Wabunge wa Afrika Mashariki, hoja zangu ndogo tatu. Moja, kwanza uchaguzi huo ulitakiwa tuioneshe nchi yetu kwa kiasi gani ina demokrasia. Wanachama wa Chama cha Mapinduzi walikuwa zaidi ya 400 tulikuwa tunawahitaji sita, lakini tuliwachuja ikafika kipindi wakabaki 12, tukawaleta Bungeni, Wabunge wenzetu wa CHADEMA mkatusaidia kuwachagua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbili, wagombea wawili kati ya Masha na Wenje. Mheshimiwa Masha aliwahi kuwa Mbunge wa Nyamagana kupitia CCM tunamfahamu vizuri, aliwahi kumwekea pingamizi Mheshimiwa Wenje kuwa siyo raia wa Tanzania, uraia wake una mashaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa basi tulikuwa tunachagua mtu kwa ajili ya kwenda kuiwakilisha Kenya au kwa ajili ya kuiwakilisha Tanzania? Mtuelewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye hilo hilo namba mbili (b) Mheshimiwa Masha aliwahi kuwa Mbunge wa CCM, aliposhindwa kwenye uchaguzi alienda Ofisi ya Mbunge akachukua *furniture* akangoa vitasa hadi vya milango, mtu mwenye tabia ya uhuni wa namna hii tusingeweza kumchagua. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, tatu, mimi ni miongoni mwa Wabunge wenye umri mdogo humu ndani, kwa umri wangu nina uwezo wa kumtambua mwanamke ama mwanamme kwa sauti, jina na mambo mengine.

Sasa basi naomba wenzetu CHADEMA mtusaidie, katika uchaguzi wote kuna *gender balance,* kati ya Wenje na Masha nani alikuwa anawakilisha jinsia ya kike na nani alikuwa anawakilisha jinsia ya kiume? *(Makofi/kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba Mwongozo wako Mheshimiwa Mbowe kwa matusi aliyotukana achukuliwe hatua kali za kisheria, kwanza kwa sababu ni kiongozi mkongwe, pili ni Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Mhagama.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nasimama kwa Kanuni ya 28(7) kuhusu kupata Mwongozo wako. Kwa vile walionitangulia tayari wamerejea huko sitafafanua sana. Nikuombe tu Mwongozo wako pale ambapo kiongozi mkubwa wa Kambi ya Upinzani anapotoa matusi na anamjumuisha Mheshimiwa Rais, anakujumuisha wewe Mheshimiwa Spika na anamjumuisha Waziri Mkuu ni hatua gani Bunge lako linatakiwa kuchukua? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jaku wa mwisho.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana mimi langu ni dogo tu. Nasimama kwa Kanuni ya 68(7) kuomba Mwongozo wako.

Mheshimiwa Spika, baada ya maswali na majibu Mheshimiwa Naibu Waziri aliniambia kuhusu Bandari ya Zanzibar. Siyo bandari ya Zanzibar nataka kumuweka sawa ni Bandari ya Dar es Salaam. Kama ingekuwa bandari ya Zanzibar ningeulizia kule nakotokea mlangoni Baraza la Wakilishi, nisingekuja kuuliza hapa.

Kwa hiyo, anipangie tu tarehe ni lini twende tukaangalie tope zilizopo pale, kuangalia afya za wafanyakazi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jaku alikuelewa na nakushukuru kwa ufafanuzi huo. Kilichokuwa kikiongelewa ni Bandari ya Dar es Salaam.

Kwanza tuna wageni wengine ambao kabla sijatoa miongozo kuna wale wa *Governing Council* ya *Tanganyika Law Society* popote pale mlipo naomba msimame. Karibuni sana na Mheshimiwa Rais wenu tunaye hapa Bungeni, Mheshimiwa Tundu Lissu. Najua mna *appointment* na mimi kwa wakati muafaka Maafisa wangu watawajulisha tunakutana sasa ngapi. *(Makofi)*

Pia nina mgeni kwenye Jukwaa la Spika Mheshimiwa Adam Omari Kimbisa. Ahsante sana Mheshimiwa Kimbisa yeye ni Mbunge Mteule wa Bunge la Afrika Mashariki katika hawa tuliowachagua juzi, kwa hiyo tunakutakia kila heri katika kutuwakilisha kule Afrika ya Mashariki, Mwenyezi Mungu akutangulie. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu hii miongozo mingine ya masuala yanayohusiana na utovu wa nidhamu hapa Bungeni na naomba tusikilizane sana.

Kama nilivyosema Waheshimiwa Wabunge tumeimarisha sana masuala ya kujua mwenendo wa kila mmoja wetu ndani ya jengo hili na hata katika viwanja vyote vya Bunge, isipokuwa vyooni peke yake, lakini maeneo yaliyobaki mengine yote tuko imara na tuko vizuri sana. Ningeomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na yote hii ni kwa ajili ya usalama wenu na ulinzi wenu. Kwa hiyo, ukiwa hapa ni vizuri ujue kabisa huko Jimboni au mahali pengine ni mahali ambapo kwa kweli unapaswa kujiheshimu Kibunge.

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu hoja zilizotolewa kuhusiana na vurugu zilizokuwa zikifanywa na baadhi yetu ile juzi wakati wa uchaguzi ule wa Wabunge wetu wa Afrika Mashariki, ambao kabla sijasema chochote niseme kwamba nafasi mbili zile ambazo hazikujazwa juzi kwa sasa bado ni nafasi za CHADEMA. Kwa wakati muafaka Katibu wa Bunge

ambaye ni Msimamizi wa Uchaguzi atawaarifu ni lini mchakato ule uweze kufanyika na ni lini sisi Bunge tunatakiwa tuwapate Wabunge hao kutoka CHADEMA.

Ikumbukwe kwamba maamuzi haya ya kusema Wabunge hawa wa chama hiki, Wabunge hawa wa Chama hiki, pamoja na mambo mengine ni Maamuzi ya Spika. Tukumbuke ni Bunge hili ambalo kwenye Bunge lililopita Maspika wenzangu hawakufanya hivyo, waliweka Upinzani katika kundi moja na hata Bunge la Mama Makinda lilikuwa hivyo, Bunge la Mheshimiwa Sitta lilikuwa hivyo, mimi nikasema twende na demokrasia hii ya wawili ambayo katika kufanya hivyo... *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Aaah.

**SPIKA:** Msiseme, aah! Ndiyo haya ninasema tuwe tunasikilizana vizuri, mimi yule yule! Mimi yule yule! Tuendelee! Hatuwezi kukubali nchi yetu ikose uwakilishi, nchi ikatekwa nyara kwa sababu fulani fulani. Kwa hiyo, mimi yule yule kwa nafasi ya Spika tutatoa nafasi ya pili, baada ya hiyo nafasi ya pili tutajua hatua itakayofuata. Niwahakikishie Watanzania kwamba hawatakosa nafasi katika Bunge hilo. *(Makofi)*

Nimewaambieni ninyi mnaomzomea Spika kwa mara nyingine sitachoka kuwaambia, tuna miezi mitatu, tutashughulika na kila mmoja ambaye anadhani kwamba yeye anajifanya hapa ana vurugu. *(Makofi)*

Sasa naanza na Mheshimiwa Halima Mdee, ambaye yeye alimtukana Spika juzi katika michezo hii mnayofanya. Watanzania wengi sana wamesikitishwa sana na jambo hili. Wameniandikia, wamenipigia simu, wamesikitishwa sana na jambo hili. Siyo utaratibu mwema, siyo utamaduni wetu Watanzania, huwa hatufiki hapo, lakini kwa vile mwenzetu amefika hapo na hii siyo mara ya kwanza kwa Mheshimiwa Halima, hata juzi nilivumilia sana yaani nilivuta nikamuomba Mungu anisaidie, nikanyamaza kimya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ndiyo maana nawaambia

mara kwa mara baadhi yenu tabia zenu na mwenendo siyo nzuri hata kidogo. Kwa hiyo, suala lake nalipeleka mara moja kwenye Kamati ya Maadili iende ikakae na kulipima. Haiwezekani Bunge hili linashughulikia kwa kuwaita watu walioko nje kwa utovu wa nidhamu halafu lifumbie macho Wabunge walioko humu ndani ambao ni watovu wa nidhamu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, anayeunga mkono mambo kama hayo lazima awe ana matatizo tu kichwani. Hatuwezi kwenda hivyo hata siku moja, hatuwezi kwenda hivyo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Halima Mdee popote pale alipo katika nchi hii, najua hayupo Dodoma, *by* saa hizi kesho, awe yeye mwenyewe amejileta hapa Bungeni, la sivyo, akamatwe na polisi popote pale alipo aletwe kwa pingu hapa Bungeni. Hatuwezi kucheza katika mambo ya msingi. Tuelewane kabisa, tumekuja mmoja mmoja hapa na tutashughulikiana mmoja mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe, pia aripoti kwenye Kamati ya Maadili, kama yuko Dodoma leo, baada ya matangazo haya Kamati ya Maadili iende kuanza kukaa *immediately* kuanza kushughulikia mambo haya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyofahamu Kamati ya Maadili ilishamuita Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam na ikazungumza naye na leo Kamati hiyo ya Maadili imemuita Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Alexander Pastory Mnyeti, ambaye pia na yeye ataitwa katika Kamati ya Maadili ambayo anatakiwa kuhudhuria leo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, narudia tena kwamba kama Spika, nitahakikisha kwamba tunaendesha mambo yetu kwa uhuru kabisa, kwa amani kabisa, kwa uwazi kabisa, lakini vitendo hivi vya utovu wa nidhamu uliopitiliza havina nafasi katika Bunge la 11. *(Makofi)*

Mwisho, namtambua pia Rais wa *TUCTA,* Ndugu yetu Tumaini Nyamhoka. Popote pale ulipo, karibu sana. *(Makofi)*

Katibu, tunaendelea.

**NDG. CHARLES MLOKA – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 - Ofisi ya Waziri Mkuu**

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, karibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa zilizowasilishwa leo katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI, zilizochambua Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge lako sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa mwaka 2016/2017 na Mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa mwaka 2017/2018.

Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha za Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zilizo chini yake pamoja na Mfuko wa Bunge kwa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/2017 Bunge lako Tukufu limeondokewa na Wabunge wenzetu, Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Dimani (CCM) na Mheshimiwa Dkt. Elly Marko Macha aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA). Pia Taifa limempoteza Mheshimiwa Samuel John Sitta, aliyekuwa Spika Mstaafu wa Bunge la Tisa la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Aidha, nchi yetu imekumbwa na majanga na maafa yaliyosababisha vifo, majeruhi na uharibifu wa mali. Ninaomba Mwenyezi Mungu awajalie nafuu na haraka wale wote waliopata majeraha na kuwapumzisha kwa amani wale waliopoteza maisha, Amina.

Mheshimiwa Spika, ninatoa pole kwa familia za wote waliopoteza ndugu na jamaa na marafiki.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii pia, kumpa pole Mheshimiwa Aida Khenani, Mbunge mwenzetu, kwa ajali mbaya iliyotokea jana mchana na kupata maumivu makali hatimaye kukimbizwa Muhimbili Hospitali. Kupitia Bunge lako, hii tena pamoja na Wabunge wote tunamuombea Mbunge mwenzetu apone na arejee kuendelea nasi kwenye shughuli zetu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar, kwa kutimiza mwaka mmoja wa uongozi wao. Sisi tunaowasaidia tunajivunia uongozi wao mahiri, uzalendo uliotukuka na dhamira njema waliyonayo kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Bunge lako Tukufu limepokea na kuwaapisha Wabunge wapya watano ambao ni Mheshimiwa Abdallah Majura Bulembo, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Juma Ali Juma, Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi na Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete.

Nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge wapya kwa heshima waliyoipata ya kujumuika nasi kwenye Bunge hili. Kama ilivyo ada tutatoa ushirikiano unaotarajiwa kwa Waheshimiwa Wabunge hawa ili watekeleze majukumu yao kwa ufanisi na tija. Kipekee ninampongeza Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi, kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii pia kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa juzi na Bunge lako Tukufu ili kuiwakilisha Tanzania katika Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki. Tunaamini kuwa Wabunge hao wateule wataipeperusha vema bendera ya Tanzania na kutetea maslahi ya Watanzania na Wanajumuiya ya Afrika

Mashariki. Vilevile kipekee naomba kupitia Bunge lako Tukufu, niwapongeze Makatibu Wakuu wapya walioteuliwa na Mheshimiwa Rais juzi tarehe 4 Aprili, 2017 akiwemo Profesa Kitila Alexander Mkumbo, kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Dkt. Leonard Akwilapo kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Bibi Maimuna Tarishi ambaye amehamishiwa katika Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Dkt. Avemaria Semakafu ambaye ameteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Nawapongeza sana wote walioteuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia, kuwashukuru Wajumbe a Kamati za Kudumu za Bunge kwa kazi kubwa ya kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara, Mikoa, Wakala, Idara za Serikali zinazojitegemea na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Ninawashukuru kipekee sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria inayoongozwa na Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji; Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni na Kamati ya Bajeti inayoongozwa na Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini, kwa kutoa mchango mkubwa wakati wa maandalizi ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, pia, niwapongeze Waheshimiwa Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kuongoza kwa umahiri mkubwa Kamati zao wakati wa kupitia makadirio ya sekta zote. Maoni na ushauri wao umesaidia sana kuboresha makadirio ya Bajeti ya Serikali kwa mafungu yote.

Mheshimiwa Spika, niruhusu pia niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu Kiongozi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Makatibu Wakuu, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Idara, Mashirika na Taasisi zote za Serikali kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa katika kutekeleza majukumu yangu.

Aidha, niwashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Serikali na Taasisi zake chini ya uongozi wa Katibu Mkuu Kiongozi kwa kukamilisha Bajeti ya Serikali ya mwaka 2017/2018. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee namshukuru Mheshimiwa Jenista Joachim Mhagama, Mbunge wa Peramiho, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu; Mheshimiwa Antony Peter Mavunde, Mbunge wa Dodoma Mjini na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana kwa ushirikiano wao mkubwa katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Aidha, ninamshukuru Mheshimiwa Dkt. Abdallah Possi, aliyekuwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kazi kubwa aliyoifanya wakati akiitumikia nafasi hiyo, ninamtakia kazi njema kwenye jukumu lake jipya la kuiwakilisha Tanzania nchini Ujerumani.

Mheshimiwa Spika, vilevile ninawashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu, chini ya uongozi wa Makatibu Wakuu Dkt. Hamisi Mwinyimvua, Bwana Erick Shitindi na aliyekuwa Katibu Mkuu Bwana Uledi Mussa, kwa ushauri wao wa kitaalam kwangu na kwa Waheshimiwa Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, ninazishukuru pia nchi marafiki, Taasisi na Mifuko ya Fedha Duniani, Mashirika ya Umma, Mashirika ya Umoja wa Mataifa, Madhehebu ya Dini na Mashirika yasiyo ya Kiserikali kwa kuunga mkono jitihada za Serikali katika kujenga uchumi wa nchi yetu. Misaada na mikopo iliyopatikana kwa wakati imechangia kutekeleza miradi ya maendeleo na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii pia kuwashukuru kwa dhati wananchi wa Jimbo la Ruangwa kwa kuendelea kuniunga mkono na kunielewa vizuri dhamana ya Kitaifa niliyonayo na kusimamia utendaji wa Serikali katika sekta zote na kuwa Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni.

Mwisho ninaishukuru familia yangu, hususan mwenza wangu mpendwa Mary na watoto wetu, kwa upendo, dua na kuendelea kunitia moyo ili nitekeleze kwa ufanisi zaidi majukumu yangu ya Kitaifa, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwelekeo wa Bajeti. Ni mwaka mmoja sasa tangu Awamu ya Tano iingie madarakani, katika kipindi hicho yako mambo mengi yaliyofanyika kwa mafanikio makubwa ambayo yataainishwa kwa kina katika bajeti za sekta, pindi Mawaziri husika watakapoziwasilisha. Baadhi ya mafanikio hayo ni utekelezaji wa ahadi ya Serikali ya elimu bila malipo, kuongezeka kwa uzalishaji na kasi ya usambazaji wa umeme vijijini, kuimarisha uwajibikaji na nidhamu katika utumishi wa umma, kuongeza ukusanyaji wa mapato na udhibiti wa matumizi ya fedha za umma, kuboresha huduma za kiuchumi na za kijamii na kutekeleza Awamu ya Kwanza ya Mpango wa Serikali Kuhamia Dodoma.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu, viongozi wa Serikali, watumishi wa umma na Watanzania wote kwa ujumla kwa kuendelea kuiunga mkono Serikali katika utekelezaji wa majukumu yake yote, kwani bila ushirikiano wao tusingeweza kupata mafanikio haya.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu imeendelea kuandaliwa na kuzingatia Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa miaka mitano, Ahadi za Mheshimiwa Rais alizotoa wakati wa kampeni pamoja na maelekezo yake wakati akizindua Bunge la Kumi na Moja la Jamhuri ya Muungamo wa Tanzania, lililofanyika tarehe 20 Novemba, 2015. Bajeti hii itaendelea kuimarisha mafanikio yaliyopatikana katika mwaka uliopita na kushughulikia utatuzi wa vikwazo vya kukuza uchumi wa haraka na baadhi ya changamoto zilizojitokeza.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali itajikita zaidi katika maeneo yatakayochangia kuimarisha uchumi wa viwanda na kuboresha huduma za jamii. Ninawaomba Waheshimiwa

Wabunge na wananchi kwa ujumla waendelee kushirikiana na Serikali katika kufikia azma hiyo ili dhamira yetu ya kuboresha maisha ya Watanzania iweze kutimia. Ni vema tukakumbuka kwamba, tuna mwaka mmoja tu wa utekelezaji wa yale tuliyoyapnga kufanya ndani ya kipindi cha miaka mitano. Tutatumia bajeti ya mwaka ujao wa fedha kukabili changamoto zilizojitokeza na ahadi ya Serikali ni kuendelea kuwatumikia wananchi kwa uadilifu na bila ubaguzi wowote huku tukitanguliza mbele maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Serikali kuhamia Dodoma; tarehe 23 Julai, 2016, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akihutubia Mkutano Mkuu Maalum wa Chama cha Mapinduzi alitangaza uamuzi wa kuhamisha rasmi shughuli za Serikali Dodoma. Kufuatia uamuzi huo mipango ya kuhamia Dodoma kwa awamu ilianza baada ya mahitaji halisi yatakayoiwezesha Serikali kuhamia Dodoma kubainishwa ikiwa ni pamoja na ofisi na nyumba za makazi kwa viongozi na watumishi wa umma. Awamu ya kwanza ilipangwa kuhamia ifikapo mwisho wa mwezi Februari, 2017.

Mheshimiwa Spika, ninafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba tayari watumishi 2,069 wakiwemo Mawaziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu na baadhi ya Wakuu wa Idara na Vitengo na Watumishi wengine wamekwishahamia Dodoma kama ilivyopangwa. Vilevile Wizara zote zimepata majengo ya ofisi yatakayotumika katika kipindi cha mpito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili Mji wa Dodoma uweze kuendelezwa kwa mpangilio mzuri, Serikali inaupitia upya mpango kabambe wa Mji wa Dodoma. Mapitio hayo yatasaidia sana kuepuka makosa yaliyofanyika katika miji mingi, hususan ujenzi holela unaochangia katika uchafuzi wa mazingira na kuharibu mandhari ya mji. Ni wazi kwamba ujenzi wa Mji wa Dodoma hautafanywa na Serikali pekee, bali tutaendelea kuhamasisha sekta binafsi na wadau wengine kuwekeza Dodoma.

Mheshimiwa Spika, nalipongeza sana Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC),* kwa kujenga nyumba 300 za makazi hapa Dodoma, ambazo watumishi wanaweza kununua au kupangishwa. Natoa wito kwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma kuongeza kasi ya upimaji wa viwanja, kuboresha miundombinu na kudhibiti ujenzi holela kwa kushirikiana kwa karibu kabisa na Manispaa ya Dodoma na taasisi nyingine za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siasa; mwaka mmoja baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, hali ya kisiasa nchini imeendelea kuwa shwari na ya kuridhisha. Aidha, chaguzi ndogo zilifanyika tarehe 22 Januri, 2017 katika Jimbo la Dimani Zanzibar na Udiwani katika Kata 20 Tanzania Bara, kwa kushirikisha wagombea kutoka vyama 15 vya siasa; ninavipongeza vyama vyote vilivyoshiriki katika uchaguzi huo. Kipekee nikipongeze Chama cha Mapinduzi kwa ushindi wa Jimbo la Dimani na viti 19 vya Udiwani katika chaguzi hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 mashauri 53 ya kupinga ushindi wa Ubunge na mashauri 194 ya kupinga ushindi wa Udiwani yalifunguliwa. Mashauri hayo yamekwishasikilizwa na hukumu kutolewa, isipokuwa shauri moja la kupinga matokeo ya Ubunge katika Jimbo la Mbagala. Ninazipongeza Ofisi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kazi kubwa waliyofanya ya kuhakikisha kuwa kesi hizo zinaendeshwa kwa kasi na kwa weledi na hivyo kuwawezesha wananchi kuendelea kupata uwakilishi.

Mheshimiwa Spika, ili kuendelea kuboresha demokrasia hapa nchini, hatuna budi kujenga jamii inayoheshimu na kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za nchi pamoja na kuwa na uvumilivu wa kisiasa. Ninatoa rai kwa wadau wa siasa kote nchini kujenga utamaduni wa masikilizano na kuendesha siasa za maendeleo badala ya siasa za malumbano, siasa za kuunganisha watu wetu badala ya kuwagawa na siasa za uwajibikaji badala ya siasa za mazoea. Serikali itaendelea kulinda na kuheshimu misingi ya

siasa zinazolenga kuleta ustawi wa wananchi na zinazotanguliza maslahi ya nchi na wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la Muungano; Serikali inaendelea kudumisha Muungano wetu ambao ni tunu na mfano wa kuigwa Barani Afrika na dunia nzima. Wananchi wanaendelea kunufaika na matunda ya Muungano wetu ambao ni imara na thabiti. Serikali zote mbili zinafanya mashauriano kupitia Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kushughulikia masuala ya Muungano chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile viongozi na watendaji wa sekta nyingine zisizo za Muungano wamekuwa wakikutana mara kwa mara ili kubadilishana uzoefu na kubaini maeneo ya ushirikiano kwa ustawi wa wananchi wa pande zote mbili. Jumla ya vikao 13 vya sekta ambazo siyo za Muungano vilifanyika kati ya Julai, 2016 na Machi, 2017. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kutumia fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais kwa kuendesha kwa ufanisi mkubwa kikao kilichofanyika tarehe 13 Januari, 2017 ambapo taarifa kuhusu hoja zilizopatiwa ufumbuzi, maagizo na maelekezo ya kufuatilia utekelezaji wa changamoto zilizobaki ilishatolewa. Serikali itaendelea kuulinda na kuuenzi Muungano wetu kwa manufaa ya wananchi wa pande zote mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali ya uchumi; mwenendo wa viashiria vya ukuaji wa uchumi wa nchi yetu kwa mwaka 2016/2017 vinaonesha kuwa uchumi wetu unakua na kuimarika. Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu, ukuaji halisi wa Pato la Taifa ulifikia asilimia 7.0 mwaka 2016. Sekta zilizochangia kwa kiwango kikubwa kwenye ukuaji huo ni uchimbaji madini na mawe, usafirishaji na uhifadhi wa mizigo, habari na mawasiliano, pamoja na shughuli za fedha na bima.

Mheshimiwa Spika, aidha, mfumuko wa Bei uliendelea kubakia katika wigo wa tarakimu moja na kasi ya upandaji bei ilipungua kutoka wastani wa asimilia 5.6 mwaka 2015 hadi asilimia 5.2 mwaka 2016. Kwa upande mwingine, tathmini ya hali ya taasisi za fedha inaonesha kuwa benki zetu ziko salama na zina mitaji na ukwasi wa kutosha. Aidha, taarifa za mashirika mbalimbali ya Kimataifa zinaonesha kwamba katika mwaka 2016 uchumi wa Taifa letu ulikua vizuri na hivyo kutufanya kuwa miongoni mwa nchi sita za Bara la Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara ambazo uchumi wake unakua kwa kasi kubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tano imeweka juhudi kubwa katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Kutokana na juhudi hizo, makusanyo ya ndani kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* yaliongezeka kutoka wastani wa shilingi bilioni 850 kwa mwezi hadi shilingi trilioni 1.2 kwa mwezi. Pamoja na kuongeza ukusanyaji kwa mapato, juhudi kubwa zimefanyika kudhibiti matumizi ya rasilimali za umma ikiwa ni pamoja na kuziba mianya ya rushwa, ubadhirifu, wizi na upotevu wa fedha za umma. Mwenendo huo umeiwezesha Serikali kuanza utekelezaji wa miradi mikubwa kwa fedha za ndani na pia utoaji huduma kwa wananchi. Serikali itaendelea kupanua wigo wa vyanzo vya mapato ya ndani na kuongeza kasi ya ukusanyaji mapato ili kila anayestahili kulipa kodi aweze kuilipa.

Mheshimiwa Spika, kuimarisha kwa viashiria vya uchumi wa nchi yetu katika kipindi cha mwaka mmoja tangu Serikali ya Awamu ya Tano iingie madarakani ni dalili njema katika kujenga uchumi imara na tulivu utakaotusaidia kuelekea katika uchumi wa viwanda na kufikia nchi ya kipato cha kati ifikapo mwaka 2020 - 2025. Serikali itaongeza juhudi katika kuchochea ukuaji wa sekta za kipaumbele zenye fursa kubwa ya kukuza uchumi kwa haraka na kuondoa umaskini kama vile kilimo na viwanda.

Mheshimiwa Spika, pia itahakikisha kwamba sekta wezeshi kama vile nishati, habari na mawasiliano, fedha na ujenzi wa miundombinu muhimu ya barabara, bandari, reli,

vivuko na viwanja vya ndege zinaimarishwa. Vilevile Serikali itaendelea kuhimiza utekelezaji thabiti wa miradi ya maendeleo na kuweka mazingira mazuri ya kufanya biashara na kuvutia uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuwezesha wananchi kupitia mipango na programu mbalimbali kwa kuelekeza nguvu zaidi kwa makundi ya wanawake, vijana na wenye ulemavu. Serikali imeweka mazingira bora kwa vikundi vya kiuchumi na vijana kujiunga na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, *SACCOS* na *VICOBA.* Aidha, Serikali imeanzisha majukwaa ya uwezeshaji wa wanawake kiuchumi katika mikoa yote na kufanya mapitio ya miongozo wa Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake wa mwaka 2007. Mapitio hayo yana lengo la kuboresha uendeshaji na usimamizi wa mfuko huo ili kuwezesha wanawake wengi zaidi kukopesheka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunatambua kwamba asilimia 56 ya nguvu kazi ya Taifa ni vijana. Hivyo, Serikali inatekeleza Programu ya Kukuza Ujuzi na Stadi za Kazi ili kuwawezesha vijana kushiriki katika ujenzi wa uchumi wa viwanda pamoja na kuinua ari ya vijana kupenda kufanya kazi. Katika mwaka 2016/2017, Serikali inatoa mafunzo kwa vijana 9,120 katika fani mbalimbali zikiwemo stadi za kushona nguo, kutengeneza bidhaa za ngozi, mafunzo ya kurasimisha ujuzi uliopatikana kwa mfumo usio rasmi na mafunzo ya kukuza ujuzi na stadi za kujiajiri katika fani mbalimbali. Jumla ya vijana 1,469 wamehitimu mafunzo hayo na kupata ajira.

Mheshimiwa Spika, vijana 7,651 waliobaki wanaendelea kupata mafunzo kupitia viwanda vya *Tooku Garments, Mazava Fabrics,* Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam *(DIT), VETA* na *Don Bosco.* Katika mwaka 2017/2018, Serikali itatoa mafunzo ya kukuza ujuzi wa kujiajiri na stadi za kazi kwa vijana 15,350 katika fani mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, imetoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 1.5 kwa vikundi vya vijana 297 katika

Halmashauri mbalimbali nchini. Aidha, Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia mapato yake ya ndani zimetoa shilingi bilioni 4.6 ikiwa ni mikopo yenye masharti nafuu kwa vikundi vya vijana 2,356. Hatua hizi zimekwenda sanjari na utengaji wa maeneo maalum yenye jumla ya ekari 85,603 kwa ajili ya shughuli za vijana za kilimo, biashara ndogo ndogo, burudani na michezo. Katika mwaka 2017/2018, Serikali itaendelea kusimamia Halmashauri zote nchini kutenga asilimia tano ya mapato yao kwa ajili ya vijana na asilimia tano kwa wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ajira na mahusiano mahali pa kazi; Serikali imeendelea kuratibu utekelezaji wa juhudi za kukuza ajira nchini kama inavyoelekezwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015. Hadi kufikia Machi 2017, jumla ya ajira 418,501 zimezalishwa nchini. Kati ya ajira hizo, ajira 239,017 sawa na asilimia 57 zimezalishwa katika sekta binafsi wakati ajira 179,484 sawa na asilimia 43 zimezalishwa kutokana na shughuli za sekta ya umma ikiwemo miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya utafiti na kubaini kuwa asilimia 58 ya migogoro ya kikazi inatokana na kutozingatiwa kwa taratibu za kuainisha kuachisha kazi. Sekta zinazoongoza kwa migogoro ya kazi ni usafirishaji, ujenzi, ulinzi binafsi, elimu, huduma za hoteli na viwanda. Katika kupunguza migogoro mahali pa kazi, Serikali imefanya kaguzi na kusimamia uundwaji wa Mabaraza ya Wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, aidha, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi imeendelea kutimiza wajibu wake wa kusuluhisha migogoro ambapo katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Februari, 2017, Tume imesajili jumla ya migogoro 8,832 kati ya hiyo migogoro 3,319 sawa na asilimia 37.6 ya migogoro yote iliyosajiliwa imesuluhishwa. Kati ya migogoro hiyo iliyosuluhishwa, migogoro 1,957 ilifikia suluhu na migogoro 1,362 haikufikia suluhu.

Aidha, migogoro 5,513 inaendelea kusuluhishwa katika hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ninatoa wito kwa waajiri na waajiriwa wote nchini, kuzingatia sheria za kazi na kuimarisha uhusiano mzuri kwenye maeneo ya kazi ili muda mwingi zaidi utumike kwenye uzalishaji mali badala ya kutatua migogoro. Vilevile ni muhimu sana kuimarisha kaguzi za kazi na kuendelea kusaini mikataba ya kuunda na kusajili mabaraza ya wafanyakazi ili kuimarisha zaidi mahusiano mahali pa kazi.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya kisekta; sekta ya uzalishaji - viwanda; ili kujenga uchumi wa viwanda Serikali inahamasisha wawekezaji wa ndani na nje kujenga viwanda vidogo, vya kati na vikubwa. Viwanda vinavyopewa kipaumbele ni vile vinavyotumia malighafi zinazopatikana hapa nchini, vinavyotoa ajira kwa watu wengi na vinavyozalisha bidhaa zenye soko hapa nchini na nje ya nchi. Katika kuhakikisha Watanzania wanashiriki kikamilifu kwenye uchumi wa viwanda, Serikali itahamasisha zaidi sekta binafsi ya hapa nchini pamoja na mashirika ya umma kujenga viwanda.

Mheshimiwa Spika, jitihada hizo zimewezesha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya *NSSF, PPF, LAPF, GEPF, PSPF* na *NHIF* kuanza kufufua, kuendeleza na kujenga viwanda vipya vipatavyo 27 katika maeneo mbalimbali nchini. Natoa pongezi kwa Bodi na Menejimenti ya mifuko hiyo kwa kuunga mkono jitihada za Serikali katika ujenzi wa viwanda nchini. Aidha, ninaendelea kuyasisitiza mashirika ya umma kuhakikisha kwamba mipango yao inaendana na utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa ambao dhima yake ni kujenga uchumi wa viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sekta ya maliasili na utalii; sekta ya utalii ni moja kati ya sekta muhimu sana katika uchumi wa nchi yetu. Kote ulimwenguni, mafanikio ya sekta ya utalii kwa kiasi kikubwa hutegemea miundombinu thabiti ya utalii, huduma bora na ulinzi na usalama. Ili kuendelea kunufaika na sekta hiyo, Serikali inaboresha miundombinu ya utalii, kupanua wigo wa vivutio vipya vya utalii na kuimarisha huduma ya usafiri wa anga. Vilevile Serikali inafanya juhudi kubwa za kudhibiti ujangili na biashara haramu ya

wanyamapori ambapo watuhumiwa 897 walitiwa mbaroni na kati yao watuhumiwa 282 wamefikishwa mahakamani.

Mheshimiwa Spika, idadi ya watalii imeongezeka kutoka 1,137,182 kwa mwaka 2015 hadi watalii 1,284,279 mwaka 2016 sawa na ongezeko la asilimia 12 na kuliingizia Taifa Dola za Marekani bilioni mbili. Juhudi zilizoanza za kuliimarisha shirika letu la ndege zinalenga pia kutoa mchango mkubwa kwenye sekta ya utalii kwa kusafirisha watalii wa ndani na kutoka nje ya nchi. Shabaha yetu ni kuongeza idadi ya watalii wanaokuja kutembelea nchi yetu na pia mapato yatokanayo na sekta hiyo.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuisihi sekta binafsi kuwekeza zaidi kwenye miundombinu muhimu ya sekta hii zikiwemo hoteli, kuboresha huduma na kubuni mbinu mpya za kuvutia watalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sekta ya kilimo; uzalishaji wa mazao ya chakula kwa msimu wa mwaka 2015/2016 ikijumuisha mazao ya nafaka na yasiyo ya nafaka ulifikia tani 16,172,841 ikilinganishwa na mahitaji ya kitaifa ya tani 13,159,326. Hivyo, katika kipindi hicho nchi ilikuwa na zaidi ya tani 3,013,515 za chakula. Katika msimu wa kilimo wa mwaka 2016/2017 hali ya upatikanaji wa mvua katika mikoa inayopata mvua za vuli haikuwa ya kuridhisha na hivyo kusababisha ukame na upungufu wa mavuno katika baadhi ya maeneo. Tathmini ya awali imebainisha kwamba Halmashauri 55 zimeathirika na ukame.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na hali hiyo, Serikali inaendelea kuhamasisha sekta binafsi kununua mazao ya chakula kutoka katika maeneo yenye ziada na kuyauza katika maeneo yenye uhaba.

Aidha, wafanyabiashara waliokuwa wamehifadhi nafaka katika maghala, walitakiwa kuzisambaza katika masoko ya ndani. Vilevile Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya walielekezwa kuwahamasisha na kuwaelekeza wakulima kupanda mbegu bora za mazao ya kilimo kufuatia

mvua zinazoendelea yanayostahamili ukame na yanayokomaa kwa muda mfupi kwa kipindi hiki cha masika.

Mheshimiwa Spika, ili kutoa msukumo katika kazi hiyo, kiasi cha tani 1,969 za mbegu bora za mazao yanayostahimili ukame zilinunuliwa na Serikali na kusambazwa katika Halmashauri zilizobainika kuathirika na ukame. Pia wakulima wanaendelea kuhamasishwa kuzitumia vizuri mvua zinazoendelea kunyesha katika msimu huu wa masika kwa kupanda mazao hayo ambayo nimeyatamka yanayostahimili ukame na yanayokomaa mapema.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa sekta ya kilimo katika uchumi wetu, Serikali imeweka dhamira ya kuongeza uzalishaji, tija na kukifanya kilimo kiwe cha kibiashara. Katika mwaka 2016/2017, Serikali ilifanikisha kupatikana kwa tani 277,937 za mbolea na tani 23,333 za mbegu bora.

Aidha, hadi Februari 2017, Serikali ilitoa tani 30,773 za mbolea ya ruzuku ya kukuzia na kupandia kupitia vituo vya mauzo ya mbolea vya Kampuni ya Mbolea Tanzania *(TFC).*

Mheshimiwa Spika, moja ya ahadi ya Serikali kwa wakulima wetu ni kupunguza kodi, tozo na ada mbalimbali zinazochangia kupunguza faida kwa wakulima.

Katika mwaka 2016/2017 Serikali ilifuta baadhi ya tozo za mazao ambazo ni kero kwa wakulima katika mazao ya pamba, chai na kahawa. Tozo zilizofutwa kwenye zao la pamba ni mchango wa mwenge wa shilingi 450,000 unaotolewa na kila kiwanda cha kuchambua pamba na ada ya vikao vya Halmashauri za Wilaya ambayo ni shilingi 250,000. Kwa zao la chai, kodi ya moto na uokoaji imeondolewa na katika zao la kahawa, ada ya leseni ya kusindika kahawa ya dola za Marekani 250 nayo pia imefutwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imeboresha mfumo wa stakabadhi za mazao ghalani kwa kuanzisha utaratibu wa wazi wa ununuzi wa mazao kupitia minada. Mathalani, katika msimu wa 2016/2017 kwenye zao la korosho, utaratibu huo umechangia kwa kiasi kikubwa kuongezeka kwa bei ya korosho kwa kilo kutoka shilingi 1,200 hadi shilingi 3,800, bei ambayo haijawahi kufikiwa katika historia ya zao la korosho nchini.

Aidha, mfumo wa stakabadhi za mazao ghalani na utaratibu wa minada umeongeza ushindani na kuvutia wafanyabiashara wa ndani na nje ya nchi hususan nchi ya Vietnam na nchi nyingine kuja wenyewe kununua korosho badala ya kutegemea soko la India pekee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/2018, Serikali itaendelea na uchambuzi wa kina wa kodi, tozo na ada zilizobaki katika sekta za kilimo, mifugo na uvuvi kwa lengo la kuziondoa au kuzipunguza ili kumwezesha mkulima kunufaika zaidi ya jasho lake na kuongeza mapato ya Halmashauri zetu. Kwa sasa, tunashughulikia zao la tumbaku kwa kupitia tozo zake na lakini pia kubaini ubadhirifu unaoendelea kwenye ushirika huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mifugo; Serikali imeongeza uzalishaji wa mitamba na uhamilishaji wa mifugo ili kuhamasisha ufugaji wa kisasa na wenye tija. Mitamba 546 imezalishwa kutoka mashamba ya Serikali na mitamba 88 kutoka *NARCO* na kusambazwa kwa wafugaji wadogo.

Aidha, Kituo cha Taifa cha Uhamilishaji – *NAIC* Usa *River* Arusha kimeimarishwa na kuongeza uzalishaji wa mbegu bora za ng'ombe hadi kufikia dozi 10,494 ikilinganishwa na dozi 8,000 zilizozalishwa na kusambazwa katika mwaka 2015/2016. Pia, ng'ombe waliohamilishwa wameongezeka kutoka 221,390 mwaka 2015/2016 hadi ng'ombe 457,557 mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2017/2018, Serikali itaendelea kuimarisha Kituo chetu cha Kuzalisha Mitamba cha Kitulo, Wilayani Makete ili kukiongezea uwezo wake. Aidha, Serikali inatoa nafasi kwa mashamba binafsi kuzalisha mitamba zaidi kama mashamba ya *ASAS* kule Iringa ili wafugaji wadogo wanufaike nayo.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia itaendelea na zoezi la kutenga, kupima na kumilikisha wafugaji maeneo ya ufugaji na kujenga miundombinu ya mifugo kwa kuongeza idadi ya malambo na mabwawa katika Mikoa. Hatua hizo zitasaidia kupunguza uzururaji wa mifugo na migogoro baina ya wafugaji na wakulima na hifadhi za misitu pia.

Mheshimiwa Spika, sekta ya madini ni muhimu kwa uchumi wetu. Serikali imetenga maeneo zaidi kwa ajili ya wachimbaji wadogo, kuweka utaratibu mzuri zaidi wa kutoa ruzuku pamoja na kuimarisha shughuli za ugani.

Katika kipindi cha mwezi Julai, 2016 hadi Februari, 2017, Serikali imetenga maeneo 11 yenye ukubwa wa hekta 38,567 kwa ajili ya wachimbaji madini wadogo. Maeneo hayo ni Msasa na Matabe Mkoani Geita, Biharamulo na Kyerwa Mkoani Kagera, Itigi Mkoani Singida, D-Reef, Ibindi na Kapanda Mkoani Katavi, Ngapa Mkoani Ruvuma, Kitowelo na Namungo Mkoani Lindi pamoja na Nzega Mkoani Tabora.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/2018, Serikali itaimarisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali yatokanayo na rasilimali za madini na kuimarisha ukaguzi wa shughuli za uzalishaji na biashara ya madini kwa migodi mikubwa, ya kati na midogo. Aidha, Serikali itaendeleza wachimbaji wadogo na wa kati wa madini pamoja na kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani wa madini hayo.

Mheshimiwa Spika, Huduma za Kiuchumi, naanza na Sekta ya Ardhi. Katika mwaka 2016/2017, Serikali iliahidi kuanza ujenzi wa mfumo unganishi wa kuhifadhi kumbukumbu za ardhi na ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kazi ya ujenzi wa mfumo huo awamu ya kwanza ilizinduliwa rasmi mwezi Agosti mwaka 2016 na mkandarasi tayari ameanza kazi. Sambamba na zoezi hilo, Serikali inakamilisha ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Taarifa za Ardhi. Kukamilika kwa mradi huo kutaboresha utendaji kazi, kutaharakisha huduma za utoaji hati miliki, kuongeza pia mapato ya Serikali na kuboresha utunzaji wa kumbukumbu za ardhi ambapo nyaraka zote za ardhi zitakuwa katika mfumo unganishi wa kielektroniki.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia iliidhinisha ramani za upimaji zenye jumla ya viwanja 78,771 na mashamba 239. Aidha, Serikali imekamilisha upimaji na upigaji picha wa picha za anga za Jiji la Dar es Salaam na inaendelea kutatua migogoro ya matumizi ya ardhi baina ya wakulima, wafugaji na hifadhi katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/2018, Serikali itaendelea kujenga mfumo unganishi wa kuhifadhi kumbukumbu za ardhi na kuboresha usimamizi wa sekta ya ardhi kwa kufanya mapitio ya sera na sheria za ardhi na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu sera, sheria, kanuni na miongozo ya ardhi ili kudhibiti viashiria vya migogoro ya matumizi ya ardhi nchini. Ninatoa wito kwa halmashauri zote nchini kuhakikisha kwamba zinashughulikia migogoro ya ardhi mapema na kuweka mazingira wezeshi ya upimaji wa ardhi katika halmashauri zao.

Mheshimiwa Spika, sekta ya umeme; Serikali imechukua hatua thabiti za kuongeza uzalishaji wa umeme, lakini pia kuimarisha miundombinu ya usafirishaji na kuongeza kasi ya usambazaji umeme. Katika mwaka 2016 umeme uliozalishwa na kuingizwa katika Gridi ya Taifa uliongezeka na kufikia *gigawatt hours* 7,092 ikilinganishwa na *gigawatt hours 6,227* zilizozalishwa mwaka 2015 sawa na ongezeko la asilimia 13.9. Vilevile Serikali imepanua na kuboresha njia ya

usafirishaji umeme kwa kukamilisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 400 na upanuzi wa vivutio vya kupooza umeme kutoka Iringa – Dodoma – Singida hadi Shinyanga. Lakini Serikali imeendelea pia kutekeleza miradi ya kusambaza umeme vijijini kote kupitia Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* katika mikoa yote ya Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2016/2017, wakala ulikamilisha ujenzi wa vituo sita vya kuongeza nguvu ya umeme kutoka msongo kilovoti 11 hadi kilovoti 33 katika Miji ya Kigoma, Kasulu, Kibondo, Ngara, Mbinga na Tunduru. Ujenzi wa njia za kusambaza umeme zenye urefu wa kilometa 17,740 za msongo wa kilovoti 33 na ujenzi wa vituo vidogo vya kupoza na kusambaza umeme 4,100 na ujenzi wa njia ndogo ya usambazaji umeme wenye urefu wa kilometa 10,970.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali itaongeza uzalishaji, kuboresha miundombinu ya usafirishaji na kuongeza kasi ya usambazaji wa umeme nchini. Aidha, Serikali itaendelea na utekelezaji wa mradi mkubwa wa ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Kabale, Uganda hadi Tanga, Tanzania. Serikali pia itawezesha uwekaji wa mtandao wa usambazaji wa gesi asilia kwenye viwanda na matumizi ya majumbani pamoja na uendelezaji wa mradi wa kusindika gesi asilia *(LNG)* Mkoani Lindi.

Mheshimiwa Spika, Barabara. Kuanzia mwezi Julai, 2016 hadi Februari, 2017, Serikali imejenga na kukarabati jumla ya kilometa 430 za barabara kuu sawa na asilimia 62 ya lengo la kilometa 692. Aidha, ujenzi wa barabara za juu kwenye makutano ya *TAZARA* unaendelea vizuri pamoja na maandalizi ya kuitisha zabuni za ujenzi wa Daraja jipya la Salander na ujenzi wa Barabara ya Dar es Salaam – Chalinze kwa kiwango cha *express way.*

Vilevile ujenzi wa barabara ya juu *(interchange)* kwenye makutano ya barabara ya Ubungo ulizinduliwa rasmi tarehe 20 Machi, 2017. Hizi ni hatua muhimu sana za kukabiliana na changamoto ya muda mrefu ya msongamano

wa magari katika Jiji la Dar es Salaam ikiwa ni utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vivuko na Usafiri Majini. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali ilipanga kujenga Kivuko kipya cha Pangani *(MV Pangani)* na kukarabati kile cha Magogoni, Kigamboni. Napenda pia kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba hadi kufikia Februari, 2017, ujenzi na ukarabati wa vivuko hivyo ulikuwa umekamilika. Aidha, ununuzi wa boti ndogo za abiria kwa ajili ya vivuko vya Kilambo - Namoto Mkoani Mtwara, Mkongo - Utete Pwani, Pangani - Bweni Tanga na Msemo - Msangamkuu Mtwara utakamilika katika mwaka huu wa fedha. Kwa upande wa huduma za usafiri kwenye maziwa, Serikali inaendelea na ujenzi wa meli moja katika Ziwa Victoria, meli mbili Ziwa Nyasa zitakazofanya safari kati ya Kyela - Mbambabay na baadaye nchini Malawi, pamoja na ukarabati wa meli za *MV Victoria* na Butiama kwa Ziwa Victoria na *MV Liemba* - Ziwa Tanganyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sekta ya bandari; Serikali inatekeleza Mpango wa Uboreshaji wa Bandari Nchini kwa kufanya upanuzi na kuimarisha miundombinu ya Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara. Mifumo ya ulinzi katika bandari hizo imeimarishwa na mashine za kisasa za kukagua mizigo zimefungwa. Kutokana na jitihada hizo tumeanza kuona mwelekeo mzuri wa kuimarika ufanisi wa kiutendaji hususan katika Bandari ya Dar es Salaam. Tutaendelea kufanya maboresho zaidi ili Bandari ya Dar es Salaam iweze kuwa chaguo namba moja katika usafirishaji wa mizigo ndani na nje ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, reli; katika mwaka 2016/2017 Serikali iliendelea kutekeleza miradi ya uboreshaji wa miundombinu ya reli ya kati ili kuongeza uwezo wa reli hiyo katika kutoa huduma za uchukuzi nchini na nchi jirani zinazotumia bandari zetu. Awamu ya kwanza ya ujenzi wa reli mpya ya Kati kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza kwa kiwango cha *standard gauge* imeanza kutekelezwa kwa kusaini mkataba wa ujenzi wa kipande cha reli ya Dar es Salaam – Morogoro (kilometa 205). Taratibu za kuwapata

wakandarasi wa ujenzi wa reli kutoka Morogoro - Makutupora (kilometa 336), Makutupora - Tabora (294), Tabora – Isaka (kilometa 133) na Isaka – Mwanza (kilometa 254) zinaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, usafiri wa anga; katika mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali imetekeleza kwa dhati azma ya kuimarisha Kampuni ya Ndege ya Tanzania *(ATCL).* Katika kipindi hicho, ndege mbili aina ya *Dash 8 Q400* zenye uwezo wa kubeba abiria 76 kila moja zilinunuliwa na kuanza kutoa huduma mwezi Oktoba, mwaka 2016. Aidha, mwishoni mwa mwaka 2016, Serikali iliingia mkataba wa ununuzi wa ndege nyingine nne, kati ya hizo, ndege moja aina ya *Dash 8 Q400* yenye uwezo wa kubeba abiria 76 inatarajiwa kuwasili mwezi Julai, 2017. Ndege nyingine mbili aina ya *CS300* zenye uwezo wa kubeba abiria 127 kila moja zinatarajiwa kuwasili mwezi Juni, 2018 na ndege moja kubwa ya masafa marefu aina ya *Boeing 787 Dreamliner* yenye uwezowa kubeba abiria 262 inatarajiwa kuwasili mwezi Julai, 2018. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kukamilika kwa ununuzi wa ndege hizi kutasaidia sana shirika letu kuongeza safari za ndani na nje ya nchi na hivyo kuchangia katika jitihada za kuongeza watalii wanaokuja nchini kutembelea vivutio vyetu na kuimarisha usafiri wa anga hapa nchini. Aidha, *ATCL* imeanzisha safari za kuja Dodoma na hivyo kuongeza uhakika wa usafiri wakati huu ambapo Serikali inahamia Mkoani Dodoma. Wigo wa upanuzi wa usafiri wa anga kwa mikoa yote unaendelea na sasa tunakamilisha kuimarisha ujenzi wa viwanja vya ndege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mawasiliano; katika mwaka 2016/2017 baadhi ya kazi zilizofanyika kwenye sekta ya mawasiliano ni pamoja na kuendelea na ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, kutekeleza mradi wa anuai ya makazi na posti kadi na kuanzisha huduma ya Kituo cha *Jamii Center* kitakachorahisisha utoaji wa huduma muhimu katika kituo kimoja. Huduma hizo ni kulipa pensheni, ankara na huduma za benki. Aidha, sekta ya mawasiliano inatekeleza programu ya minundombinu ya kikanda ambayo inahusisha

mradi wa shule mtandao *(e–school),* mradi wa *video conference* ambao unahusisha ununuzi, usimikaji na ufungaji wa vifaa vya TEHAMA kama kompyuta katika mikoa 26 na taasisi za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia inatekeleza mradi wa ujenzi wa miundombinu ya mawasiliano vijijini kwa kushirikiana na Kampuni ya Viettel ya Vietnam. Mradi huu unatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu kutoka mwaka 2015 hadi mpaka mwaka huu wa 2017. Viettel wamekwishafikisha miundombinu ya mtandao wa *internet* kwenye shule 417 mpaka sasa, ofisi za Halmashauri za Wilaya 123, Hospitali za Wilaya 74, Vituo vya Polisi vya Wilaya 131 na Ofisi za Posta 68.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha ujenzi wa kituo cha kuhifadhi taarifa na mifumo ya Serikali *(Government Data Center).* Lengo ni kuongeza na kuimarisha usalama wa mfumo wa taarifa na taarifa unaendelea sambamba na uhakika wa upatikanaji wa taarifa za Serikali katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku. Pamoja na ujenzi wa vituo hivyo, matumizi ya TEHAMA yameongezeka na hivyo kuziwezesha taasisi za Serikali kutoa mchango mkubwa kwenye uboreshaji na utoaji huduma, kuongeza mapato na kuokoa gharama mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, sekta ya huduma za jamii, elimu. Serikali imeendelea kujenga uwezo wa walimu wa shule za msingi kwa kuwapa mafunzo hasa katika ufundishaji wa stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu (KKK). Jumla ya walimu 22,994 wa shule za msingi na walimu 519 wanaofundisha elimu maalum kwa wanafunzi wasioona na wenye ulemavu wa kusikia wamepewa mafunzo hayo. Lengo ni kuhakikisha kwamba kila mwanafunzi anayemaliza darasa la saba anajua kusoma na kuandika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/2017, Serikali iliendelea na mpango wa kutoa elimu msingi bila malipo. Tangu utekelezaji wa mpango huo uanze Serikali imekuwa ikipeleka wastani wa shilingi bilioni 18.77 kila mwezi ambapo

shule za msingi 16,088 na shule za sekondari 3,602 zimenufaika na mpango huu.

Mheshimiwa Spika, mpango huu umeleta manufaa kwa Watanzania wengi wa kipato cha chini na cha kati na wameongeza uandikishaji wa wanafunzi kwenye shule za msingi na sekondari pia. Kufuatia ongezeko hilo tulijikuta tukilazimika kupambana na upungufu wa madawati, jambo ambalo liliifanya Serikali ianzishe kampeni maalum ya kumtoa sakafuni mtoto wa Kitanzania. Hivi sasa madawati si tatizo tena kwa shule nyingi nchini, na nitumie nafasi hii kutoa pongezi kwa Watanzania wote walioshirikiana na Serikali katika kutatua changamoto za upungufu wa madawati. Nitumie nafasi hii pia kuwapongeza na kuwashukuru taasisi binafisi, watu binafsi, lakini pia Waheshimiwa Wabunge nanyi mmechangia sana katika kuondoa changamoto ya upungufu wa madawati, tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uchumi wa viwanda kwa kiasi kikubwa unahitaji rasilimali watu yenye weledi, hasa katika masomo ya hisabati na sayansi. Kama zilivyo nchi nyingine Barani Afrika, Tanzania inakabiliwa na changamoto ya wanafunzi kutopenda kusoma masomo ya hisabati na sayansi na hivyo kuchangia katika ufaulu duni kwenye masomo hayo. Ni dhahiri kuwa watoto wetu wasipoweka bidii katika masomo ya hisabati na sayansi, viwanda vyetu vitalazimika kutegemea wataalam kutoka nje ya nchi, jambo litakalowafanya Watanzania kuwa watazamaji.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali imefanya juhudi za kuwahamasisha wanafunzi kupenda masomo ya sayansi katika ngazi zote za shule. Aidha, Serikali inaendelea na mpango wa ujenzi wa maabara katika shule za sekondari na vyuo vikuu pamoja na ununuzi wa vifaa. Katika mwaka 2016/2017 Serikali imenunua vifaa vya maabara kwa ajili ya shule 1,625 za sekondari zilizokamilisha ujenzi wa maabara na usambazaji wa vifaa umeanza mwezi Machi, 2017 katika Mkoa wa Dar es Salaam, na kazi hiyo inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Aprili mwaka 2017, kwa nchi nzima.

Aidha, Serikali inatoa mafunzo kwa walimu 5,920 wanaosoma Shahada Maalum ya Sayansi, Hisabati na TEHAMA.

Mheshimiwa Spika, Serikali inakusudia kuimarisha ufundishaji wa masomo ya TEHAMA kwa shule za sekondari. Serikali inaendelea na mpango wake wa kujenga maabara za kompyuta ili wanafunzi wawe na uelewa wa TEHAMA, utekelezaji wake utafanyika hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imetoa vibali vya ajira kwa walimu wa hisabati na sayansi 4,129. Natoa wito kwa wazazi wenzangu kuhamasisha watoto wetu kupenda masomo ya hisabati na sayansi. Naagiza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia wakishirikiana na TAMISEMI na wadau wengine, kuandaa mkakati maalum wa kuhamasisha na kuwavutia wanafunzi kusoma masomo ya hisabati na sayansi. Mkakati huo pia uwezeshe upatikanaji wa walimu watakaofundisha masomo ya hisabati na sayansi katika shule za msingi na sekondari kwa kipindi kifupi bila kuathiri ubora wa ufundishaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea na ukarabati wa ujenzi wa miundombinu katika Chuo Kikuu cha Mzumbe, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya, Chuo Kikuu Kishiriki cha Mkwawa na Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam. Ujenzi wa majengo 20 ya mabweni ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 3,840 umekamilika. Vilevile Serikali inaimarisha miundombinu katika Vyuo vya Ufundi vya Taasisi na Teknolojia Dar es Salaam, Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya na Chuo cha Ufundi Arusha kwa lengo la kuimarisha mafunzo ya ufundi wa sayansi nchini. Katika mwaka 2017/2018, Serikali itaimarisha vyuo vya elimu ya juu ili kuwezesha upatikanaji wa wataalam mahiri katika nyanja mbalimbali hususan sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Spika, sekta ya maji; Serikali inatambua umuhimu wa kusogeza huduma za maji karibu zaidi na wananchi ili wasitumie muda mwingi kutafuta maji, badala yake wajikite katika shughuli za uzalishaji mali. Ili kutimiza

azma hiyo Serikali inatekeleza miradi mbalimbali ya maji mijini na vijijini ikiwemo miradi ya vijiji 10 chini ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji. Kati ya mwezi Julai na Desemba mwaka 2016, miradi 90 ya maji vijijini ilikamilika na kufanya idadi ya miradi iliyokamilika kufikia 1,301 kati ya miradi 1,810 iliyolengwa. Miradi 509 iliyobaki ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji na yote inatarajiwa kukamilika kabla ya mwezi Juni, 2017.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutekeleza miradi ya maji vijijini katika halmashauri zote nchini ikiwemo Mradi wa Maji wa Same - Mwanga - Korogwe unaoendelea kuhudumia wananchi zaidi ya 456,000 katika vijiji 38 kwenye Miji ya Same, Mwanga na Korogwe Vijijini. Ili utoaji wa huduma ya maji uwe endelevu, wananchi waendelee kuelimishwa kuhusu umuhimu wa kutunza vyanzo vya maji, uvunaji wa maji ya mvua na matumizi bora ya maji. Nitumie fursa hii kuwakumbusha watendaji katika halmashauri zote nchini kusimamia kikamilifu sheria inayokataza shughuli za kibinadamu katika vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, sekta ya afya. Serikali imeendelea kuhamasisha wananchi kujikinga dhidi ya magonjwa ikiwemo kuhimiza lishe bora. Aidha, Serikali inaboresha upatikanaji wa huduma za afya nchini kwa kujenga vituo vya kutolea huduma za afya na tiba pamoja na kuboresha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba. Bajeti ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba imeongezeka kutoka shilingi bilioni 31 mwaka 2015/2016 hadi shilingi bilioni 251 mwaka 2016/2017. Vilevile Serikali imeanzisha taratibu za kununua dawa na vifaa tiba moja kwa moja kutoka kwa wazalishaji kwa lengo la kupunguza gharama. Serikali pia imeanzisha maduka ya dawa yanayouza bidhaa zake kwa bei nafuu kwa wananchi katika hospitali za mikoa, ambapo hadi sasa maduka nane yameshaanzishwa na ujenzi wa maduka mengine katika mikoa iliyobaki inaendelea.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia inaimarisha huduma za afya ya uzazi na mtoto nchini kwa kutengeneza mpango mkakati wa kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na vifo

vya watoto wa mwaka 2016 - 2020. Lengo ni kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2020 asilimia 50 ya vituo vya afya nchini vinakuwa na uwezo wa kutoa huduma za dharura kwa matatizo ya uzazi ikiwemo upasuaji na huduma za watoto wachanga. Hadi sasa vituo vya afya 159 vinatoa huduma za upasuaji ambapo vituo 106 ni vya Serikali. Vilevile Serikali imeimarisha utoaji wa huduma za kinga na hivyo kuchangia kutokomezwa kwa ugonjwa wa Polio hapa nchini na hatimaye nchi yetu kuwa miongoni mwa nchi zilizopatiwa hati ya kutokomeza ugonjwa huo. Katika mwaka 2017/2018 Serikali itaendelea kuimarisha huduma za afya nchini kwa kuongeza kasi ya utekelezaji wa mpango wa maendeleo ya afya ya msingi na kuimarisha huduma za kinga ili kupunguza vifo vya watoto na akina mama pamoja na makundi mengine.

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo la afya, naomba kutoa wito kwa Watanzania, tumeanzisha mpango wa bima kwa watumishi wa umma na mpango wa bima kwa wananchi wa kawaida kwa mpango wa *CHF.* Natoa wito kwa Watanzania kujiunga na *CHF* popote walipo ili waweze kuchangiwa na Serikali na waweze kupata huduma kupitia hospitali zetu, zahanati na vituo vya afya vilivyo katika Halmashauri zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bunge; Ofisi ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa. Katika mwaka wa fedha wa 2016/2017, Ofisi ya Bunge iliratibu na kusimamia shughuli za mikutano mitatu ya Bunge ambapo maswali 1,054 ya kawaida, nyongeza na ya papo kwa papo kwa Waziri Mkuu yaliulizwa. Miswada kumi ya sheria ilijadiliwa na kupitishwa na Bunge.

Aidha, Bunge liliratibu na kusimamia shughuli za Mikutano ya Kamati za Kudumu za Bunge, kutoa huduma za *Hansard,* utafiti, utawala na kutoa mafunzo kwa Waheshimiwa Wabunge na watumishi wa Ofisi ya Bunge. Ofisi ya Bunge pia ilisimamia kazi ya ukarabati wa jengo la Bunge pamoja na kuratibu ujenzi wa Ofisi za Waheshimiwa Wabunge. Katika mwaka 2017/2018, Serikali itaendelea

kuliwezesha Bunge kutekeleza majukumu yake ya Kikatiba kama kawaida.

Mheshimiwa Spika, sekta ya mahakama; utendaji wa mhimili wa Mahakama nchini umezidi kuimarika. Katika mwaka 2016/2017 Mahakama imesikiliza na kukamilisha mashauri 279,331 kati ya mashauri 333,962 katika ngazi zote za Mahakama sawa na asilimia 83.1 ya mashauri yote. Naomba nitumie nafasi hii kuwapongeza watendaji, Majaji, Mahakimu kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kuhakikisha kwamba tunapunguza mashauri yote kwenye maeneo yetu. Pamoja na kazi kubwa ya kusikiliza mashauri, Mahakama imesogeza huduma zake karibu na wananchi kwa kukamilisha ukarabati na ujenzi wa majengo ya Mahakama Kuu katika mikoa ya Tanga na Dar es Salaam. Pia kazi za ukarabati wa Mahakama Kuu katika Mkoa wa Mbeya inaendelea na ujenzi wa Mahakama ya Wilaya na Mahakama za Mwanzo Kibaha Mkoa wa Pwani umekamilika na umeshazinduliwa.

Mheshimiwa Spika, ni matarajio yangu kwamba katika mwaka 2017/2018 Mahakama itaendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi ili kupunguza mlundikano wa mashauri yaliyopo Mahakamani. Hata hivyo, ili Mahakama ifanye kazi zake vizuri, shughuli za upelelezi wa kesi na uendeshaji wa mashtaka zinatakiwa pia kuimarishwa zaidi. Serikali itafanya kila liwezalo kuimarisha taasisi zote zinazohusika katika mlolongo wa utoaji haki ili wananchi wapate haki zao kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika, masuala mtambuka; Mfumo wa Ufuatiliaji wa Shughuli za Serikali. Katika mwaka 2016/2017, Serikali iliahidi kuanzisha mfumo wa wazi wa kielektroniki wa kufuatilia uwajibikaji na utendaji Serikalini. Mfumo huu utasaidia kuongeza ufanisi katika uratibu wa shughuli za Serikali kwa kuwawezesha viongozi kutoa maelekezo na kufuatilia utekelezaji wake. Aidha, mfumo huo utasaidia ufuatiliaji wa utekelezaji wa ilani ya Chama cha Mapinduzi, ahadi na maagizo ya Mheshimiwa Rais na Mpango wa Taifa wa Maendeleo. Lakini pia napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu

kwamba, mfumo huo umekamilika, kuzinduliwa rasmi na mafunzo kutolewa kwa wataalamu katika Wizara zote. mfumo huo pamoja na mambo mengine utaongeza kasi ya utoaji taarifa za utekelezaji wa kazi za Serikali kwa wakati na pia kuongeza uwajibikaji kwa watumishi wa umma; lakini pia Wizara na Taasisi zote za Serikali zinatakiwa kuutumia mfumo huo kikamilifu ili kurahisisha ufuatiliaji wa utekelezaji wa kazi za Serikali na kusaidia viongozi kutatua vikwazo pale vinapojitokeza.

Mheshimiwa Spika, vita dhidi ya rushwa; Serikali inapambana na rushwa kwa nguvu zake zote na haina mzaha wala uvumilivu na vitendo vya rushwa. Hatua zilizochukuliwa kupambana na rushwa tangu Serikali ya Awamu ya Tano ilipoingia madarakani Novemba, 2015 zimetambulika hata na Mashirika ya Kimataifa yanayojishughulisha na tafiti kuhusu masuala ya rushwa duniani. Taarifa ya Shirika la *Transparency International* kwenye utafiti wake kuhusu mtazamo wa rushwa mwaka 2016 imeonesha kuwa viwango vya rushwa vinaendelea kupungua kwa kasi hapa nchini kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/2017, Serikali kupitia TAKUKURU imefanya uchunguzi wa majalada 306 ya tuhuma za rushwa na kupata kibali cha Mkurugenzi wa Mashitaka nchini kuendelea na mashtaka kwa majalada 104. Katika kipindi hicho, TAKUKURU iliendesha kesi 674 zikiwemo kesi mpya 182 ambapo katika kesi 97 watuhumiwa walipatikana na hatia na kuhukumiwa kifungo au kulipa faini. Kesi 407 zinaendelea kusikilizwa mahakamani na kutokana na operesheni zilizofanywa na TAKUKURU, kiasi cha Shilingi bilioni 9.75 ziliokolewa.

Katika mwaka 2017/2018, Serikali itaendelea na mapambano yake dhidi ya rushwa hususani katika eneo la ukusanyaji mapato ya Serikali, kudhibiti matumizi ya fedha za umma na malipo hewa na matumizi mabovu ya fedha za ushirika na kuimarisha ufuatiliaji na ukaguzi wa miradi ya maendeleo. Nawasihi Watanzania, kwenye mapambano

haya tuungane mkono tuhakikishe kwamba tunatokomeza rushwa nchini kwetu.

Mheshimiwa Spika, vita dhidi ya UKIMWI; mapambano dhidi ya UKIMWI yamekuwa yakitegemea kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa rasilimali fedha kutoka kwa Wadau wa Maendeleo. Ninapenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Mfuko wa Udhamini wa UKIMWI ulioanzishwa na Serikali miaka miwili iliyopita, ulizinduliwa tarehe 01 Desemba, 2016, ambapo kupitia harambee iliyofanyika kwa ajili ya kuchangia mfuko huo, shilingi milioni 347 zilipatikana kama ahadi. Vilevile Serikali imetenga kiasi cha Shilingi bilioni 5.6 kwa ajili ya mfuko wa UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutoa huduma kwa Wadau Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (WAVIU) ambapo hadi Desemba, 2016 WAVIU 839,574 sawa na asilimia 63 ya WAVIU wote walikuwa wamepatiwa dawa. Juhudi zinaendelea kufanyika ili kuwahamasisha WAVIU kujitokeza na kuingia kwenye mpango wa tiba ya kufubaza athari za UKIMWI. Aidha, Serikali imekamilisha uandaaji wa miongozo minne ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI ikijumuisha Mpango Kazi wa Kinga, Mkakati wa Kondomu, Mkakati wa Uwekezaji na Mpango Kazi wa Jinsia.

Mheshimiwa Spika, Serikali katika mwaka 2017/2018, itaimarisha uratibu wa afua za UKIMWI kwa wadau wote wa sekta ya umma na binafsi na kupitia mifumo ya uratibu iliyoanzishwa. Serikali kwa kushirikiana na wadau pia itazijengea uwezo Kamati zilizo katika ngazi ya jamii hususan vijiji na kata ili kufikia malengo ya kitaifa na kimataifa ya kupunguza na kumaliza UKIMWI ifikapo mwaka 2030 kwa kutumia mfumo ulio katika jamii. Vilevile, Serikali itakamilisha utafiti wa nne wa kubainisha viwango vya maambukizo ya UKIMWI nchini na kuboresha ushiriki wa sekta binafsi ili kuleta ufanisi katika kuchangia mwitikio wa Taifa dhidi ya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, huduma kwa watu wenye ulemavu; katika 2016/2017, Serikali imeendelea kutoa huduma pamoja na kuongeza upatikanaji wa haki na fursa

kwa watu wenye ulemavu. Katika kutimiza azma hiyo, Serikali imewaagiza Wakuu wa Mikoa kuhakikisha kuwa Kamati za watu wenye ulemavu zinaanzishwa katika ngazi za Mikoa, Wilaya, Mitaa na Vijiji. Aidha, Serikali imeanzisha kampeni za kupinga unyanyapaa na vitendo vya kikatili dhidi ya watu wenye Ualbino katika mikoa ya Shinyanga, Mwanza, Geita, Simiyu, Kagera, Tabora, Kigoma, Mara, Mbeya, Katavi na Rukwa na kampeni hiyo itaendelea nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia inahakikisha kwamba watumiaji wa lugha ya alama wanapata haki ya kupata habari na vituo vyote vya televisheni vimeelekezwa kutumia wakalimani wa lugha ya alama. Napenda kuvikumbusha tena vituo vya televisheni kuweka wakalimani wa lugha katika vituo vyao. Katika mwaka 2017/2018 Serikali itaendelea kutoa huduma kwa watu wenye ulemavu ikiwa ni pamoja na kutoa vifaa saidizi kwa wanafunzi wenye ulemavu shuleni na vifaa vya kufundishia.

Mheshimiwa Spika, vita dhidi ya dawa za kulevya; dawa za kulevya zinaathiri maisha ya vijana wetu wengi na hivyo kuzima ndoto za maisha yao na kupunguza nguvu kazi ya Taifa letu. Ili kupambana na janga hilo, katika mwaka 2016/2017 Bunge lako Tukufu lilifanya marekebisho ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Dawa za Kulevya Namba Tano ya mwaka 2015. Marekebisho hayo yameipa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya nguvu ya kukamata, kupeleleza na kushitaki watuhumiwa wanaohusika na biashara ya dawa za kulevya. Aidha, hivi karibuni Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli amefanya uteuzi wa watendaji wakuu watakaosimamia mamlaka hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Januari, 2017 watuhumiwa 11,503 walikamatwa kwa tuhuma za kujihusisha na biashara ya uzalishaji, usambazaji, uuzaji na matumizi ya dawa za kulevya katika sehemu mbalimbali nchini. Kati ya watuhumiwa hao, kesi 9,813 ziko katika hatua mbalimbali ambapo 974 walikutwa na hatia, watuhumiwa 238 waliachiwa huru na kesi 478 bado zinaendelea. Ni imani

yangu kuwa, Mamlaka ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya itaendeleza kwa kasi zaidi juhudi za kupambana na uingizaji, uzalishaji na usambazaji na matumizi ya dawa za kulevye hapa nchini. Watanzania wana imani kubwa na Mamlaka hii, na ninaomba wote tuipe ushirikiano wakati wote kwani vita hii ni kubwa na ni ya Kimataifa. Aidha, nawasihi wazazi wenzangu, tuwe karibu na vijana wetu na kufuatilia nyendo zao ili wasijekuingia kwenye mtego huu wa dawa za kulevya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uratibu wa maafa; Serikali wakati wote inahakikisha kuwa nchi ipo katika hali ya utayari wa kukabiliana na maafa na pia kutoa misaada ya kibinadamu ikiwemo huduma za matibabu, ushauri wa kisaikolojia na vifaa pale maafa yanapotokea. Serikali imejenga vituo vipya 20 vya upimaji wa hali ya hewa katika Halmashauri 11 za Tarime, Nyamagana, Muleba, Longido, Geita, Maswa, Kigoma, Sikonge, Kongwa, Serengeti na Kahama. Kuwepo kwa vituo hivyo kutaongeza ufanisi katika upatikanaji wa taarifa za tahadhari hasa kwa majanga ya mafuriko na ukame.

Mheshimiwa Spika, kufuatia tetemeko la ardhi lililotokea katika mikoa ya Kanda ya Ziwa mwezi Septemba, 2016, Serikali kwa kushirikiana na wadau imechukua hatua za kushughulikia athari zilizotokana na tetemeko hilo. Huduma za afya na tiba na za kibinadamu za chakula na malazi zilitolewa kwa walioathirika. Vilevile Serikali ilirejesha hali ya miundombinu iliyobomolewa yakiwemo majengo ya Serikali na taasisi za umma 686, Kituo cha Wazee Kilima pamoja na kutoa maturubai 6,237, mahema 367, mabati 7,300 na mifuko ya saruji 1,825 kwa walioathirika. Serikali itaendelea na ujenzi wa shule za Ihungo, Nyakato na Omumwani pamoja na ukarabati wa Kituo cha Afya Kabyaile Ishozi. Napenda kuwashukuru sana wananchi wote na wadau waliotoa michango yao kusaidia waathirika wa tetemeko la ardhi lililotokea mkoani Kagera.

Mheshimiwa Spika, habari na michezo; sekta ya habari; Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria ya Huduma za

Habari Namba 12 ya mwaka 2016 ambayo ni muhimu katika kuimarisha usimamizi na uwajibikaji katika Sekta ya Habari nchini. Kanuni za Sheria hiyo zimeandaliwa na tayari zimeanza kutumika. Natoa wito kwa wadau wa sekta ya habari kuzingatia sheria na kanuni hizo ili kuimarisha weledi katika tasnia ya habari. Aidha, nashauri wadau wa habari kujikita zaidi katika kuandika na kutangaza habari za masuala ya maendeleo na uchumi ili kuwasaidia wananchi kutekeleza azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kujenga uchumi wa viwanda na kuboresha huduma za kijamii.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya michezo; tumeanza kuona dalili nzuri za kuimarika kwa shughuli za michezo hapa nchini. Mathalani mwezi Mei, 2017 timu ya mpira wa miguu yetu, *Serengeti Boys* imefuzu kushiriki Mashindano ya Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa vijana wa umri wa chini ya miaka 17 nchini Gabon. Nitumie nafasi hii kumshukuru pia Mheshimiwa Makamu wa Rais Mama Samia Suluhu Hassan ambaye amewaaga na kuwakabidhi bendera ya Taifa tayari kwa kwenda kupambana vita hiyo. Watanzania tuungane pamoja kuiombea timu yetu, lakini kuiunga mkono kwa michango ya hali na mali ili iweze kufuzu fainali hizo Afrika ili iweze kucheza Kombe la Dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa riadha, Mtanzania mwenzetu Alphonce Simbu alipata medali katika mbio za marathon huko Mumbai nchini India. Aidha, mwezi Septemba, 2016 timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu ya Wanawake Tanzania *(Twiga Stars)* iliweka historia ya kuwa timu ya kwanza kutwaa taji la *CECAFA* hapan Tanzania. *(Makofi)*

Nitumie nafasi hii kutoa pongezi zangu kwa wale wote waliolietea Taifa hili sifa katika sekta ya michezo, *Twiga Stars,* Alphonce Simbu na wengine wote ambao watajitokeza kuhakikisha kwamba tunaendelea kuweka *record* nzuri kwa Taifa letu kwenye sekta ya michezo. Tunaziombea dua, nawatakia jitihada njema ili tuweze kufika hatua nzuri ya kushiriki mashindano ya dunia.

Mheshimiwa Spika, michezo ni sekta muhimu katika kuongeza ajira, kuimarisha afya, kukuza uchumi, kuimarisha umoja wa kitaifa na kuitangaza nchi kimataifa. Nchi nyingi zilizofanikiwa kimichezo ziliwekeza zaidi kujenga vipaji vya vijana katika michezo. Kwa hiyo basi, ni vyema sasa Baraza la Michezo Tanzania lihakikishe linafanya jitihada kuunganisha vyama vyetu vya michezo nchini ili kuhakikisha kwamba vijana wa nchi yetu wanajitokeza kwa wingi kushiriki katika michezo mbalimbali. Kufuatia timu yetu ya *Serengeti Boys,* natoa wito kwa *TFF* ihakikishe kuwa vijana hawa wa *Serengeti Boys* wanawekewa mpango endelevu wa kukuza vipaji vyao na kutunzwa vyema ili waweze kuiwakilisha nchi yetu katika mashindano mengine ya kimataifa. *(Makofi)*

Aidha, vyama vingine vya michezo vitoe msukumo mkubwa kwenye kuwekeza zaidi kwa vijana wa shule za msingi na sekondari kwani hao ndio watakuwa wawakilishi wetu katika miaka ijayo. Na mwaka huu, michezo ya shule za msingi na sekondari itarejea kufanyika Mkoani Mwanza kama ilivyotangazwa mwaka jana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nazisihi Wizara husika; TAMISEMI na Wizara ya Elimu kuanza maandalizi mapema na kuandaa mpango huo na kutoa taarifa ili timu hizo ziweze kujiandaa na ziweze kushindana tupate wachezaji watakaounda timu zetu za kitaifa na hatimaye Taifa lipate wachezaji imara.

Mheshimiwa Spika, ulinzi na usalama; hali ya ulinzi na usalama nchini ni shwari kutokana na kazi kubwa na nzuri inayofanywa na vikosi vyetu vya ulinzi na usalama katika kulinda mipaka ya nchi yetu. Serikali imeendelea kuimarisha Jeshi la Wananchi wa Tanzania kwa kulipatia zana na vifaa vya kivita na kukamilisha mradi mkubwa wa ujenzi wa nyumba 6,064 za makazi ya askari ulioanza mwaka 2013/2014. Kwa upande mwingine, Serikali kupitia Jeshi la Magereza inakamilisha ujenzi wa nyumba zilizojengwa kwa njia ya ubunifu katika baadhi ya Magereza ikiwemo ujenzi unaoendelea sasa katika Gereza la Ukonga wa ghorofa 12 zenye uwezo wa kuishi askari na familia 320.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuimarisha usalama wa raia na mali zao kwa kufanya operesheni za kuzuia uhalifu nchini, kufanya upelelezi wa kesi kwa kasi ili kupunguza mlundikano wa kesi zilizopo Mahakamani na kusimamia sheria za barabarani ili kupunguza ajali zinazoleta madhara kwa wananchi. Aidha, Serikali itaendelea kutoa mafunzo kwa askari na maafisa wa jeshi ili kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi, kupambana na vitendo vya rushwa, kupambana na biashara ya dawa za kulevya na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa; kudumisha ushirikiano mzuri na mataifa mengine duniani pamoja na mashirika ya kimataifa ni moja kati ya misingi ya sera yetu ya mambo ya nje. Tumeendelea kuimarisha ujirani mwema baina yetu na nchi jirani, nchi marafiki pamoja na mashirika ya kikanda na kimataifa, jitihada ambazo zimetuwezesha kuvutia mitaji mikubwa ya uwekezaji, utalii pamoja na kupanua fursa za kibiashara. Katika mwaka 2016/2017, Serikali imefungua Balozi mpya sita katika nchi za Algeria, Israel, Korea Kusini, Sudan, Qatar na Uturuki. Balozi hizo zina kazi kubwa ya kuendeleza juhudi za kuitangaza Tanzania kama nchi yenye vivutio vingi vya utalii na rasilimali zinazoweza kutumika kuvuta uwekezaji kutoka mataifa hayo ikizingatiwa utulivu na amani iliyopo inaweza kuleta mvuto mkubwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kulinda na kutetea maslahi ya Tanzania nje ya nchi na kuweka mikakati ya kunufaika na nafasi ya nchi yetu kihistoria. Hivyo, ninatoa wito kwa Mabalozi wetu wote waendelee kuitangaza nchi yetu popote walipo kama eneo muafaka lenye fursa nyingi za utalii, uwekezaji na biashara.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; ili kujenga uchumi wa viwanda tunahitaji nidhamu ya kazi, ubunifu, elimu na matumizi makubwa ya sayansi na teknolojia. Vilevile tunahitaji kuimarisha sekta binafsi, miundombinu ya huduma za kijamii na kiuchumi na kuondoa urasimu usio wa lazima kwenye ofisi zetu. Nafarijika kwamba misingi tunayoendelea

kujenga katika kutekeleza azma hiyo imeanza kuzaa matunda kama nilivyoeleza awali ili kufanya mafanikio hayo yawe endelevu. Naomba nihitimishe hotuba yangu kwa kusisitiza mambo makuu yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, moja, ustawi wa nchi yetu na mafanikio ya mipango yetu ya maendeleo vinategemea amani na utulivu wetu. Hivyo, kila mmoja wetu aweke nadhiri ya kuendelea kuilinda na kuienzi amani ya nchi yetu ili mipango yetu iweze kufanikiwa. Tunalo jukumu la kuhimiza amani ili tufanye kazi zetu kwenye mazingira ya amani na utulivu.

Mheshimiwa Spika, pili, jukumu la kujenga uchumi wa nchi yetu ni wajibu wa kila mwananchi. Njia pekee ya kuijenga nchi yetu ni kufanya kazi kwa bidii, kulipa kodi kwa hiari na kufichua wakwepa kodi na wala rushwa.

Mheshimiwa Spika, tatu, ujenzi wa uchumi wa viwanda unahitaji wananchi wenye afya njema na maarifa ya kufanya kazi na ubunifu. Tujenge utamaduni wa kupima afya zetu na kufanya mazoezi ya viungo ili kuepuka magonjwa yasiyo ya kuambukiza ambayo yanapoteza nguvu kazi kubwa ya Taifa ikiwemo UKIMWI.

Nne, rasilimali tulizonazo ipo siku zitaisha, hivyo ni wajibu wa kila mmoja wetu kuzitumia kwa uangalifu ili zitufae sisi na vizazi vijavyo. Tuepuke matumizi mabaya ya rasilimali zetu kama vile maji, madini na misitu ili ziweze kunufaisha kizazi hiki na kizazi kijacho.

Mheshimiwa Spika, tano, tuongeze nidhamu na uwajibikaji katika kila jambo la maendeleo tunalolifanya na kuzingatia matumizi ya muda. Tamaduni na mila zinazohamasisha uvivu na uzembe ni lazima tuzipige vita kwa nguvu zetu zote.

Mheshimiwa Spika, na mwisho, dawa za kulevya ni janga kubwa linalolitafuna Taifa letu kwa kasi. Tunahitaji ushiriki wa kila mmoja katika vita hii kwa kufichua mtandao

wa wahusika wa dawa za kulevya. Ahadi yetu katika jambo hili, tutawapa ushirikiano na tutachukua hatua kali dhidi ya yeyote atakayepatikana kwenye matukio ya dawa za kulevya.

Mheshimiwa Spika, sasa nije kwenye Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha za Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge letu kwa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha ujao wa 2017/2018, Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 171,664, 055,000; kati ya fedha hizo, shilingi 74,643,339,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 97,020,716,000 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, vilevile ninaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 121, 652, 262,000 ni kwa ajili ya Mfuko wa Bunge; kati ya fedha hizo, shilingi 114,452,262,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 7,200,000,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (Makofi)

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Tunakushukuru sana kwa hotuba hiyo nzuri. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Ahsanteni sana mnaweza kukaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge wamekusikiliza kwa umakini mkubwa sana. Tunakushukuru.

# HOTUBA YA WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MHESHIMIWA KASSIM M. MAJALIWA (MB), KUHUSU MAPITIO NA MWELEKEO WA KAZI ZA SERIKALI NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA ZA OFISI YA WAZIRI MKUU NA OFISI YA BUNGE KWA MWAKA 2017/2018 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa Hoja kwamba kutokana na taarifa zilizowasilishwa leo katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI zilizochambua Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge lako sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa mwaka 2016/2017 na Mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa mwaka 2017/2018. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake pamoja na Mfuko wa Bunge kwa mwaka 2017/2018.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, Bunge lako Tukufu limeondokewa na Wabunge wenzetu, Mheshimiwa Hafidh Ally Tahir aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Dimani - CCM na Mheshimiwa Dkt. Elly Marko Macha, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum - CHADEMA. Pia, Taifa lilimpoteza Mheshimiwa Samwel John Sitta aliyekuwa Spika Mstaafu wa Bunge la Tisa la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, nchi yetu imekumbwa na majanga na maafa yaliyosababisha vifo, majeruhi na uharibifu wa mali. Ninaomba Mwenyezi Mungu awajalie nafuu ya haraka wale wote waliopata majeraha, na kuwapumzisha kwa amani wale waliopoteza maisha, **Amina!** Ninatoa pole kwa familia za wote waliopoteza ndugu, jamaa na marafiki. Pia ninatoa pole kwa Mheshimiwa Aida Khenani aliyepata ajali ya kugongwa na pikipiki wakati akitoka Bungeni. Tunamuombea apone haraka na aweze kurejea Bungeni ili kuendelea na majukumu yake.

## PONGEZI NA SHUKRANI

3. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar kwa kutimiza mwaka mmoja wa uongozi wao. Sisi tunaowasaidia tunajivunia uongozi wao mahiri, uzalendo uliotukuka na dhamira njema waliyonayo kwa Watanzania.

4. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2016/2017, Bunge lako Tukufu limepokea na kuwaapisha Wabunge wapya watano, ambao ni Mheshimiwa Abdallah Majura Bulembo (Mb.), Mheshimiwa Anne Killango Malecela (Mb.), Mheshimiwa Juma Ali Juma (Mb.), Mheshimiwa Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi (Mb.) na Mheshimiwa Salma Rashidi Kikwete (Mb.). Ninawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge wapya kwa heshima waliyoipata ya kujumuika nasi kwenye Bunge hili. Kama ilivyo ada, tutatoa ushirikiano unaotarajiwa kwa Waheshimiwa Wabunge hawa ili watekeleze majukumu yao kwa ufanisi na tija. Kipekee, ninampongeza Mheshimiwa Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi (Mb.) kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria. Pia ninatumia nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote walioteuliwa kuingia kwenye Bunge la Afrika Mashariki, Makatibu Wakuu wapya walioteuliwa na Mheshimiwa Rais yaani Profesa Kitila Alexander Mkumbo, Dk. Leonard Akwilapo, Maimuna Tarishi na Dk. Ave Maria Semakafu. Nawapongeza sana wote walioteuliwa kushika nyadhifa hizo.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kazi kubwa ya kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara, Mikoa, Wakala, Idara za Serikali zinazojitegemea na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Ninawashukuru kipekee sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria inayoongozwa na Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji; Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni na Kamati ya Bajeti inayoongozwa na Mheshimiwa Hawa

Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini kwa kutoa mchango mkubwa wakati wa maandalizi ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Pia, niwapongeze Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kuongoza kwa umahiri mkubwa Kamati zao wakati wa kupitia makadirio ya sekta zote. Maoni na ushauri wao umesaidia sana kuboresha Makadirio ya Bajeti ya Serikali kwa mafungu yote.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** niruhusu pia niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu Kiongozi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Makatibu Wakuu, Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Wakuu wa Idara, Mashirika na Taasisi zote za Serikali kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa katika kutekeleza majukumu yangu. Aidha, ninawashukuru Wafanyakazi wote wa Serikali na Taasisi zake chini ya Uongozi wa Katibu Mkuu Kiongozi, kwa kukamilisha Bajeti ya Serikali ya mwaka 2017/2018.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee, ninamshukuru Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama (Mb.), Mbunge wa Peramiho, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu); Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde (Mb.), Mbunge wa Dodoma Mjini na Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira na Vijana) kwa ushirikiano wao mkubwa katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Aidha, ninamshukuru Mheshimiwa Dkt. Abdallah Possi aliyekuwa Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kazi kubwa aliyofanya wakati akiitumikia nafasi hiyo. Ninamtakia kazi njema kwenye jukumu lake jipya la kuiwakilisha Tanzania nchini Ujerumani. Vilevile, ninawashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu, chini ya Uongozi wa Makatibu Wakuu, Dkt. Hamisi H. Mwinyimvua; Bwana Eric F. Shitindi na aliyekuwa Katibu Mkuu Bwana Uledi A. Mussa kwa ushauri wao wa kitaalam kwangu na kwa Waheshimiwa Mawaziri.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** ninazishukuru pia nchi marafiki, Taasisi na Mifuko ya Fedha Duniani, Mashirika ya Umoja wa Mataifa, Madhehebu ya Dini na Mashirika yasiyo ya Kiserikali kwa

kuunga mkono jitihada za Serikali katika kujenga uchumi wa nchi yetu. Misaada na mikopo iliyopatikana kwa wakati imechangia kutekeleza miradi ya maendeleo na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.

**9.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kutumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati wananchi wa Jimbo la Ruangwa kwa kuendelea kuniunga mkono na kuielewa vizuri dhamana ya Kitaifa niliyonayo ya kusimamia utendaji wa Serikali katika sekta zote na kuwa Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni. Mwisho ninaishukuru familia yangu hususan mwenza wangu mpendwa, Mary na watoto wetu kwa upendo, dua na kuendelea kunitia moyo ili nitekeleze kwa ufanisi zaidi majukumu yangu ya Kitaifa. **Asanteni sana!**

**MWELEKEO WA BAJETI**

**10.** ***Mheshimiwa Spika,*** ni mwaka mmoja sasa tangu Serikali ya Awamu ya Tano iingie madarakani. Katika kipindi hicho, yapo mambo mengi yaliyofanyika kwa mafanikio makubwa ambayo yataanishwa kwa kina katika bajeti za Sekta pindi Mawaziri husika watakapoziwasilisha. Baadhi ya mafanikio hayo ni utekelezaji wa ahadi ya Serikali ya Elimu Bila Malipo; kuongezeka kwa uzalishaji na kasi ya usambazaji wa umeme vijijini; kuimarika uwajibikaji na nidhamu katika Utumishi wa Umma; kuongeza ukusanyaji wa mapato na udhibiti wa matumizi ya fedha za Umma; kuboresha huduma za kiuchumi na za kijamii; na kutekeleza Awamu ya Kwanza ya Mpango wa Serikali Kuhamia Dodoma. Nitumie fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge, Viongozi wa Serikali, Watumishi wa Umma na Watanzania wote kwa ujumla kwa kuendelea kuiunga mkono Serikali katika utekelezaji wa majukumu yake, kwani bila ushirikiano wao, tusingeweza kupata mafanikio hayo.

**11.** ***Mheshimiwa Spika***, Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu imeendelea kuandaliwa kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2015; Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano; ahadi za Mheshimiwa Rais alizotoa wakati wa Kampeni, pamoja na maelekezo yake

wakati anazindua Bunge la 11 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 20 Novemba, 2015. Bajeti hii itaendelea kuimarisha mafanikio yaliyopatikana katika mwaka uliopita na kushughulikia utatuzi wa vikwazo vya kukuza uchumi kwa haraka na baadhi ya changamoto zilizojitokeza. Aidha, Serikali itajikita zaidi katika maeneo yatakayochangia kuimarisha uchumi wa viwanda na kuboresha huduma za jamii.

Ninawaomba Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla, kuendelea kushirikiana na Serikali katika kufikia azma hiyo ili dhamira yetu ya kuboresha maisha ya Watanzania iweze kutimia. Ni vyema tukakumbuka kwamba tuna mwaka mmoja tu wa utekelezaji wa yale tuliyopanga kufanya ndani ya kipindi cha miaka mitano. Tutatumia bajeti ya mwaka ujao wa fedha kukabili changamoto zilizojitokeza. Ahadi ya Serikali ni kuendelea kuwatumikia wananchi kwa uadilifu na bila ubaguzi wowote, huku tukitanguliza mbele maslahi ya Taifa.

**SERIKALI KUHAMIA DODOMA**

**12.** ***Mheshimiwa Spika,*** tarehe 23 Julai 2016, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akihutubia Mkutano Mkuu Maalum wa Chama Cha Mapinduzi, alitangaza uamuzi wa kuhamishia rasmi Shughuli za Serikali Kuu Dodoma. Kufuatia uamuzi huo, mipango ya kuhamia Dodoma kwa awamu ilianza baada ya mahitaji halisi yatakayoiwezesha Serikali kuhamia Dodoma kubainishwa, ikiwa ni pamoja na ofisi na nyumba za makazi kwa viongozi na watumishi wa umma. Awamu ya kwanza ilipangwa kuhama ifikapo mwisho wa mwezi Februari, 2017.

**13.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba tayari watumishi 2,069 wakiwemo Mawaziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu, baadhi ya Wakuu wa Idara na Vitengo na watumishi wengine wamekwishahamia Dodoma kama ilivyopangwa. Vilevile, Wizara zote zimepata majengo ya Ofisi yatakayotumika katika kipindi cha mpito.

**14.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili Mji wa Dodoma uweze kuendelezwa kwa mpangilio mzuri, Serikali inaupitia upya Mpango Kabambe wa Mji wa Dodoma. Mapitio hayo yatasaidia sana kuepuka makosa yaliyofanyika katika miji mingi hususan ujenzi holela unaochangia katika uchafuzi wa mazingira na kuharibu mandhari ya miji. Ni wazi kwamba, ujenzi wa Mji wa Dodoma hautafanywa na Serikali pekee, bali tutaendelea kuhamasisha Sekta binafsi na wadau wengine kuwekeza Dodoma. Ninalipongeza sana Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kwa kujenga nyumba 300 za makazi hapa Dodoma ambazo watumishi wanaweza kununua au kupangishwa. Ninatoa wito kwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma kuongeza kasi ya upimaji wa viwanja, kuboresha miundombinu na kudhibiti ujenzi holela kwa kushirikiana kwa karibu na Manispaa ya Dodoma na Taasisi nyingine za Serikali.

**SIASA**

**15.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwaka mmoja baada ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015, hali ya kisiasa nchini imeendelea kuwa shwari na ya kuridhisha. Aidha, Chaguzi Ndogo zilifanyika tarehe 22 Januari, 2017 katika Jimbo la Dimani - Zanzibar na Udiwani katika kata 20 Tanzania Bara kwa kushirikisha wagombea kutoka vyama 15 vya siasa. Ninavipongeza vyama vyote vilivyoshiriki katika chaguzi hizo, na kipekee nakipongeza Chama cha Mapinduzi kwa ushindi wa Jimbo la Dimani na viti 19 vya udiwani katika chaguzi hizo.

**16.** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, mashauri 53 ya kupinga ushindi wa Ubunge na mashauri 194 ya kupinga ushindi wa Udiwani yalifunguliwa. Mashauri hayo yamekwishasikilizwa na hukumu kutolewa, isipokuwa shauri moja la kupinga matokeo ya Ubunge katika Jimbo la Mbagala. Nizipongeze Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kazi kubwa waliyofanya ya kuhakikisha kesi hizo zinaendeshwa kwa kasi na kwa weledi na hivyo kuwezesha wananchi kuendelea kupata uwakilishi.

**17.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuendelea kuboresha demokrasia hapa nchini, hatuna budi kujenga jamii inayoheshimu na kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za nchi pamoja na kuwa na uvumilivu wa kisiasa. Ninatoa rai kwa wadau wa siasa kote nchini kujenga utamaduni wa masikilizano na kuendesha siasa za maendeleo badala ya siasa za malumbano; siasa za kuunganisha watu wetu badala ya kuwagawa; na siasa za uwajibikaji badala ya siasa za mazoea. Serikali itaendelea kulinda na kuheshimu misingi ya siasa zinazolenga kuleta ustawi wa wananchi na zinazotanguliza maslahi ya nchi na wananchi.

## MUUNGANO

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea kudumisha muungano wetu ambao ni tunu na mfano wa kuigwa barani Afrika na dunia nzima. Wananchi wanaendelea kunufaika na matunda ya Muungano wetu ambao ni imara na dhabiti. Serikali zote mbili zinafanya mashauriano kupitia Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kushughulikia masuala ya Muungano chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, viongozi na watendaji wa sekta nyingine zisizo za Muungano wamekuwa wakikutana mara kwa mara ili kubadilishana uzoefu na kubaini maeneo ya ushirikiano kwa ustawi wa wananchi wa pande zote mbili. Jumla ya vikao 13 vya sekta ambazo siyo za Muungano vilifanyika kati ya Julai 2016 na Machi 2017.

**19.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kutumia fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendesha kwa ufanisi mkubwa kikao kilichofanyika tarehe 13 Januari, 2017 ambapo taarifa kuhusu hoja zilizopatiwa ufumbuzi, maagizo na maelekezo ya kufuatilia utekelezaji wa changamoto zilizobaki ilitolewa. Serikali itaendelea kuulinda na kuuenzi Muungano wetu kwa manufaa ya wananchi wa pande zote mbili.

## HALI YA UCHUMI

**20.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwenendo wa viashiria vya ukuaji wa uchumi wa nchi yetu kwa mwaka 2016/2017 vinaonesha kuwa uchumi wetu unakua na kuimarika. Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu, ukuaji halisi wa Pato la Taifa ulifikia **asilimia 7.0** mwaka 2016. Sekta zilizochangia kwa kiwango kikubwa kwenye ukuaji huo ni uchimbaji madini na mawe; usafirishaji na uhifadhi wa mizigo; habari na mawasiliano; pamoja na shughuli za fedha na bima. Mfumuko wa Bei uliendelea kubakia katika wigo wa tarakimu moja na kasi ya upandaji bei ilipungua kutoka wastani wa **asimilia 5.6** mwaka 2015 hadi **asilimia 5.2** mwaka 2016. Kwa upande mwingine, tathmini ya hali ya Taasisi za Fedha inaonesha kuwa Benki zetu ziko salama na zina mitaji na ukwasi wa kutosha. Aidha, taarifa za Mashirika mbalimbali ya Kimataifa zinaonesha kwamba katika mwaka 2016 uchumi wa Taifa letu ulikua vizuri na hivyo kutufanya kuwa miongoni mwa nchi sita (6) za Bara la Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara ambazo uchumi wake unakua kwa kasi kubwa zaidi.

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Awamu ya Tano imeweka juhudi kubwa katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Kutokana na juhudi hizo, makusanyo ya ndani kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) yaliongezeka kutoka wastani wa **Shilingi Bilioni 850** kwa mwezi katika mwaka 2015/2016 hadi **Shilingi Trilioni 1.2** kwa mwezi katika mwaka 2016/2017. Pamoja na kuongeza ukusanyaji wa mapato, juhudi kubwa zimefanyika kudhibiti matumizi ya rasilimali za umma ikiwa ni pamoja na kuziba mianya ya rushwa, ubadhirifu, wizi na upotevu wa fedha za umma. Mwenendo huo umeiwezesha Serikali kuanza utekelezaji wa miradi mikubwa kwa fedha za ndani na pia utoaji huduma kwa wananchi. Serikali itaendelea kupanua wigo wa vyanzo vya mapato ya ndani na kuongeza kasi ya ukusanyaji mapato ili kila anayestahili kulipa kodi aweze kuilipa.

**22.** ***Mheshimiwa Spika,*** kuimarika kwa viashiria vya uchumi wa nchi yetu katika kipindi cha mwaka mmoja tangu

Serikali ya Awamu ya Tano iingie madarakani ni dalili njema katika kujenga uchumi imara na tulivu utakaotusaidia kuelekea katika Uchumi wa Viwanda na kufikia nchi ya kipato cha kati ifikapo mwaka 2025. Serikali itaongeza juhudi katika kuchochea ukuaji wa sekta za kipaumbele zenye fursa kubwa ya kukuza uchumi kwa haraka na kuondoa umaskini kama vile Kilimo na Viwanda. Pia, itahakikisha kwamba sekta wezeshi kama vile Nishati, Habari na Mawasiliano, Fedha na ujenzi wa miundombinu muhimu ya barabara, bandari, reli, vivuko na viwanja vya ndege zinaimarishwa. Vilevile, Serikali itaendelea kuhimiza utekelezaji thabiti wa miradi ya maendeleo na kuweka mazingira mazuri ya kufanya biashara na kuvutia uwekezaji.

**Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi**

**23.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuwezesha Wananchi kupitia Mipango na Programu mbalimbali kwa kuelekeza nguvu zaidi kwa makundi ya wanawake, vijana na wenye ulemavu. Serikali imeweka mazingira bora kwa vikundi vya kiuchumi na vijana kujiunga na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, SACCOS na VICOBA. Aidha, Serikali imeanzisha majukwaa ya uwezeshaji wa wanawake kiuchumi katika mikoa yote na kufanya mapitio ya Mwongozo wa Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake wa mwaka 2007. Mapitio hayo yana lengo la kuboresha uendeshaji na usimamizi wa Mfuko huo ili kuwezesha wanawake wengi zaidi kukopesheka.

**24.** ***Mheshimiwa Spika,*** tunatambua kwamba asilimia 56 ya nguvu kazi ya Taifa ni vijana. Hivyo, Serikali inatekeleza Programu ya Kukuza Ujuzi na Stadi za Kazi ili kuwawezesha vijana kushiriki katika ujenzi wa uchumi wa viwanda pamoja na kuinua ari ya vijana kupenda kufanya kazi. Katika mwaka 2016/2017, Serikali inatoa mafunzo kwa vijana 9,120 katika fani mbalimbali zikiwemo stadi za kushona nguo, kutengeneza bidhaa za ngozi, mafunzo ya kurasimisha ujuzi uliopatikana kwa mfumo usio rasmi na mafunzo ya kukuza ujuzi na stadi za kujiajiri katika fani mbalimbali. Jumla ya vijana 1,469 wamehitimu mafunzo hayo na kupata ajira. Vijana 7,651 waliobaki wanaendelea kupata mafunzo kupitia

viwanda vya TOOKU GARMENTS, MAZAVA FABRICS, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), VETA na Don Bosco. Katika mwaka 2017/2018, Serikali itatoa mafunzo ya kukuza ujuzi wa kujiajiri na stadi za kazi kwa vijana 15,350 katika fani mbalimbali.

**25.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, imetoa mikopo yenye thamani ya Shilingi bilioni 1.5 kwa vikundi vya vijana 297 katika Halmashauri mbalimbali nchini. Aidha, Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia mapato yake ya ndani zimetoa Shilingi bilioni 4.6 ikiwa ni mikopo yenye masharti nafuu kwa vikundi vya vijana 2,356. Hatua hizi zimekwenda sanjari na utengaji wa maeneo maalum yenye jumla ya ekari 85,603 kwa ajili ya shughuli za vijana za kilimo, biashara ndogo ndogo, burudani na michezo. Katika mwaka 2017/2018, Serikali itaendelea kusimamia Halmashauri zote nchini kutenga asilimia tano (5) ya mapato yao kwa ajili ya vijana na asilimia tano (5) kwa wanawake.

## Ajira na Mahusiano Mahali pa Kazi

**26.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuratibu utekelezaji wa juhudi za kukuza ajira nchini kama inavyoelekezwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015. Hadi kufikia Machi 2017, jumla ya ajira 418,501 zimezalishwa nchini. Kati ya ajira hizo, ajira 239,017 sawa na asilimia 57 zimezalishwa katika sekta binafsi wakati ajira 179,484 sawa na asilimia 43 zimezalishwa kutokana na shughuli za sekta ya umma ikiwemo miradi ya maendeleo.

**27.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imefanya utafiti na kubaini kuwa asilimia 58 ya migogoro ya kikazi inatokana na kutozingatiwa kwa taratibu za kuachisha kazi. Sekta zinazoongoza kwa migogoro ya kazi ni usafirishaji, ujenzi, ulinzi binafsi, elimu, huduma za hoteli na viwanda. Katika kupunguza migogoro mahali pa kazi, Serikali imefanya kaguzi na kusimamia uundwaji wa Mabaraza ya Wafanyakazi. Aidha, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi imeendelea kutimiza wajibu wake wa kusuluhisha migogoro ambapo katika

kipindi cha Julai 2016 hadi Februari 2017, Tume imesajili jumla ya migogoro 8,832 kati ya hiyo migogoro 3,319 sawa na asilimia 37.6 ya migogoro yote iliyosajiliwa imesuluhishwa. Kati ya migogoro hiyo iliyosuluhishwa, migogoro 1,957 ilifikia suluhu (mediation) na migogoro 1,362 haikufikia suluhu. Aidha, migogoro 5,513 inaendelea kusuluhishwa katika hatua mbalimbali.

Ninatoa wito kwa waajiri na waajiriwa wote nchini, kuzingatia Sheria za Kazi na kuimarisha uhusiano mzuri kwenye maeneo ya kazi, ili muda mwingi zaidi utumike kwenye uzalishaji mali badala ya kutatua migogoro. Vilevile, ni muhimu sana kuimarisha kaguzi za kazi na kuendelea kusaini mikataba ya kuunda na kusajili mabaraza ya wafanyakazi ili kuimarisha zaidi mahusiano mahali pa kazi.

## MAENDELEO YA KISEKTA

### *Sekta za Uzalishaji*

### Viwanda

**28.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kujenga uchumi wa viwanda, Serikali inahamasisha wawekezaji wa ndani na nje kujenga viwanda vidogo, vya kati na vikubwa. Viwanda vinavyopewa kipaumbele ni vile vinavyotumia malighafi zinazopatikana hapa nchini, vinavyotoa ajira kwa watu wengi na vinavyozalisha bidhaa zenye soko hapa nchini na nje ya nchi. Katika kuhakikisha Watanzania wanashiriki kikamilifu kwenye uchumi wa viwanda, Serikali inahamasisha zaidi sekta binafsi ya hapa nchini pamoja na mashirika ya umma kujenga viwanda. Jitihada hizo zimewezesha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya NSSF, PPF, LAPF, GEPF, PSPF na NHIF kuanza kufufua, kuendeleza na kujenga viwanda vipya vipatavyo 27 katika maeneo mbalimbali nchini. Natoa pongezi kwa Bodi na Menejimenti ya Mifuko hiyo, kwa kuunga mkono jitihada za Serikali katika ujenzi wa viwanda nchini. Aidha, ninaendelea kuyasisitiza mashirika ya umma kuhakikisha kwamba mipango yao inaendana na utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa ambao dhima yake ni kujenga uchumi wa viwanda.

## Maliasili na Utalii

**29.** ***Mheshimiwa Spika,*** sekta ya utalii ni moja kati ya sekta muhimu sana katika uchumi wa nchi yetu. Kote ulimwenguni, mafanikio ya sekta ya utalii kwa kiasi kikubwa hutegemea miundombinu thabiti ya utalii, huduma bora na ulinzi na usalama. Ili kuendelea kunufaika na sekta hiyo, Serikali inaboresha miundombinu ya utalii, kupanua wigo wa vivutio vipya vya utalii na kuimarisha huduma ya usafiri wa anga. Vilevile, Serikali inafanya juhudi kubwa za kudhibiti ujangili na biashara haramu ya wanyamapori ambapo watuhumiwa **897** walitiwa mbaroni na kati yao watuhumiwa **282** wamefikishwa Mahakamani.

**30.** ***Mheshimiwa Spika***, idadi ya watalii imeongezeka kutoka 1,137,182 mwaka 2015 hadi watalii 1,284,279 mwaka 2016 sawa na ongezeko la asilimia 12 na kuliingizia Taifa Dola za Marekani bilioni 2. Juhudi zilizoanza za kuliimarisha shirika letu la ndege zinalenga pia kutoa mchango mkubwa kwenye sekta ya utalii kwa kusafirisha watalii wa ndani na kutoka nje ya nchi. Shabaha yetu ni kuongeza idadi ya watalii wanaokuja kutembelea nchi yetu na pia mapato yatokanayo na sekta hiyo. Nitumie fursa hii kuisihi sekta binafsi kuwekeza zaidi kwenye miundombinu muhimu ya sekta hii zikiwemo hoteli, kuboresha huduma na kubuni mbinu mpya za kuvutia watalii.

### *Kilimo*

**31.** ***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa mazao ya chakula kwa msimu wa mwaka 2015/2016 ikijumuisha mazao ya nafaka na yasiyo ya nafaka ulifikia **tani 16,172,841** ikilinganishwa na mahitaji ya kitaifa ya **tani 13,159,326**. Hivyo, katika kipindi hicho nchi ilikuwa na ziada ya **tani 3,013,515** za chakula. Katika msimu wa kilimo wa mwaka 2016/2017, hali ya upatikanaji wa mvua katika Mikoa inayopata mvua za vuli haikuwa ya kuridhisha na hivyo kusababisha ukame na upungufu wa mavuno katika baadhi ya maeneo. Tathmini ya awali imebainisha kwamba Halmashauri 55 zimeathirika na ukame.

**32.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kukabiliana na hali hiyo, Serikali inaendelea kuhamasisha sekta binafsi kununua mazao ya chakula kutoka katika maeneo yenye ziada na kuyauza katika maeneo yenye uhaba. Aidha, wafanyabiashara waliokuwa wamehifadhi nafaka katika maghala, walitakiwa kuzisambaza katika masoko ya ndani. Vilevile, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya walielekezwa kuwahamasisha na kuwaelekeza wakulima kupanda mbegu bora za mazao ya kilimo yanayostahimili ukame na yanayokomaa kwa muda mfupi kwa kipindi hiki cha mvua za masika. Ili kutoa msukumo katika kazi hiyo, kiasi cha **tani 1,969** za mbegu bora za mazao yanayostahimili ukame zilinunuliwa na Serikali na kusambazwa katika Halmashauri zilizobainika kuathirika na ukame. Pia, wakulima wanaendelea kuhamasishwa kuzitumia vizuri mvua zinazonyesha katika msimu huu wa masika kwa kupanda mazao hayo yanayostahimili ukame na kukomaa mapema.

**33.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kutambua umuhimu wa sekta ya kilimo katika uchumi wetu, Serikali imeweka dhamira ya kuongeza uzalishaji, tija na kukifanya kilimo kiwe cha kibiashara. Katika mwaka 2016/2017, Serikali ilifanikisha kupatikana kwa **tani 277,935** za mbolea na **tani 23,333** za mbegu bora. Aidha, hadi Februari 2017, Serikali ilitoa **tani 30,773** za mbolea ya ruzuku ya kukuzia na kupandia kupitia vituo vya mauzo ya mbolea vya Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC).

**34.** ***Mheshimiwa Spika***, moja ya ahadi ya Serikali kwa wakulima wetu ni kupunguza kodi, tozo na ada mbalimbali zinazochangia kupunguza faida kwa mkulima. Katika mwaka 2016/2017, Serikali ilifuta baadhi ya tozo za mazao ambazo ni kero kwa wakulima katika mazao ya pamba, chai na kahawa. Tozo zilizofutwa kwenye zao la pamba ni mchango wa Mwenge wa Shilingi 450,000 unaotolewa na kila kiwanda cha kuchambua Pamba na ada ya vikao vya Halmashauri za Wilaya ambayo ni shilingi 250,000. Kwa zao la chai, kodi ya moto na uokoaji imeondolewa na katika zao la kahawa, ada ya leseni ya kusindika kahawa ya Dola za Marekani 250 nayo pia imefutwa.

**35.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali pia imeboresha Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani kwa kuanzisha utaratibu wa wazi wa ununuzi wa mazao kupitia minada. Mathalani, katika msimu wa 2016/2017 kwenye zao la korosho, utaratibu huo umechangia kwa kiasi kikubwa kuongezeka kwa bei ya korosho kwa kilo kutoka shilingi 1,200 hadi shilingi 3,800, bei ambayo haijawahi kufikiwa katika historia ya zao la korosho nchini. Aidha, Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani na utaratibu wa minada umeongeza ushindani na kuvutia wafanyabiashara wa ndani na nje ya nchi hususan nchi ya Vietnam na nchi nyingine kuja wenyewe kununua korosho badala ya kutegemea soko la India pekee. Katika mwaka 2017/2018, Serikali itaendelea na uchambuzi wa kina wa kodi, tozo na ada zilizobaki katika sekta za kilimo, mifugo na uvuvi kwa lengo la kuziondoa au kuzipunguza ili kumwezesha mkulima, mvuvi na mfagaji anufaike zaidi na jasho lake na kuongeza mapato ya Halmashauri zetu. Kwa sasa, tunashughulikia zao la tumbaku kwa kupitia tozo zake na pia kubaini ubadhirifu unaoendelea kwenye ushirika huo.

**Mifugo**

**36.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeongeza uzalishaji wa mitamba na uhimilishaji wa mifugo ili kuhamasisha ufugaji wa kisasa na wenye tija. Mitamba 546 imezalishwa kutoka mashamba ya Serikali na mitamba 88 kutoka NARCO na kusambazwa kwa wafugaji wadogo. Aidha, Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji – NAIC Usa River, Arusha kimeimarishwa na kuongeza uzalishaji wa mbegu bora za ng'ombe hadi kufikia **dozi 10,494** ikilinganishwa na **dozi 8,000** zilizozalishwa na kusambazwa katika mwaka 2015/2016. Pia, ng'ombe waliohimilishwa wameongezeka kutoka **221,390** mwaka 2015/2016 hadi ng'ombe **457,557** mwaka 2016/2017.

**37.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2017/2018, Serikali itaendelea kuimarisha kituo chetu cha kuzalisha mitamba cha Kitulo wilayani Makete ili kukiongezea uwezo wake. Aidha, Serikali inatoa nafasi kwa mashamba binafsi kuzalisha mitamba zaidi kama mashamba ya ASAS kule Iringa ili

wafugaji wadogo wanufaike. Serikali pia itaendelea na zoezi la kutenga, kupima na kumilikisha wafugaji maeneo ya ufugaji na kujenga miundombinu ya mifugo kwa kuongeza idadi ya malambo na mabwawa katika mikoa. Hatua hizo zitasaidia kupunguza uzururaji wa mifugo na migogoro baina ya wafugaji na wakulima na hifadhi za misitu.

**Madini**

**38.** ***Mheshimiwa Spika***, Sekta ya madini ni muhimu kwa uchumi wetu. Serikali imetenga maeneo zaidi kwa ajili ya wachimbaji wadogo, kuweka utaratibu mzuri zaidi wa kutoa ruzuku pamoja na kuimarisha shughuli za ugani. Katika kipindi cha mwezi Julai 2016 hadi Februari 2017, Serikali imetenga maeneo 11 yenye ukubwa wa **hekta 38,567** kwa ajili ya wachimbaji madini wadogo. Maeneo hayo ni Msasa na Matabe mkoani Geita, Biharamulo na Kyerwa mkoani Kagera, Itigi mkoani Singida, D-Reef, Ibindi na Kapanda Mkoani Katavi, Ngapa mkoani Ruvuma, Kitowelo na Namungo mkoani Lindi pamoja na Nzega mkoani Tabora.

**39.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2017/2018, Serikali itaimarisha ukusanyaji wa Mapato ya Serikali yatokanayo na rasilimali za madini na kuimarisha ukaguzi wa shughuli za uzalishaji na biashara ya madini kwa migodi mikubwa, ya kati na midogo. Aidha, Serikali itaendeleza wachimbaji wadogo na wa kati wa madini pamoja na kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani wa madini hayo.

***Huduma za Kiuchumi***

***Ardhi***

**40.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa 2016/2017, Serikali iliahidi kuanza ujenzi wa Mfumo Unganishi wa Kuhifadhi Kumbukumbu za Ardhi. Ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kazi ya ujenzi wa mfumo huo awamu ya kwanza ilizinduliwa rasmi Agosti, 2016 na Mkandarasi tayari ameanza kazi. Sambamba na zoezi hilo, Serikali inakamilisha ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Taarifa za Ardhi. Kukamilika kwa mradi huo kutaboresha utendaji kazi, kuharakisha huduma za utoaji

hati miliki, kuongeza mapato ya Serikali na kuboresha utunzaji wa kumbukumbu za ardhi ambapo nyaraka zote za ardhi zitakuwa katika mfumo unganishi wa kielektroniki.

**41.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali pia iliidhinisha ramani za upimaji zenye jumla ya **viwanja 78,771** na **mashamba 239**. Aidha, Serikali imekamilisha upigaji wa picha za anga za Jiji la Dar es Salaam na inaendelea kutatua migogoro ya matumizi ya ardhi baina ya wakulima, wafugaji na hifadhi katika maeneo mbalimbali nchini.

**42.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2017/2018, Serikali itaendelea kujenga Mfumo Unganishi wa Kuhifadhi Kumbukumbu za Ardhi na kuboresha usimamizi wa sekta ya ardhi kwa kufanya mapitio ya Sera na Sheria za Ardhi na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu sera, sheria, kanuni na miongozo ya ardhi ili kudhibiti viashiria vya migogoro ya matumizi ya ardhi nchini. Ninatoa wito kwa Halmashauri zote nchini kuhakikisha kwamba zinashughulikia migogoro ya ardhi mapema na kuweka mazingira wezeshi ya upimaji wa ardhi katika Halmashauri zao.

**Umeme**

**43.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imechukua hatua thabiti za kuongeza uzalishaji, kuimarisha miundombinu ya usafirishaji na kuongeza kasi ya usambazaji umeme. Katika mwaka 2016, umeme uliozalishwa na kuingizwa katika Gridi ya Taifa uliongezeka na kufikia **Gigawatt hours (*GWh*) 7,092** ikilinganishwa na **Gigawatt hours (*GWh*) 6,227** zilizozalishwa mwaka 2015 sawa na ongezeko la **asilimia 13.9**. Vilevile, Serikali imepanua na kuboresha njia za usafirishaji umeme kwa kukamilisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovolti 400 na upanuzi wa vituo vya kupoza umeme kutoka Iringa – Dodoma – Singida – Shinyanga.

**44.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali iliendelea kutekeleza miradi ya kusambaza umeme vijijini kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) katika mikoa yote ya Tanzania Bara. Katika kipindi cha mwaka 2016/2017, Wakala ulikamilisha ujenzi wa vituo sita

(6) vya kuongeza nguvu ya umeme kutoka msongo wa kilovolti 11 hadi kilovolti 33 katika miji ya Kigoma, Kasulu, Kibondo, Ngara, Mbinga na Tunduru; ujenzi wa njia za kusambaza umeme zenye urefu wa **kilometa 17,740** za msongo wa **kilovolti 33**; ujenzi wa vituo vidogo vya kupoza na kusambaza umeme **4,100**; na ujenzi wa njia ndogo ya usambazaji umeme wenye urefu wa **kilometa 10,970**.

**45.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2017/2018, Serikali itaongeza uzalishaji, kuboresha miundombinu ya usafirishaji na kuongeza kasi ya usambazaji wa umeme nchini. Aidha, Serikali itaendelea na utekelezaji wa Mradi mkubwa wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta kutoka Kabaale (Uganda) hadi Tanga (Tanzania). Serikali pia, itawezesha uwekaji wa mtandao wa usambazaji wa gesi asilia kwenye viwanda na matumizi ya majumbani pamoja na uendelezaji wa mradi wa kusindika gesi asilia *(Liquefied Natural Gas - LNG)* mkoani Lindi.

**Barabara**

**46.** ***Mheshimiwa Spika,*** kuanzia mwezi Julai 2016 hadi Februari 2017, Serikali imejenga na kukarabati jumla ya **kilometa 430** za barabara kuu sawa na **asilimia 62** ya lengo la **kilometa 692.** Aidha, ujenzi wa barabara za juu kwenye makutano ya TAZARA unaendelea vizuri pamoja na maandalizi ya kuitisha zabuni za ujenzi wa Daraja Jipya la Selander na ujenzi wa Barabara ya Dar es Salaam – Chalinze kwa kiwango cha *Expressway*. Vilevile, ujenzi wa barabara za juu *(Interchange)* kwenye makutano ya Barabara ya Ubungo ulizinduliwa rasmi tarehe 20 Machi, 2017. Hizi ni hatua muhimu za kukabiliana na changamoto ya muda mrefu ya msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam ikiwa ni utekelezaji wa Ilani ya CCM ya mwaka 2015.

***Vivuko na Usafiri Majini***

**47.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2016/2017, Serikali ilipanga kujenga kivuko kipya cha Pangani (MV Pangani) na kukarabati kile cha Magogoni – Kigamboni. Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba hadi kufikia

Februari, 2017 ujenzi na ukarabati wa vivuko hivyo ulikuwa umekamilika. Aidha, ununuzi wa boti ndogo za abiria kwa ajili ya vivuko vya Kilambo – Namoto (Mtwara), Mkongo – Utete (Pwani), Pangani – Bweni (Tanga) na Msemo – Msangamkuu (Mtwara) utakamilika katika mwaka huu wa fedha. Kwa upande wa huduma za usafiri kwenye maziwa, Serikali inaendelea na ujenzi wa meli moja katika Ziwa Victoria, meli mbili katika Ziwa Nyasa zitakazofanya safari kati ya Kyela na Mbambabay pamoja na ukarabati wa meli za MV Victoria na Butiama (Ziwa Victoria) na MV Liemba (Ziwa Tanganyika).

## Bandari

**48.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inatekeleza Mpango wa Uboreshaji wa Bandari nchini kwa kufanya upanuzi na kuimarisha miundombinu ya Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara. Mifumo ya Ulinzi katika bandari hizo imeimarishwa na mashine za kisasa za kukagua mizigo zimefungwa. Kutokana na jitihada hizo, tumeanza kuona mwelekeo mzuri wa kuimarika ufanisi wa kiutendaji hususan katika Bandari ya Dar es Salaam. Tutaendelea kufanya maboresho zaidi ili Bandari ya Dar es Salaam iwe chaguo namba moja katika usafirishaji wa mizigo ndani na nje ya nchi yetu.

## Reli

**49.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, Serikali iliendelea kutekeleza miradi ya uboreshaji wa miundombinu ya Reli ya Kati ili kuongeza uwezo wa reli hiyo kutoa huduma za uchukuzi nchini na nchi jirani zinazotumia bandari zetu. Awamu ya kwanza ya ujenzi wa reli mpya ya kati kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza kwa kiwango cha *standard gauge* imeanza kutekelezwa kwa kusaini mkataba wa ujenzi wa kipande cha reli ya Dar es Salaam - Morogoro (**kilometa 205**). Taratibu za kuwapata makandarasi wa ujenzi wa reli kutoka Morogoro – Makutupora (**kilometa 336**), Makutupora- Tabora (**kilometa 294**), Tabora- Isaka (**kilometa 133**) na Isaka- Mwanza (**kilometa 254**) zinaendelea.

**Usafiri wa anga**

**50.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, Serikali imetekeleza kwa dhati azma ya kuimarisha Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL). Katika kipindi hicho, ndege mbili (2) aina ya Dash 8 – Q400 zenye uwezo wa kubeba abiria 76 kila moja zilinunuliwa na kuanza kutoa huduma mwezi Oktoba, 2016. Aidha, mwishoni mwa mwaka 2016, Serikali iliingia mkataba wa ununuzi wa ndege nyingine nne (4). Kati ya hizo, ndege moja ya aina ya Dash 8 - Q400 yenye uwezo wa kubeba abiria 76 inatarajiwa kuwasili mwezi Julai, 2017. Ndege nyingine mbili (2) aina ya CS300 zenye uwezo wa kubeba abiria 127 kila moja zinatarajiwa kuwasili mwezi Juni, 2018 na ndege kubwa moja ya masafa marefu aina ya Boeing 787 Dreamliner yenye uwezo wa kubeba abiria 262 inatarajiwa kuwasili mwezi Julai, 2018.

**51.** ***Mheshimiwa Spika,*** kukamilika kwa ununuzi wa ndege hizi kutaisaidia ATCL kuongeza safari za ndani na nje ya nchi na hivyo kuchangia katika jitihada za kuongeza watalii wanaokuja nchini kutembelea vivutio vyetu na kuimarisha usafiri wa anga hapa nchini. Aidha, ATCL imeanzisha safari za kuja Dodoma na hivyo kuongeza uhakika wa usafiri wakati huu ambapo Serikali inahamia Dodoma. Wigo wa upanuzi kwa viwanja vyote nchini unaendelea na sasa hivi tunakamilisha ujenzi wa viwanja vya ndege.

***Mawasiliano***

**52.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, baadhi ya kazi zilizofanyika kwenye sekta ya mawasiliano ni pamoja na kuendelea na ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano; kutekeleza Mradi wa Anuani za Makazi na Postikadi; na kuanzisha huduma ya kituo cha *Jamii Centre* kitakachorahisisha utoaji wa huduma muhimu katika kituo kimoja. Huduma hizo ni kulipa pensheni, ankara na huduma za kibenki. Aidha, Sekta ya Mawasiliano inatekeleza Programu ya Miundombinu ya Kikanda ambayo inahusisha Mradi wa Shule Mtandao (e-school), Mradi wa *Video Conference*

ambao unahusisha ununuzi, usimikaji na ufungaji wa vifaa vya TEHAMA katika Mikoa 26 na Taasisi za Serikali.

**53.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali pia inatekeleza mradi wa ujenzi wa miundombinu ya Mawasiliano Vijijini kwa kushirikiana na Kampuni ya Viettel ya Vietnam. Mradi huu unatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu 2015-2017. Viettel wamekwishafikisha miundombinu ya mtandao wa intaneti kwenye shule 417, Ofisi za Halmashauri za Wilaya 123, Hospitali za Wilaya 74, Vituo vya Polisi vya Wilaya 131 na Ofisi za Posta 68.

**54.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imekamilisha ujenzi wa kituo cha kuhifadhi taarifa na mifumo ya Serikali (*Government Data Centre*). Lengo ni kuongeza na kuimarisha usalama wa mifumo na taarifa unaoenda sambamba na uhakika wa upatikanaji wa taarifa za Serikali katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku. Pamoja na ujenzi wa vituo hivyo, matumizi ya TEHAMA yameongezeka na hivyo kuziwezesha taasisi za Serikali kutoa mchango mkubwa kwenye uboreshaji na utoaji wa huduma, kuongeza mapato na kuokoa gharama mbalimbali.

***Sekta ya Huduma za Jamii***
**Elimu**

**55.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kujenga uwezo wa walimu wa shule za msingi kwa kuwapa mafunzo hasa katika ufundishaji wa stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK). Jumla ya walimu 22,995 wa shule za msingi na walimu 519 wanaofundisha elimu maalum kwa wanafunzi wasioona na wenye ulemavu wa kusikia wamepewa mafunzo hayo. Lengo ni kuhakikisha kila mwanafunzi anayemaliza darasa la saba anajua kusoma na kuandika.

**56.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, Serikali iliendelea na mpango wa kutoa Elimumsingi bila malipo. Tangu utekelezaji wa mpango huo uanze, Serikali imekuwa ikipeleka wastani wa **Shilingi bilioni 18.77** kila mwezi, ambapo shule za msingi 16,088 na shule za sekondari 3,602

zimenufaika na mpango huo. Mpango huo umeleta manufaa kwa Watanzania wengi wa kipato cha chini na cha kati na umeongeza uandikishaji wa wanafunzi kwenye shule za Msingi na Sekondari. Kufuatia ongezeko hilo, tulijikuta tukilazimika kupambana na upungufu wa madawati, jambo ambalo liliifanya Serikali ianzishe kampeni maalum ya kumtoa sakafuni mtoto wa Kitanzania. Hivi sasa madawati sio tatizo tena kwenye shule nyingi nchini. Nitumie fursa hii kutoa pongezi kwa Watanzania wote walioshirikiana na Serikali katika kutatua changamoto ya upungufu wa madawati. Natoa pongezi kwa taasisi binafsi, watu binafsi na Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao yote.

**57.** ***Mheshimiwa Spika,*** uchumi wa viwanda kwa kiasi kikubwa unahitaji rasilimaliwatu yenye weledi hasa katika masomo ya hisabati na sayansi. Kama zilivyo nchi nyingine Barani Afrika, Tanzania inakabiliwa na changamoto ya wanafunzi kutopenda kusoma masomo ya hisabati na sayansi na hivyo kuchangia katika ufaulu duni kwenye masomo hayo. Ni dhahiri kuwa watoto wetu wasipoweka bidii katika masomo ya hisabati na sayansi viwanda vyetu vitalazimika kutegemea wataalamu kutoka nje ya nchi jambo litakalowafanya Watanzania kuwa watazamaji.

**58.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali imefanya juhudi za kuhamasisha wanafunzi kupenda masomo ya sayansi katika ngazi zote za shule. Aidha, Serikali inaendelea na Mpango wa Ujenzi wa Maabara katika shule za sekondari na vyuo vikuu pamoja na ununuzi wa vifaa. Katika mwaka 2016/2017, Serikali imenunua vifaa vya maabara kwa ajili ya **shule 1,625** za sekondari zilizokamilisha ujenzi wa maabara na usambazaji wa vifaa umeanza mwezi Machi, 2017 katika Mkoa wa Dar es Salaam na kazi hiyo inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Aprili, 2017 kwa nchi nzima. Aidha, Serikali inatoa mafunzo kwa **walimu 5,920** wanaosoma Stashahada maalum ya Sayansi, Hisabati na TEHAMA.

**59.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inakusudia kuimarisha ufundishaji wa masomo ya TEHAMA kwa shule za Sekondari.

Serikali inaendelea na mpango wake wa kujenga maabara za kompyuta ili wanafunzi wawe na uelewa wa TEHAMA. Utekelezaji wake utafanyika hatua kwa hatua.

**60.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imetoa vibali vya ajira kwa walimu wa **Hisabati na Sayansi 4,129**. Natoa wito kwa wazazi wenzangu kuhamasisha watoto wetu kupenda masomo ya Hisabati na Sayansi. Naagiza Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia kwa kushirikiana na TAMISEMI na wadau wengine waandae Mkakati Maalum wa kuhamasisha na kuwavutia wanafunzi kusoma masomo ya Hisabati na Sayansi. Mkakati huo pia uwezeshe upatikanaji wa walimu watakaofundisha masomo ya Hisabati na Sayansi katika shule za msingi na sekondari kwa kipindi kifupi bila kuathiri ubora wa ufundishaji.

**61.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea na ukarabati na ujenzi wa miundombinu katika Chuo Kikuu cha Mzumbe, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya, Chuo Kikuu Kishiriki cha Mkwawa na Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam. Ujenzi wa majengo 20 ya mabweni ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam yenye uwezo wa kuchukua **wanafunzi 3,840** umekamilika. Vilevile, Serikali inaimarisha miundombinu katika vyuo vya ufundi vya Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam, Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya na Chuo cha Ufundi Arusha kwa lengo la kuimarisha mafunzo ya Ufundi na Sayansi nchini. Katika mwaka 2017/2018, Serikali itaimarisha Vyuo vya Elimu ya Juu ili kuwezesha upatikanaji wa wataalam mahiri katika nyanja mbalimbali hususan Sayansi na Teknolojia.

## Maji

**62.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inatambua umuhimu wa kusogeza huduma za maji karibu zaidi na wananchi ili wasitumie muda mwingi kutafuta maji badala yake wajikite katika shughuli za uzalishaji mali. Ili kutimiza azma hiyo, Serikali inatekeleza miradi mbalimbali ya maji mijini na vijijini ikiwemo miradi ya vijiji 10 chini ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji. Kati ya mwezi Julai na Desemba 2016, miradi **90** ya

maji vijijini ilikamilika na kufanya idadi ya miradi iliyokamilika kufikia **1,301** kati ya miradi **1,810** iliyolengwa. Miradi **509** iliyobaki ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji na yote inatarajiwa kukamilika kabla ya mwezi Juni, 2017.

**63.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali itaendelea kutekeleza miradi ya maji vijijini katika Halmashauri zote nchini ukiwemo mradi wa maji wa Same – Mwanga – Korogwe unaolenga kuhudumia wananchi zaidi ya **456,000** katika **vijiji 38** kwenye miji ya Same, Mwanga na Korogwe Vijijini. Ili utoaji wa huduma ya maji uwe endelevu, wananchi waendelee kuelimishwa kuhusu umuhimu wa kutunza vyanzo vya maji, uvunaji wa maji ya mvua na matumizi bora ya maji. Nitumie fursa hii kuwakumbusha watendaji katika Halmashauri zote kusimamia kikamilifu sheria inayokataza shughuli za kibinadamu katika vyanzo vya maji.

**Afya**

**64.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuhamasisha wananchi kujikinga dhidi ya magonjwa ikiwemo kuhimiza lishe bora. Aidha, Serikali inaboresha upatikanaji wa huduma za afya nchini kwa kujenga vituo vya kutolea huduma za afya na tiba pamoja na kuboresha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba. Bajeti ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba imeongezeka kutoka **Shilingi bilioni 31 mwaka 2015/2016** hadi **Shilingi bilioni 251 mwaka 2016/2017**. Vilevile, Serikali imeanzisha utaratibu wa kununua dawa na vifaa tiba moja kwa moja kutoka kwa wazalishaji kwa lengo la kupunguza gharama. Serikali pia imeanzisha maduka ya dawa yanayouza bidhaa zake kwa bei nafuu kwa wananchi katika hospitali za mikoa ambapo hadi sasa maduka manane (8) yameanzishwa, na ujenzi wa maduka mengine katika mikoa iliyobakia unaendelea.

**65.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali pia inaimarisha huduma za Afya ya Uzazi na Mtoto nchini kwa kutekeleza Mpango Mkakati wa Kupunguza Vifo Vitokanavyo na Uzazi na Vifo vya Watoto wa mwaka 2016-2020. Lengo ni kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2020, asilimia 50 ya vituo vya Afya nchini

vinakuwa na uwezo wa kutoa huduma za dharura kwa matatizo ya uzazi ikiwemo upasuaji na huduma za watoto wachanga. Hadi sasa, vituo vya afya 159 vinatoa huduma za upasuaji ambapo vituo 106 ni vya Serikali. Vilevile, Serikali imeimarisha utoaji wa huduma za kinga na hivyo kuchangia kutokomezwa kwa ugonjwa wa Polio hapa nchini na hatimaye nchi yetu kuwa miongoni mwa nchi zilizopatiwa hati ya kutokomeza ugonjwa huo. Katika mwaka 2017/2018, Serikali itaendelea kuimarisha huduma za afya nchini kwa kuongeza kasi ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi na kuimarisha huduma za kinga ili kupunguza vifo vya watoto na akina mama pamoja na makundi mengine. Naomba nitoe wito kwa wote Watanzania wajiunge kwa wingi na Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) ili Serikali iweze kuwachangia kupitia mfumo huo.

**BUNGE**

**66.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa. Katika mwaka 2016/2017, Ofisi ya Bunge iliratibu na kusimamia shughuli za Mikutano mitatu ya Bunge ambapo **maswali 1,054** ya kawaida, nyongeza na ya papo kwa papo kwa Waziri Mkuu yaliulizwa. **Miswada kumi** (10) ya Sheria ilijadiliwa na kupitishwa na Bunge. Aidha, Bunge liliratibu na kusimamia shughuli za Mikutano ya Kamati za Kudumu za Bunge, kutoa huduma za *Hansard,* utafiti, utawala na kutoa mafunzo kwa Waheshimiwa Wabunge na Watumishi wa Ofisi ya Bunge. Ofisi ya Bunge pia ilisimamia kazi ya ukarabati wa jengo la Bunge pamoja na kuratibu ujenzi wa Ofisi za Waheshimiwa Wabunge. Katika mwaka 2017/2018, Serikali itaendelea kuliwezesha Bunge kutekeleza majukumu yake ya Kikatiba kama kawaida.

**MAHAKAMA**

**67.** ***Mheshimiwa Spika,*** utendaji wa mhimili wa Mahakama nchini umezidi kuimarika. Katika mwaka 2016/2017, Mahakama imesikiliza na kukamilisha **mashauri 279,331** kati ya **335,962** katika ngazi zote za Mahakama sawa na **asilimia**

**83.1** ya mashauri yote. Pamoja na kazi kubwa ya kusikiliza mashauri, Mahakama imesogeza huduma zake karibu na wananchi kwa kukamilisha ukarabati na ujenzi wa majengo ya Mahakama Kuu katika mikoa ya Tanga na Dar es Salaam. Pia, kazi za ukarabati wa Mahakama Kuu katika Mkoa wa Mbeya inaendelea na ujenzi wa Mahakama ya Wilaya na Mahakama ya Mwanzo Kibaha Mkoa wa Pwani umekamilika na kuzinduliwa.

**68.** ***Mheshimiwa Spika,*** ni matarajio yangu kwamba, katika mwaka 2017/2018, Mahakama itaendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi ili kupunguza mlundikano wa mashauri yaliyopo mahakamani. Hata hivyo, ili Mahakama ifanye kazi zake vizuri, shughuli za upelelezi wa kesi na uendeshaji wa mashtaka zinatakiwa pia kuimarishwa zaidi. Serikali itafanya kila liwezekanalo kuimarisha taasisi zote zinazohusika katika mlolongo wa utoaji haki ili wananchi wapate haki zao kwa wakati.

## MASUALA MTAMBUKA

### Mfumo wa Ufuatiliaji wa Shughuli za Serikali

**69.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, Serikali iliahidi kuanzisha Mfumo wa Wazi wa Kielektroniki wa kufuatilia uwajibikaji na utendaji Serikalini. Mfumo huo utasaidia kuongeza ufanisi katika uratibu wa shughuli za Serikali kwa kuwawezesha Viongozi kutoa maelekezo na kufuatilia utekelezaji wake. Aidha, Mfumo huo utasaidia ufuatiliaji wa utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Ahadi na Maagizo ya Mheshimiwa Rais na Mpango wa Taifa wa Maendeleo. Napenda kulialifu Bunge lako Tukufu kwamba, Mfumo huo umekamilika, kuzinduliwa rasmi na mafunzo kutolewa kwa wataalamu katika Wizara zote. Mfumo huo pamoja na mambo mengine utaongeza kasi ya utoaji taarifa za utekelezaji wa kazi za Serikali kwa wakati na pia kuongeza uwajibikaji kwa watumishi wa Umma. Wizara na Taasisi zote za Serikali zinatakiwa kuutumia Mfumo huo kikamilifu ili kurahisisha ufuatiliaji wa utekelezaji wa kazi za Serikali na kusaidia viongozi kutatua vikwazo pale vinapojitokeza.

## Vita dhidi ya Rushwa

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inapambana na rushwa kwa nguvu zake zote na haina mzaha wala uvumilivu na vitendo vya rushwa. Hatua zilizochukuliwa kupambana na rushwa tangu Serikali ya Awamu ya Tano ilipoingia madarakani Novemba, 2015 zimetambulika hata na Mashirika ya Kimataifa yanayojishughulisha na tafiti kuhusu masuala ya rushwa Duniani. Taarifa ya Shirika la *Transparency International* kwenye utafiti wake kuhusu mtazamo wa rushwa mwaka 2016 imeonesha kuwa viwango vya rushwa vinaendelea kupungua hapa nchini.

**71.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2016/2017, Serikali kupitia TAKUKURU imefanya uchunguzi wa majalada 306 ya tuhuma za rushwa na kupata kibali cha Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini kuendelea na mashtaka kwa majalada 104. Katika kipindi hicho, TAKUKURU iliendesha kesi 674 zikiwemo kesi mpya 182, ambapo katika kesi 97 watuhumiwa walipatikana na hatia na kuhukumiwa kifungo au kulipa faini. Kesi 407 zinaendelea kusikilizwa mahakamani. Kutokana na operesheni zilizofanywa na TAKUKURU, kiasi cha **Shilingi bilioni 9.75** ziliokolewa. Katika Mwaka 2017/2018, Serikali itaendelea na mapambano yake dhidi ya rushwa hususan katika eneo la ukusanyaji mapato ya Serikali, kudhibiti matumizi ya fedha za umma, malipo hewa, matumizi mabaya ya fedha za ushirika na kuimarisha ufuatiliaji na ukaguzi wa miradi ya maendeleo.

## Vita dhidi ya UKIMWI

**72.** ***Mheshimiwa Spika,*** mapambano dhidi ya UKIMWI yamekuwa yakitegemea kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa rasilimali fedha kutoka kwa Wadau wa Maendeleo. Ninapenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Mfuko wa Udhamini wa UKIMWI ulioanzishwa na Serikali miaka miwili iliyopita, ulizinduliwa tarehe 01 Desemba, 2016 ambapo kupitia harambee iliyofanyika kwa ajili ya kuchangia Mfuko

huo, shilingi milioni 347 zilipatikana kama ahadi. Vilevile, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 5.6 kwa ajili ya Mfuko wa UKIMWI.

**73.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea kutoa huduma kwa Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (WAVIU) ambapo hadi Desemba, 2016 WAVIU 839,574 sawa na asilimia 63 ya WAVIU wote, walikuwa wamepatiwa dawa. Juhudi zinaendelea kufanyika ili kuwahamasisha WAVIU kujitokeza na kuingia kwenye Mpango wa Tiba ya Kufubaza Athari za UKIMWI. Aidha, Serikali imekamilisha uandaaji wa miongozo minne ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI ikijumuisha Mpango Kazi wa Kinga, Mkakati wa Kondomu, Mkakati wa Uwekezaji na Mpango kazi wa jinsia.

**74.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali katika mwaka 2017/2018, itaimarisha uratibu wa afua za UKIMWI kwa wadau wote wa sekta ya umma na binafsi na kupitia mifumo ya uratibu iliyoanzishwa. Serikali kwa kushirikiana na wadau pia itazijengea uwezo Kamati zilizo katika ngazi ya jamii hususan vijiji na kata ili kufikia malengo ya kitaifa na kimataifa ya kupunguza na kumaliza UKIMWI ifikapo mwaka 2030 kwa kutumia mfumo ulio katika jamii. Vilevile, Serikali itakamilisha utafiti wa nne wa kubainisha viwango vya maambukizo ya UKIMWI nchini na kuboresha ushiriki wa sekta binafsi ili kuleta ufanisi katika kuchangia mwitikio wa Taifa dhidi ya UKIMWI.

### Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu

**75.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika 2016/2017, Serikali imeendelea kutoa huduma pamoja na kuongeza upatikanaji wa haki na fursa kwa watu wenye ulemavu. Katika kutimiza azma hiyo, Serikali imewaagiza Wakuu wa Mikoa kuhakikisha kuwa Kamati za Watu wenye Ulemavu zinaanzishwa katika ngazi za Mikoa, Wilaya, Mitaa na Vijiji. Aidha, Serikali imeanzisha kampeni za kupinga unyanyapaa na vitendo vya kikatili dhidi ya watu wenye ualbino katika mikoa ya Shinyanga, Mwanza, Geita, Simiyu, Kagera, Tabora, Kigoma, Mara, Mbeya, Katavi na Rukwa na kampeni hiyo itaendelea nchi nzima.

**76.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali pia inahakikisha kwamba watumiaji wa lugha ya alama wanapata haki ya kupata habari na vituo vyote vya televisheni vimeelekezwa kutumia wakalimani wa lugha ya alama. Napenda kuvikumbusha Vituo vya Televisheni kuweka wakalimani wa lugha katika vituo vyao. Katika mwaka 2017/2018, Serikali itaendelea kutoa huduma kwa watu wenye ulemavu ikiwa ni pamoja na kutoa vifaa saidizi kwa wanafunzi wenye ulemavu shuleni na vifaa vya kufundishia.

**Vita Dhidi ya Dawa za Kulevya**

**77.** ***Mheshimiwa spika,*** dawa za kulevya zinaathiri maisha ya vijana wetu wengi na hivyo kuzima ndoto za maisha yao na kupunguza nguvu kazi ya Taifa. Ili kupambana na janga hilo, katika mwaka 2016/2017, Bunge lako Tukufu lilifanya marekebisho ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Dawa za Kulevya Na. 5 ya Mwaka 2015. Marekebisho hayo yameipa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya nguvu ya kukamata, kupeleleza na kushitaki watuhumiwa wanaohusika na biashara ya dawa za kulevya. Aidha, hivi karibuni Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli amefanya uteuzi wa Watendaji Wakuu watakaosimamia Mamlaka hiyo.

**78.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Januari, 2017 watuhumiwa 11,303 walikamatwa kwa tuhuma za kujihusisha na uzalishaji, usambazaji, uuzaji na matumizi ya dawa za kulevya katika sehemu mbalimbali nchini. Kati ya watuhumiwa hao, watu 9,811, walikutwa na kesi za kujibu ambapo 9,174 wametiwa hatiani, 238 hawakukutwa na hatia na wengine 478 upelelezi wa kesi zao unaendelea. Pia alisema tangu Tume mpya iundwe Februari mwaka huu, jumla ya watuhumiwa 79 wametiwa mbaroni na uchunguzi wa kesi zao unaendelea. Ni imani yangu kuwa, Mamlaka ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya itaendeleza kwa kasi zaidi juhudi za kupambana na uingizaji, uzalishaji, usambazaji na matumizi ya dawa za kulevya hapa nchini. Watanzania wana imani kubwa na Mamlaka hii na ninaomba wote tuipe ushirikiano wakati wote kwani vita hii ni kubwa na ni ya Kitaifa!

Aidha, nawasihi wazazi wenzangu, tuwe karibu na vijana wetu na kufuatilia nyendo zao ili wasiingie kwenye mtego huu wa dawa za kulevya.

**Uratibu wa Maafa**

**79.** ***Mheshimiwa Spika*,** Serikali wakati wote inahakikisha kuwa nchi ipo katika hali ya utayari wa kukabiliana na maafa na pia kutoa misaada ya kibinadamu ikiwemo huduma za matibabu, ushauri wa kisaikolojia, na vifaa pale maafa yanapotokea. Serikali imejenga vituo vipya 20 vya upimaji wa hali ya hewa katika Halmashauri 11 za Tarime, Nyamagana, Muleba, Longido, Geita, Maswa, Kigoma, Sikonge, Kongwa, Serengeti, na Kahama. Kuwepo kwa vituo hivyo kutaongeza ufanisi katika upatikanaji wa taarifa za tahadhari hasa kwa majanga ya mafuriko na ukame.

**80.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia tetemeko la ardhi lililotokea katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa mwezi Septemba 2016, Serikali kwa kushirikiana na wadau imechukua hatua za kushughulikia athari zilizotokana na tetemeko hilo. Huduma za afya na tiba na za kibinadamu za chakula na malazi zilitolewa kwa walioathirika. Vilevile, Serikali ilirejesha hali ya miundombinu iliyobomoka, yakiwemo majengo ya Serikali na Taasisi za Umma 686, Kituo cha wazee Kilima pamoja na kutoa maturubai 6,237, mahema 367, mabati 7,300 na mifuko ya saruji 1,825 kwa walioathirika. Serikali inaendelea na ujenzi wa Shule za Ihungo, Nyakato na Omumwani pamoja na ukarabati wa Kituo cha afya Kabyaile Ishozi. Ninapenda kuwashukuru sana wananchi wote na wadau waliotoa michango yao kusaidia waathirika wa tetemeko la ardhi.

## HABARI NA MICHEZO

### Habari

**81.** ***Mheshimiwa Spika,*** Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria ya Huduma za Habari Na. 12 ya mwaka 2016 ambayo ni muhimu katika kuimarisha usimamizi na uwajibikaji katika Sekta ya Habari nchini. Kanuni za Sheria hiyo zimeandaliwa

na tayari zimeanza kutumika. Natoa wito kwa wadau wa sekta ya habari kuzingatia sheria na kanuni hizo ili kuimarisha weledi katika tasnia ya habari. Aidha, nashauri wadau wa habari kujikita zaidi katika kuandika na kutangaza habari za masuala ya maendeleo na uchumi ili kuwasaidia wananchi kutekeleza azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kujenga uchumi wa viwanda na kuboresha huduma za kijamii.

**Maendeleo ya Michezo**

**82.** ***Mheshimiwa Spika,*** tumeanza kuona dalili nzuri za kuimarika kwa shughuli za michezo hapa nchini. Mathalan, timu ya Mpira wa Miguu ya *Serengeti Boys* imefuzu kushiriki Mashindano ya Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa vijana wenye umri chini ya miaka 17 yatakayofanyika Gabon, Mei 2017. Napenda nimshukuru sana Makamu wa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan ambaye amewaaga na kuwakabidhi bendera ya Taifa tayari kwenda kushiriki vita hiyo. Nawaomba Watanzania wote tuungane pamoja kuiombea na kuiunga mkono timu yetu kwa michango ya hali na mali ili kuiwezesha kushiriki kikamilifu. Kwa upande wa riadha, Mtanzania mwenzetu Alphonce Simbu alipata medali katika mbio za marathon huko Mumbai nchini India. Aidha, mwezi Septemba 2016, Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu ya Wanawake Tanzania (Twiga Stars) iliweka historia ya kuwa timu ya kwanza kutwaa taji la CECAFA. Ninatoa pongezi kwa wale wote walioliletea Taifa sifa kupitia michezo. Naziombea dua ili ziweze kushiriki michuano ya kimataifa.

**83.** ***Mheshimiwa Spika,*** michezo ni sekta muhimu katika kuongeza ajira, kuimarisha afya, kukuza uchumi, kuimarisha umoja wa Kitaifa na kuitangaza nchi Kimataifa. Nchi nyingi zilizofanikiwa kimichezo ziliwekeza zaidi kujenga vipaji vya vijana katika michezo. Natoa wito kwa TFF ihakikishe kuwa vijana wa Timu ya Serengeti Boys wanawekewa Mpango Endelevu wa Kukuza Vipaji Vyao na kutunzwa vyema ili waweze kuiwakilisha nchi yetu katika mashindano mengine ya kimataifa. Aidha, vyama vingine vya michezo vitoe msukumo mkubwa kwenye kuwekeza zaidi kwa vijana wa shule za msingi na sekondari kwani hao ndio watakuwa

wawakilishi wetu katika miaka ijayo. Na mwaka huu, michezo ya shule za msingi na sekondari itarejea na kufanyika mkoani Mwanza kama ilivyotangazwa mwaka jana. Nazisihi wizara husika za TAMISEMI na Wizara ya Elimu zianze maandalizi mapema na kuandaa mpango huo na kutoa taarifa timu hizo ziweze kujiandaa na kushindana ili tupate wachezaji imara wa kushiriki michuano hiyo.

## ULINZI NA USALAMA

**84.** ***Mheshimiwa Spika***, hali ya ulinzi na usalama nchini ni shwari kutokana na kazi kubwa na nzuri inayofanywa na vikosi vyetu vya ulinzi na usalama katika kulinda mipaka ya nchi yetu. Serikali imeendelea kuimarisha Jeshi la Wananchi wa Tanzania kwa kulipatia zana na vifaa vya kivita na kukamilisha mradi mkubwa wa ujenzi wa nyumba 6,064 za makazi ya askari ulioanza mwaka 2013/2014. Kwa upande mwingine, Serikali kupitia Jeshi la Magereza inakamilisha ujenzi wa nyumba zilizojengwa kwa njia ya ubunifu katika baadhi ya Magereza ikiwemo ujenzi unaoendelea katika Gereza la Ukonga wa ghorofa 12 zenye uwezo wa kuishi askari na familia 320.

**85.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itaendelea kuimarisha usalama wa raia na mali zao kwa kufanya operesheni za kuzuia uhalifu nchini, kufanya upelelezi wa kesi kwa kasi ili kupunguza mlundikano wa kesi zilizopo mahakamani, na kusimamia sheria za barabarani ili kupunguza ajali zinazoleta madhara kwa wananchi. Aidha, Serikali itaendelea kutoa mafunzo kwa askari na maafisa wa jeshi ili kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi, kupambana na vitendo vya rushwa na kupambana na biashara ya dawa za kulevya.

## MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA

**86.** ***Mheshimiwa Spika,*** kudumisha uhusiano mzuri na mataifa mengine duniani pamoja na mashirika ya kimataifa ni moja kati ya Misingi ya Sera yetu ya Mambo ya Nje. Tumeendelea kuimarisha ujirani mwema baina yetu na nchi jirani, nchi marafiki pamoja na mashirika ya kikanda na

kimataifa, jitihada ambazo zimetuwezesha kuvutia mitaji mikubwa ya uwekezaji, utalii pamoja na kupanua fursa za kibiashara. Katika mwaka 2016/2017, Serikali imefungua Balozi mpya sita (6) katika nchi za Algeria, Israel, Korea Kusini, Sudan, Qatar na Uturuki. Balozi hizo zina kazi kubwa ya kuendeleza juhudi za kuitangaza Tanzania kama nchi yenye vivutio vingi vya utalii na rasilimali zinazoweza kutumika kuvuta uwekezaji kutoka mataifa hayo ikizingatiwa utulivu na amani iliyopo. Serikali itaendelea kulinda na kutetea maslahi ya Tanzania nje ya nchi na kuweka mikakati ya kunufaika na nafasi ya nchi yetu kihistoria. Hivyo, ninatoa wito kwa mabalozi wetu wote waendelee kuitangaza nchi yetu kama eneo mwafaka lenye fursa nyingi za utalii, uwekezaji na biashara.

**HITIMISHO**

**87.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kujenga uchumi wa viwanda tunahitaji nidhamu ya kazi, ubunifu, elimu na matumizi makubwa ya sayansi na teknolojia. Vilevile, tunahitaji kuimarisha sekta binafsi, miundombinu ya huduma za kiuchumi na jamii na kuondoa urasimu usio wa lazima. Nafarijika kwamba misingi tunayoendelea kujenga katika kutekeleza azma hiyo imeanza kuzaa matunda kama nilivyoeleza awali. Ili kufanya mafanikio hayo yawe endelevu, naomba nihitimishe hotuba yangu kwa kusisitiza mambo makuu yafuatayo:-

**(i)** **Mosi,** ustawi wa nchi yetu na mafanikio ya mipango yetu ya maendeleo vinategemea amani na utulivu. Hivyo, kila mmoja wetu aweke nadhiri ya kuendelea kuilinda na kuienzi amani ya nchi yetu ili mipango yetu iweze kufanikiwa. Tunalo jukumu la kuhimiza amani ili tufanye kazi zetu kwenye mazingira ya amani na utulivu.

**(ii)** **Pili,** jukumu la kujenga uchumi wa nchi yetu ni wajibu wa kila mwananchi. Njia pekee ya kuijenga nchi yetu ni kufanya kazi kwa bidii, kulipa kodi kwa hiari na kufichua wakwepa kodi wote na wala rushwa.

**(iii)** **Tatu,** ujenzi wa uchumi wa viwanda unahitaji wananchi wenye afya njema na maarifa ya kufanya kazi na ubunifu. Tujenge utamaduni wa kupima afya zetu na kufanya mazoezi ya viungo ili kuepuka magonjwa yasiyo ya kuambukiza ambayo yanapoteza nguvu kazi kubwa ya Taifa;

**(iv)** **Nne,** rasilimali tulizonazo ipo siku zitaisha. Hivyo ni wajibu wa kila mmoja wetu kuzitumia kwa uangalifu ili zitufae sisi na vizazi vijavyo. Tuepuke matumizi mabaya ya rasilimali zetu kama vile maji, madini na misitu ili zinufaishe kizazi hiki na vizazi vijavyo;

**(v)** **Tano**, tuongeze nidhamu na uwajibikaji katika kila jambo la maendeleo tunalolifanya na kuzingatia matumizi ya muda. Tamaduni na mila zinazohamasisha uvivu na uzembe ni lazima tuzipige vita kwa nguvu zetu zote; na

**(vi)** **Mwisho,** dawa za kulevya ni janga kubwa linaloitafuna kwa kasi nguvukazi ya nchi yetu. Tunahitaji ushiriki wa kila mmoja katika vita hii kwa kufichua mtandao wa wahusika wa dawa za kulevya. Ahadi yetu ni kuwapa ushirikiano na kuchukua hatua kali dhidi ya wote waliohusika.

**MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA ZA OFISI YA WAZIRI MKUU NA OFISI YA BUNGE KWA MWAKA 2017/2018**

**88.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2017/2018, Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi Bilioni Mia Moja Sabini na Moja; Milioni Mia Sita Sitini na Nne, na Hamsini na Tano Elfu (Sh.171,664,055,000)**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni Sabini na Nne, Milioni Mia Sita Arobaini na Tatu, na Mia Tatu Thelathini na Tisa Elfu (Sh.74,643,339,000)** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi Bilioni Tisini na Saba, Milioni Ishirini, na Mia Saba na Kumi na Sita Elfu (Sh.97,020,716,000)** ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.

Vilevile, ninaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi Bilioni Mia Moja Ishirini na Moja, Milioni Mia sita**

**Hamsini na Mbili na Mia Mbili Sitini na Mbili Elfu (Sh.121,652,262,000)** kwa ajili ya Mfuko wa Bunge. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni Mia Moja Kumi na Nne, Milioni Mia Nne Hamsini na Mbili, na Mia Mbili Sitini na Mbili Elfu (Sh.114,452,262,000)** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi Bilioni Saba na Milioni Mia Mbili (Sh.7,200,000,000)** ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.

**89. *Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaendelea, naomba nimkaribishe Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria na Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti asogee karibu. *(Makofi)*

Karibu sana Mheshimiwa.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA (K.n.y. MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupa afya, uzima na nafasi nyingine ya kukutana hapa Dodoma katika Mkutano huu wa Saba wa Bunge la Kumi na Moja.

Mheshimiwa Spika, pili kwa niaba ya Kamati yangu ninaomba kutoa pole kwako binafsi na kwa Wabunge wote kwa kuondokewa na Mbunge mwenzetu Dkt. Elly Marko Macha, Mbunge wa Viti Maalum - CHADEMA aliyefariki tarete 31 Machi, 2017 huko Uingereza. Kamati pia inatoa pole kwa ndugu wa marehemu kwa msiba huo mzito.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee naomba kutoa pongezi za dhati kwa Mjumbe wa Kamati hii Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi, Mbunge, ambaye ameteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri wa Katiba na Sheria. Tunamtakia utumishi uliotukuka katika dhamana hii aliyopewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati naomba kutoa pongezi za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wa

Bunge la Afrika Mashariki ambao wamechaguliwa kwenda kuiwakilisha Tanzania katika Bunge hilo. Tunawatakia utumishi mwema katika Bunge la Afrika Mashariki na tunatoa rai kwao wakasimamie maslahi mahsusi ya Tanzaia katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na maslahi mapana ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2016/2017, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 6 (2) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, kimeipa Kamati ya Katiba na Sheria jukumu la kusimamia shughuli za Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu. Aidha, Nyongeza ya Nane kifungu cha 7(1)(a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 inatoa mamlaka kwa Kamati zote za Kisekta kushughulikia bajeti za Wizara inazozisimamia. Jukumu hili la uchambuzi wa bajeti linaendana sambamba na jukumu la ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha unaoisha kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ilifanya ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, iliyotengewa na kupokea fedha katika mwaka wa fedha 2016/2017 kuanzia tarehe 22 hadi 24 Machi, 2017. Kamati pia ilifanya uchambuzi wa Bajeti za Wizara na taasisi inazozisimamia kuanzia tarehe 29 Machi hadi 2 Aprili, 2017 ikiwemo Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu ina Mafungu sita ya bajeti kama ifuatavyo:-

(i) Fungu 37 - Ofisi ya Waziri Mkuu;
(ii) Fungu 25 - Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu;
(iii) Fungu 65 - Kazi na Ajira;
(iv) Fungu 15 - Tume ya Usuluhishi na Uamuzi *(CMA);*
(v) Fungu 61 - Tume ya Taifa ya Uchaguzi *(NEC);* na
(vi) Fungu 27 - Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa Tanzania

Mheshimiwa Spika, taarifa hii inatoa maelezo kuhusu maeneo manne yafuatayo:-

Matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo, mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/2017, uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na maoni na ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili ni ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 98(1) inazitaka Kamati za Kisekta kutembelea na kukagua miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha unaoisha. Katika kutekeleza masharti ya Kanuni hiyo, Kamati ya Katiba na Sheria ilitembelea, kukagua na kupokea taarifa ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyosimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu tarehe 22 na 23 Machi 2017. Miradi hiyo ni ujenzi wa soko na barabara Pemba (Fungu 37); ujenzi wa soko na barabara Unguja (Fungu 37) na mfuko wa fidia kwa wafanyakazi (Fungu 65).

Mheshimiwa Spika, pamoja na miradi iliyoko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kamati ilitembelea na kukagua miradi mingine ya Maendeleo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais na Wizara ya Katiba na Sheria. Katika taarifa hii Kamati inajikita

kutoa matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kama ilivyotajwa hapo juu.

Mheshimiwa Spika; yatokanayo na ukaguzi wa miradi. Sehemu hii inatoa maelezo ya kina kuhusu miradi ya maendeleo iliyokaguliwa, gharama za hiyo miradi na namna miradi hiyo inavyosaidia wananchi wa sehemu husika kama ilivyoelezwa katika kila mradi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ufinyu wa muda wa kukagua miradi ya maendeleo Kamati ililazimika kujigawa katika makundi mawili; kundi la kwanza lilikwenda Pemba na kundi la Pili lilikwenda Unguja.

Mheshimiwa Spika, miradi ya ujenzi wa soko na barabara (Pemba). Kundi lililokwenda Pemba lilikagua Miradi ya Ujenzi wa Soko na Barabara zilizo chini ya mradi wa *Marketing Infrastructure, Value Addition and Rural Financing Support Programme (MIVARF)* ambao ni mradi wa kuboresha miundo mbinu ya masoko, uongezaji thamani mazao na huduma za fedha vijijini. Mradi huu unatekelezwa katika Wilaya zote za Unguja na Pemba na unafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika na Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Pemba mradi huu umegharamia ukarabati wa barabara 19 zenye urefu wa kilometa 80. Ukarabati wa barabara hizi umegharimu kiasi cha shilingi bilioni 6.4 za Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ufinyu wa muda, Kamati iliweza kukagua sehemu tu ya barabara hii yenye urefu wa kilometa 4.8 kutoka Chanjamjawiri mpaka Matale ambayo imegharimu shilingi 384,672,252. Barabara hii inatoa huduma kwa wazalishaji wa Shehia za Matale, Pujini, Dodo, Chonga na nyinginezo.

Kabla ya kukarabati barabara hii magari makubwa na madogo hayakuweza kupita kutokana na ubovu uliokuwepo na badala yake usafiri wa punda na mikokoteni

ulikua unatumika kusafirisha mazao na watu. Baada ya ukarabati wa barabara hii magari makubwa na madogo yameanza kutumia barabara hii kwa ajili ya usafirishaji wa mazao na hivyo kuongeza wigo wa masoko na faida kwa wazalishaji wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilitembelea mradi wa soko la Tibirinzi, Chake Chake Pemba ambalo limejengwa kwa fedha za *MIVARF*. Gharama ya ujenzi wa soko hili ni shilingi 972,000,000. Soko hili linahudumia Mkoa wote wa Kusini Pemba na ujenzi wa soko hili unatarajiwa kukamilika ifikapo Julai, 2017. Soko hili, kama mengine yanayojengwa litakuwa na huduma ya chumba cha baridi kwa ajili ya kuhifadhia na kuongeza thamani ya mazao ya mbogamboga, matunda na samaki. Aidha, soko hili la Tibirinzi litakuwa na mtambo wa barafu ambao utatumika kuzalisha barafu ambayo itatumika kuhifadhia samaki kwa ajili ya wavuvi na wachuuzi wa samaki.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilikagua ukarabati wa kituo cha ya uhifadhi na kupunguza upotevu wa mazao baada ya mavuno *(Post-Harvest Training Centre)* kilichoko Pujini, Wilaya ya Chake Chake Pemba, ambacho kitatumika kutoa mafunzo ya mbinu bora za usindikaji na uhifadhi wa mazao mbalimbali ya kilimo yanayolimwa na wakulima kwa ajili ya kupunguza upotevu na kuongeza thamani ya mazao hayo kwa lengo la kuongeza kipato. Aidha, kituo hiki kitahudumia wananchi wote wa Pemba ambao watakuwa wanapata mafunzo kwa awamu tofauti baada ya kukamilika kwake. Ukarabati wa Kituo cha mafunzo ya uhifadhi wa mazao wenye thamani ya shilingi 214,000,000 unalipiwa kwa 100% na Benki ya Maendeleo Afrika.

Mheshimiwa Spika, miradi ya ujenzi wa soko na barabara Unguja. Kundi la pili la Kamati lilikwenda Unguja kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo iliyojengwa kwa fedha za *MIVARF.* Miradi iliyokaguliwa kwa upande wa Unguja ni barabara ya Dongongwe- Mchangani, soko la Kinyasini, Unguja na barabara ya Chaani mpaka Donge.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Dongongwe - Mchangani yenye urefu wa kilometa nne ni moja kati ya barabara zilizofanyiwa ukarabati ili kuwasaidia wazalishaji na wasafirishaji wa mazao mchanganyiko yakiwemo muhogo, ndizi na matunda kwa wazalishaji wa Shehia za Mchangani na Ghana. Kabla ya ukarabati wa kiwango cha kifusi barabara hii ilikua ikitumika kusafirishia mazao kwa mikokoteni na baiskeli na wakati wa kiangazi tu. Mara baada ya ukarabati, barabara hii ilianza kutumiwa na idadi kubwa ya magari makubwa na madogo yanayobeba mizigo tofauti ikiwemo vifaa vya ujenzi (mawe/mchanga) pamoja na magari ya huduma za watalii. Barabara hii ni moja kati ya barabara zenye urefu wa kilometa 68 ambazo zimekarabatiwa Unguja kwa fedha za Mradi wa *MIVARF* wa thamani ya shilingi 3,100,000,000.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Chaani – Donge yenye urefu wa kilometa 6.7 ilipendekezwa kufanyiwa ukarabati mahsusi kwa ajili ya kuwasaidia wazalishaji wa mananasi eneo la ekari 3,200, kuongeza thamani katika mnyororo wake wa thamani *(value chain).* Jumla ya Shehia tano ambazo ni Dongwe Vijibweni, Donge Pwani, Chaani Kubwa, Chaani Masingini na Bandamaji zenye kaya 2,552 na wakazi 12,968 zinafaidika na uwepo wa barabara kwa matumizi ya kilimo na shughuli zingine za kiuchumi na kijamii. Aidha, maeneo inayopita barabara hii yanalimwa muhogo na mazao mengine.

Mheshimiwa Spika, soko la Kinyasini linahudumia Mkoa wote wa Kaskazini Unguja pamoja na baadhi ya wakazi wa Wilaya ya Kati iliyo kwenye Mkoa wa Kusini Unguja. Aidha, soko hili pia, linategemewa na sekta ya utalii kwa wamiliki wa mahoteli ukanda wa Kaskazini Mashariki ya kisiwa hiki. Kwa mujibu wa mkataba, mkandarasi anatakiwa kukabidhi soko hili pamoja na jengo la utawala ifikapo Julai, 2017. Gharama ya ujenzi wa soko hili ni shilingi 2,500,000,000.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi; tarehe 23 Machi, 2017 Kamati ilitembelea Mfuko wa Fidia kwa

Wafanyakazi na kupokea taarifa ya utekelezaji ya mfuko kwa nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2016/2017 (Julai - Desemba, 2016).

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi ni taasisi ya hifadhi ya jamii iliyoundwa kwa mujibu wa kifungu cha 5 cha Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi Sura ya 263 Marejeo ya mwaka 2015 ili kushughulikia masuala ya fidia kwa wafanyakazi waliopo katika sekta ya umma na binafsi Tanzania bara ambao wataumia, kuugua au kufariki kutokana na kazi wanazofanya kwa mujibu wa mikataba ya ajira zao.

Mheshimiwa Spika, maoni na mapendekezo ya Kamati kuhusu miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2016/2017; lengo la kufanya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo pamoja na mambo mengine ni kujiridhisha na uwepo wa miradi hiyo *(field inspection)* na matumizi sawia ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge katika utekelezaji wa miradi hiyo. Kamati imejiridhisha na uwepo wa miradi hiyo na baada ya kuilinganisha miradi hiyo na fedha iliyotumika katika kutekeleza, inaweza kuishauri vema Serikali katika jukumu lake la kuleta na kusimamia maendeleo katika nchi.

Mheshimiwa Spika, maoni na mapendekezo ya jumla kuhusu miradi ya maendeleo ni kuwa kwa miradi ya ujenzi wa barabara na masoko iliyoko pemba na unguja , kamati kwa sehemu kubwa imeridhishwa na maendeleo ya miradi hii na inatoa rai kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia miradi wa *MIVARF* kukamilisha kwa haraka miradi hii ili wananchi wengi wa maeneo hayo waweze kunufaika.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kwamba makandarasi wote waliopewa kazi ya ujenzi wa miradi hii ya barabara na masoko kwa upande wa Unguja na Pemba kukamilisha miradi hiyo ndani ya muda uliopangwa ili shughuli nyingine za kiuchumi zinazotegemea kukamilika kwa miradi hiyo ziendelee na ziweze kuwasaidia wananchi wengi katika uzalishaji na kuongeza kipato chao.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliona kwamba kuna haja kubwa ya kuhakikisha kwamba thamani ya fedha iliyotumika katika miradi hiyo inaonekana. Katika mradi wa ujenzi wa soko la Kinyasini, Unguja Kamati ilitilia shaka aina ya soko lililojengwa na kiwango cha fedha shilingi bilioni 2.9 kilichotajwa kutumika katika mradi huo. Kamati inatoa rai kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kujiridhisha na matumizi ya fedha hizo katika mradi huo na kufuatilia kama fedha iliyotengwa kwa ajili ya mradi huo ilitumika ipasavyo *(value for money).*

Mheshimiwa Spika, Kamati kwa ujumla inawashukuru sana wahisani wa mradi huu (Benki ya Maendeleo Afrika na Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo) kwa kutoa fedha za miradi hii. Kamati inatoa rai kwa Halmashauri na Mikoa yote inayohusika na utekelezaji wa miradi hii katika maeneo yao kutoa ushirikiano wa kutosha na kufuatilia kwa karibu usimamizi, utekelezaji na uendelevu *(sustainability)* wa miradi hii katika kuwasaidia wakulima na wananchi wa maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea taarifa ya utekelezaji ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi, Kamati ilitoa maoni yafuatayo:-

(i) Mfuko uweke mkazo zaidi katika ulipaji wa fidia kwa wafanyakazi jambo ambalo ndio lengo kuu la mfuko huo.

(ii) Elimu kuhusu mfuko iendelee kutolewa kwa wananchi, wadau wote ili waajiri na waajiriwa wengi waweze kufahamu sahihi usahihi wa mfuko huo.

(iii) Mfuko uchukue jitihada za kutosha kufanya kazi na sekta binafsi/isiyo rasmi ili kuongeza wigo wa watu wanaotumia huduma za mfuko na kutii matakwa ya sheria inayounda mfuko huo.

(iv) Mfuko uzingatie sera na miongozo ya uwekezaji wa fedha za mifuko *(investment policy and guidelines)* ili kuwekeza kwa faida na kulinda uimara wa kifedha wa

mifuko *(financial liquidity)* na kulinda usalama wa fedha za wanachama.

(v) Mfuko uchukue jitihada za kutosha kupambana na kudhibiti mianya yote ya rushwa hasa katika eneo la uwekezaji wa fedha za mifuko na uendeshaji wa mfuko kwa ujumla.

(vi) Mfuko uhakikishe una kanzidata *(database)* sahihi ya idadi ya waajiri Tanzania ili kuongeza wigo wa michango ya fidia kwa wafanyakazi.

(vii) Mfuko uendelee kusimamia vizuri utekelezaji wa sheria inayounda mfuko pamoja na kanuni zake.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu ni kuhusu uchambuzi wa taarifa; Ofisi ya Waziri Mkuu, kuhusu utekelezaji wa mpango wa Bajeti na uzingatiaji wa maoni ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea na kuchambua taarifa za utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2016/2017 na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kwa mujibu wa Kanuni ya 98(2) ya kanuni ya Kudumu za Bunge toleo la Januari 2016, tarehe 29 na 30 Machi, 2017.

Mheshimiwa Spika, naomba uchambuzi wa mapitio ya utekelezaji wa mpango wa bajeti wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na taarifa kuhusu ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka huo wa fedha uingie kwa rekodi rasmi za Bunge kama ilivyo katika taarifa ya Kamati iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako kuanzia ukurasa wa 12 mpaka wa 16.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti ya maendeleo. Katika mwaka wa fedha 2016/2017 Ofisi ya Waziri Mkuu (Fungu 37) ilitengewa jumla ya shilingi 159,174,011,629 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia

tarehe 28 Februari, 2017 jumla ya shilingi 70,484,634,086 sawa na asilimia 44 ya fedha iliyoidhinishwa ilipokelewa. Hali hii kwa kiasi kikubwa imechangiwa na kupungua kwa fedha za miradi ya maendeleo kutoka kwa wahisani.

Mheshimiwa Spika, kuna miradi ambayo ilitengewa fedha za maendeleo katika bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017, hadi kufikia 28 Februari, 2017 baadhi ya miradi hiyo haikupokea fedha yoyote ya ndani wala ya nje. Miradi hiyo ni kama Mradi Namba 6510 kuhusu uendelezaji wa Makao Makuu Dodoma *(CDA),* Mradi Namba 4945 - Mfuko wa Maendeleo ya Vijana na Mradi Namba 6577 - Mradi wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, mchanganuo wa uwiano wa bajeti iliyoidhinishwa mwezi Aprili, 2016 na upatikanaji wa fedha ya maendeleo unapatikana katika jedwali namba mbili lililomo katika taarifa ya Kamati, ukurasa wa 18.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi huu unaonyesha kuwa fedha nyingi za maendeleo zinategemea fedha ya nje hali ambayo inaleta utegemezi na ugumu katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha za nje. Hali hii inasababisha miradi mingi kutotekelezeka kwa wakati. Ni mapendekezo ya Kamati kuwa Serikali ijitahidi kupunguza utegemezi kwa kutenga fedha yake ya ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Aidha, uchambuzi unaonesha hata fedha ya ndani iliyoidhinishwa na Bunge haikuweza kutolewa kama ilivyokusudiwa kama inavyoonekana katika jedwali. Kwa mfano Mradi Namba 6510 kuhusu uendelezaji wa Makao Makuu Dodoma ulitengewa na kuidhinishiwa na Bunge kiasi cha shilingi 50,000,000, hadi kufikia Februari, 2017 hakuna fedha yoyote ilipokelewa. Hali hii inaweza ikawa imesababishwa na kupungua kwa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchambuzi wa Mpango na Makadirio na Mapato kwa Matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/2018; Kamati ilipokea na kuchambua Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zilizo chini yake kwa mwaka wa fedha 2016/2017 tarehe 29 na 30 Machi 2017.

Mpango huu wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/2018 umeandaliwa kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 – 2020. Mwongozo wa Mpango wa Bajeti uliotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango ambao umelenga utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/2017 - 2020/2021).

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa vipaumbele vya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Mpango wa Bajeti wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2017/2018 umeainisha maeneo 22 ya viapumbele yakiwemo:-

(i) Kujenga uwezo wa Serikali kukabiliana na maafa;

(ii) Kuratibu utekelezaji wa mpango wa utoaji wa shilingi 50,000,000 kwa kila Kijiji/Shehia;

(iii) Kuratibu utekelezaji wa mpango wa ushiriki wa Watanzania kwenye uwekezaji *(local content);*

(iv) Kuratibu shughuli za Bunge na kushughulikia kero na malalamiko ya wananchi;

(v) Kuratibu utekelezaji wa sera, sheria na mikakati ya kukuza ajira nchini na kuongeza nafasi za ajira za Watanzania nchi za nje;

(vi) Kuratibu na kusimamia uwezeshaji na maendeleo ya vijana;

(vii) Kusimamia, kuratibu na kutoa huduma kwa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliridhishwa na vipaumbele viliyowekwa na Ofisi ya Waziri Mkuu kwa sababu vinaendana na Mpango wa Taifa wa mwaka 2017/2018 na Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Kamati pia imejiridhisha

na vipaumbele hivi kwa sababu vinajumuisha maeneo yote ya msingi ambayo yapo katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na vipaumbele hivyo Kamati inatoa rai kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kuhakikisha kwamba vipaumbele vyake vinaakisi kauli mbiu ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuwa na Tanzania ya viwanda ili kuweza kutengeneza ajira kwa wananchi wengi na kuongeza fursa mbalimbali za biashara na mapato kwa nchi na wananchi.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nne na 4(1) ya Taarifa ya Kamati inahusu uchambuzi wa Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na Uchambuzi wa vipaumbele vya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Sehemu ya 4(2) ya Taarifa ya Kamati inaelezea uchambuzi wa makadirio ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na sehemu ya 3(4) inatoa Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Ninaomba sehemu hizi kuanzia ukurasa wa 20 mpaka 24 wa taarifa ya Kamati ziingie kwenye rekodi.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2017/2018; katika mwaka wa fedha 2017/2018, Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zilizo chini yake zimeombewa shilingi 83,565,372,763 kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo. Kati ya fedha hizi shilingi 22,000,000,000 ni fedha za ndani na shilingi 61,565,372,763 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, fedha iliyotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo katika mwaka wa fedha 2017/2018 ni pungufu kwa kiasi cha shilingi 56,902,247,237 ya fedha iliyotengwa katika mwaka wa fedha 2016/2017 kwa taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambazo zilitengewa kiasi shilingi 140,467,620,000. Kiasi hiki ni pungufu ya asilimia 40 ikilinganishwa na bajeti ya Maendeleo kwa Ofisi ya Waziri Mkuu iliyoidhinishwa na Bunge hili Tukufu mwezi Aprili, 2016.

Mheshimiwa Spika, mpango wa Ofisi ya Waziri Mkuu katika miradi ya maendeleo katika mwaka huu wa fedha inalenga katika maeneo nane:-

(i) Kuboresha mandhari na ujenzi wa miundombinu ya Makao Makuu Dodoma;

(ii) Kujenga uwezo wa Serikali kukabiliana na maafa;
(iii) Kuimarisha ushindani katika sekta binafsi;

(iv) Kuendelea kuwajengea uwezo wa kiuchumi vijana kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana.

Mheshimiwa Spika, kutokana na vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Ofisi ya Waziri Mkuu katika mwaka wa fedha 2017/2018, miradi hiyo iliyopewa kipaumbele ni kama ifuatavyo:-

(i) Mradi wa ujenzi wa makazi ya Waziri Mkuu;

(ii) Mradi wa programu ya kukuza uchumi nchini uliotengewa shilingi 15,000,000 fedha za ndani;

(iii) Mradi Namba 4944 wa kuimarisha ushindani katika sekta binafsi uliotengewa shilingi…

**SPIKA:** Mheshimiwa ni vizuri sasa ukaanza kumalizia malizia maana yake ikigonga tu.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA (K.n.y. MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa kutoa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu masuala mbalimbali yaliyojitokeza katika uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na taarifa za Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/2018 wa Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zake. Maoni na Ushauri wa Kamati pia umezingatia ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, Fungu 37 - Ofisi ya Waziri Mkuu; Kamati imeridhishwa kwa kiasi kikubwa na utekelezaji wa maoni na mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa na Kamati kwa Ofisi ya Waziri Mkuu katika mwaka wa fedha uliopita. Aidha Kamati inatoa wito kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kufanya rejea ya maagizo ambayo hayakutekelezwa kikamilifu kuyatekeleza kwa wakati na hususani upatikanaji wa Sheria ya Uanzishwaji wa Makao Makuu Dodoma, Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, masuala yote ya kukabiliana na maafa na maboresho mbalimbali ya sheria.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kwamba Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali ni ofisi muhimu katika kuendesha shughuli za Serikali lakini haijatengewa fedha ya maendeleo katika mwaka ujao wa fedha. Kamati inaishauri Ofisi ya Waziri Mkuu kuhakikisha kwamba ofisi hii inapewa kipaumbele katika Mpango wa Maendeleo wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kadri upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo mengine yaingie kwenye kumbukumbu za Kudumu za Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; napenda kukupongeza kwa kuendelea kuliongoza Bunge hili vema na kwa weledi wa hali ya juu. Nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha maoni ya Kamati kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria. Napenda nikupongeze pia kwa umahiri wako katika kasi ya kuliendesha Bunge hili katika kutekeleza kauli mbiu ya Hapa Kazi Tu na kuishauri vema Serikali kwa manufaa ya wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Napenda kumpongeza Naibu Spika, Mheshmiwa Dkt. Tulia Ackson (Mbunge) kwa weledi na umahiri wake katika kukusaidia kuongoza Bunge. Nichukue fursa hii ya kipekee kuwapongeza pia Wenyeviti wote wa Bunge, nichukue fursa hii pia kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, na nimtakie kazi njema ya kuliongoza taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa kwa kazi nzuri anayoifanya katika kusimamia utekelezaji wa bajeti na shughuli za Serikali Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Walemavu, Mheshimiwa Jenista Mhagama (Mbunge), Naibu Waziri, Mheshimiwa Antony Mavunde, Makatibu Wakuu Ndugu Erick Shitindi na Ndugu Hamisi Mwinyimkuu pamoja na wataalam wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ushirikiano waliotoa kwa Kamati wakati wa uchambuzi wa bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Napenda pia kutoa...

**SPIKA:** Malizia, omba pesa.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA KUDUMU YA KATIBA NA SHERIA):** Mheshimiwa Spika, mwisho, kabisa lakini si kwa umuhimu napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashililah kwa kuiwezesha Kamati kukamilisha kazi yake na watumishi wote wa Bunge.

**SPIKA**: Ndugu yangu naomba utii kiti kinavyokuagiza...

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA KUDUMU YA KATIBA NA SHERIA):** Mheshimiwa Spika, mwisho, baada ya maelekezo hayo...

**SPIKA:** Achana na habari za shukrani.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA KUDUMU YA KATIBA NA SHERIA):** Mheshimiwa Spika, baada ya maelekezo hayo naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge,

Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kama ilivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA WAZIRI MKUU KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupa afya, uzima na nafasi nyingine ya kukutana hapa Dodoma katika Mkutano huu wa Saba wa Bunge la 11.

**Mheshimiwa Spika**, Pili kwa niaba ya Kamati yangu ninaomba kutoa pole kwako binafsi na kwa Wabunge wote kwa kuondokewa na Mbunge mwenzetu Dkt. Elly Marko Macha, Mbunge wa Viti Maalumu (CHADEMA) aliyefariki tarehe 31 Machi, 2017 huko Uingereza. Kamati pia inatoa pole kwa ndugu wa marehemu kwa msiba huu mzito.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee naomba kutoa pongezi za dhati kwa Mjumbe wa Kamati hii, Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi, Mb, ambaye ameteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri wa Katiba na Sheria. Tunamtakia Utumishi Uliotukuka katika dhamana hii aliyopewa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Kamati naomba kutoa pongezi za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la

Afrika Mashariki ambao wamechaguliwa kwenda kuiwakilisha Tanzania katika Bunge hilo.Tunawatakia Utumishi mwema katika Bunge la Afrika Mashariki na tunatoa rai kwao wakasimamie maslahi ya Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na Maslahi mapana ya Jumuiya ya Afrika Mashariki Kimataifa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 6 (2) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, kimeipa Kamati ya Katiba na Sheria jukumu la kusimamia shughuli za Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu.

Aidha, Kanuni ya 7(1) (a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 inatoa Mamlaka kwa Kamati zote za Kisekta kushughulikia bajeti za Wizara inazozisimamia. Jukumu hili la Uchambuzi wa Bajeti linaendana sambamba na jukumu la ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha unaoisha kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ilifanya ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, iliyotengewa na kupokea fedha katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 kuanzia tarehe 22 hadi 24 Machi 2017. Kamati pia ilifanya uchambuzi wa Bajeti za Wizara na Taasisi inazozisimamia kuanzia tarehe 29 Machi hadi 02 Aprili 2017 ikiwemo Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake.

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu ina Mafungu 6 ya bajeti kama ifuatavyo;

i) Fungu 37 - Ofisi ya Waziri Mkuu
ii) Fungu 25 - Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu
iii) Fungu 65 - Kazi na Ajira
iv) Fungu 15 - Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA)
v) Fungu 61 - Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC)
vi) Fungu 27 - Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa Tanzania

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hii inatoa maelezo kuhusu maeneo Manne yafuatayo:-

i) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo;
ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017;
iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na;
iv) Maoni na Ushauri wa Kamati

**2.0 UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017**

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni ya 98 (1) inazitaka Kamati za Kisekta kutembelea na kukagua Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha unaoisha. Katika kutekeleza masharti ya Kanuni hiyo, Kamati ya Katiba na Sheria ilitembelea, kukagua na kupokea taarifa ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo inayosimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu tarehe 22 na 23 Machi 2017. Miradi hiyo ni:-

i. Mradi Na. 4494 – Ujenzi wa Soko na Barabara Pemba (Fungu 37)
ii. Mradi Na. 4494 - Ujenzi wa Soko na Barabara Unguja (Fungu 37)
iii. Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (Fungu 65)

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na miradi iliyoko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kamati ilitembelea na kukagua Miradi mingine

ya Maendeleo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais na Wizara ya Katiba na Sheria. Katika Taarifa hii Kamati inajikita kutoa matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kama ilivyotajwa hapo juu.

### 2.1 Yatokanayo na Ukaguzi wa Miradi

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii inatoa maelezo ya kina kuhusu Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa, gharama za hiyo miradi na namna miradi hiyo inavyosaidia Wananchi wa sehemu husika kama ilivyoelezwa katika kila mradi.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na ufinyu wa muda wa kukagua Miradi ya Maendeleo Kamati ililazimika kujigawa katika makundi mawili; kundi la kwanza lilikwenda Pemba na kundi la Pili lilikwenda Unguja.

### 2.2 Miradi ya Ujenzi wa Soko na Barabara (Pemba)

**Mheshimiwa Spika**, kundi lililokwenda Pemba lilikagua miradi ya Ujenzi wa Soko na Barabara zilizo chini ya Mradi wa Marketing Infrastructure, Value Addition and Rural Financing Support Programme (MIVARF) ambao ni mradi wa kuboresha Miundo Mbinu ya Masoko, Uongezaji Thamani Mazao na Huduma za Fedha Vijijini. Mradi huu unatekelezwa katika Wilaya zote za Unguja na Pemba na unafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD).

**Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa Pemba Mradi huu umegharamia Ukarabati wa Barabara 19 zenye urefu wa Km 80. Ukarabati wa Barabara hizi umegharimu kiasi cha Shilingi Bilioni 6.4 za Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na ufinyu wa muda, Kamati iliweza kukagua sehemu tu ya barabara hii yenye urefu wa Km 4.8 kutoka Chanjamjawiri mpaka Matale ambayo imegharimu **Shilingi Milioni Mia Tatu Themanini na Nne, Laki Sita na Sabini na Mbili, Mia Mbili na Hamsini na Mbili (384,672,252.24/=).** Barabara hii inatoa huduma kwa wazalishaji wa Shehia za Matale, Pujini, Dodo, Chonga na nyinginezo. Kabla ya kukarabatiwa barabara hii magari

makubwa na madogo hayakuweza kupita kutokana na ubovu uliokuwepo na badala yake usafiri wa Punda na Mikokoteni ulikua unatumika kusafirisha mazao na watu. Baada ya Ukarabati wa barabara hii magari makubwa na madogo yameanza kutumia barabara hii kwa ajili ya usafirishaji wa mazao na hivyo kuongeza wigo wa masoko na faida kwa wazalishaji wa maeneo hayo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilitembelea mradi wa Soko la Tibirinzi, Chake Chake Pemba ambalo limejengwa kwa fedha za MIVARF. Gharama ya ujenzi wa Soko hili ni **Shilingi Milioni Mia Tisa Sabini na Mbili (972,000,000/=).** Soko hili linahudumia Mkoa wote wa Kusini Pemba na ujenzi wa Soko hili unatarajiwa kukamilika ifikapo Julai, 2017. Soko hili kama mengine yanayojengwa litakuwa na huduma ya chumba cha baridi kwa ajili ya kuhifadhia na kuongeza thamani ya mazao ya mboga mboga, matunda na samaki. Aidha soko hili la Tibirinzi litakuwa na mtambo wa barafu ambao utatumika kuzalisha barafu ambayo itatumika kuhifadhia samaki kwa wavuvi na wachuuzi wa samaki.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilikagua ukarabati wa kituo cha ya uhifadhi na kupunguza upotevu wa mazao baada ya mavuno (Post-Harvest Training Centre) kilichoko Pujini, Wilaya ya Chake Chake, Pemba ambacho kitatumika kutoa mafunzo ya mbinu bora za usindikaji na uhifadhi wa mazao mbalimbali ya kilimo yanayolimwa na Wakulima kwa ajili ya kupunguza upotevu na kuongeza thamani ya mazao yao kwa lengo la kuongeza kipato. Aidha Kituo hiki kitahudumia Wananchi wote wa Pemba ambao watakuwa wanapata mafunzo kwa awamu tofauti baada ya kukamilika kwake. Ukarabati wa Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Mazao wenye Thamani ya **Shilingi Milioni Mia Mbili Kumi na Nne (214,000,000/=)** unalipiwa kwa asilimia Mia Moja (100%) na Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB).

### 2.3 Miradi ya Ujenzi wa Soko na Barabara Unguja

**Mheshimiwa Spika**, kundi la Pili la Kamati lilikwenda Unguja kukagua Miradi mbalimbali ya Maendeleo iliyojengwa kwa fedha za MIVARF. Miradi iliyokaguliwa kwa upande wa Unguja

ni; Barabara ya Dongongwe mpaka Mchangani, Soko la Kinyasini, Unguja na barabara ya Chaani mpaka Donge.

**Mheshimiwa Spika**, barabara ya Dongongwe - Mchangani yenye urefu wa Kilometa 4 ni moja kati ya barabara zilizofanyiwa ukarabati ili kuwasaidia wazalishaji na wasafirishaji wa mazao mchanganyiko yakiwemo muhogo, ndizi na matunda kwa wazalishaji wa Shehia za Mchangani na Ghana. Kabla ya ukarabati wa kiwango cha kifusi Barabara hii ilikua ikitumika kusafirishia mazao kwa Mikokoteni na Baiskeli na wakati wa kiangazi tu. Mara baada ya ukarabati, barabara hii ilianza kutumiwa na idadi kubwa ya magari makubwa na madogo yanayobeba mizigo tofauti ikiwemo vifaa vya ujenzi (mawe/mchanga) pamoja na magari ya huduma za Watalii. Barabara hii ni moja kati ya Barabara zenye urefu wa Km 68 ambazo zimekarabatiwa Unguja kwa fedha za Mradi wa MIVARF kwa Thamani ya **Shilingi Bilioni Tatu na Milioni Mia Moja (3,100,000,000/=).**

**Mheshimiwa Spika**, Barabara ya Chaani-Donge yenye urefu wa Kilomita 6.7 ilipendekezwa kufanyiwa ukarabati mahsusi kwa ajili ya kuwasaidia wazalishaji wa mananasi eneo la ekari 3,200 kuongeza Thamani katika mnyororo wake wa thamani (Value Chain). Jumla ya Shehia tano ambazo ni Dongwe Vijibweni, Donge Pwani, Chaani Kubwa, Chaani Masingini na Bandamaji zenye kaya 2,552 na Wakazi 12,968 zinafaidika na uwepo wa barabara kwa matumizi ya kilimo na shughuli nyingine za Kiuchumi na Kijamii. Aidha, maeneo inayopita barabara hii yanalimwa muhogo na mazao mengine.

**Mheshimiwa Spika**, Soko la Kinyasini linahudumia Mkoa wote wa Kaskazini Unguja pamoja na baadhi ya wakazi wa Wilaya ya Kati iliyo kwenye Mkoa wa Kusini Unguja. Aidha soko hili pia, linategemewa na Sekta ya Utalii kwa wamiliki wa mahoteli Ukanda wa Kaskazini Mashariki ya kisiwa hiki. Kwa mujibu wa Mkataba Mkandarasi anatakiwa kulikabidhi Soko hili pamoja na jengo la utawala ifikapo Julai 2017. Gharama ya ujenzi wa Soko hili ni **Shilingi Bilioni Mbili na Milioni Mia Tano (2,500,000,000/=)**.

### 2.4 Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi ( WCF)

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 23 Machi 2017 Kamati ilitembelea Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi na kupokea Taarifa ya Utekelezaji ya Mfuko kwa Nusu ya Kwanza ya Mwaka wa Fedha 2016/2017 (Julai -Desemba, 2016).

**Mheshimiwa Spika**, Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) ni Taasisi ya Hifadhi ya Jamii iliyoundwa kwa mujibu wa Kifungu cha 5 cha Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi Sura ya 263 marejeo ya Mwaka 2015 ili kushughulikia masuala ya Fidia kwa Wafanyakazi waliopo katika Sekta ya Umma na Binafsi Tanzania Bara ambao wataumia, kuugua au kufariki kutokana na kazi wanazofanya kwa mujibu wa Mikataba ya Ajira zao.

### 2.5 Maoni na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2016/ 2017

**Mheshimiwa Spika**, lengo la kufanya ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo, pamoja na mambo mengine, ni kujiridhisha na uwepo wa miradi hiyo (Field inspection) na matumizi sawia ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge katika utekelezaji wa miradi hiyo. Kamati inapojiridhisha na uwepo wa miradi hii; na baada ya kulinganisha miradi hiyo na fedha iliyotumika katika kuitekeleza, inaweza kuishauri vema Serikali katika jukumu lake la kuleta na kusimamia maendeleo katika nchi.

### 2.6 Maoni na Mapendekezo ya Jumla Kuhusu Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** kwa Miradi ya Ujenzi wa Barabara na Masoko iliyoko Pemba na Unguja , Kamati kwa sehemu kubwa imeridhishwa na maendeleo ya miradi hii na inatoa rai kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Mradi wa MIVARF kukamilisha kwa haraka miradi hii ili Wananchi wengi wa maeneo husika waweze kufaidika.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba Makandarasi wote waliopewa kazi ya ujenzi wa

miradi hii ya Barabara na Masoko kwa upande wa Unguja na Pemba kukamilisha miradi hiyo ndani ya muda uliopangwa ili shughuli nyingine za Kiuchumi zinazotegemea kukamilika kwa miradi hiyo ziendelee na ziweze kuwasaidia Wananchi wengi katika uzalishaji na kuongeza kipato chao.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati iliona kwamba kuna haja kubwa ya kuhakikisha kwamba Thamani ya fedha iliyotumika katika miradi hiyo inaonekana. Katika mradi wa ujenzi wa Soko la Kinyasini Unguja Kamati ilitilia shaka aina ya Soko lililojengwa na kiwango cha fedha (**Bilioni Mbili Milioni MiaTisa)** kilichotajwa kutumika katika mradi huo. Kamati inatoa rai kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kujiridhisha na matumizi ya fedha hizo katika mradi huo na kufuatilia kama fedha iliyotengwa kwa ajili ya mradi huo ilitumika ipasavyo. (Value for money).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati kwa ujumla inawashukuru sana Wahisani wa mradi huu, Benki ya Maendeleo Afrika na Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo kwa kutoa fedha za miradi hii. Kamati inatoa rai kwa Halmashauri na Mikoa yote inayohusika na utekelezaji wa miradi hii katika maeneo yao kutoa ushirikiano wa kutosha na kufuatilia kwa karibu usimamizi, utekelezaji na uendelevu (Sustainability) wa miradi hii katika kuwasaidia Wakulima na Wananchi wa maeneo husika.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kupokea taarifa ya Utekelezaji ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi, Kamati ilitoa maoni yafuatayo:-

- Mfuko uweke mkazo zaidi katika ulipaji wa Fidia kwa Wafanyakazi jambo ambalo ndio lengo kuu la Mfuko (Core Objective);

- Elimu kuhusu Mfuko iendelee kutolewa kwa Wananchi na Wadau wote ili Waajiri na Waajiriwa wengi wawe na ufahamu sahihi kuhusu Mfuko;

- Mfuko uchukue jitihada za kutosha kufanya kazi na Sekta Binafsi/isiyo rasmi ili kuongeza wigo wa watu wanaotumia huduma za Mfuko na kutii matakwa ya Sheria inayounda Mfuko;

- Mfuko uzingatie Sera au Miongozo ya Uwekezaji wa fedha za Mifuko (Investment Policies/Guidelines) ili kuwekeza kwa faida na kulinda uimara wa kifedha wa Mfuko (Financial Liquidity) na kulinda usalama wa fedha za Wanachama;

- Mfuko uchukue jitihada za kutosha kupambana na kudhibiti mianya yote ya rushwa hasa katika eneo la uwekezaji wa fedha za Mfuko na uendeshaji wa Mfuko kwa ujumla;
- Mfuko uhakikishe una ''Data Base - Kanzi Data'' sahihi ya idadi ya Waajiri Tanzania ili kuongeza wigo wa michango ya Fidia kwa Wafanyakazi;

- Mfuko uendelee kusimamia vizuri utekelezaji wa Sheria inayounda Mfuko pamoja na Kanuni zake.

## 3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA OFISI YA WAZIRI MKUU KUHUSU UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa fedha 2017/2018, kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016 tarehe 29 na 30 Machi, 2017. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuhusu uchambuzi huo kama ifuatavyo:-

### 3.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi uliofanywa na Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 ulitazama

mlinganisho wa kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge Aprili 2016 na kiwango ambacho kimepokelewa hadi Machi 2017 katika Robo ya Tatu ya Mwaka huu wa fedha 2016/2017. Uchambuzi huu pia ulitazama kiasi cha fedha kilichoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 na kiasi cha Fedha kilichopokelewa katika Miradi ya Maendeleo hadi kufikia Mwezi Machi 2017. Lengo la kufanya tathmini ya namna hii ni kufahamu Mwelekeo wa Mpango wa Bajeti ya Mapato na Matumizi ya Serikali katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 ili kujua vipaumbele vya kibajeti katika mwaka wa fedha ujao.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi uliofanywa na Kamati ulitazama pia eneo la ukusanyaji wa Maduhuli kwa kulinganisha kiasi kilichokusanywa hadi Machi 2017 na lengo la ukusanyaji lililowekwa wakati wa kupitisha bajeti Mwezi Aprili 2016. Lengo la uchambuzi wa namna hii ni kufahamu uwezo wa Serikali katika kukusanya Maduhuli. Kamati ilitumia njia mbalimbali katika uchambuzi wake kama kutazama hali halisi ya kila Taasisi, kujiridhisha na taarifa mbalimbali zilizowahi kuwasilishwa kwenye Kamati na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu kwenye Kamati.

### 3.2 Uchambuzi wa Taarifa Kuhusu Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 Bunge liliidhinisha Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli yenye jumla ya **Shilingi Bilioni Thelathini na Nane, Milioni Hamsini na Moja, Laki Saba na Tatu Elfu (38,051,703,000/=).** Hadi kufikia 28 Februari , 2017 kiasi cha Maduhuli kilichokusanywa na Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake ni **Shilingi Bilioni Ishirini , Milioni Mia sita Arobaini na Tatu, Laki Tisa Sabini na Nane MiaTano Sabini na Saba (20,643,978,577)** sawa na asilimia 54 ya lengo lililokusudiwa. Kamati imegundua kwamba ukusanyaji wa Maduhuli umepungua katika mwaka huu wa fedha ukilinganisha na Maduhuli yaliyokusanywa na

Serikali mpaka kufikia Machi 2016 wakati wa utekelezaji wa bajeti ya Mwaka wa Fedha 2015/2016 ambapo lengo la ukusanyaji Maduhuli lilifikiwa kwa zaidi ya asilimia 100.

**3.3 Upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida kutoka Hazina**

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 Mafungu yanayosimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Taasisi zilizo chini yake yalitengewa **Shilingi Bilioni Sitini na Nne, Milioni Mia Sita,Laki Tano Hamsini na Nne Elfu, Mia Tisa Arobaini na Nane (64,600,554,948 /=)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Februari 2017 Taasisi hizo zilipokea **Shilingi Bilioni Thelathini na Saba,Milioni Mia Tano Thelathini na Sita, Laki Nne Elfu Tisa na Thelathini na Tisa (37,536,409,039)** sawa na asilimia 58 ya fedha iliyoidhinishwa. **Uchambuzi wa uwiano wa bajeti iliyoidhinishwa na upatikanaji wa fedha ya Matumizi ya Kawaida hadi kufikia Februari 28, 2017 umeonyeshwa katika jedwali Na. 1**

**JEDWALI NA. 1**

| NA. | FUNGU | BAJETI ILIYOIDHINISHWA | FEDHA ILIYOPATIKANA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 37-OFisi ya Waziri Mkuu | 23,857,728,000/= | 12,709,618,127/= | 53% |
| 2 | 25- Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu | 4,034,253,000/= | 2,966,702,626.2/= | 74.5% |
| 3 | 65 – Kazi, Ajira ,Vijana na Wenye Ulemavu | 11,561,196,000/= | 7,236,597,069/= | 63% |
| 4 | 27- Msajili wa Vyama vya Siasa | 19,624,351,948.2/= | 11,141,142,633/= | 57% |
| 5 | 15-Tume ya Usuluhishi na Uamuzi | 2,435,301,000/= | 1,415,295,800/= | 58.11% |
| 6 | 61- Tume ya Taifa ya Uchaguzi | 3,117,626,000/= | 2,067,051,784/= | 66% |

Uchambuzi huu unaonyesha kuwa kumekuwa na upungufu wa upatikanaji wa fedha kwa kila Fungu. Hali hii inaweza ikawa imesababishwa na Mipango isiyowiana na Matumizi halisi au ikawa imesababishwa na Serikali kuwa na makusanyo kidogo. Kamati inashauri Serikali kupanga bajeti kwa kuzingatia mapato ya Serikali na mahitaji halisi ya Taasisi husika.

### 3.4 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 Ofisi ya Waziri Mkuu (Fungu 37) ilitengewa jumla ya **Shilingi Bilioni Mia Moja Hamsini na Tisa, Milioni Mia Moja Sabini na Nne, Elfu Kumi na Moja, Mia Sita Ishirini na Tisa (159,174,011,629/=)** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Februari 28, 2017 jumla ya **Shilingi Bilioni Sabini, Milioni Mia Nne Themanini na Nne, Laki Sita Thelathini na Nne Elfu na Thelathini na Sita (70,484,634,036/=)** sawa na asilimia 44 ya fedha iliyoidhinishwa ilipokelewa. Hali hii kwa kiasi kikubwa imechangiwa na kupungua kwa fedha za Miradi ya Maendeleo kutoka kwa Wahisani.

**Mheshimiwa Spika**, kuna miradi ambayo ilitengewa fedha za Maendeleo katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2016/2017, hadi kufikia Februari 28, 2017 baadhi ya miradi hiyo haikupokea fedha yoyote ya ndani wala ya nje. Miradi hiyo ni kama Mradi Na. 6510 kuhusu Uendelezaji wa Makao Makuu Dodoma (CDA), Mradi Na. 4945 Mfuko wa Maendeleo ya Vijana na Mradi Na. 6577 Mradi wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

**Uchambuzi wa uwiano wa bajeti iliyoidhinishwa na upatikanaji wa fedha ya Maendeleo hadi Februari 2017 umeonyeshwa katika jedwali Na. 2**
**JEDWALI NA. 2**

| NA | MRADI | BAJETI ILIYOIDHINISHWA/SHS | | FEDHA ILIYOPATIKANA | | Asilimia ya Fedha Iliyopokelewa | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | NDANI | NJE | NDANI | NJE | NDANI | NJE |
| 1. | Mradi NA. 4494.MIVARF | 50,000,000/= | 99,769,951,000/= | 0 | 38,462,065,529/= | 0 | 38.5% |
| 2. | NA. 6351 Ujenzi Ofisi ya Waziri Mkuu | 4,500,000,000/= | | 4,467,949,414/= | | 99.28% | |
| 3. | Na.5306 Mraddi wa kuimarisha taarifa na mabaddiliko ya tabia nchi na mifumo ya tahadhali | 0 | 1,929,852,000/= | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 4 | Na. 6575 mradi wa kujianndaa na kukabidhi maafa | 0 | 244,970,000/= | 0 | 153,300,000/= | | 62.5% |
| 5. | Na. 4937 kujenga uwezo wa mitambo ya uchapishaji | 150,000,000/= | | 29,644,000/= | | 19.76% | |

**Uchambuzi wa uwiano wa bajeti iliyoidhinishwa na upatikanaji wa fedha ya Maendeleo hadi Februari 2017 umeoneshwa katika jedwali Na. 2**

Uchambuzi huu unaonyesha kuwa fedha nyingi za Maendeleo zinategemea fedha ya nje hali ambayo inaleta utegemezi na ugumu katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayotegemea fedha za nje. Hali hii inasababisha miradi mingi kutotekelezeka kwa wakati. Ni mapendekezo ya Kamati kuwa Serikali ijitahidi kupunguza utegemezi kwa kutenga fedha yake ya ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Aidha uchambuzi unaonyesha hata fedha ya ndani iliyoidhinshwa na Bunge haikuweza kutolewa kama ilivyokusudiwa kama inavyoonekana katika jedwali. Kwa mfano Mradi Na. 6510 kuhusu uendelezaji wa Makao Makuu Dodoma ulitengewa na kuidhinishiwa na Bunge kiasi cha Shilingi Milion Hamsini (50,000,000) hadi kufikia Februari 2017 hakuna fedha yoyote ilipokelewa. Hali hii inaweza ikawa imesababishwa na kupungua kwa mapato ya Serikali . Kamati inashauri kuwa ni vema Mipango ya Serikali ikaendana na utekelezaji.

## 4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kuchambua Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 tarehe 29 na 30 Machi 2017. Mpango huu wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 umeandaliwa kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 - 2020, Mwongozo wa Mpango wa Bajeti uliotolewa na Wizara ya Fedha na Mpango ambao umelenga utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17-2020/2021).

### 4.1 Uchambuzi wa Vipaumbele vya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Bajeti wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 umeainisha maeneo 22 ya viapumbele yakiwemo;

i) Kujenga uwezo wa Serikali kukabiliana na Maafa;

ii) Kuratibu Utekelezaji wa Mpango wa Utoaji wa Shilingi Milioni Hamsini (50,000,000) kwa kila Kijiji/Shehia;

iii) Kuratibu Utekelezaji wa Mpango wa Ushiriki wa Watanzania kwenye Uwekezaji (Local Content);

iv) Kuratibu Shughuli za Bunge na kushughulikia kero na malalamiko ya Wananchi;

v) Kuratibu Utekelezaji wa Sera, Sheria na Mikakati ya Kukuza Ajira nchini na kuongeza nafasi za ajira za Watanzania nchi za nje

vi) Kuratibu na kusimamia Uwezeshaji na Maendeleo ya Vijana

vii) Kusimamia, Kuratibu na kutoa huduma kwa Watu wenye Ulemavu

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliridhishwa na Vipaumbele viliyowekwa na Ofisi ya Waziri Mkuu kwa sababu vinaendana na Mpango wa Taifa wa Mwaka 2017/2018 na Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/2017-2020/2021). Kamati pia imeridhika na vipaumbele hivi kwa sababu vinajumuisha maeneo yote ya msingi ambayo yapo katika

Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na vipaumbele hivyo Kamati inatoa rai kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kuhakikisha kwamba vipaumbele vyake vinaakisi Kauli Mbiu ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuwa na Tanzania yenye Viwanda ili kuweza kutengeneza Ajira kwa Wananchi wengi na kuongeza fursa mbalimbali za biashara na mapato kwa nchi na Wananchi.

### 4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Ofisi ya Waziri Mkuu inatarajia kukusanya kiasi cha **Shilingi Bilioni Thelathini na Saba, Milioni Mia Tano Hamsini na Nne, Mia Tisa Tisini na Nane na Mia Moja (37,554,998,100/=).** Maduhuli haya yatakusanywa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Fungu 37), Tume ya Taifa ya Uchaguzi (Fungu 61) na Fungu 65 (Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu). Sehemu kubwa ya Makadirio ya Maduhuli haya yatatokana na shughuli za Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali katika kuchapa Nyaraka mbalimbali za Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, pamoja na Nyaraka za matukio maalumu. Sehemu nyingine inayotegemewa kutoa Maduhuli zaidi ni Fungu 65 ambalo linahusisha Taasisi mbalimbali zilizo katika Sekta ya Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu.

**Mheshimiwa Spika**, kiasi cha Maduhuli kinachotegemewa kukusanywa kutoka Fungu 65 ni **Shilingi Bilioni Thelathini na Tano, Milioni Ishirini na Tisa, Laki Sita Elfu Tano na Mia Moja. (35,029,605,100).**
Kiasi hicho ni pungufu ya lengo la Mwaka 2016/2017 kwa kiasi cha **Shilingi Bilioni Tatu,Milioni Ishirini na Moja,Laki Sita Ishirini na Nane Elfu na Mia Tatu (3,021,628,300 /=)** ambayo ni sawa na asilimia 8.6%

### 4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Ofisi ya Waziri Mkuu inaomba jumla ya **Shilingi Bilioni Sabini na**

**Nane,Milioni Hamsini na Saba,Laki Saba Ishirini na Saba na Elfu,Mia Tatu Sabini na Saba (78,057.727,377/=)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Matumizi Mengineyo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni Kumi na Sita, Milioni Mia Tano na Mbili, Laki Nne na Sabini na Sita Elfu, Mia Tatu Thelathini na Nne (16,502,476,334/=)** ni kwa ajili ya Mishahara, **Shilingi Bilioni Ishirini na Tisa, Milioni Mia Sita Kumi na Nane, Laki Nane Tisini na Tisa Elfu, Mia Tisa Kumi na Sita (29,618,899,916/=)** ni ruzuku kwa Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na **Shilingi Bilioni Thelathini na Moja, Milioni Mia Tisa Thelathini na Sita, Laki Tatu Hamsini na Moja Elfu, Mia Moja Ishirini na Saba (31,936,351,127/=**) ni fedha za Matumizi Mengineyo.

**Mheshimiwa Spika,** katika mchanganuo wa Mapato na Matumizi kwa Mafungu yaliyo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Mafungu ambayo yametengewa fedha nyingi kuliko mengine katika Mwaka wa Fedha ujao ni Ofisi ya Msajili wa Vyama Vya Siasa (Fungu 27) ambalo limetengewa **Shilingi Bilioni Kumi na Tisa, Milioni Mia Nne Themanini na Mbili,Laki Tatu Kumi na Saba Elfu,Mia Saba Arobaini (19,482,317,740/=)** na Ofisi ya Waziri Mkuu (Fungu 37) ambalo limetengewa **Shilingi Bilioni Ishirini na Moja, Milioni Mia Nane Tisini na Moja, Laki Nne Themanini na Tatu Elfu, Mia Saba Sitini na Nne (21,891,483,764/=).**

### 4.4 Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake zimeombewa **Shilingi Bilioni Themanini na Tatu, Milioni Mia Tano Sitini na Tano, Laki Tatu Sabini na Mbili Elfu,Mia Saba Sitini na Tatu (83,565,372,763/=)** kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo. Kati ya fedha hizi **Shilingi Bilioni Ishirini na Mbili, (22,000,000,000/=)** ni fedha za ndani na **Shilingi Bilioni Sitini na Moja, Milioni Mia Tano Sitini na Tano, Laki Tatu Sabini na Mbili Elfu, Mia Saba Sitini na Tatu (61,565,372,763/=)** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** fedha iliyotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 ni pungufu kwa kiasi cha **Shilingi Bilioni Hamsini na Sita, Milioni Mia Tisa**

**na Mbili, Laki Mbili na Arobaini na Saba Elfu, Mia Mbili Thelathini na Saba (56,902,247,237/=)** ya fedha iliyotengwa katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 kwa Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambazo zilitengewa kiasi **Shilingi Bilioni Mia Moja Arobaini, Milioni Mia Nne na Sitini na Saba, Laki Sita na Ishirini Elfu (140,467,620,000/=).** Kiasi hiki ni Pungufu ya Asilimia 40 ikilinganishwa na Bajeti ya Maendeleo kwa Ofisi ya Waziri Mkuu iliyoidhinishwa na Bunge hili Tukufu Mwezi Aprili 2016.

**Mheshimiwa Spika**, Mpango wa Ofisi ya Waziri Mkuu katika Miradi ya Maendeleo katika Mwaka huu wa Fedha umelenga katika maeneo 8 yakiwemo:-
i) Kuboresha mandhari na Ujenzi wa Miundombinu ya Makao Makuu Dodoma;
ii) Kujenga uwezo wa Serikali kukabiliana na Maafa
v) Kuimarisha Ushindani katika Sekta Binafsi
vii) Kuendelea kuwajengea uwezo wa Kiuchumi Vijana kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Ofisi ya Waziri Mkuu katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, miradi iliyopewa kipaumbele ni kama ifuatavyo; Mradi Na.6351 kuhusu Ujenzi wa Makazi ya Waziri Mkuu, Mlimwa - Dodoma uliotengewa **Shilingi Bilioni Tatu (3,000,000,000/=)** fedha za ndani, Mradi Na. 6581 kuhusu Programu ya Kukuza Ujuzi nchini uliotengewa **Shilingi Bilioni Kumi na Tano (15,000,000/=)** Fedha za ndani, Mradi Na. 4944 wa kuimarisha ushindani katika Sekta Binafsi uliotengewa **Shilingi Bilioni Kumi na Sita, Milioni Mia Mbili Hamsini na Nane Elfu, Laki Tano Tisini na Nne Elfu, Mia Nane Arobaini na Nne. (16,258,594,844/=)** fedha za Nje na Mradi Na. 4494 kuhusu Uendelezaji wa Mifumo ya Masoko na Huduma ya Kifedha Vijijini (MIVARF) uliotengewa **Shilingi Bilioni Arobaini na Mbili, Milioni Mia Nne na Arobaini na Tano, Laki Moja Hamsini na Tisa Elfu, Mia Tisa Kumi na Tisa (42,445,159,919/=)** ambazo ni fedha za nje kutoka Benki ya Maendeleo Afrika (ADB) na Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD)

**Mheshimiwa Spika,** mwenendo wa fedha za Bajeti ya Maendeleo kwa miaka michache iliyopita inaonyesha

kwamba nchi imekua inategemea fedha za nje kuliko fedha za ndani. Katika Mwaka ujao wa fedha, Bajeti ya jumla ya Serikali kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni asilimia 38 ya Bajeti yote ambayo ni pungufu ya asilimia 2 ya bajeti ya maendeleo ya Serikali iliyotengwa katika Mwaka wa Fedha 2016/2017. Kupungua kwa Bajeti ya Maendeleo ya Ofisi ya Waziri Mkuu kunachangiwa pamoja na sababu nyingine, na kupungua kwa utayari wa Wahisani na Wadau mbalimbali wa Maendeleo kutoa fedha za Miradi ya Maendeleo kutokana na mabadiliko mbalimbali ya Sera za nchi Wahisani na Taasisi za maendeleo za Kimataifa.

**Jedwali Na. 03: Ulinganisho wa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 na 2017/2018**

| **2016/2017** | | **2017/2018** | |
|---|---|---|---|
| Kawaida | Maendeleo | Kawaida | Maendeleo |
| 61,912,319,016/= | 140,467,620,000/= | 78,057,727,377/= | 83,565,372,763/= |

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi huu unaonyesha kuwa bajeti ya Matumizi ya Kawaida (Recurrent) imeongezeka kwa asilimia 19.3 % na bajeti ya Maendeleo imepungua kwa asilimia 40% ya malengo katika Mwaka uliopita wa fedha. Hali hii haiakisi Kauli Mbiu ya Serikali ya Uchumi wa Viwanda. Kamati inashauri Serikali kupanua wigo wa vyanzo vya mapato ili kuweza kufikia azma yake ya uchumi wa viwanda. Haiwezekani Serikali kujenga Uchumi wa Viwanda kwa kutegemea fedha ya Wahisani.

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** ninaomba sasa kutoa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu masuala mbalimbali yaliyojitokeza katika uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 na Taarifa za Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 wa Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake. Maoni na Ushauri wa Kamati pia umezingatia ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2016/2017.

## 5.1 FUNGU 37-Ofisi ya Waziri Mkuu

i) **Mheshimiwa Spika**, Kamati imeridhishwa kwa kiasi kikubwa na utekelezaji wa maoni na mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa na Kamati kwa Ofisi ya Waziri Mkuu katika Mwaka wa Fedha uliopita. Aidha Kamati inatoa wito kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kufanya rejea ya maagizo ambayo hayakutekelezwa kikamilifu kuyakamilisha kwa wakati hususani upatikanaji wa Sheria ya Uanzishwaji wa Makao Makuu Dodoma, Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, Masuala yote ya Kukabiliana na Maafa na Maboresho mbalimbali ya Sheria.

ii) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kwamba Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali ni Ofisi Muhimu katika kuendesha shughuli za Serikali lakini haijatengewa fedha ya Maendeleo katika Mwaka ujao wa Fedha. Kamati inaishauri Ofisi ya Waziri Mkuu kuhakikisha kwamba Ofisi hii inapewa kipaumbele katika Mpango wa Maendeleo wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kadri Upatikanaji wa Fedha unavyoruhusu.

iii) **Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia Umuhimu wa Ofisi na Shughuli za Waziri Mkuu, Kamati inashauri Ofisi ya Waziri Mkuu kukamilisha hatua iliyobaki ya ujenzi wa Makazi na Ofisi ya Waziri Mkuu hapa Dodoma katika Mwaka huu wa fedha (2017/2018)

iv) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri kwamba mara tu miradi ya MIVARF inapokamilika katika maeneo husika,Watendaji wa Maeneo hayo waendelee kuisimamia miradi hiyo kwa ukaribu ili iweze kudumu na kuleta faida kwa Wananchi wengi zaidi.

v) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri Zabuni za ujenzi wa Miradi ya Maendeleo zitolewe kwa uwazi (Transparent and Competitive Bidding Process) na kipaumbele kitolewe kwa Makampuni ya Ndani ya wakandarasi yaliyokidhi vigezo na yenye uwezo wa kutekeleza na kukamilisha miradi kwa wakati na kwa mujibu wa Mikataba ya Miradi husika.

vi) **Mheshimiwa spika**, katika Miradi yote ya Maendeleo iliyotengewa fedha Mwaka uliopita wa Bajeti (2016/2017) na ile iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha ujao (2017/ 2018), hususani Miradi ya MIVARF, Kamati inashauri Ofisi ya Waziri Mkuu kuhakikisha kwamba fedha zote za Miradi ya Maendeleo zinatumika kwa tija na kwa kuzingatia Kanuni ya thamani ya fedha kwa miradi husika (Value For Money).

## 5.2 Fungu 27 - Ofisi ya Msajili wa Vyama Vya Siasa

i. **Mheshimiwa Spika**, kufuatia mgogoro unaoendelea katika Chama cha CUF Kamati inashauri Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kuchukua jitihada za kutosha kusuluhisha mgogoro huo ili kuepusha athari kubwa zinazoweza kujitokeza katika Muungano.

ii. **Mheshimiwa Spika**, Kamati pia inaigiza Ofisi ya Msajili wa vyama vya Siasa kuzingatia Sheria, Kanuni,Taratibu na weledi katika usimamizi na utoaji wa ruzuku kwa vyama vya siasa na kuhakikisha kwamba taratibu hizo zinafuatwa katika utoaji ruzuku kwa vyama vya siasa.

## 5.3 Mfuko wa Fidia Kwa Wafanyakazi (WCF)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri Mfuko kuweka mkazo zaidi katika ulipaji fidia kwa Wafanyakazi ambalo ndilo lengo kuu la Mfuko na kuweka Mfumo mzuri wa kufanya tathmini za fidia kwa Wafanyakazi wanaopata ajali kazini na kuhakikisha kwamba malipo ya fidia yanafanyika kwa haraka kwa kila Mfanyakazi aliyetimiza vigezo vya fidia.

## 5.4 Fungu 65 - Kazi na Ajira

i) **Mheshimiwa spika**, kuhusu mpango wa kuunganisha Mifuko ya Pensheni, Kamati inaishauri Serikali kujiridhisha na masuala yote ya kitaalamu pamoja na kufanya mapitio na maboresho ya Sheria yanayohitajika katika kutekeleza mpango huu wenye nia nzuri ya kuwa na Sekta ya Pensheni imara na yenye ufanisi kwa Wafanyakazi wote. Kamati inatambua kwamba baadhi ya Mifuko ya Pensheni ina hali nzuri Kifedha (Financial Liquidity) na mingine ina hali mbaya

Kifedha na madeni mengi (Liabilities). Sababu za Kitaalamu zizingatiwe ili mwisho wa siku maamuzi sahihi na ya kitaalamu yafanyike kwa faida ya mifuko yote na Wafanyakazi wote.

ii) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri Mamlaka ya Usalama na Afya Mahala pa Kazi (OSHA) kuendelea kusimamia Afya na Usalama wa Wafanyakazi Mahali Pa Kazi na hasa kwa Wafanyakazi wanaofanya kazi katika maeneo hatarishi kama Migodini au Viwandani na kuchukua hatua kali za kisheria kwa Waajiri wote wasiozingatia masuala ya Afya na Usalama wa Wafanyakazi wao.

### 5.5 Fungu 61-Tume ya Taifa ya Uchaguzi

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuendelea kuboresha Daftari la Wapiga Kura na kuchukua jitihada za kutosha katika uboreshaji wa Daftari hili. Hatua hizi zijumuishe utoaji Elimu ya Uraia hususan uandikishaji wa Wapiga Kura kwa Vijana wengi zaidi ili waweze kutumia haki yao ya Kikatiba ya kupiga au kupigiwa kura. Hali hii itaongeza idadi ya Watanzania wengi zaidi watakaokua na sifa na vigezo vya kupiga kura katika chaguzi mbalimbali zinazokuja.

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukupongeza kwa kuendelea kuliongoza Bunge hili vema na kwa weledi wa hali ya juu. Nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Maoni ya Kamati kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria. Napenda nikupongeze pia kwa umahiri wako katika kasi ya kuliendesha Bunge hili katika kutekeleza Kauli Mbiu ya **HAPA KAZI TU** na kuishauri vema Serikali kwa manufaa ya Wananchi wa Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumpongeza Naibu Spika Mheshmiwa Tulia Ackson ,Mb, kwa weledi na umahiri wake katika kukusaidia kuongoza Bunge. Niwapongeze pia Wenyeviti wa Bunge kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kukushauri na kukusaidia kuendesha vikao vya Bunge. Wote

kwa pamoja tunawaombea afya na uzima katika kutekeleza majukumu mliyopewa.

**Mheshimiwa Spika**, nichukue fursa ya kipekee kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, na nimtakie kazi njema ya kuliongoza Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika**, nimpongeze Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Majaliwa Kassimu Majaliwa kwa kazi nzuri anayoifanya katika kusimamia utekelezaji wa bajeti na shughuli za Serikali Bungeni.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge Kazi, Ajira, Vijana, na Walemavu, Mhe. Jenista J. Mhagama, (Mb) Naibu waziri, Mhe. Antony Mavunde, (Mb), Makatibu Wakuu Ndg. Erick Shitindi (Kazi na Ajira) na Ndg. Hamisi H. Mwinyimkuu (Sera, Bunge na Uratibu) pamoja na Wataalam wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ushirikiano waliotoa kwa Kamati wakati wa uchambuzi wa bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Napenda pia kumtakia utumishi mwema Ndg. Maimuna Tarishi ambaye ameteuliwa na Mhe. Rais kuwa Katibu Mkuu,Ofisi ya Waziri Mkuu.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao mizuri wakati wa kupitia na kuchambua Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Walemavu. Naomba majina yao kama yalivyo katika Taarifa hii yaingie Katika Hansard:-

1. Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb – **Makamu /Mwenyekiti**
3. Mhe. Ajali Rashid Akbar, Mb - Mjumbe;
4. Mhe. Ally Saleh Ally, Mb - Mjumbe;
5. Mhe. Anna Joram Gidarya, Mb - Mjumbe;
6. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb - Mjumbe;
7. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb - Mjumbe;
8. Mhe. Juma Hamad Kombo, Mb - Mjumbe;

9. Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki, Mb - Mjumbe;
10. Mhe. Joram Ismael Hongoli, Mb - Mjumbe;
11. Mhe. Joseph Kizito Mhagama, Mb - Mjumbe;
12. Mhe. Makame Mashaka Foum, Mb - Mjumbe;-
13. Mhe. Mboni Mohamed Mhita, Mb - Mjumbe;
14. Mhe. Nassor Suleiman Omar, Mb - Mjumbe;
15. Mhe. Omary Ahmad Badwel, Mb - Mjumbe;
16. Mhe. Wanou Hafidhi Ameir, Mb - Mjumbe;
17. Mhe. Riziki Shahari Mngwali, Mb - Mjumbe;
18. Mhe. Saumu Heri Sakala, Mb - Mjumbe;
19. Mhe. Seif Ungando Ally, Mb - Mjumbe;
20. Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb - Mjumbe;
21. Mhe. Taska Restituta Mbogo, Mb - Mjumbe;
22. Mhe. Twahir Awesu Mohammed, Mb - Mjumbe;
23. Mhe. Suleiman Masoud Nchambi, Mb - Mjumbe
24. Mhe. David Mathayo David, Mb - Mjumbe
25. Mhe. Ussi Pondeza,Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, mwisho, kabisa lakini si kwa umuhimu napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashililah kwa kuiwezesha Kamati kukamilisha kazi yake bila kukwama. Aidha, napenda kumshukuru Mkurugenzi wa Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Angelina L. Sanga, Makatibu wa Kamati hii, Ndg. Stella Bwimbo, Ndg. Dunford Mpelumbe na Msaidizi wa Kamati Ndg. Raheli Masima kwa kuihudumia vyema Kamati pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati. Napenda kuwashukuru Makatibu Muhtasi wa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuchapa taarifa hii. Napenda pia kumshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard) Ndg. Hanifa Masaninga na Watendaji wote wa Idara hiyo kwa kuhakikisha kwamba Taarifa hii inatoka wa wakati na kwa ubora.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera,Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Walemavu, kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii.

Mohamed Omary Mchengerwa, Mb.
**MWENYEKITI,**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA**
06 APRILI, 2017

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge tunakushukuru sana sana. Ahsante sana.

Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali Kamati imezungumzia habari ya Sheria ya Dodoma kuwa Makao Makuu, hii sheria kwa kweli ni wakati sasa ije. Mwezi Oktoba hapa kama itakuwa haijaja hapa itabidi tuulizane vizuri inasubiri nini. *(Makofi)*

Naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti. Naomba wote mnaosoma hotuba za Kamati na kadhalika kitu muhimu kuliko vyote kwenu ni maoni na mapendekezo ya Kamati. Hizi pongezi na nini zikiwa na muda haya, lakini mjitahidi sana maoni na mapendekezo ndio iwe *central* ya mawasilisho yenu, karibuni sana. Karibu Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti.

**MHE. HAWA A. GHASIA- MWENYEKITI WA KAMATI KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nianze na kutoa pole kwa kuondokewa na Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Dkt. Elly Macha, nimwombe Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi na pia ndugu wa marehemu Mwenyezi Mungu awajalie moyo wa subira. Pia niwapongeze wote waliopata teuzi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2016; naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bajeti kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikutana na Waziri wa Fedha na Mipango, Waziri wa Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Walemavu pamoja na Katibu wa Bunge na kufanya mashauriano kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Mashauriano haya yamefanyika kwa mujibu kifungu cha 71(b) cha Sheria ya Bajeti Namba 11 ya mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuipongeza Ofisi ya Bunge kwa kutekeleza vyema malengo yake kwa mwaka uliotangulia ikiwa ni pamoja na mipango mizuri waliyojiwekea kwa mwaka huu wa fedha. Ni matumaini ya Kamati kuwa katika mwaka huu wa fedha (2017/2018) Ofisi ya Bunge itajitahidi kufikia malengo yake kwa usahihi na kwa wakati. Hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2017, Ofisi ya Bunge ilitekeleza majukumu mbalimbali yaliyopangwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuratibu na kusimamia shughuli za Mikutano ya Tano na Sita ya Bunge ambapo katika kipindi hicho maswali ya kawaida 336 na maswali 676 ya nyongeza yaliulizwa na kujibiwa Bungeni na Serikali. Waziri Mkuu aliulizwa na kujibu maswali ya msingi 14 na maswali 28 ya nyongeza; Kauli za Mawaziri tano zilitolewa Bungeni; Mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa mwaka 2017/2018 yalijadiliwa na kuidhinishwa na Bunge; Hati 33 ziliwasilishwa mezani na Miswada ya Sheria kumi ilipitishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, pia kuratibu na kusimamia shughuli za Mikutano ya Kamati za Kudumu za Bunge ambapo Kamati nne za Kudumu za Bunge ziliwezeshwa kuchambua Miswada 11 ya sheria; Sheria Ndogo 132 zilifanyiwa uchambuzi; taarifa 18 za uwekezaji nchini zilifanyiwa uchambuzi. Kamati 11 za Kudumu za Bunge ziliwezeshwa kufanya ziara za ufuatiliaji kwenye Wizara na taasisi mbalimbali za Serikali kwenye jumla ya mikoa 19.

Mheshimiwa Spika, Kamati za usimamizi wa matumizi ya fedha za umma ziliwezeshwa kuandaa na kuwasilisha

taarifa kuhusu hesabu zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2013 na 30 Juni, 2014.

Mheshimiwa Spika, shughuli nyingine zilizotekelezwa na Bunge lako Tukufu ni kama zinavyooneshwa katika kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Mfuko wa Bunge - Fungu 42 uliidhinishiwa jumla ya kiasi cha shilingi 99,066,117,000. Kati ya fedha hizo shilingi 23,798,609,000 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 68,267,508,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 7,000,000,000 kwa ajili ya mpango wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Ofisi ya Bunge ilipanga kukusanya kiasi cha shilingi 42,811,800 kama maduhuli. Hadi kufikia mwezi Februari 2017, Ofisi ya Bunge ilikuwa imekusanya kiasi cha shilingi 30,240,000 za maduhuli. Makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa kipindi cha mwezi Machi hadi Juni, 2017 ni shilingi 12,571,800 hivyo kufanya jumla ya makadirio ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kufikia shilingi 42,811,800. Makusanyo hayo yatatokana na marejesho ya masurufu na malipo ya pango.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa mpango kazi na mtiririko wa fedha kwa mwaka 2016/2017 *(cash flow* na *action plan),* hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2017 Ofisi ya Bunge ilikuwa imepokea shilingi 77,478,684,120. Kati ya fedha hizo shilingi 59,929,188,200 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 17,478,684,120 kwa ajili ya mishahara.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, pamoja na kupokea fedha hizo bado kumeonekana kuwa na changamoto kubwa ya kutolewa fedha kwa wakati kwa fungu husika na hivyo kuathiri utekelezaji wa baadhi ya majukumu ya Mfuko wa Bunge. Takwimu zinaonesha kuwa hadi sasa Mfuko wa Bunge unabakaa ya bajeti ya matumizi mengineyo ya kiasi cha shilingi 8,338,319,800 kulingana na bajeti iliyoidhinishwa.

Hata hivyo, bakaa hiyo ya bajeti haitoshi kutekeleza shughuli zilizobaki katika kipindi cha Aprili hadi Juni, 2017.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa Mfuko umebaini kuwepo kwa upungufu wa bajeti ya matumizi mengineyo ya shilingi 21,195,894,797 ambapo utaathiri utekelezaji wa shughuli za Bunge kwa kipindi cha robo ya tatu na nne. Aidha, Kamati ya Bajeti ilifanya mashauriano na Serikali na kukubaliana kwamba upatikanaji wa bajeti hii ya nyongeza utafanyiwa kazi kabla ya tarehe 30 Juni, 2017.

Mheshimiwa Spika, Kamati imethibitisha kuwepo kwa changamoto ya mgawo wa fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali, kutoendana na ratiba ya shughuli za ofisi. Hivyo, Ofisi ya Bunge imejikuta ikiingia katika madeni ya kiasi cha shilingi bilioni 5.7. Katika mwaka wa fedha 2016/2017 Mfuko wa Bunge uliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni saba kwa ajili ya mpango wa maendeleo. Hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2017 Ofisi ya Bunge imepokea jumla ya shilingi 234,090,000 tu sawa na asilimia tatu ya fedha yote iliyopangwa kwa ajili ya mpango wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, fedha za mpango wa maendeleo ambazo zimepokelewa zimetumika katika kulipia gharama za usimikaji wa mfumo wa mawasiliano ya video kwenye Ukumbi wa Bunge. Aidha, miradi mingine ambayo ni ukarabati wa majengo ya Bunge pamoja na Ukumbi wa Bunge haikutekelezwa kutokana na kutokupokea fedha kutoka Hazina.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru Serikali kwa kuiahidi Kamati kuwa bakaa ya fedha hizo za maendeleo, kiasi cha shilingi bilioni 6.77 itatolewa kabla ya kufikia tarehe 30 Juni, 2017. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018 fedha zilizokasimiwa zimetengwa katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya kuhakikisha kuwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linatekeleza majukumu yake ya Kikatiba. Baadhi ya majukumu ambayo yamepangwa kutekelezwa katika

Bajeti ya mwaka 2017/2018 ni kama ambavyo yanaonekana katika kitabu chetu cha hotuba.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Ofisi ya Bunge imepanga kukusanya maduhuli kiasi cha shilingi 42,500,000. Makusanyo hayo yatatokana na marejesho ya masufuru na malipo ya kodi ya pango.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Mfuko wa Bunge umepanga kutumia jumla ya shilingi 121,652,262,000. Kati ya fedha hizo shilingi 24,454,715,000 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 89,997,547,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 7,200,000,000 ni kwa ajili ya maendeleo ambapo kati ya kiasi hicho shilingi 7,000,000,000 ni fedha za ndani na shilingi 200,000,000 ni fedha za nje. Mchanganuo wa namna fedha za matumizi ya kawaida na maendeleo zitakavyotumika umeainishwa kwenye jedwali lifuatalo ambalo lipo katika kitabu chetu cha hotuba.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati, kwa kuwa, Mfuko wa Bunge unakabiliwa na changamoto ya madeni iliyosababishwa na kutokupatikana kwa fedha za kutosha wakati wa utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2016/2017. Hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inamalizia kupeleka kwenye Mfuko wa Bunge bakaa ya bajeti ya matumizi mengineyo kiasi cha shilingi 8,338,919,800 katika bajeti ya mwaka 2016/2017. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Kamati imeelezwa kuwa bakaa hiyo ya shilingi 8,338,319,800 haitatosha kutekeleza haitatosha kutekeleza shughuli zilizobaki katika kipindi cha Aprili hadi Juni, 2017 hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuridhia maombi ya bajeti ya nyongeza kiasi cha shilingi 21,195,894,797 ili Bunge liweze kutekeleza majukumu yake ya Kikatiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mfuko wa Bunge umekuwa ukikabiliwa na changamoto ya kutokupokea kwa wakati mgawo wa fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na wakati mwingine kupokea fedha pungufu tofauti na

ilivyoombwa; hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali ihakikishe inazingatia maelekezo ya kifungu cha 48 cha Sheria ya Bajeti Namba 11 ya mwaka 2015, kinachoitaka Hazina kutoa fedha kwenda Mfuko wa Bunge kwa kila robo ya mwaka. Pia Serikali ihakikishe inatoa fedha zinazohitajika kabla ya kuanza kwa vikao vya Kamati na Bunge ili kuwezesha utekelezaji mzuri wa shughuli husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa mwaka wa fedha 2016/2017 hadi kufikia mwezi Machi, 2017 imeonesha Mfuko wa Bunge kukabiliwa na changamoto ya kutokupokea fedha kwa wakati na wakati mwingine kupokea fedha pungufu tofauti na ulivyoomba, hivyo basi Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Mfuko wa Bunge unapatiwa fedha kwa wakati kwa mujibu wa maelekezo ya Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015 na kama zitakavyoidhinishwa na Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nihitimishe kwa kukushukuru wewe mwenyewe pamoja na Mheshimiwa Naibu Spika, Dkt. Tulia Ackson kwa ushirikiano mkubwa na ushauri ambao unatupatia Kamati ya Bajeti pamoja na Serikali. Pia nichukue fursa hii kumshukuru Dkt. Philip Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango na Dkt. Ashatu Kijaji, Mbunge wa Kondoa na Naibu Waziri wa Fedha, kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Aidha, Kamati inamshukuru pia Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiho na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kwa kushirikiana na Kamati wakati wote wa majadiliano.

Mheshimiwa Spika, nifurahi kwamba kwa mwaka huu kwa bajeti iliyopitishwa, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, hatutegemei kukwama, tofauti na bajeti iliyopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa maoni na mapendekezo mbalimbali kuhusu Bajeti ya Mfuko wa Bunge. Na pia kwa namna ya kipekee napenda kumshukuru

Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo na Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii kwa ushirikiano mkubwa sana ambao ananipatia katika kutekeleza majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii pia kumshukuru Dkt. Thomas Kashililah, Katibu wa Bunge, kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo na Sekretarieti ya Kamati kwa kuipa ushauri wa kitaalamu Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Bunge, Fungu 42 kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MFUKO WA BUNGE KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bajeti, kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2016/17 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18.

**Mheshimiwa Spika,** kamati ilikutana na Waziri wa Fedha na Mipango, Waziri wa Sera, Bunge, kazi, Vijana, Ajira na

Walemavu pamoja na Katibu wa Bunge na kujadiliana na kufanya mashauriano kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2016/17 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18. Mashauriano haya yamefanyika kwa mujibu kifungu cha 71 (b) cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015.

## 2.0 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA MFUKO WA BUNGE KWA MWAKA 2016/17

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua fursa hii kuipongeza Ofisi ya Bunge kwa kutekeleza vyema malengo yake kwa mwaka uliotangulia ikiwa ni pamoja na mipango mizuri waliyojiwekea kwa Mwaka huu wa Fedha. Ni matumaini ya Kamati kuwa katika mwaka huu wa Fedha 2017/18; Ofisi ya Bunge itajitahidi kufikia malengo yake kwa usahihi na kwa wakati. Hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2017, Ofisi ya bunge ilitekeleza majukumu mbali mbali yaliyopangwa kama ifuatavyo:-

a) Kuratibu na kusimamia shughuli za Mikutano ya Tano na Sita ya Bunge ambapo katika kipindi hicho Maswali ya kawaida 336 na maswali 676 ya nyongeza yaliulizwa na kujibiwa Bungeni na Serikali; Waziri Mkuu aliulizwa na kujibu maswali ya msingi 14 na maswali 28 ya nyongeza; Kauli za Mawaziri tano (5) zilitolewa Bungeni; Mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo kwa Mwaka wa fedha 2017/2018 yalijadiliwa na kuidhinishwa na Bunge; Hati 33 ziliwasilishwa mezani na Miswada ya Sheria Kumi (10) ilipitishwa na Bunge;

b) Kuratibu na kusimamia shughuli za Mikutano ya Kamati za Kudumu za Bunge ambapo Kamati nne (4) za Kudumu za Bunge ziliwezeshwa kuchambua Miswada Kumi na Moja (11) ya Sheria; Sheria Ndogo *(Subsidiary Legislations)* mia moja thelathini na mbili (132) zilifanyiwa uchambuzi; taarifa kumi na nane (18) za Uwekezaji nchini zilifanyiwa uchambuzi . Kamati kumi na moja (11) za Kudumu za Bunge ziliwezeshwa kufanya ziara za ufuatiliaji kwenye wizara na taasisimbalimbali za serikali kwenye jumla ya mikoa kumi na tisa (19).

c) Kamati za Usimamizi wa matumizi ya Fedha za Umma ziliwezeshwa kuandaa na kuwasilisha Taarifa kuhusu Hesabu zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2013 na 30 Juni, 2014;

d) Shughuli za Kuchapisha, kurekodi, kuandika, kuhariri na kupanga taarifa rasmi za Bunge katika Mikutano yote ya Bunge zilifanyika ambapo nyaraka mbalimbali ikiwa ni pamoja na nakala 1,520 za Taarifa Rasmi *(Hansard)* za Majadiliano ya Bunge; nakala 7,030 za Miswada ya Sheria ya Serikali; nakala 573 za Kanuni za Kudumu za Bunge; nakala 600 za Kitabu cha kumbukumbu za Wabunge; nakala 15,069 za Taarifa za kamati na nakala 4,850 za Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani zilitolewa;

e) Katika kipindi husika ushauri kuhusu miswada binafsi ya Wabunge wanne (4), hoja binafsi sita (6) na maelezo binafsi ya Wabunge wanne (4) ulitolewa;

f) Kutoa huduma za Utafiti *"Information Research"* kwa lengo la kuboresha mijadala kwa ajili ya Wabunge wakati wa Mikutano ya Kimataifa ambapo katika kipindi husika huduma za ushauri *(advisory support)* kwa Wabunge zaidi ya 76 zilitolewa katika masuala mbalimbali ikiwa ni pamoja na huduma za uandishi wa mada mbalimbali *(background papers)* kwa ajili ya Wabunge na viongozi wengine wa Bunge waliohudhuria mikutano ya Kimataifa;

g) Kuratibu na kusimamia kazi na majukumu ya Tume ya Utumishi wa Bunge.

h) Shughuli zinazohusu kuimarisha ushiriki wa Bunge katika Mikutano ya Kimataifa zilifanyika ambapo Ofisi iliratibu upatikanaji wa hati za kusafiria za Kidiplomasia kwa ajili ya Wabunge 24 na ushiriki wa Wabunge hao katika Mikutano ya Bunge la Afrika (PAP), Umoja wa abunge wa Jumuiya ya Madola (CPA) Kanda ya Afrika, *CPA- International*, *Africa Caribbean Pacific and European Union (ACP/EU)* na Jukwaa la Kibunge la Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC-

PF), Bunge la Afrika Mashariki na Umoja wa Mabunge Duniani ( IPU);

i) Kuandaa vipindi vya televisheni na kurusha matangazo ya Bunge; pamoja na Kuratibu utoaji wa habari kwa wananchi kuhusu shughuli za Bunge na Kamati;

j) Kufanya mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa kipindi cha kuanzia Mwezi Julai hadi Disemba, 2016; pamoja na Kufanya maandalizi ya Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa mwaka wa fedha 2017/18;

k) Kuwezesha malipo ya posho na stahiki za Wabunge (Posho ya Jimbo, vikao, kujikimu na posho ya usafiri) pamoja na watumishi, wakati wa Mkutano wa Tano na Sita wa Bunge la Kumi na Moja (11);

l) Kuratibu shughuli mbalimbali za utawala (huduma kwa Wabunge, ununuzi wa vifaa vya Ofisi, malipo ya maji, umeme na simu, usafi na ulinzi);

m) Kuwezesha matibabu ya Waheshimiwa Wabunge ndani na nje ya nchi;

n) Kuwezesha Watumishi 21 kushiriki mafunzo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi;

o) Kugharamia uendeshaji wa Ukumbi wa Bunge; pamoja na kuratibu kazi ya kukarabati Jengo la ukumbi wa Bunge na majengo ya Ofisi ya Bunge;

## 3.0. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2016/17 Mfuko wa Bunge – Fungu 42 uliidhinishiwa jumla ya kiasi cha **Sh.99,066,117,000.** Kati ya fedha hizo **Sh.23,798,609,000** ni kwa ajili ya Mishahara (PE), **Sh.68,267,508,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC), na **Sh.7,000,000,000.00** kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo.

### 3.1 Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,**Katika mwaka wa fedha 2016/2017 Ofisi ya Bunge ilipanga kukusanya maduhuli ya kiasi cha **Sh.42,811,800** hadi kufikia mwezi Februari 2017, Ofisi ya Bunge ilikuwa imekusanya kiasi cha **Sh.30,240,000** za maduhuli. Makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa kipindi cha mwezi Machi hadi Juni, 2017 ni **Sh.12,571,800** hivyo kufanya jumla ya makadirio ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kufikia **Sh.42,811,800**. Makusanyo hayo yatatokana na marejesho ya masurufu *(Recovery of Public Money)* na malipo ya kodi ya Pango.

### 3.2 Matumizi ya Kawaida kwa mwaka 2016/17

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Mpango Kazi na Mtiririko wa Fedha kwa mwaka 2016/*2017 (Cash Flow and Action Plan)*, hadi kufikia mwezi tarehe 31 Machi 2017 Ofisi ya Bunge imepokea kiasi cha **Sh.77,478,684,120** kati ya fedha hizo **Sh.59,929,188,200** ni kwa ajili ya matumizi ya mengineyo (OC) na **Sh.17,478,684,120** kwa ajili ya Mishahara (PE).

**Mheshimiwa Spika,** Hata hivyo pamoja na kupokea fedha hizi bado kumeonekana kuna changamoto kubwa ya kutolewa fedha kwa wakati kwa fungu husika na hivyo kuathiri utekelezaji wa baadhi ya majukumu ya Mfuko wa Bunge. Takwimu zinaonyesha kuwa hadi sasa Mfuko wa Bunge una bakaa ya bajeti ya matumizi mengineyo (OC) ya kiasi cha **Sh.8,338,319,800** kulingana na bajeti iliyoidhinishwa. Hata hivyo, bakaa hiyo ya bajeti haitoshi kutekeleza shughuli zilizobaki katika kipindi cha Aprili hadi June 2017.

**Mheshimiwa Spika**, hadi sasa Mfuko umebaini kuwepo kwa upungufu wa bajeti ya matumizi mengineyo ya **Sh.21,195,894,797** ambao utaathiri utekelezaji wa shughuli za Bunge kwa kipindi cha Robo ya Tatu na Nne. Aidha, Kamati ya Bajeti ilifanya mashauriano na Serikali na kukubaliana kuwa patikanaji wa Bajeti hii ya nyongeza itafanyiwa kazi kabla ya tarehe 30 Juni 2017.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imethibitisha kuwepo kwa changamoto ya mgao wa fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kutoendana na ratiba za shughuli za Ofisi. Hivyo, Ofisi ya Bunge imejikuta ikiingia katika madeni ya kiasi cha shilingi bilioni 5.7.

### 2.3 Matumizi ya Maendeleo kwa Mwaka wa fedha 2016/17

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha **2016/17** Mfuko wa Bunge uliidhinishiwa jumla ya **Sh.7,000,000,000** kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo. Hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2017, Ofisi ya Bunge imepokea jumla ya **Sh.234,090,000** sawa na **asilimia 3** ya fedha yote iliyopangwa kwa ajili ya mpango wa Maendeleo kwa mwaka mzima.

**Mheshimiwa Spika,** Fedha za mpango wa maendeleo ambazo zimepokelewa zimetumika katika kulipia gharama za usimikaji wa mfumo wa mawasiliano ya video kwenye Ukumbi wa Bunge. Aidha, miradi mingine ambayo ni ukarabati wa majengo ya bunge pamoja na ukumbi wa bunge haikutekelezwa kutokana na kutopokea fedha kutoka Hazina.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuishukuru Serikali kwa kuiahidi Kamati kuwa bakaa ya fedha ya maendeleo kiasi cha shilingi **bilioni 6.77** itatolewa kabla ya kufikia tarehe 30 Juni 2017.

## 4.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA MFUKO WA BUNGE KWA MWAKA WA FEDHA 2017/18.

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa Fedha 2017/18, fedha zilizokasimiwa zimetengwa katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya kuhakikisha kuwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linatekeleza majukumu yake ya Kikatiba. Baadhi ya majukumu ambayo yamepangwa kutekelezwa katika bajeti ya mwaka 2017/18 ni kama yafuatayo:

a) Kuratibu na kusimamia shughuli za Mkutano wa Bajeti na Mikutano Midogo Mitatu (3) ya Bunge;
b) Kuratibu na kusimamia shughuli za Mikutano Minne (4) ya Kamati za Kudumu za Bunge ambayo ni Mkutano Mmoja wa Kamati kuhusu uchambuzi wa bajeti na Mikutano Midogo Mitatu (3);
c) Kuwezesha shughuli za Wabunge katika majimbo na maeneo ya uwakilishi;
d) Kuratibu na kuchapisha Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard);*
e) Kutoa ushauri wa kisheria kwa Wabunge na uchambuzi wa miswada;

f) Kutoa huduma za Utafiti kwa Wabunge (*"Information Research")*;
g) Kuratibu na kusimamia kazi na majukumu ya Tume ya Utumishi wa Bunge.
h) Kuwezesha Wabunge kushiriki kwenye Mikutano ya Kimataifa kama vile Mikutano ya Bunge la Afrika (PAP), Umoja wa Wabunge wa Jumuiya ya Madola (CPA) Kanda ya Afrika, *CPA- International*, Africa Caribbean Pacific and European Union (ACP/EU) na Jukwaa la Kibunge la Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC- PF), Bunge la Afrika Mashariki na Umoja wa Mabunge Duniani ( IPU);
i) Kuandaa vipindi vya televisheni na kurusha matangazo ya Bunge;

j) Kuratibu utoaji wa habari kwa wananchi kuhusu shughuli za Bunge na Kamati;
k) Kuratibu ushiriki wa Wabunge kwenye vikao vya Kamati na Bunge kwa kuwawezesha malipo ya posho na stahiki zao (Posho ya Jimbo, vikao, kujikimu na usafiri);

l) Kuratibu shughuli mbalimbali za utawala (huduma kwa Wabunge, ununuzi wa vifaa vya Ofisi, malipo ya maji, umeme na simu, usafi na ulinzi);
m) Kuwezesha matibabu ya Waheshimiwa Wabunge ndani na nje ya nchi;

n) Kuwezesha Watumishi 23 kushiriki mafunzo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi;
o) Kuwa wenyeji wa mashindano ya michezo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki;
p) Kuwajengea Wabunge uwezo ili waweze kutekeleza majukumu yao kikatiba;
q) Kusimamia uendeshaji wa Ukumbi wa Bunge, mitambo na mashine;
r) Kuratibu kazi ya kukarabati Jengo la ukumbi wa Bunge na majengo ya Ofisi ya Bunge;
s) Kugharamia uanzishwaji wa Bunge Mtandao *(e-Parliament)* na Studio ya Bunge;
t) Kugharamia usimikaji wa lifti katika Jengo la Utawala.

### 4.1 Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2017/18 Ofisi ya Bunge imepanga kukusanya maduhuli ya kiasi cha **Sh.42,500,000** Makusanyo hayo yatatokana na marejesho ya masurufu*(Recovery of Public Money)* na malipo ya kodi ya Pango.

### 4.2 Matumizi ya Kawaida na Maendeleo

Mh Katika mwaka wa fedha 2017/18 Mfuko wa Bunge umepanga kutumia jumla ya **Sh.121,652,262,000** Kati ya fedha hizo **Sh.24,454,715,000** ni kwa ajili ya Mishahara, **Sh.89,997,547,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Mengineyo *(OC)* na **Sh.7,200,000,000** ni kwa ajili ya maendeleo ambapo kati ya kiasi hicho **Sh.7,000,000,000** ni fedha za ndani na **Sh.200,000,000** ni fedha za nje. Mchanganuo wa namna fedha za Matumizi ya Kawaida na maendeleo zikakavyotumika zimeanishwa kwenye jedwali lifuatalo.

**JEDWALI : Mchanganuo wa Makisio kwa mwaka 2017/18**

| NA. | MAELEZO | BAJETI YA MWAKA 2016/2017 | MAKISIO YA MWAKA 2017/2018 |
|---|---|---|---|
| **1.** | **MISHAHARA** | **23,798,609,000.00** | **24,454,715,000.00** |
| 1.1 | Programu 10 – Utawala na Uendeshaji | 919,896,000.00 | 954,624,000.00 |
| 1.2 | Programu 20 – Shughuli za Bunge | 20,639,801,000.00 | 21,584,909,000.00 |
| 1.3 | Programu 30 – Ofisi ya Katibu wa Bunge | 2,238,912,000.00 | 1,915,182,000.00 |
| | | | |
| **2.** | **MATUMIZI MENGINE (OC)** | **68,267,508,000.00** | **89,997,547,000.00** |
| 2.1 | Programu 10 – Utawala na Uendeshaji | 7,516,468,000.00 | 7,085,361,000.00 |
| 2.2 | Programu 20 – Shughuli za Bunge | 53,579,288,000.00 | 77,125,872,000.00 |
| 2.3 | Programu 30 – Ofisi ya Katibu wa Bunge | 7,171,752,.000.00 | 5,786,314,000.00 |
| **3** | **MPANGO WA MAENDELEO** | **7,000,000,000.00** | **7,200,000,000.00** |
| 3.1 | Ikarabati wa Majengo ya unge | 3,000,000,000.00 | 3,000,000,000.00 |
| 3.2 | Miundombinu ya Bunge | 2,500,000,000.00 | 1,200,000,000.00 |
| 3.3 | Kuanzishwa kwa Bunge *Mtandao (e-Parliament)* | - | 2,800,000,000.00 |
| 3.4 | Usimikaji wa studio ya Bunge | 1,500,000,000.00 | - |
| 3.5 | Mradi wa PFMRP | - | 200,000,000.00 |
| **4** | **MAKUSANYO** | **42,812,000.00** | 42,500,000.00 |
| 4.1 | Maduhuli | 42,812,000.00 | 42,500,000.00 |
| | **JUMLA YA FUNGU (1+2+3)** | **99,066,117,000.00** | **121,652,262,000.00** |

## 6.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

6.1 **Kwa kuwa,** Mfuko wa Bunge unakabiliwa na changamoto ya madeni iliyosababishwa na kutopatikana kwa fedha za kutosha wakati wa utekelezaji wa Bajeti ya 2016/17,

**Hivyo basi,** Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inamalizia kupeleka kwenye Mfuko wa Bunge bakaa ya bajeti ya matumizi mengineyo kiasi cha **Sh.8,338,319,800** katika bajeti ya mwaka 2016/17.

6.2 **Kwa kuwa**, Kamati imeelezwa kuwa bakaa hiyo ya **Sh.8,338,319,800** haitatosha kutekeleza shughuli zilizobaki katika kipindi cha Aprili hadi Juni 2017,

**Hivyo basi**, Kamati inaishauri Serikali kuridhia maombi ya Bajeti ya Nyongeza ya **Sh.21,195,894,797** ili Bunge liweze kutekeleza majukumu yake ya kikatiba;

6.3 **Kwa kuwa**, Mfuko wa Bunge umekuwa ukikabiliwa na changamoto ya kutopokea kwa wakati mgao wa fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na wakati mwingine kupokea fedha pungufu tofauti na ilivyoombwa,

**Hivyo basi**, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inazingatia maelekezo ya kifungu cha 48 cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 kinachoitaka Hazina kutoa fedha kwenda Mfuko wa Bunge kwa kila robo mwaka. Pia, Serikali ihakikishe inatoa fedha zinazohitajika kabla ya kuanza kwa vikao vya Kamati na Bunge ili kuwezesha utekelezaji mzuri wa shughuli husika

6.5 **Kwa kuwa**, Tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa mwaka wa fedha 2016/2017 hadi kufikia mwezi Machi 2017 imeonesha Mfuko wa Bunge kukabiliwa na changamoto ya kutopokea fedha kwa wakati na wakati mwingine kupokea fedha pungufu tofauti na ilivyoombwa ,

**Hivyo basi,** Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba ' a mwaka wa fedha wa 2017/2018 Mfuko wa Bunge unapatiwa fedha kwa wakati kwa mujibu wa maelekezo ya Sheria ya Bajeti (2015) na kama zitakavyoidhinishwa na Bunge.

**6.6 Kwa kuwa,** Bunge la Tanzania linatarajiwa kuwa mwenyeji wa mashindano ya michezo kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki yatakayofanyika mwishoni mwa mwaka 2017. Na kwa kuwa katika bajeti ya mwaka 2017/18 zimetengwa shilingi milioni 147 tu kwa ajili ya shuguli hiyo ambazo kiuhalisia hazitatosha kugharamia michezo hiyo.

**Hivyo basi,** Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kutoa nyongeza ya bajeti kwa ajili ya kugharamia

michezo hiyo muhimu katika kukuza mahusiano ya nchi husika.

## 7.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** naomba nihitimishe kwa kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson (Mb), Naibu Spika kwa kuongoza vema mashauriano kati ya Kamati ya Bajeti na Serikali. Namshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango (Mb), Waziri wa Fedha na Mipango na Mheshimiwa Dkt Ashatu Kijaji, Mbunge wa Kondoa na Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Aidha, Kamati inamshukuru pia Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiho na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu) kwa kushirikiana na Kamati wakati wa majadiliano.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa maoni na mapendekezo mbalimbali kuhusu Bajeti ya Mfuko wa Bunge. Naomba kuwatambua wajumbe hao kama ifuatavyo:-

1) Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia, Mb – Mwenyekiti
2) Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb - M/ Mwenyekiti
3) Mhe. Hamida Mohamedi Abdallah, Mb
4) Mhe. David Ernest Silinde, Mb
5) Mhe. Mbaraka Kitwana Dau, Mb
6) Mhe. Mendrad Lutengano Kigola, Mb
7) Mhe. Maria Ndilla Kangoye, Mb
8) Mhe. Susan Peter Maselle, Mb
9) Mhe. Agustino Manyanda Masele, Mb
10) Mhe. Freeman AikaelMbowe, Mb
11) Mhe. Flatei Gregory Massay, Mb
12) Mhe. Makame Kassim Makame, Mb
13) Mhe. Janet ZebedayoMbene, Mb
14) Mhe. Cecil David Mwambe, Mb
15) Mhe. Susana Chogisasi Mgonukulima, Mb
16) Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb
17) Mhe. Juma Hamad Omar, Mb
18) Mhe. Ali Hassan Omari, Mb

19) Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mb
20) Mhe. Jerome Bwanausi, Mb
21) Mhe. Jitu Vrajlal Soni, Mb
22) Mhe. Abdallah M. Bulembo, Mb
23) Mhe. Andrew John Chenge, Mb
24) Mhe. Mussa A. Zungu, Mb
25) Mhe. Japhet Ngalilonga Hasunga, Mb
26) Mhe. Dalali Peter Kafumu, Mb
27) Mhe. Albert Obama Ntabaliba, Mb

**MheshimiwaSpika,** napenda kuchukua fursa hii, pia kumshukuru Dkt Thomas Kashililah Katibu wa Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo, pamoja na Sekretarieti ya Kamati kwa kuipa ushauri wa kitaalamu Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Bunge – Fungu 42, kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii.

Hawa A. Ghasia, Mb.
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI**
06 APRILI, 2017

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Hawa Ghasia. Nakushukuru sana, na huo ndio mfano wa Wenyeviti wa Kamati wote mtakaofuata kuanzia leo mpaka mwisho wa shughuli zetu. Unapokuja hapa njoo ukiwa *focused* na utumie muda mfupi unavyowezekana, itatusaidia sana. Ametusaidia ku-*save* dakika kumi nzima! Nakushukuru sana. Sasa nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Masuala ya UKIMWI. *(Makofi)*

Karibu sana, Dkt. Hadji Mponda!

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA – K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MASUALA YA UKIMWI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuwepo hapa Dodoma katika utekelezaji wa majukumu yetu ya kawaida. Lakini pili kwa niaba ya Kamati naomba kutoa pole kwa kifo cha Mbunge mwenzetu, Dkt. Elly Marko Macha, Mbunge wa Viti Maalum – CHADEMA. Pole hizi pia, ziwafikie ndugu na jamaa na wote wanaohusika na msiba huo.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2016 naomba kuwasilisha Maoni na Ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kuhusu Utekelezaji Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya – Fungu 91 na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* – Fungu 92 kwa mwaka wa fedha 2016/2017 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, mtiririko wa taarifa hii umezingatia masuala makubwa manne ambayo bila kuathiri matakwa ya Kanuni ya 123 kuhusu muundo wa taarifa ya Kamati; moja, utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati kwa kipindi kilichopita, mbili Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mamlaka ya Kupambana na Kudhibiti Dawa za Kulevya Tanzania kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* kwa mwaka wa fedha ambao tunauzungumzia na maoni na ushauri wa Kamati na hatimaye tutahitimisha.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchambuzi wa Kamati. Sehemu hii inaeleza masuala mbalimbali yaliyobainika katika utekelezaji wa shughuli za Kamati. Hata hivyo, kabla ya kueleza masuala hayo naomba kutoa pongezi za Kamati kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, kwa kuunda mamlaka mahususi ya kudhibiti na

kupambana na dawa za kulevya na kumteuwa Kamishna Mkuu wa Mamlaka hiyo, Ndugu Rogers William Sianga. Lakini pia, ninawapongeza Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kutekeleza vema mapandekezo ya Kamati ya mwaka uliopita, hususan suala la kukomesha uuzaji na matumizi ya pombe kali aina ya viroba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, masuala muhimu yaliyobainika. Sehemu hii inaeleza mambo muhimu yaliyobainika katika utekelezaji wa shughuli za Kamati. Kutokana na masuala hayo Kamati imeandaa maoni na mapendekezo yatakayotolewa katika sehemu yetu ya tatu kwa ajili ya kuishauri Serikali kufanya maboresho zaidi katika majukumu ya kudhibiti dawa za kulevya na UKIMWI nchini.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mapendekezo (Hoja za Kamati). Katika mwaka wa fedha uliopita, Kamati ilitoa maoni 11 kwa ajili ya kutekelezwa na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya hususan kuhusiana na bajeti yake. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Tume imetekeleza vizuri maoni yote 11. Aidha, maoni saba yaliyotolewa na Kamati kwa ajili ya kutekelezwa na Tume ya Kudhibiti UKIMWI *(TACAIDS)* yametekelezwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mpango wa maendeleo wa mwaka wa fedha 2016/2017. Katika eneo hili, Kamati huainisha Mipango ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI nchini na Mipango ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa ya Kulevya ili kuona kama kuna uwiano wa moja kwa moja na matakwa ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2017/2018 – 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, kilichobainika ni kwamba mipango na vipaumbele vyao vipo vema, tatizo lipo kwenye kiasi kidogo cha fedha kinachotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mipango na vipaumbele hivyo. Kwa mfano, Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania imeendelea kuwa na utegemezi wa fedha za nje ili kutekeleza afua za UKIMWI hali inayosababisha zoezi hili kutokuwa endelevu.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Kudhibiti UKIMWI; katika mwaka wa fedha wa 2016/2017, Tume ya Kudhibiti UKIMWI *(TACAIDS)*, ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 10.1 kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 4.95 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 5.2 kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo hadi kufikia tarehe 28 Februari mwaka huu, Tume ilikuwa imepokea jumla ya shilingi bilioni 2.8, sawa na asilimia 27 tu ya bajeti yote; kati ya fedha hizo, mishahara ni shilingi milioni 986.7 sawa na asilimia 49 ya fedha iliyotengwa. Hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2017, Tume ilipokea jumla ya shilingi milioni 516.2 sawa na asilimia 141 ya bajeti kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2017, Mfuko wa UKIMWI ulipokea shilingi 400,000,000, sawa na asilimia 16 ya bajeti kwa ajili ya shughuli za maendeleo, hii ikiwa ni pungufu ya shilingi bilioni 7.4, sawa na asilimia 73 ya kiasi chote cha bajeti kilichotengwa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kupewa fedha chini ya kiasi kilichoombwa, Tume imelegalega katika kutekeleza majukumu yake. Kwa mfano, imeshindwa kuajiri watumishi katika baadhi ya Idara na Vitengo.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya; katika mwaka wa fedha 2016/2017 iliyokuwa Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya ambayo kwa sasa haipo na imeundwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ilitengewa kiasi cha shilingi bilioni 2.3 kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Hadi kufikia mwezi Machi, 2017, kiasi kilichopokelewa ni shilingi milioni 851.1 ambayo ni sawa na asilimia 49 ya fedha iliyotengwa. Aidha, fedha za mishahara ya watumishi zilizoidhinishwa ni shilingi milioni 610.8 na shilingi bilioni 1.7 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (*OC).* Kiasi cha mishahara kilichopokelewa hadi kufikia mwezi Machi, mwaka huu ni shilingi 425,500,000 sawa na asilimia 69 ya fedha zilizotengwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaridhishwa na mwenendo huu wa utoaji wa fedha kwani ikumbukwe kuwa

dawa za kulevya ni kama janga la Taifa linaloathiri zaidi vijana ambao ndiyo nguvu kazi katika nchi yetu. Mwenendo huu wa utoaji wa fedha utasaidia kuongeza kasi ya mapambano dhidi ya dawa hizo, hivyo kuendelea kuwabaini na kuwakamata watuhumiwa na kuokoa vizazi vyetu na kuwa na Taifa lenye afya njema.

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Mapato na Matumizi 2017/2018; Tume ya Kudhibiti UKIMWI *(TACAIDS);* vipaumbele vya Bajeti katika Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kwa mwaka wa fedha ujao imebainisha maeneo ya vipaumbele katika mpango wa bajeti hiyo kama ilivyoelezwa katika taarifa yetu. Hivyo basi, katika mapitio ya mapato na matumizi yake Kamati ilikuwa na jukumu la kuainisha kiasi cha fedha kilichoombwa na uzito wa majukumu, yaani vipaumbele vitakavyotekelezwa.

Mheshimiwa Spika, kilichobainika ni kwamba endapo Tume itapewa fedha zote zilizotengwa kwa kuzingatia mpango wa mahitaji ya fedha *(cash flow plan)* fedha hizo anagalau zitasaidia sana Tume kukamilisha mipango yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI; kwa mwaka wa fedha huu tunaozungumzia Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania inaomba jumla ya shilingi bilioni 5.9 bilioni kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo, kiasi cha shilingi bilioni 3.4 kwa ajili ya shughuli za maendeleo na shilingi bilioni 2.5 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliridhishwa na mpangilio wa vipaumbele vya Tume japokuwa kuna changamoto ya ufinyu wa bajeti kwa ajili ya utekelezaji vipaumbele hivyo. Ufinyu huo wa bajeti umekuwa ukiimbwa kila mwaka na haijulikani utaisha lini. (*Makofi*)

Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2016/2017 kati ya shilingi bilioni 10.1 zilizokuwa zimetengwa shilingi bilioni 2.7, sawa na asilimia 27 ya bajeti ndizo zilizokuwa zimetolewa

hadi kufikia tarehe 28 Februari mwaka huu. Hali hii huathiri kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa majukumu ya Tume na morali ya watumishi wa Tume katika kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya; vipaumbele vya Bajeti vya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa mwaka wa fedha 2017/2018 vimeainishwa katika maeneo ya vipaumbele katika mpango wa bajeti kama tulivyotoa katika taarifa yetu. Kamati imejiridhisha kwamba vipaumbele hivi vinawiana moja kwa moja na majukumu ya msingi ya tume na vinastahili kupewa fedha kwa ajili ya utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya bajeti ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa Mwaka 2017/2018; katika mwaka huu wa fedha 2017/2018 Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya inaomba jumla ya shilingi bilioni nne kwa Matumizi ya Kawaida kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 3.4 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo *(OC)* na shilingi milioni 567.3 kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa mamlaka hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, iliyokuwa Tume ya Kuratibu Udhitibi wa Dawa za Kulevya ambayo kwa sasa imebadilishwa na kuundwa Tume ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, inatengewa kiasi cha shilingi bilioni 2.3, kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kiasi cha shilingi bilioni nne kilichotengwa kwa mwaka 2017/2018 zimeongezeka kwa shilingi bilioni 1.6 ikilinganishwa na zilizotengwa kwa mwaka uliopita yaani 2016/2017 ambayo ni sawa na asilimia 71. *(Makofi)*

Aidha, kwa kuzingatia umuhimu wa mamlaka hii katika kudhibiti janga la dawa za kulevya nchini, kamati inapendekeza Mamlaka ya Kupambana na Kudhibiti Dawa za Kulevya Tanzania itengewe fedha za miradi ya maendeleo kiasi cha shilingi bilioni moja kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na kuiwezesha mamlaka hiyo kutekeleza majukumu ya

maendeleo ikiwa ni pamoja na utoaji wa elimu juu ya madhara ya dawa za kulevya na huduma za utengamao kwa wanarahibu wa dawa za kulevya.

Mheshimiwa Spika, katika sehemu hii ya tatu, naomba kuwasilisha maoni na mapendekezo kumi na nne ya Kamati kuhusiana na masuala yote yaliyobainika kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kutokana na sababu kuwa bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* kwa mwaka 2017/2018 imeshuka kutoka shilingi bilioni 10.1 hadi shilingi bilioni 5.9 sawa na asilimia 50; *pamoja* na Serikali kuanzisha Mpango wa *Test and Treat* kwa ajili ya kutoa dawa pale mtu atakapopatikana na maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU) kuanza kutumia dawa za kufubaza maambukizi ya UKIMWI bado bajeti hii imepungua. Kamati inashauri kwamba ni vyema Serikali ikabuni chanzo mahususi cha kutunisha Mfuko wa UKIMWI *(Aids Trust Fund)* kama ilivyo kwa mifuko mingine kama vile *REA* na maji ili kufanikisha mapambano hayo. Aidha, ihakikishe kuwa na upatikanaji wa fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, pili, kwa kuwa ipo baadhi ya Mikoa na Halmashauri zilizoshindwa kusimamia utekelezaji wa shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali *(NGOs)* katika maeneo yao ambayo yanajishughulisha na shughuli za UKIMWI, Kamati inaishauri Serikali kuweka utaratibu wa kufuatilia fedha zinazotolewa na wafadhili kwenye mashirika hayo pamoja na kuweka utaratibu wa kuzikagua fedha za mapambano ya UKIMWI kama zinatumika ipasavyo katika Halmshauri zote nchini.

Mheshimiwa Spika, tatu; kwa kuwa mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI yanahitaji nguvu ya pamoja ya kuzuia maambukizi mapya na kufikia lengo la 90 -90-90 pamoja sifuri tatu, Kamati inawashauri waratibu wa UKIMWI kuanzia ngazi ya Mkoa, Wilaya hadi Kata wafuatilie kwa ukaribu zaidi masuala ya UKIMWI na kuboresha mahusiano yao kwa kufanya kazi na vikundi mbalimbali vya WAVIU (Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI) ili kuhakikisha kuwa wanapata fursa na kunufaika na misaada mbalimbali

inayotolewa na Serikali na wadau wengine, badala ya kukaa ofisini kusubiri kupokea taarifa. Ushauri huu ukitekelezwa utalisaidia sana Taifa kupata taarifa sahihi ya maambukizi ya UKIMWI na kufahamu matatizo walionayo wanaoishi na Virusi vya UKIMWI na kufahamu maendeleo yao.

Aidha, Kamati inashauri Baraza la Taifa la Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI *(NACOPHA)* kufanya kazi kupitia vikundi mbalimbali vya KONGA kuanzia ngazi ya Kata hadi Wilaya na katika Mikoa iliyopo pembezoni mwa nchi. Serikali iendelee kushirikiana na taasisi nyingine zinazo jishughulisha na masuala ya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, nne; kwa kuwa maambukizi ya UKIMWI yanashabihiana na matumizi ya dawa za kulevya, na kwa kuwa imethibitishwa kuwa dawa za kulevya zinachangia kwa kiwango kikubwa maambukizi ya Virusi vya Ukimwi na UKIMWI kwa vijana, Kamati inaishauri Serikali kutoa elimu kwa mbinu mbalimbali ikiwemo elimu kwa njia ya sinema katika shule zote kuanzia msingi pamoja na kuandaa mitaala ya elimu ya UKIMWI katika ngazi zote za elimu, elimu ya msingi hadi chuo kikuu.

Vilevile vilabu vya kuhamasisha mapambano dhidi ya UKIMWI na dawa za Kulevya viwepo katika shule zote nchini ili kupata fursa ya kujadili masuala ya UKIMWI na dawa za kulevya. Aidha, Halmashauri zote nchini kusimamia uanzishwaji wa klabu hizo. Kamati inaona bado upo umuhimu wa *matron* na *patron* mashuleni wapatiwe elimu ya kutosha kuhusu jinsi ya kuwalea watoto wanaoishi na VVU ili kupunguza unyanyapaa. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tano; kwa kuwa bado kuna upungufu wa vituo vya afya na kliniki inayotembea kwa kuhamishika *(mobile clinic)* pamoja na uhaba wa watumishi wa afya wenye ujuzi na elimu ya utoaji nasaha na upimaji kwenye baadhi ya Halmashauri nchini, Kamati inaishauri Serikali kuongeza vituo pamoja *CTC machine* na wahudumu wa afya ili kupunguza umbali wa kupata huduma hiyo kwa wakati.

Aidha, Halmashauri zote zihakikishe kuwa wahudumu wa afya katika vituo vyote vya *CTC* wanazingatia maadili ya taaluma zao, kutunza siri za wateja wao na kutoa huduma rafiki kwa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI. Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Bohari Kuu ya Madawa kuhakikisha kuwa dawa za kuzuia magonjwa nyemelezi aina ya *septrine* na vitendanishi vinapatikana na kusambazwa kwa wakati ili kuwapunguzia gharama Watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI(WAVIU).

Mheshimiwa Spika, sita; ipo baadhi ya Mikoa na Wilaya zina mwingiliano mkubwa wa watu unaotokana na biashara mbalimbali ikiwemo madini katika Mikoa ya Manyara, Shinyanga na Geita. Aidha, huduma za miundombinu zimeboreka kwa kiasi kikubwa na hivyo, kusababisha watu wengi kuingia na kufanya biashara ndani ya mikoa hiyo na kuchangia ongezeko la maambukizi ya VVU na UKIMWI. Kamati inaishauri Serikali kuwekeza nguvu kubwa zaidi ya kutoa elimu kwa jamii hususan kubadili tabia hatatarishi na kujikinga na VVU na UKIMWI pamoja na kusisitiza matumizi sahihi ya kondomu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, saba; Kamati ilipata fursa ya kufanya ziara katika Mikoa ya Manyara, Arusha, Njombe na Iringa. Kutokana na ziara hizo, Kamati imebaini bado upo ukatili kwa wanawake na watoto unaosabaishwa na mila na desturi pamoja na mfumo dume uliotawala katika jamii hizo ambao unachangia kwa kiasi kikubwa ongezeko la maambukizi ya Virusi Vya UKIMWI. Licha ya jitihada zinazoendelea kufanywa na Serikali pamoja na wadau mbalimbali katika kupambana na janga hili. Kamati inaishauri Serikali kuchukua jitihada katika kukomesha mila na desturi potofu zinazochangia kuongezeka kwa maambukizi ya VVU na hata ikibidi kutumia vyombo vya dola pale inapobidi. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nane*;* Kamati inaupongeza Mkoa wa Manyara na Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, kwa juhudi wanazofanya kuhakikisha maambukizi yanashushwa kwa kiwango cha chini kitaifa pamoja na Mkoa kuwa na

changamoto ya mwingiliano wa watu kutoka sehemu mbalimbali. Kamati inaishauri Mikoa mingine kwenda kujifunza na kuiga mfano mzuri unaotumiwa katika mapambano haya ya kupunguza maambukizi na jinsi ya kuwahudumia WAVIU. Aidha, *TACAIDS* kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali wafanye utafiti katika maeneo yenye maambukizi madogo hususan Wilaya ya Mbulu ili kubaini kwa nini Wilaya hiyo ina maambukizi ya kiwango cha chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tisa; kutokana na matumizi ya dawa za kulevya kuchangia ongezeko la maambukizi ya VVU/UKIMWI na magonjwa ya akili miongoni mwa watumiaji wa dawa hizo hata kusababisha vifo, Kamati inaishauri Serikali kuongeza vituo vya tiba ya *methadone* angalau kituo kimoja kwa kila Mkoa ili huduma hii iwafikie wananchi wengi zaidi. Aidha, inashauriwa kuongeza nyumba za upataji nafuu za Serikali *(sober houses)* katika mikoa yote nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kumi; kwa kuwa nchi yetu imekuwa na mipaka mingi yenye vipenyo vingi pamoja na ukanda mrefu wa bahari ambao hufanya udhibiti wa uingizwaji wa dawa za kulevya kuwa mgumu, Kamati inaishauri Serikali kupitia Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa kutoa elimu kwa jamii zinazoishi katika mipaka hiyo ili zishirikiane na vyombo vya dola, hatua ambayo itasadia udhibiti wa uingizwaji wa dawa hizo hatari nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kumi na moja; Kamati imebaini kuwa bado dawa za kulevya aina ya bangi hulimwa kisiri katika maeneo ambayo hayafikiki kwa urahisi. Kamati inaishauri Serikali kufanya utafiti wa kina katika Mikoa hiyo ili kubaini ni mazao gani mbadala ambayo yanaweza kustawi kwenye maeneo husika ili kumaliza kabisa tatizo hilo la kilimo cha bangi hapa nchini pamoja na kufanya ustawi wa wakulima wetu; kutafuta mbinu mbalimbali na kuachana kabisa kuendelea na kulima mazao mbadala. Aidha, sheria kali zichukuliwe kwa yeyote atakayebainika kuendelea na kilimo hicho ikiwa ni pamoja na kutaifisha mashamba hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho bado upo ushiriki na mwamko mdogo kwa wananchi katika vita dhidi ya dawa za kulevya; pengine kwa kuwa imejengeka dhana kwamba jukumu hili ni la vyombo vya dola pekee. Kamati inaona bado elimu inahitajika zaidi kwa jamii na kwa vyombo vya ulinzi ili mapambano haya yaweze kufanikiwa. Aidha, wananchi wakihakikishiwa usalama wao na motisha ikaongeza ari ya mapambano haya na kuokoa vijana wetu ambao ndiyo nguvu kazi ya Taifa letu itaongezeka.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati kwa uchapaji kazi wao ambao kama orodha yao ilivyoonyeshwa katika taarifa yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza wewe binafsi pamoja na Naibu Spika kwa utendaji wako mzuri wa kuliongoza ipasavyo Bunge letu. Mmekuwa watu wa busara sana wakati wote wa uongozi wenu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Ajira, Vijana na wenye Ulemavu, Mheshimiwa Jenista Mhagama, kwa kutoa ufafanuzi mzuri wakati wa uchambuzi wa Bajeti hii. Aidha nampongeza pia Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania, Dkt. Leonard Maboko na Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa ushirikiano waliotupa wakati wa kipindi chote hasa pale walipohitajika kufika mbele ya kamati kwa ajili ya kutoa ufafanuzi, ambapo walifanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa muda unakaribia kuishi, pongezi hizi vilevile ziwafikie watendaji wa Bunge pamoja na Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashililah, kwa ushirikiano anaotupa na Makatibu wa Kamati yetu.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya -

Fungu 91 kiasi cha shilingi bilioni nne na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania - Fungu 92 kiasi cha shilingi bilioni 5.9.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwsilisha na nainga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA WAZIRI MKUU MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA NA TUME YA KUDHIBITI UKIMWI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

**1.1 Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Bajeti ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya – Fungu 91 na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* – Fungu 92 kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**1.2 Mheshimiwa Spika**, mtiririko wa Taarifa hii umezingatia masuala makubwa manne (4) yafuatayo bila ya kuathiri matakwa ya Kanuni ya 123 kuhusu Muundo wa taarifa za Kamati:

1.2.1 Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kamati kwa kipindi kilichopita.

1.2.2 Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

1.2.3 Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mamlaka ya Kupambana na Kudhibiti Dawa za Kulevya Tanzania kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

1.2.4 Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

1.2.5 Maoni na Ushauri wa Kamati.

1.2.6 Hitimisho

**1.3 Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Kwanza (Utangulizi) imeeleza mtiririko wa Taarifa hii ulivyo. Sehemu ya Pili inabainisha masuala muhimu yaliyojitokeza katika utekelezaji wa shughuli hizo. Kimsingi ni uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi ya Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za kulevya kwa kila kipengele kilichopo katika aya ya 1.2 hapo juu.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI WA KAMATI

**2.1 Mheshimiwa Spika,** Sehemu hii inaeleza masuala mbalimbali yaliyobainika katika utekelezaji wa shughuli za Kamati. Hata hivyo, kabla ya kueleza masuala hayo, naomba kutoa pongezi za Kamati kwa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, Mheshimiwa Dkt.John Pombe Magufuli kwa kuunda Mamlaka mahsusi ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya na kumteua Kamishina Mkuu wa Mamlaka hiyo Ndg Rogers William Siyanga. Lakini pia tunaipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kutekeleza vema mapendekezo ya Kamati ya mwaka uliopita hususan suala la kukomesha uuzaji na matumizi ya pombe kali aina ya viroba.

## 2.2MASUALA MUHIMU YALIYOBAINIKA (FINDINGS)

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu hii inaeleza mambo muhimu yaliyobainika katika utekelezaji wa shughuli za Kamati. Kutokana na masuala hayo, Kamati imendaa Maoni na Mapendekezo yatakayotolewa katika Sehemu ya Tatu kwa

ajili ya kuishauri serikali kufanya maboresho zaidi katika majukumu ya kudhibiti dawa za kulevya na UKIMWI chini.

**2.3Utekelezaji wa Mapendekezo (Hoja) ya Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha wa 2016/2017, Kamati ilitoa maoni kumi na moja (11) kwa ajili ya kutekelezwa na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kuhusiana na bajeti yake. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Tume imetekeleza vizuri maoni yote kumi na moja (11). Aidha, maoni saba (7) yaliyotolewa na Kamati kwa ajili ya kutekelezwa na Tume ya Kudhibiti UKIMWI (TACAIDS) yametekelezwa vizuri.

**2.4Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017**

**Mheshimiwa Spika**, katika eneo hili, Kamati huainisha Mipango ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI nchini na Mipango ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ili kuona kama ina uwiano wa moja kwa moja na matakwa ya Mpango wa maendeleo wa Taifa (2017/2018 - 2020/2021). Kilichobainika ni kwamba mipango na vipaumbele vyao vipo vema, tatizo lipo kwenye kiasi kidogo cha fedha kinachotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mipango na vipaumbele hivyo. Kwa mfano: Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania imeendelea kuwa na utegemezi wa fedha za nje ili kutekeleza afua za UKIMWI hali inayopelekea zoezi hili kutokuwa endelevu.

**(a)Tume ya Kudhibiti UKIMWI**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha wa 2016/2017, Tume ya Kudhibiti UKIMWI (TACAIDS), ilitengewa jumla ya shilingi **10,192,509,413/= (bilioni kumi, milioni mia moja na tisini na mbili, laki tano na tisa ,mia nne na kumi na tatu elfu),** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo, shilingi **4,957,129,000/= (bilioni nne, milioni mia tisa na hamsini na saba, laki moja na ishirini na tisa elfu)** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi **5,235,832,413/=( bilioni tano, milioni mia mbili na thelathini na tano, laki nane thelathini na mbili,mia nne kumi na tatu elfu)** kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Hata hivyo:

(i) Hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2017, Tume ilikuwa imepokea jumla ya shilingi **2,786,331,551/=** sawa na asilimia **27** ya bajeti yote. Kati ya fedha hizo, mishahara ni shilingi **986,773,800/= (milioni mia tisa themanini na sita, laki saba sabini tatu na mia nane)** sawa na asilimia **49**.

(ii)Hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2017, Tume ilipokea jumla ya shilingi **516,299,601.07/= (milioni mia tano na kumi na sita, laki mbili na tisini na tisa, mia sita na moja na sent saba)** sawa na asilimia **141** ya bajeti kwa ajili ya Matumizi mengineyo.

(iii)Hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2017, Mfuko wa UKIMWI ulipokea shilingi **400,000,000/= (milioni mia nne)** sawa na asilimia **16** ya bajeti, kwa ajili ya shughuli za maendeleo. hii ikiwa ni pungufu ya shilingi **7,411,168,962/=** sawa na asilimia **73** ya kiasi chote cha bajeti kilichotengwa.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na kupewa fedha chini ya kiasi kilichoombwa, Tume imelegalega katika kutekeleza majukumu yake. Kwa mfano, imeshindwa kuajiri watumishi katika baadhi ya Idara na vitengo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati haijaridhishwa kabisa na mwenendo wa utoaji huu wa fedha kwa Tume ya Kudhibiti UKIMWI, kwani UKIMWI ni Janga la Taifa linaloathiri zaidi nguvu kazi katika nchi yetu. Mwenendo huu wa utengaji na utoaji wa fedha kidogo unachangia mapambano dhidi ya maambukizi ya virusi vya UKIMWI kuwa magumu hivyo kutokufikia malengo ya kuzuia maambukizi mapya.

**(b)Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 iliyokuwa Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya ambayo kwa sasa haipo na imeundwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ilitengewa kiasi cha shilingi **2,340,236,000/= (bilioni mbili, milioni mia tatu na arobaini na laki mbili thelathini na sita elfu),** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake.

Hadi kufikia mwezi Machi, 2017, kiasi kilichopokelewa ni shilingi **851,170,608.08/=(milioni mia nane na hamsini na moja, laki moja na sabini, mia sita na nane na senti nane)** ambayo ni sawa na asiliia **49**. Aidha, fedha za mishahara ya watumishi zilizoidhinishwa ni shilingi **610,799,000/= (milioni mia sita na kumi, laki saba na tisini na tisa elfu)** na shilingi **1,729,437,000/ = (bilioni moja, milioni mia saba ishirini na tisa na laki nne na thelathini na saba elfu)** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo *(OC).* Kiasi cha Mishahara kilichopokelewa hadi kufikia mwezi Machi, 2017 ni shilingi **425,520,000.00/=(milioni mia tano na ishini na tano, laki tano na ishirini elfu)** sawa na asilimia **69.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaridhishwa na mwenendo huu wa utoaji wa fedha kwani ikumbukwe kuwa dawa za kulevya ni kama Janga la Taifa linaloathiri zaidi vijana ambao ndiyo nguvu kazi katika nchi yetu. Mwenendo huu wa utoaji wa fedha utasaidia kuongeza kasi ya mapambano dhidi ya dawa hizo, hivyo kuendelea kuwabaini na kuwakamata watuhumiwa na kuokoa vizazi vyetu na kuwa na Taifa lenye afya njema. Hata hivyo, kasi na juhudi za mapambano dhidi ya dawa za kulevya inapaswa kushirikiana na kasi na juhudi za mapambano dhidi ya UKIMWI.

**2.5 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI (2017/2018)**
**2.5.1 Tume ya Kudhibiti UKIMWI (TACAIDS)**
**(a)Vipaumbe vya Bajeti katika Tume**

**Mheshimiwa Spika,** Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 imeainisha maeneo ya kipaumbele katika Mpango wa Bajeti kuwa ni:-

(i)Kuboresha uratibu wa wadau wa UKIMWI na uendeshaji wa Afua za VVU/UKIMWI katika ngazi zote.

(ii)Kuboresha ushiriki wa Sekta Binafsi ili kuleta ufanisi katika kuchangia mwitikio wa Taifa dhidi ya UKIMWI.

(iii)Kuboresha upatikanaji wa taarifa za mkakati wa VVU/ UKIMWI ili kusaidia kufanya maamuzi sahihi.
(iv)Kutafuta rasilimali fedha kutoka ndani kwa ajili ya ugharimiaji wa Programu za UKIMWI nchini.

(v)Kuimarisha uwezo na ufanisi wa Tume katika kusimamia uratibu wa mwitikio wa Taifa dhidi ya UKIMWI. Hivyo, katika mapitio ya mapato na matumizi yake, Kamati ilikuwa na jukumu la kuwianisha kiasi cha fedha kilichoombwa na uzito wa majukumu (vipaumbele) vitavyotekelezwa. Kilichobainika ni kwamba endapo Tume itapewa fedha zote zilizotengwa kwa kuzingatia mpango wa mahitaji ya fedha (cash flow plan), fedha hizo angalau zitaisaidia sana Tume kukamilisha Mipango yake kwa ufanisi.

**(b)Mapitio ya Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI**
**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa Fedha 2017/2018 Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania inaomba jumla ya shilingi **5,983,975,859/=(bilioni tano, milioni mia tisa themanini na tatu, laki tisa sabini na tano, mia nane hamsini na tisa)** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo, kiasi cha shilingi **3, 455, 342, 560/=bilioni tatu, milioni mia nne hamsini na tano, laki tatu na arobaini na mbili, mia tano sitini elfu)** kwa ajili ya shughuli za Maendeleo na shilingi **2,528,633,299/= (bilioni mbili, milioni mia tano ishirini na nane,laki sita thelethini na tatu elfu na mia mbili tisini na tisa )** kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliridhishwa na mpangilio wa vipaumbele vya Tume japokuwa kuna changamoto ya ufinyu wa bajeti kwa ajili ya kutekeleza vipaumbele hivyo. Ufinyu huo wa Bajeti umekuwa ukiimbwa kila mwaka na haijulikani utaisha lini. Ni vema serikali ikajirekebisha na kuipatia Tume fedha za kutosha. Hata kama ni kidogo, basi zitolewe kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** Tume imekuwa ikijitahidi kutoa huduma chini ya mamlaka yake. Hata hivyo, kiasi cha fedha kinachotengwa na kutolewa ni kidogo sana ambacho hakiwezi kukidhi mahitaji yake, ukilinganisha na uzito wa majukumu yake. Kwa mfano, katika mwaka wa Fedha 2016/2017, kati ya shilingi **10,192,509,413/=(bilioni kumi, milioni mia moja tisini na mbili, laki tano na tisa elfu, mia nne na kumi na tatu)** zilizokuwa zimetengwa ni shilingi **2,786,331,551.07/=(bilioni mbili ,milioni mia saba themanini na sita, laki tatu**

**na thelethini na moja, mia tano hamsini na moja elfu)** sawa na asilimia **27** ya bajeti ndizo zimetolewa hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2017. Hali hii huathiri kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa majukumu ya Tume na morali ya watumishi wa Tume kutekeleza majukumu yao.

### 2.5.2 Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya

**(a)Vipaumbele vya Bajeti**

**Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 imeainisha maeneo yaliyopewa kipaumbele katika Mpango wa Bajeti kuwa:-

(i)Kuelimisha umma kuhusu madhara ya matumizi na biashara ya dawa za kulevya;

(ii)Kupata taarifa sahihi za Kiintelijensia kuhusiana na zoezi la usafirishaji, usambazaji na utumiaji wa dawa za kulevya; na

(iii)Kufanya operesheni za kukamata wanaojihusisha na biashara ya dawa za kulevya. Kamati imejiridhisha kwamba vipaumbele hivi vinavyouwiano wa moja kwa moja na majukumu ya msingi ya Tume na yatastahili kupewa fedha kwa ajili ya utekelezaji wake.

**(b)Mapitio ya Bajeti ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka huu wa Fedha wa 2017/2018, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya inaomba jumla ya shilingi **4,015,912,991/=(bilioni nne, milioni kumi tano na laki tisa na kumi na mbili elfu, mia tisa tisini na moja)**. Kati ya fedha hizo, shilingi **3,448,552,991/= (bilioni tatu, milioni mia nne arobaini na nane, laki tano hamsini na mbili elfu na mia tisa tisini na moja)** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na shilingi **567,360,000/=(milioni mia tano sitini na saba, laki tatu na sitini elfu),** kwa ajili ya Mishahara ya watumishi wa Mamlaka.

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, iliyokuwa Tume ya Kuratibu Udhitibi wa Dawa za Kulevya ambayo kwa sasa imebadilishwa na kuundwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, imetengewa kiasi cha shilingi **2,340,236,000/= (bilioni mbili, milioni mia tatu na arobaini, laki mbili thelathini na sita elfu)**, kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kiasi cha Shilingi **4,015,912,991/=(bilioni nne, milioni kumi tano laki tisa na kumi na mbili elfu mia tisa tisini namoja)** kilichotengwa kwa Mwaka 2017/2018 kimeongezeka ikilinganishwa na zilizotengwa kwa mwaka 2016/2017, imeongezeka kwa shilingi **1,675,676,991/= (bilioni moja, milioni mia sita sabini natano, laki sita sabini na sita elfu na mia tisa tisini na moja)** ambayo ni sawa na asilimia **71.**

Aidha, Kwa kuzingatia umuhimu wa Mamlaka hii katika kudhibiti janga la dawa za kulevya nchini, Kamati inapendekeza Mamlaka ya Kupambana na Kudhibiti Dawa za Kulevya Tanzania itengewe fedha za Miradi ya Maendeleo kiasi cha shilingi **Bilioni 1** kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ili kuiwezesha Mamlaka hiyo kutekeleza shughuli zake za maendeleo ikiwa ni pamoja na utoaji elimu juu ya madhara ya dawa za kulevya na huduma za utengamao kwa warahibu wa dawa za kulevya.

**MAONI:** Kamati imeridhishwa na vipaumbele na malengo yaliyowekwa na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya na Tume ya Kudhititi UKIMWI Tanzania (TACAIDS), kwa kuwa vipaumbele vyao vinaendana na Mpango wa Taifa wa Mwaka 2017/2018 na Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2017/2018 – 2020/2021). Hata hivyo, Kamati inaendelea kusisitiza serikali iendelee kutoa fedha kwa wakati kwa mamlaka hizo.

## SEHEMU YA TATU
## 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** Katika Sehemu hii ya Tatu, naomba kuwasilisha Maoni na Mapendekezo kumi na Nne (14) ya

Kamati kuhusiana na Masuala yote yaliyobainika kama ifuatavyo:

(1)Kutokana na sababu kuwa Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) kwa mwaka 2017/2018 imeshuka kutoka *shilingi* **10,192,509,413/= (bilioni kumi, milioni mia moja na tisini na mbili, laki tano na tisa, mia nne na kumi na tatu elfu),** hadi shilingi **5,983,975,859/=(bilioni tano, milioni mia tisa themanini na tatu, laki tisa sabini na tano, mia nane hamsini na tisa)** sawa asilimia **50**, pamoja na serikali kuanzisha Mpango wa Test and Treat kwa ajili ya kutoa dawa pale mtu atakapopatikana na maambukizi ya VVU kuanza kutumia dawa za kufubaza maambukizi ya UKIMWI bado bajeti hii imepungua.

Kamati inashauri kwamba ni vema serikali ikabuni chanzo mahususi cha kutunisha mfuko wa UKIMWI (AIDS TRUST FUND) kama ilivyo kwa mifuko mingine kama vile REA na maji, ili kufanikisha mapambano hayo na serikali ifikie mahali na kupata ufumbuzi wa upatikanaji wa fedha hizo.

(2)Kwa kuwa ipo baadhi ya Mikoa na Halmashauri zilizoshindwa kusimamia utekelezaji wa shughuli za mashirika yasiyo ya kiserikali *(NGOs)* katika maeneo yao ambayo yanajishughulisha na UKIMWI, Kamati inaishauri Serikali kuweka utaratibu wa kufuatilia fedha zinazotolewa na wafadhili kwenye Mashirika hayo pamoja na kuweka utaratibu wa kuzikagua fedha za mapambano ya UKIMWI kama zinatumika ipasavyo katika Halmshauri zote nchini.

(3)Kwa kuwa mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI yanahitaji nguvu ya pamoja ya kuzuia maambukizi mapya na kufikia lengo la 90 -90-90 pamoja sifuri tatu, Kamati inawashauri waratibu wa UKIMWI kuanzia ngazi ya Mkoa, Wilaya hadi Kata wafuatilie kwa ukaribu zaidi masuala ya UKIMWI na kuboresha mahusiano yao kwa kufanya kazi na vikundi mbalimbali vya WAVIU ili kuhakikisha kuwa wanapata fursa na kunufaika na misaada mbalimbali inayotolewa na Serikali na wadau wengine, badala ya kukaa ofisini kusubiri kupokea taarifa. Ushauri huu ukitekelezwa kutalisaidia Taifa kupata taarifa

sahihi ya maambukizi ya UKIMWI na kufahamu matatizo walionayo WAVIU na kufahamu maendeleo yao.

Aidha, Kamati inawashauri Baraza la Taifa la Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (NACOPHA), kufanya kazi kupitia vikundi mbalimbali vya KONGA kuanzia ngazi ya kata hadi wilaya na katika Mikoa iliyopo pembezoni mwa nchi. Serikali iendelee kushirikiana na taasisi nyingine zinazo jishughulisha na masuala ya UKIMWI.

(4) Kwa kuwa maambukizi ya UKIMWI yanashabiliana na matumizi ya dawa za kulevya, na kwa kuwa imethibitishwa kuwa dawa za kulevya zinachangia kwa kiwango kikubwa maambukizi ya VVU na UKIMWI kwa vijana, Kamati inaishauri Serikali kutoa elimu kwa mbinu mbalimbali ikiwemo elimu kwa njia ya Sinema katika shule zote kuanzia msingi pamoja na kuandaa mitaala ya elimu ya UKIMWI katika ngazi zote za elimu (elimu ya msingi hadi vyuo vikuu).
Vilevile vilabu vya kuhamasisha mapambano dhidi ya UKIMWI na dawa za Kulevya viwepo katika shule zote nchini ili kupata fulsa ya kujadili masuala ya UKIMWI na dawa za kulevya. Aidha, Halmashauri zote nchini kusimamia uanzishwaji wa Klabu hizo, Kamati inaona bado upo umuhimu wa Matron na Patron mashuleni wapatiwe elimu ya kutosha kuhusu jinsi ya kuwalea watoto wanaishi na VVU ili kupunguza unyanyapaa.

(5) Kwa kuwa bado kuna upungufu wa vituo vya afya na kiliniki inayotembea na kuhamishika (Mobile Clinic) pamoja na uhaba wa watumishi wa afya wenye ujuzi na elimu ya utoaji nasaha na upimaji kwenye baadhi ya Halmashauri nchini. Kamati inaishauri serikali kuongeza vituo pamoja CTC *mashine* na wahudumu wa afya ili kupunguza umbali wa kupata huduma hiyo kwa wakati. Aidha, Halmashauri zote zihakikishe kuwa wahudumu wa afya katika vituo vyote vya CTC wanazingatia maadili ya taaluma zao, kutunza siri za wateja wao na kutoa huduma rafiki kwa WAVIU. Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Bohari Kuu ya Madawa) kuhakikisha kuwa dawa za kuzuia magonjwa nyemelezi aina ya **Septrine** na vitendanishi

vinapatikana na kusambazwa kwa wakati ili kuwapunguzia gharama WAVIU.

(6) **Mheshimiwa Spika**, ipo baadhi ya Mikoa na Wilaya zina mwingiliano mkubwa wa watu unaotokana na biashara mbalimbali ikiwemo Madini katika Mikoa ya Manyara, Shinyanga na Geita. Aidha, huduma za miundombinu zimeboreshwa kwa kiasi kikubwa na hivyo, kusababisha watu wengi kuingia na kufanya biashara ndani ya Mikoa hiyo na kuchangia ongezeko la maambukizi ya VVU na UKIMWI. Kamati inaishauri Serikali kuwekeza nguvu kubwa zaidi ya kutoa elimu kwa jamii hususan ya kubadili tabia hatatarishi na kujikinga na VVU na UKIMWI  pamoja na kusisitiza matumizi  sahihi ya kondomu.

**(7) Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata fursa ya kufanya ziara katika Mikoa ya Manyara, Arusha, Njombe na Iringa. Kutokana na ziara hizo, Kamati imebaini bado upo ukatili kwa wanawake na watoto unaosabaishwa na mila na desturi pamoja na mfumo dume uliotawala katika jamii hizo, ambao unachangia kwa kiasi kikubwa ongezeko la maambukizi ya VVU licha ya jitihada zinazoendelea kufanywa na Serikali pamoja na wadau mbalimbali katika kupambana na janga hili. Kamati inaishauri Serikali kuchukua jitihada katika kukomesha mila na desturi potofu zinazochangia kuongezeka kwa maambukizi ya VVU hata ikibidi kutumia vyombo vya dola pale inapobidi.

**(8)Mheshimiwa Spika,** Kamati inaupongeza Mkoa wa Manyara na Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu kwa juhudi wanazofanya kuhakikisha maambukizi yanashushwa kwa kiwango cha chini kitaifa, pamoja na Mkoa kuwa na changamoto ya  mwingiliano wa watu kutoka sehemu mbalimbali. Kamati inaishauri Mikoa mingine inashauriwa kwenda kujifunza na kuiga mfano mzuri unaotumiwa katika mapambano haya ya kupunguza maambukizi na jinsi ya kuwahudumia WAVIU. Aidha, TACAIDS kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali wafanye utafiti katika maeneo yenye maambukizi madogo hususan Wilaya ya Mbulu ili kubaini kwa nini wilaya hiyo ina maambukizi ya kiwango cha chini.

**(9)Mheshimiwa Spika,** kutokana na matumizi ya dawa za kulevya kuchangia ongezeko la maambukizi ya VVU/UKIMWI na magonjwa ya akili miongoni mwa watumiaji wa dawa hizo hata kusababisha vifo, Kamati inaishauri Serikali kuongeza vituo vya *tiba* ya *Methadone* angalau kituo kimoja kwa kila mkoa ili huduma hii iwafikie Wananchi wengi zaidi. Aidha, inashauriwa kuongeza nyumba za upataji nafuu za serikali (Sober Houses) katika Mikoa yote nchini.

**(10)Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa nchi yetu imekuwa na mipaka mingi yenye vipenyo vingi pamoja na ukanda mrefu wa bahari ambavyo hufanya udhibiti wa uingizwaji wa dawa za kulevya kuwa mgumu, Kamati inaishauri Serikali kupitia Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa kutoa elimu kwa jamii zinazoishi mipakani ili zishirikiane na vyombo vya dola hatua ambayo itasadia udhibiti wa uingizwaji wa dawa hizo hatari nchini.

**(11)Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa bado dawa za kulevya aina ya bangi hulimwa kisiri na katika maeneo ambayo hayafikiki kwa urahisi. Kamati inaishauri Serikali kufanya Utafiti wa kina katika Mikoa hiyo, ili kubaini ni mazao gani mbadala ambayo yanaweza kustawi kwenye maeneo husika ili kumaliza kabisa tatizo hilo la kilimo cha bangi hapa nchini pamoja na kufanya ushawishi kwa wakulima kutafuta mbinu mbalimbali za kuacha kuendelea kulima mazao mbadala. Aidha, sheria kali ichukuliwe kwa yeyote atakae bainika kuendelea na kilimo hicho ikiwa ni pamoja na kutaifisha mashamba hayo.

**(12)Mheshimiwa Spika**, bado upo ushiriki na mwamko mdogo kwa wananchi katika vita dhidi ya dawa za kulevya pengine kwa kuwa imejengeka dhana kwamba, jukumu hili ni la vyombo vya dola pekee. Kamati inaona bado elimu inahitajika zaidi kwa jamii na kwa vyombo vya ulinzi ili mapambano haya yaweze kufanikiwa. Aidha, wananchi wakihakikishiwa usalama wao na motisha itaongeza ari ya mapambano haya na kuokoa vijana wetu ambao ndiyo nguvu kazi ya Taifa letu.

## 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee napenda niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati kwa uchapakazi wao wakati wote wa kutekeleza majukumu ya Kamati. Wajumbe wamefanya kazi kubwa katika kuhakikisha Kamati inaisimamia na kuishauri vyema Serikali kwa mujibu wa Katiba ya nchi na Kanuni za Kudumu za Bunge. Napenda kuwatambua Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, Mb -Mwenyekiti
2. Mhe. Dkt. Jasmine Tiisekwa Bunga, Mb Makamu Mwenyekit
3. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Dkt. Haji Hussein Mponda, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Daniel Edward Mtuka, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki, Mb- Mjumbe
7. Mhe. Joseph Kizito Mhagama, Mb- Mjumbe
8. Mhe. Juliana Daniel Shonza , Mb-Mjumbe
9. Mhe. Kemirembe Julius Lwota, Mb- Mjumbe
10. Mhe. Lucia Ursula Michael Mlowe, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Mary Deo Muro, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Martha Mosses Mlata, Mb- Mjumbe
13. Mhe. Masoud Abdallah Salim, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Oscar Rwegasira Mukasa, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo, Mb- Mjumbe
16. Mhe. Yussuf Kaiza Makame, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Zainab Matitu Vullu , Mb - Mjumbe
18. Mhe.Omary Ahmad Badwel, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** napenda kukupongeza wewe binafsi kwa utendaji wako mzuri na kuliongoza ipasavyo Bunge. Umekuwa mtu wa busara sana wakati wote wa uongozi wako.

**Mheshimiwa Spika,** naomba na chukua fursa hii kumpongeza Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Ajira, Vijana na Walemavu, Mhe. Jenista Mhagama, kwa kutoa ufafanuzi mzuri wakati wa uchambuzi wa Bajeti hii. Aidha, nampongeza pia Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania, Dkt. Leonard Maboko na Kamishna Jenerali

wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Ndg Rogers William Siyanga, chini ya Uongozi wa Katibu Mkuu Dkt. Hamisi Mwinyimvua na Watendaji wote wa Tume na Mamlaka kwa ushirikiano walioipa Kamati kwa kipindi chote hasa pale walipohitajika kufika mbele ya Kamati na kutoa ufafanuzi walifanya hivyo na kutoa ufafanuzi wa kina na kwa umakini mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashililah, kwa ushirikiano ambao amekuwa akiipa Kamati. Pamoja na yeye, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndg. Athumani Hussein, Wakurugenzi Wasaidizi, Makatibu wa Kamati hii; Ndg. Asia Msangi, Ndg. Happiness Ndalu na Ndg. Susan Ngole pamoja na Msaidizi wao Ndg. Grace Mwenye, kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika. Aidha, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge, kwa ushirikiano wanaoipa Kamati katika majukumu yetu ya kila siku kama Wabunge na Wajumbe wa Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (Fungu 91), kiasi cha Shilingi **4,015,912,991/= (bilioni nne, milioni kumi na tano, laki tisa na kumi , mia tisa tisini na moja elfu)** na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (Fungu 92) kiasi cha Shilingi **5,983,975,859/= (bilioni tano, milioni mia tisa themenini na tatu, laki tisa sabini na tano mia nane na hamsini na tisa elfu).**

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii.

Dkt. Jasmine Tiisekwa Bunga, (Mb)
**MAKAMU MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI**
**6 Aprili, 2017**

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Dkt. Hadji Mponda kwa niaba ya Kamati ya Masuala ya Ukimwi kwa mawasilisho yenu mazuri sana, nashukuru sana. Kwa dakika zilizobaki ni chache sana hatuwezi kumpa Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwa hiyo, yeye atakuwa msemaji wetu wa kwanza leo jioni. *(Makofi)*

Nina matangazo mawili kabla ya kusitisha shughuli. Waheshimiwa Wabunge, kesho tarehe 7 Aprili, saa itatajwa baadaye. Lakini kesho kutakuwa na semina inayohusu rushwa na Utawala Bora, semina ambayo itafanyika katika Ukumbi wa *African Dreams Conference Centre Area D* hapa Dodoma. Wale wanachama wa *APNAC* wanatangaziwa kwamba kesho kutakuwa na semina ya rushwa na utawala bora kwenye hoteli inaitwa *African Dreams* hapa Dodoma.

Narudia tena tangazo kwenu Waheshimiwa Wabunge wote wa imani ya Kikristo na imani nyingine kwamba mara tu baada tu ya kusitisha shughuli za Bunge mchana huu kutakuwa na Mtumishi wa Mungu Mwalimu Mwakasege ambaye ataongoza ibada maalum ukumbi utakaohusika ni *basement* hapo chini na siyo Ukumbi wa Msekwa kama ilivyotangazwa mwanzoni. Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa muweze kumkaribia Mungu. Labda baada ya haya mashetani yanayozungukazunguka hapa yanaweza yakapungua kidogo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, naomba kuchukua fursa hii kwa heshima kubwa kumtambulisha Mtumishi wa Mungu Mwalimu Christopher Mwakasege katika Ukumbi wa Bunge na amefuatana na Mama Mwakasege. Karibu sana Mchungaji na karibu mama, karibuni sana Dodoma. Karibuni sana hapa Bungeni. Tunaomba sana mtuombee, mkiweza mtufukuzie mapepo. *(Makofi)*

Baada ya maelezo hayo naomba sasa nisitishe shughuli za Bunge hadi saa 10.00 jioni.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 10.00 jioni)*

*(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea na kama nilivyowaambia wakati wa *session* ya asubuhi sasa ni fursa ya Kiongozi wa Upinzani Bungeni. Moja kwa moja Mheshimiwa Freeman Mbowe, nakukaribisha. *(Makofi)*

**MHE. FREEMAN A. MBOWE – KIONGOZI WA UPINZANI BUNGENI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha hotuba ya Kambi ya Upinzani Bungeni katika hoja ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imepokea kwa masikitiko makubwa taarifa za kifo cha Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Dkt. Elly Macha (Viti Maalum – CHADEMA) kilichotokea tarehe 30, Machi, 2017 huko nchini Uingereza alikokuwa matibabuni.

Mheshimiwa Spika, Marehemu alikuwa kielelezo cha mtu jasiri, mwenye kujiamini na aliyekuwa mstari wa mbele kivitendo kujiendeleza na kuwapigania wengine, tena wasio na ulemavu licha ya yeye mwenyewe kuwa na ulemavu. Ni dhahiri Taifa kwa ujumla limempoteza mpiganaji madhubuti aliyeamini na kusimamia misingi ya haki na aliyependa kuona haki ikitamalaki na kutendeka katika makundi yote ya jamii.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi, Ofisi ya Katibu wa Bunge na Ubalozi wa Tanzania nchini Uingereza chini ya Balozi Dkt. Asha-Rose Migiro, kwa namna ambavyo mmekuwa wa msaada kwa njia mbalimbali kwa Marehemu na familia yake tangu wakati wa kuugua kwake hadi sasa wakati juhudi na mipango ikiendelea ya kuurejesha nchini kwa mazishi mwili wa marehemu Dkt. Elly Macha.

Mheshimiwa Spika, tunatoa pole nyingi kwa wote walioguswa na msiba huu na tunaiombea roho ya Marehemu ilazwe mahali pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunilinda na kuniimarisha katika kuitenda kazi yake kwa njia ya siasa. Ni dhahiri siasa sasa siyo salama tena kuifanya nchini mwetu, kwani matukio kadhaa yanayotukumba wanasiasa na viongozi wa upinzani siyo ya kawaida na hayaakisi utamaduni wetu tuliouzoea kama Taifa la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa nchi na viongozi wanaoheshimu demokrasia huviona vyama vya upinzani vya siasa kama vyombo muhimu vya kuwasaidia katika kupata mawazo mbadala *(free consultancy)*, hujipima mafanikio yao kwa kuchambua kwa makini maoni ya Wapinzani na kujirekebisha pale inapobidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka mmoja na nusu wa utawala wa awamu hii tumeshuhudia manyanyaso na uonevu kwa baadhi ya viongozi na Watendaji wetu kuuawa au kupotea. Mfano aliyekuwa Mwenyekiti wetu wa Mkoa wa Geita, Mheshimiwa Alphonce Mawazo aliyeuawa mchana kweupe na watu wakishuhudia na waliohusika wanajulikana; Msaidizi wangu binafsi Ben Rabiu Saanane kupotea baada ya kupokea vitisho kadhaa vyenye asili ya kisiasa na hadi sasa vyombo vyetu vya dola havijatoa maelezo ya kina ya uwezekano wa Ben yuko wapi.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wetu nao hawajawa salama hata kidogo; tumeshuhudia Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Peter Lijualikali kufungwa kwa uonevu mkubwa; Mbunge mwenzetu mwingine, Mheshimiwa Godbless Lema kunyimwa dhamana kwa zaidi ya miezi minne kwa shitaka lenye dhamana na wengine wengi nikiwemo mimi mwenyewe na Mheshimiwa Tundu Lissu kukamatwa mara kwa mara na vyombo vya dola na kufunguliwa mashtaka mbalimbali yasiyo na nia njema wala afya kwa ujenzi wa demokrasia katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaamini mapito haya mazito ya kisiasa katika nchi yetu yanalenga kujaribu kufifisha ndoto ya kuwa Taifa huru linalosimamia misingi ya haki za

binadamu, uhuru wa maoni ya kila raia, demokrasia ya kweli, ndoto ya kuwa Taifa linaloheshimu Katiba ya nchi na ndoto ya kuwa Taifa lenye uchumi unaomnufaisha kila mwananchi.

Mheshimiwa Spika, Mwenyezi Mungu ameendelea kuwa upande wetu na hila hizo za baadhi ya wenye mamlaka hazijatuondoa kwenye lengo kubwa la kuwavusha wananchi wa Tanzania kuifikia ndoto hiyo ya Taifa, kwa sababu hiyo tuna kila sababu ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kila jambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ya Tanzania imesifika duniani kote kwa tunu zake za amani, umoja, mshikamano kutokana na waasisi wa Taifa hili kuheshimu na kuenzi misingi ya utawala wa sheria, demokrasia na uhuru wa kupata habari. Kwa mujibu wa Ibara ya 20(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ni kwamba, nanukuu:

"Kila mtu anao uhuru wa kukutana na watu wengine kwa hiari yake na kwa amani, kuchanganyika, kushirikiana na watu wengine; na kwa ajili hiyo kutoa mawazo yake hadharani na kuanzisha na kujiunga na vyama au mashirika yaliyoanzishwa kwa madhumuni ya kuhifadhi au kuendeleza imani au maslahi yake au maslahi mengineyo."

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 18 ya Katiba imeweka msingi wa uhuru wa maoni na uhuru wa kupata habari kwa kusema kwamba, nanukuu:-

"Kila mtu-

(a) Anao uhuru wa kuwa na maoni na kueleza fikra zake;

(b) Anayo haki ya kutafuta, kupokea na kutoa habari bila ya kujali mipaka ya nchi;

(c) Anao uhuru wa kufanya mawasiliano na haki ya kutoingiliwa katika mawasiliano yake; na

(d) Anayo haki ya kupewa taarifa wakati wote kuhusu matukio mbalimbali muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi na pia kuhusu masuala muhimu kwa jamii." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, tangu Serikali ya Awamu ya Tano imeingia madarakani zimeonekana dalili za wazi za Serikali hiyo kuvunja Katiba ya Nchi kwa kutupilia mbali misingi ya utawala wa sheria, demokrasia na uhuru wa kupata habari, jambo ambalo linaweza kuitumbukiza nchi yetu kwenye dola la kidikteta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matukio mahususi ya ukandamizaji wa haki na demokrasia yaliyofanywa na Serikali kinyume cha Katiba na sheria za nchi ni pamoja na haya yafuatayo: kupiga marufuku mikutano ya Vyama vya Siasa; kupiga marufuku urushwaji wa moja kwa moja *(live coverage)* kwa mijadala ya Bunge; kudhibiti Wabunge wa Upinzani wawapo Bungeni; kuingilia mhimili wa Mahakama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika...

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Kuhusu utaratibu!

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbowe, kuhusu utaratibu. Naomba ukae kidogo Kiongozi wa Upinzani.

**KUHUSU UTARATIBU**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Spika, ninayo heshima kubwa sana kwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani. Naomba kutumia Kanuni ya 68(1) lakini nitakwenda kusoma pamoja na Kanuni ya 64. Nitatumia Kanuni ya 64(1)(a), (d) na (g). Kifungu hiki cha kuingilia uhuru wa Mahakama kwa kanuni hizo nilizozisema, naomba kifungu hiki kiondolewe katika hotuba hii na sababu nilizonazo ni kama zifuatazo:-

**SPIKA:** Kifungu namba ngapi? Ukurasa wa ngapi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, ukurasa wa tano, ile namba (iv) kile kifungu chote kinachozungumzia kuingilia mhimili wa Mahakama. Yale maneno yaliyoandikwa katika kifungu hicho kwa mtazamo wangu na kwa mtazamo wa kisheria na kwa mtazamo wa Kikatiba, anayepaswa...

Mheshimiwa Spika, sijui kama umenipata hapo ninapotaka kuonesha. Natumia kitabu cha hotuba, ni kuingilia mhimili wa Mahakama.

**SPIKA:** Endelea tu maana nilikuwa natafuta kwenye kabrasha langu kubwa huku kumbe... endelea.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Katiba na kwa mujibu wa sheria, anayepaswa kulalamika kwamba ameingiliwa ni Mahakama yenyewe. Mahakama yenyewe ndiyo inayopaswa ku-*appeal* na kusema kwamba imeingiliwa uhuru wake.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Taarifa!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Spika, kilichosemwa na Mheshimiwa Rais ambacho kinaelezwa hapa na kinataka kukiuka Kanuni ile ya 64(1)(d); kutumia sasa jina la Rais hapa kuelezea hiki kilichosemwa kwenye kifungu hiki, ni kutaka kuonesha kwamba ni kama vile Mheshimiwa Rais alichokisema hakikuwa na maana halisi ya kuagiza mihimili yote...

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** ...inayoshughulika na ukusanyaji wa kodi nchini kuheshimu na kutambua.

Mheshimiwa Spika, labda nirudie tena ninachotaka kukimaanisha. Ninachotaka kusema ni kwamba hoja yangu itajengwa katika kuendelea kusisitiza ili wote tukubaliane kwamba mhimili huu umeingiliwa, ilikuwa ni lazima mhimili wenyewe utoke na kusema kwa mujibu wa sheria na Katiba, umeingiliwa; lakini haiko hivyo. Kwa hiyo, kifungu hiki kama tutakiacha kisomeke kwenye hotuba hii, ni kuvunja pia Kanuni ya 64(1)(d) ya kutumia jina la Mheshimiwa Rais kwa dhihaka na kutaka kushawishi mjadala ndani ya Bunge hili uamuliwe kwa maneno ambayo yamewekwa katika kifungu hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile kwa sababu nisingependa kusimama tena, ukienda ukurasa wa nane na ukurasa wa tisa yametumika maneno ambayo ningeomba pia kwa heshima kubwa hotuba hii itakapokuwa inasomwa maneno haya kama kunajisi, haramu na yenyewe yangeondolewa kwa sababu yanakiuka Kanuni ya 64(1)(g) ambacho kinakataza Bunge hili kutumia lugha za kuudhi ama za kudhalilisha watu wengine. Kwa hiyo, nilikuwa na hayo ya kusema. Sasa naomba unisaidie utaratibu.

**SPIKA:** Kiongozi wa Upinzani ukianza na hilo la utaratibu; *no, no, no* ngoja kwanza. Samahani Kiongozi wa Upinzani.

Mheshimiwa Ester ulisema taarifa, sijui kama unataka kuendelea nayo au tuendelee! Rudi kwanza Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani.

**TAARIFA**

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, namheshimu sana dada yangu, Mheshimiwa Jenista Mhagama. Hayo anayoyasema naona anapoteza tu muda wa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni. Sisi kama tunaona kuna viashiria vya mhimili kuingiliwa, hili ni Bunge na haya ni maoni ya Kambi ya Upinzani Bungeni. Tunatoa maoni yetu. Ni sehemu gani, ni sheria ipi, ni Kanuni gani ambayo inasema kwamba eti Mahakama wenyewe ndiyo

wana *mandate* ya kusema wanaingiliwa? Siyo kweli! Sisi ni Wawakilishi wa Wananchi na tunapaswa kutoa maoni yetu kwa mujibu wa taratibu. Tunachofanya sisi ni kutoa maoni, kama ninyi mtajibu, mtajibu baadaye. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Watu wakionewa huko nje, Bunge...

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Huko nje sisi tusiseme? Ndiyo kazi yetu kusema. Kwa hiyo, wewe subiri, utakapojibu, ndiyo ujibu. Siyo kumkataza Kiongozi wa Kambi ya Upinzani asitoe maoni yake. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ester. Hiyo ilikuwa taarifa kwa Mheshimiwa Mhagama halafu Mheshimiwa Profesa nilikuona; lakini subiri kidogo Mheshimiwa Mhagama kwanza apewe haki yake ya hiyo taarifa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Spika, wote humu ndani tunaheshimiana, namheshimu sana Mheshimiwa Ester Bulaya, kama alivyosema ananiheshimu, nami namheshimu sana.

Mheshimiwa Spika, tunaongozwa na Kanuni, Katiba na sheria za nchi. Tunaporuhusu ndani ya Bunge tukubaliane kwamba mhimili wa Mahakama ambao upo Kikatiba umeingiliwa ni lazima tuwe na ushahidi uliopindukia wa kuthibitisha jambo hilo kwamba ...

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio )*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa!

**SPIKA:** Kama nilivyosema mwanzoni, uvumilivu ni muhimu sana. Tupeane nafasi, kwa sababu tumempa Mheshimiwa Ester hapa, mmeona ameongea tu vizuri na watu wote wamenyamaza...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa!

**SPIKA:** Sasa nawaomba sana, nanyi muwe mnatulia kidogo. Halafu kumbukeni atasimama Kiongozi wa Upinzani mwenye maneno yake ndiye hasa atapewa nafasi afafanue hasa alimaanisha nini.

Niwaambie Makatibu, naambiwa Wabunge wote hawana nakala hizi, kwa hiyo, fanyeni haraka sana. Taarifa hii ilichelewa kupelekwa ofisini kwa ajili ya kuchapishwa, naamini ndiyo imesababisha kidogo ucheleweshwaji huu, mtuvumilie. Kwa sababu mpaka saa saba mchana, wakati tunaahirisha Bunge ilikuwa bado haijafika kwenye *printing.*

Kwa hiyo, hata mimi mwenyewe kitabu ambacho nakitumia hata Mheshimiwa Waziri anakitumia mimi bado sijapata pia. Kwa hiyo, akiniambia ukurasa nahangaika kweli kwenda huku na huku. Nawaomba Makatibu wangu hata kama ni vichache ambavyo viko tayari vingekuja kwanza vigawiwe haraka sana.

Mheshimiwa Waziri, tafadhali!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naendelea kujenga hiyo hoja. Mhimili huo kama tunakubali wote humu ndani kwamba hiki kifungu tunapokiacha kiingie kwenye *Hansard* ni kwamba Bunge limekubaliana jambo hili. Kwa hiyo, kwa mujibu wa Katiba, kwa mujibu wa sheria tulizonazo, naomba kipengele hiki kiweze kuondolewa na hivyo taarifa ya Mheshimiwa Ester kwa kweli namheshimu sana lakini sitaipokea kama hivyo alivyoileta mbele yako.

**SPIKA:** Waziri wa Sheria, Mheshimiwa Profesa Kabudi, nilikuona!

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, kuku mgeni hakosi kamba mguuni, kwa hiyo, ndiyo maana hata nimeshindwa

kubonyeza *microphone*. Ahsante sana binti yangu, Mheshimiwa.

Mheshimiwa Spika, mimi pia sijaona hotuba yote, lakini ningesihi jambo moja; tunayo mihimili inayojisimamia, inayojitegemea na kila mhimili umepewa mipaka yake na maeneo yake ya kushughulikia. Mahakama haiwezi kuuingilia mhimili wa Bunge mpaka Bunge lenyewe liwe limeomba kupata maelekezo ya Mahakama na kama kuna mhimili ambao ningelisihi sana Taifa hili tusili-*politicize* ni Mahakama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, lugha yoyote inayohusu Mahakama kwa kiasi kikubwa ni lazima tuwe na tahadhari kwa sababu tutakapoanza kukizungumzia chombo hiki na sisi hatukai na *Acting Chief Justice,* sisi hatukai na Majaji, sisi hatukai ndani ya Mahakama, tunaweza kuwa tunapeleka picha isiyokuwa sahihi. Kwa hiyo, kama yapo maelezo hayo ya mhimili wa Mahakama kuingiliwa, nashauri sehemu hiyo katika hotuba iondolewe ili tusonge mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema nitaipata hotuba niisome; kuhusu Mheshimiwa Rais napenda pia ndani ya hotuba hii, maeneo ambayo yanamhusu Mheshimiwa Rais, kwa sababu haturuhusiwi kumjadili Mheshimiwa Rais katika ngazi zake zifuatazo:-

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio )*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Ngoja; ngazi ya kuwa Mkuu wa Nchi na ngazi ya kuwa Amiri Jeshi Mkuu. Inapokuwa katika ngazi ya yeye kuwa Mkuu wa Nchi, anapokosea au tunapohisi amekosewa watu wa kuwajibishwa kwa mujibu wa Ibara ya 36 ya Katiba hii ni wale aliotuteua.

Kwa hiyo, maelekezo hayo yataelekezwa kwa Serikali bila kumtaja yeye, kwa Mawaziri bila kumtaja yeye. Kwa nini? Rais huyu ana kofia ya Ukuu wa Nchi, ana kofia ya Uamiri Jeshi Mkuu. Ndiyo maana katika nchi zote za *Commonwealth,*

ikifika katika *level* hiyo, iwe ni India au Uingereza, wenzetu wana bahati kwamba Mkuu wa Nchi hasimamii Serikali, hatajwi na pale anapotajwa kama sisi kwetu, hayo hayo.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** *South Africa!*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, *South Africa* Rais wao ni tofauti na wa kwetu; yeye ni sehemu ya Bunge kwa maana anakaa Bungeni. Yule anatumia *Roman-Dutch Law,* hatumii *Commonwealth* peke yake Mheshimiwa Msigwa, anatumia *Roman-Dutch Law.*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nashauri *reference* zinazokwenda kwa Mheshimiwa Rais zielekezwe kwa Serikali, zielekezwe kwa Mawaziri bila kuziondoa; yaani ziwemo lakini *reference* iletwe kwa Serikali. Narudia tena, *reference* iletwe kwa Serikali, iletwe kwa Mawaziri. Sijasema hayo yanayosemwa yaondolewe, yanayosemwa yasemwe lakini *reference* iwe *refered* kwa Serikali, kwa Mawaziri na siyo kwa yeye. Huo ndiyo utaratibu. Ni pamoja na mimi. Hata akifanya yeye, tuko hapa kwa sababu yeye ametuleta hapa.

Kwa hiyo, naomba *reference* ya kwa Mheshimiwa Rais iondolewe ndani ya hotuba na badala yake *reference* hiyo iwe kwa Serikali na sisi aliotuteua kumfanyia kazi humu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni, ushauri huo uliopewa, ushauri wa busara.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE – KIONGOZI WA UPINZANI BUNGENI:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu Waheshimiwa Wabunge wengi walikuwa hawajaipata hotuba yenyewe na mimi nilijaribu kuokoa muda kwa kusoma tu *headline,* pengine nisome *paragraph* yenyewe ili waelewe nashangaa tunabishana nini.

Mheshimiwa Spika, nilichokisema, naomba nirudie; na naomba muda wangu unilindie Mkuu. Nilisema kuhusu

kuingilia mhimili wa Mahakama. Maneno niliyosema ni haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ya CCM kupitia Rais kwa nyakati tofauti imeonekana kujaribu kuingilia uhuru wa Mahakama jambo ambalo ni hatari kwa utoaji wa haki nchini. Katika hotuba yake, wala sijaingilia Mahakama wala sijagusa Mahakama, wala sijagusa mhimili wa Mahakama; nagusa kauli zilizotolewa ambazo zinaashiria kutaka kuingilia mhimili wa Mahakama. Nikasema hivi, kupitia hotuba yake wakati wa maadhimisho ya Siku ya Sheria Duniani, Mheshimiwa Rais alinukuliwa akisema kwamba Mahakama iwahukumu haraka haraka watu waliokwepa kodi halafu atatumia asilimia fulani ya fedha ambazo zitakuwa zimepatikana kutokana na *fine* za wale walioshindwa kesi kuwapa Mahakama ili wafanye kazi vizuri ya kuendelea kuwahukumu na kuwafunga wakwepa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa hatujaingilia uhuru wa Mahakama kabisa. Nilisema kauli kama hizi zinapotolewa na Mkuu wa nchi ndiyo hapo inapoashiria kwamba Mahakama inaweza ikaingiliwa, ikakosa uhuru wa kutenda kazi yake kwa weledi ambao unaostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba niseme tu, hatutumii kwa dhihaka kabisa jina la Rais mahali hapa, ila tumetoa tu nukuu ambayo ilikuwa ni wazi kabisa katika jambo hili.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Kuhusu utaratibu.

**SPIKA:** Kuhusu utaratibu Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni. Mheshimiwa Simbachawene, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, utaratibu huo ni kutoka Kanuni ya 68(1), lakini nainukuu kanuni iliyovunjwa ambayo ni Kanuni ya 64...

**MBUNGE FULANI:** (Aliongea nje ya *microphone*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Huwezi kunifundisha mambo haya. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 64(1)(c); neno lililotumika ni rahisi sana na Mheshimiwa Mbowe kwa sababu ni Kiongozi wa Upinzani Bungeni, anafahamu vizuri anachokizungumza. Kanuni hii inakataza kuzungumzia mwenendo wa Rais, ni kanuni. Kusema kitu ambacho kinamu-*implicate* Rais au shughuli anazofanya Rais au matamko aliyoyafanya Rais, siyo jambo sahihi kwa mujibu wa kanuni hii.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio )*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Ndiyo! Kanuni inakataza kwamba bila ya kuathiri masharti ya ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge:-

(e) Hatazungumzia mwenendo wa Rais, Spika, Mbunge, Jaji, Hakimu au mtu mwingine yeyote anayeshughulikia utoaji wa haki isipokuwa tu kama kumetolewa hoja mahususi juu ya jambo hilo. Sasa hapa hakuna hoja mahususi iliyotolewa juu ya mwenendo wa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama kunajadiliwa masuala yanayomhusu Rais au wewe Spika au Jaji au mtu yeyote anayetoa haki, hairuhusiwi kujadili mwenendo wake. Katika kusema yale, huwezi kujua kuna maslahi mapana mangapi ya Taifa alikuwa anajitahidi kuyaokoa. Katika kusema vile yeye kama Mkuu wa Nchi na Amiri Jeshi Mkuu ana mambo mangapi anayoyafahamu ambayo wewe kwa sababu huna vyombo huyajui? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Rais ni kitu cha tofauti tunapomzungumzia katika ukuu wake. Ndiyo maana kinachowajibika humu ndani, ni upande wa pili wa kofia ya Rais ya *Executive.* Ukuu wa nchi haumo humu ndani mpaka kuwe kuna hoja mahususi. Kwa hiyo, kwa kofia ya pili ya Rais ya ukuu wa nchi, hiyo ya kwanza hakuna mtu mwenye hadhi ya kujadili mwenendo wa Rais humu, kama tu ambavyo ilivyo kwamba Spika mwenendo wako, maamuzi unayoyafanya hawezi mtu hapa akasema tuyajadili ikapika hoja hapa ya kujadili mwenendo wako. Ila watu wanaweza wakakushauri, wakakuelekeza kwa mujibu wa kanuni kwamba kuna jambo fulani limeenda vibaya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, huo ndiyo mwongozo nilitaka utoe juu ya kanuni hii, mbona inavunjwa?

**SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Mbowe nakupa nafasi ya mwisho. Nakushauri ili hotuba yako iwe na maana na iendelee, nafikiri busara umeiona lakini naomba urudi tukusikie, umesikia ushauri wote huo.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE - KIONGOZI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu siyo lengo langu kulumbana, nakubali sehemu hiyo iondolewe katika *Hansard* lakini ujumbe utakuwa umefika. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakushauri vilevile ule ushauri mwingine uliopatikana kwa huko mbele, dakika zako tumezitunza, naomba sasa uendelee.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE - KIONGOZI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI:** Mheshimiwa Spika, naomba niendelee sasa. Uonevu unaofanywa na vyombo vya dola dhidi ya wananchi wa visiwa vya Unguja na Pemba. Wananchi wa Zanzibar waliukataa utawala wa CCM kupitia sanduku la kura katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2015. Serikali ya Muungano ikishirikiana na Serikali ya Mapinduzi

Zanzibar wakafanya hila kupora ushindi wa Wazanzibari kwa kufuta uchaguzi ule bila sababu za msingi za kuitisha uchaguzi mwingine haramu ambapo ulisusiwa na Chama cha Wananchi - *CUF* kilichokuwa kimeshinda uchaguzi uliofutwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na tukio hilo, Serikali ya Muungano ikishirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imeamuru vyombo vya dola vikiwemo Jeshi la Polisi, Jeshi la Wananchi Tanzania na Usalama wa Taifa kuwaadhibu wananchi wa Zanzibar hususan wanaounga mkono Chama cha Wananchi – *CUF* kwa kuwavamia nyakati za usiku na kuwakamata, kuwapiga, kuwafungulia mashtaka bandia na kupora mali zao ikiwemo mifugo. Huu ni ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu unaopaswa kulaaniwa na watu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kilio cha hitaji la Katiba Mpya ya nchi yetu kilianza kusikika tangu mfumo wa siasa ya vyama vingi uanze hapa nchini miaka 25 iliyopita. Haina shaka kwamba Vyama vya Upinzani ndivyo vilivyoanza kutoridhishwa na mfumo wa uchaguzi, madaraka makubwa ya Rais na mfumo mzima wa utawala na uendeshaji wa Serikali mambo yaliyoanzisha ajenda ya madai ya Katiba Mpya.

Mheshimiwa Spika, baada ya mapambano hayo ya kudai Katiba mpya, hatimaye Serikali ilianzisha mchakato wa Katiba mpya. Mchakato huo ulianza kwa Bunge kutunga Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, Sura ya 83 mnamo mwezi Novemba, 2011 na baadaye kufanyiwa marekebisho mwaka 2012 na 2013. Aidha, Bunge lilitunga Sheria ya kura ya maoni mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho chote, Rais Mstaafu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete aliunda Tume ya Mabadiliko ya Katiba ambayo ilifanya kazi kubwa ya kukusanya na kuyachambua maoni ya wananchi hadi kupata Rasimu ya kwanza ya Katiba mnamo tarehe 3 Julai, 2013.

Mheshimiwa Spika, rasimu hiyo ilipelekwa kwa wananchi kupitia Mabaraza ya Katiba kwa ajili ya maoni zaidi na hatimaye baada ya kuzingatia maoni ya wananchi ikatengenezwa rasimu ya pili ya Katiba ambayo ilikabidhiwa katika Bunge Maalum la Katiba kwa ajili ya kujadiliwa ili kupata Rasimu ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wananchi wa Tanzania Bara wanahitaji mabadiliko makubwa ya kimuundo na kimfumo katika uendeshaji wa Serikali, mabadiliko ambayo msingi wake ni Katiba mpya; na kwa kuwa Mgombea wa Urais na sasa Rais kupitia CCM aliwaahidi wananchi kuleta mabadiliko hayo na kuongeza kuwa hatawaangusha; hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutekeleza ahadi hiyo kwa kurejesha tena mchakato wa Katiba Mpya.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kuwa mchakato wa Katiba mpya urudishwe nyuma katika ngazi ya Bunge Maalum ili kujadili maoni ya wananchi katika Rasimu ya Pili ya Katiba iliyowasilishwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba bila kuathiri maudhui ya maoni ya wananchi kuhusu Katiba mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uchumi ndiyo msingi wa maisha ya binadamu. Hitilafu yoyote inayotokea katika ukuaji wa uchumi inakuwa na athari ya moja kwa moja kwa maisha ya wananchi. Tangu Serikali hii ya Awamu ya Tano iingie madarakani, imekuwa ikijinasibu kuwa uchumi wa nchi unakuwa kwa kasi ikilinganishwa na Serikali za awamu zilizotangulia, lakini kumekuwa na kilio kikuu kwa upande wa wananchi kuhusu hali ya maisha kuendelea kuwa ngumu kuliko wakati wote katika historia ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kilio hiki cha wananchi kinamaanisha kwamba ukuaji wa uchumi unaohubiriwa na Serikali haujawafikia wananchi ambao ndio wadau wakubwa wa nchi hii. Wanazuoni wa uchumi wanasema kwamba, naomba kunukuu kwa lugha ya Kiingereza;

*"Growth is inclusive when it takes place in the sectors in which the poor work (e.g. agriculture); occurs in places where the poor live (e.g. underveloped areas with few resources); uses the factors of production that the poor possess (e.g. unskilled labour); and reduces the prices of consumption items that the poor consume (e.g. food, fuel and clothing)."*

Mheshimiwa Spika, kwa tafsiri isiyo rasmi ni kwamba ukuaji wa uchumi unakuwa shirikishi unapotokea kwenye sekta ambazo watu maskini wanafanya kazi kama vile kilimo; unatokea katika maeneo ambayo watu maskini wanaishi kwa mfano maeneo ambayo hayajaendelea na yasiyo na rasilimali nyingi; unatumia nyenzo za uzalishaji ambazo watu maskini wanazo kwa mfano nguvukazi isiyo ya kitaalam; na unapunguza bei za bidhaa ambazo watu maskini wanatumia kwa mfano chakula, mafuta na nguo.

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huo, ukipima hali ya Tanzania utaona kwamba uchumi wetu siyo shirikishi kwa kuwa ukuaji wake hautokei katika sekta ambazo watu maskini wanafanya kazi au maeneo ambayo watu maskini wanaishi. Aidha, ukuaji wa uchumi wetu hautumii nyenzo za uzalishaji ambazo watu maskini wanazo na pia ukuaji huo haujapunguza bei za bidhaa ambazo watu maskini wanatumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwa makini vipaumbele vya Serikali ya Awamu ya Tano, utagundua Serikali haina mkakati wowote madhubuti wa kuinua uchumi wa wananchi waishio vijijini *(Rural economy).* Uchumi wa Vijijini unagusa kilimo, uvuvi na ufugaji na sekta hizo ndizo zenye uwezo mkubwa wa kuajiri watu na kupunguza umaskini. Tukumbuke asilimia zaidi ya 70 ya Watanzania wanaishi vijijini na wanategemea sekta hizi.

Mheshimiwa Spika, duniani kote, hakuna nchi iliyowahi kufanikiwa kuingia kwenye uchumi wa viwanda kabla ya kupitia mageuzi ya kilimo. Nchi zote za Asia ambazo tunapenda kuiga *economic model* zao ziliendeleza kwanza

kilimo na bado pamoja na kuingia kwenye uchumi wa viwanda, bado idadi kubwa ya watu wao wanaendelea na sekta hizi za *rural economy.*

Mheshimiwa Spika, kilicho dhahiri ni kuwa Serikali ya Awamu ya Tano haikujiandaa na sera hii na inakurupuka kufanya mambo mbalimbali bila kuwa na mpango madhubuti wenye maeneo yanayopimika *(Integrated Rural Development Plan).* Kwa miaka ya karibuni mchango wa Sekta ya Kilimo unazidi kushuka na sasa ni pungufu ya asilimia 2.5 ya *GDP. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sekta hizi za Kilimo, Ufugaji na Uvuvi zilipewa asilimia 2.22 tu ya fedha zilizoidhinishwa kwa shughuli za maendeleo ambazo ni sawa na shilingi bilioni 2.2 kati ya shilingi bilioni 101.5 zilizowekwa na bajeti ilhali zaidi ya shilingi bilioni 128 zimetumika kama malipo ya awali kununulia ndege za *Air Tanzania*, bila hata ya kuwepo *Business Plan*. Serikali hii, ndege zinazohudumia wananchi wasiozidi 100,000 ni muhimu na kipaumbele kuliko sekta inayogusa zaidi ya 70 *percent* ya wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uchambuzi uliofanywa na wataalam wa uchumi inaonesha kwamba uchumi wa Tanzania upo hatarini kuporomoka kutokana na mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Tanzania bado iko katika hali tete ya kisiasa kufuatia uchaguzi wa mwaka 2015, ambapo suala la Zanzibar bado halijatatuliwa na kuendelea kukiukwa kwa misingi ya kidemokrasia, kubinywa kwa uhuru wa siasa za vyama vingi na uhuru wa vyombo vya habari. Jambo hili limeathiri uhuru wa kiuchumi na limewatia hofu wafanyabiashara wa ndani na nje hivyo kupunguza kasi ya uwekezaji na ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya Umoja wa Mataifa ya *Human Development Indicator,* bado Tanzania inashika nafasi ya chini katika vigezo vya Kimataifa vya ustawi wa jamii na utawala bora. Kwa mujibu wa taarifa hiyo,

Tanzania inashika nafasi ya 151 kati ya 187. Aidha, kigezo cha ustawi kijinsia kinaishusha Tanzania kwenye nafasi ya chini zaidi, yaani 129 kati ya nchi 159, yaani ni wa 20 kutoka mkiani.

Mheshimiwa Spika, kukwama kwa mchakato wa Katiba mpya ya wananchi kumesababisha kuwa na hali ya *Constitutional uncertainity* jambo ambalo wachambuzi wa masuala ya kiuchumi wanaliona kuwa na tishio au *'threat'* kiuchumi. Hii ni kwa sababu nchi inapokuwa katika mkwamo wa kupata Katiba inayoridhiwa na wananchi huweza kusababisha machafuko ya kisiasa *(Political instability)* na jambo hili huwatia hofu sana wafanyabiashara na wawekezaji wakubwa jambo ambalo huwafanya kuzuia mitaji yao mikubwa kwenda katika nchi yenye hali kama hiyo. Hili nalo limetuathiri kwa kiwango kikubwa na ndiyo maana kumekuwa na malalamiko miongoni mwa wananchi kwamba mzunguko wa fedha ni mdogo.

Mheshimiwa Spika, tayari Shirika la Fedha Duniani *(IMF)* limeionya Tanzania kuwa uchumi wake uko hatarini kuporomoka kutokana na kubana matumizi kulikopitiliza, kushuka kwa idadi ya mikopo, utekelezaji hafifu wa uwekezaji wa umma na kutotabirika kwa sera za Serikali kuhusu sekta binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *IMF* wanasema hivi kuhusu uchumi wa Tanzania, naomba kunukuu kwa lugha ya Kiingereza: *"There are risks that could adversely affect economic growth going forward, arising from the currently tight stance of macroeconomic policies, the slow pace of credit growth that may become protracted, slow implementation of public investment and private sector uncertainty about the government's new economic strategies."*

Mheshimiwa Spika, *IMF* wanapendekeza Sera za Fedha zilegezwe ili kuondoa tatizo la mzunguko mdogo wa fedha unaotokana na kubana matumizi pamoja na kuisadia sekta binafsi kupata mikopo. Nanukuu kwa Kizungu:

*"Monetary policy should be eased to address the tight liquidity situation and support credit to the private sector."* Hii ni pamoja na kulipa wakandarasi mbalimbali wanaoidai Serikali, kwani deni la ndani sasa linakaribia kufikia trilioni tano.

Mheshimiwa Spika, angalizo hili la *IMF* limechangiwa na wabobezi wa uchumi akiwemo Profesa Gabagambi wa Chuo Kikuu cha Mzumbe anayesema, nanukuu kwa Kiingereza*: "In fact right now, you could say we are in the stage of a recession and if we don't take heed of the IMF advice and act, the country may enter the stage of depression, which is worse."*

Mheshimiwa Spika, ushauri unaotolewa na mchumi huyu ni kwamba tutekeleze ushauri wa *IMF*, tusipotekeleza ushauri wa *IMF* ni kwamba nchi itaingia kwenye anguko kuu la uchumi, *(economic depression).*

Mheshimiwa Spika, pamoja na umuhimu wa kuhakikisha rasilimali za nchi zinainufaisha nchi yetu, ni muhimu kwa viongozi wetu kutambua *sensitivity* ya *Multinational Corporations* inapokuja kwenye suala la kubadilisha au kutokuheshimu mikataba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pale ambapo Serikali inaona kuna mambo hayako sawa itake mazungumzo ya kurejea mikataba kabla ya kutoa makatazo hadharani kama ilivyokuwa kwa katazo la kupeleka mchanga wa dhahabu nje ya nchi kwa uchenjuaji linalohusu Kampuni ya *Acacia* inayochimba dhahabu nchini. Mambo haya yanahitaji muda na mpango na kamwe kukurupuka kutakuja kulisababishia Taifa hili ulipaji wa fidia kubwa sana na kibaya zaidi kuua kabisa imani ya wawekezaji wakubwa hususan wa Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, madeni ya Taifa hadi Desemba, 2016 yamefikia zaidi ya Dola za Kimarekani bilioni 20.7 yakiwemo ya ndani na nje ikiwa ni pamoja na mifuko ya hifadhi ya jamii.

Mheshimiwa Spika, kiwango hiki ni takriban shilingi za Kitanzania trilioni 46.66. Kasi ya kukua kwa deni hili inazidi kushika kasi kutokana na riba na adhabu mbalimbali zitokanazo na kuchelewa kulipa kwa wakati madeni yetu. Aidha, kuongezeka huku kunachangiwa vilevile na Serikali kuendelea kukopa hususan kwenye vyanzo vya kibiashara ambazo riba zake ni kubwa.

Mheshimiwa Spika, deni la nje sasa hivi linaigharimu Serikali karibu nusu ya makusanyo yake yatokanayo na kodi. Ukichanganya na mishahara, karibu asilimia 70 ya mapato ya ndani yanatumika kulipia deni la nje na mishahara ya watumishi mbalimbali wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, mara kadhaa watu wengi wametahadharisha kuhusu athari za kukopa kuliko uwezo wetu; na Serikali imejitetea kwamba deni la nchi ni stahimilivu. Pamoja na ustahimilivu huo, sasa athari zake zinaanza kuwa kubwa katika kutekeleza bajeti na hivyo mipango ya Serikali ikiwemo miradi ya maendeleo mbalimbali kukwama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa rai kwa Rais kuacha kukwepa kuhudhuria Mikutano ya Kimataifa na ya Kikanda ambayo ni muhimu kwa ajili ya kujenga mustakabali wa diplomasia ya uchumi pamoja na uhusiano wa Kimataifa kwa ujumla kama ambavyo umekuwa ni utamaduni wa Taifa letu. Aidha, washauri wa Rais hasa wa masuala ya Kimataifa wamshauri Mheshimiwa Rais juu ya umuhimu wa ushiriki wake katika vikao na mikutano hiyo pamoja na kuzingatia itifaki za Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna udhaifu mkubwa sana katika Serikali hii wa kutozingatia itifaki za Kimataifa. Wengi walishangazwa wakati Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa anakuja nchini na kupokelewa na Waziri wa Mambo ya nje bila kupata fursa ya kuonana na Mheshimiwa Rais. Inaweza kukaonekana kuwa ni jambo la kawaida tu, lakini Rais

kutompokea Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa na katika jicho la kidiplomasia, kuna makosa makubwa sana ya kiitifaki yanayofanywa na wasaidizi wa Ofisi ya Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uhusiano wa Kimataifa unaweza kuathiriwa na namna sisi kama Taifa tunavyowatendea raia wa nchi nyingine wanaoishi au kufanya kazi katika nchi yetu. Mataifa mengine huwa yanajali sana hali za raia wao wanaoishi au kufanya kazi katika Mataifa mengine. Hivyo, Mataifa hayo huwa yako tayari hata kupigana vita kwa ajili ya raia wao wanaonyanyaswa au kutendewa visivyo katika nchi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitendo cha hivi karibuni cha Kiongozi wetu kuagiza pasi ya kusafiria ya Mkandarasi kutoka India ambaye anajenga mradi wa maji Nganga huko Lindi kutokana na makosa aliyoyafanya katika mradi huo, unaweza kuingiza nchi yetu katika mgogoro wa kidiplomasia kwa sababu pasi ya kusafiria ni mali ya Taifa lingine ambalo limetoa pasi hiyo. Katika pasi hiyo kuna tamko la Rais wa nchi husika linaloomba raia huyo apewe ulinzi na msaada wowote utakaokidhi katika nchi anayokuwa ameingia kuishi na kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, agizo la kiongozi la kushikilia *passport* ya mkandarasi huyo tayari limeripotiwa katika vyombo mbalimbali vya habari vya Kimataifa ambavyo kwa vyovyote vile vinasomwa na watu mbalimbali duniani wakiwemo wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina vyombo vya ulinzi na usalama mpaka mipakani, kama mwekezaji au mkandarasi kutoka nje amepewa maelekezo ya kumaliza mradi kwa muda fulani, ni vyema akapewa nafasi ya kufanya hivyo bila kuchukua pasi yake ya kusafiria. Mambo yote hayo yanafanyika kwa mujibu wa mikataba ambayo Serikali imeingia na wawekezaji au Wakandarasi na hivyo ni vyema mikataba ikazingatiwa na/au maelekezo/makubaliano mengine kuliko kuanza kuchukua pasi za kusafiria za Mataifa mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, athari za maamuzi au amri za viongozi zinaweza zisionekane leo, lakini kwa utafiti wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ni kuwa agizo la Kiongozi la kuamuru pasi ya raia mwingine kuchukuliwa liliripotiwa katika vyombo vya habari vingi duniani pamoja na nchi ya India yenyewe. Jambo hili siyo tu linatia doa nchi yetu katika masuala ya uhusiano wa Kimataifa, lakini pia linaweza kuleta athari katika Sekta ya Uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Utumishi wa Umma imegubikwa na hofu kubwa hivi sasa kutokana na utumbuaji holela wa Watumishi usiozingatia sheria za nchi. Watu wachache wanaamini wao wana mamlaka ya kuamua vile wanavyoona inafaa wao kwa utashi wao bila kuzingatia sheria za nchi. Ifahamike kuwa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeti haipuuzi hata kidogo jitihada zinazofanywa na kila mmoja wetu katika kuhakikisha Sekta ya Umma inafanya kazi kwa weledi ili kuleta tija katika Taifa. Jitihada hizi ni lazima zizingatie sheria na taratibu tulizojiwekea kama Taifa ili kuepusha uonevu na matumizi mabaya ya madaraka kwa waliopewa dhamana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendesha zoezi la uhakiki wa Watumishi wa Umma ikiwa ni pamoja na vyeti vya taaluma zao ili kukabiliana na tatizo la Watumishi hewa pamoja na Watumishi wasio na sifa. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haina tatizo na zoezi la namna hiyo kwa kuwa linalenga kuokoa fedha za umma zinazopotea kutokana na watumishi hewa na kudhibiti ubora wa huduma zinazotolewa katika Sekta ya Umma kwa kuhakikisha watumishi wote wana taaluma au sifa stahiki katika kazi wanazozifanya.

Mheshimiwa Spika, pamoja na dhamira hiyo njema ya Serikali ni muhimu kazi hii ikafanywa kwa weledi bila kuathiri masharti ya Ibara ya 13(1) ya Katiba ya nchi inayoonya ubaguzi wa aina yoyote kwa mtu yeyote bila kujali cheo chake, kabila lake, dini yake, elimu yake na hata jinsia yake.

Mheshimiwa Spika, wapo Watanzania wengi waliochukuliwa hatua baada ya kukutwa na vyeti feki, lakini cha ajabu ni kuwa kitendo cha Mheshimiwa Kiongozi Mkuu kuendelea kumkingia kifua Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Christian Makonda, ambaye anashutumiwa kutumia cheti ambacho siyo chake na kushindwa hata kuamuru uchunguzi wa jambo hili ufanyike, ni kitendo cha kufedhehesha sana kwani kinawagawa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ubaguzi wa namna hiyo unalifanya kundi fulani kujisikia wanyonge na hawana haki na kundi lingine kujisikia wao wana haki zaidi ya wengine. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutenda haki katika zoezi hili la uhakiki kwani limeshaanza kuonesha dalili za ubaguzi na upendeleo jambo ambalo linasababisha matabaka ya watu katika Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kutambua jitihada za Serikali, Waheshimiwa Wabunge na jamii kwa ujumla kwa kushirikiana kwa pamoja katika kupambana na biashara ya madawa ya kulevya pamoja na matumizi ya aina yoyote ya madawa ya kulevya. Sote tunatambua madhara makubwa ya madawa haya kwa kuwa tumepoteza ndugu, jamaa, marafiki na nguvu kazi ya Taifa kutokana na matumizi ya dawa za kulevya.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni harakati hizi zilichukua sura mpya baada ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam kuwataja hadharani watuhumiwa wa dawa za kulevya. Jambo hili lilizua mtanzuko mkubwa kwa wanajamii huku kila mmoja akilipokea kwa namna yake.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha kuwataja watu hadharani nikiwemo mimi mwenyewe ninayesoma hotuba hii, bila kuwa na ushahidi wowote, kilifanywa kibabe kwa kuwakejeli, kuwadhihaki na kwa uonevu mkubwa kwa kuwa hakukuwa na ushahidi wowote na pia Mahakama haikuhusishwa katika hatua za awali. Hii ina maana kuwa Mkuu huyo wa Mkoa aliamua kuwa hakimu kwa kutumia

cheo chake na mamlaka yake kuchafua majina ya watu na haiba waliyoitengeneza kwa muda mrefu na kwa gharama kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tabia ya viongozi wa namna hii wanaotumia madaraka yao vibaya na kuvunja sheria kwa makusudi, ni lazima ipingwe kwa nguvu zote na hatua kali zichukuliwe dhidi yao bila kujali nafasi zao au vyeo vyao. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeshangazwa sana na kitendo cha Mkuu wetu kuendelea kumkingia kifua Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam katika matukio tofauti tofauti huku ushahidi wa wazi ukionesha matumizi mabaya ya madaraka pamoja na ukiukwaji wa haki za binadamu, umiliki wa mali ulio wa mashaka ikiwemo magari ya anasa ya wafanyabiashara aliowatuhumu kujihusisha na madawa ya kulevya, vitisho kwa vyombo vya habari, kuingilia uhuru wa habari nchini, matumizi mabaya ya rasilimali za nchi ikiwa ni pamoja na kufanya tafrija ya kutimiza mwaka mmoja kazini kwa kivuli cha kampeni ya kutokomeza dawa za kulevya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kusikitisha sana kuona Mkuu akimtoa kafara Waziri wake kwa gharama ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam. Tunajiuliza kuna jambo gani lililojificha baina ya Mkuu na Mkuu huyo wa Mkoa? Tatizo la madawa ya kulevya siyo tatizo la mtu mmoja na wala halihitaji kufanywa kama vita ya mtu binafsi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua Rais ana mamlaka ya kuteua na kutengua uteuzi, lakini hana mamlaka ya kumkingia kifua mtu yeyote pale anapovunja sheria za nchi hata kama ndiye Rais ndiye aliyempa dhamana hiyo. Kwa hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inawataka viongozi wote waliopewa dhamana kuheshimu utu na haki za kila raia. Ugomvi binafsi, kutofautiana kiitikadi, kiimani na hata kimtazamo, kusimfanye yeyote mwenye dhamana kutumia mamlaka yake katika kumwonea mtu yeyote. Kama Taifa tuna jukumu la kusimamia misingi ya utu na kuheshimiana.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inamtaka Kiongozi Mkuu kumchukulia mara moja hatua za kinidhamu Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam. Aidha, Mkuu aache ubaguzi katika maamuzi ya kinidhamu kwa baadhi ya Viongozi wa Umma kwani hii ni kuwa na *double standard* katika utekelezaji wa majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, majiji makubwa duniani yanakabiliwa na changamoto za kuongezeka kwa wakazi wake, jambo ambalo limepelekea kuwepo kwa mahitaji makubwa ya huduma za kijamii na za kiuchumi kama vile, afya, elimu, maji, huduma za uokozi, usalama wa raia na huduma za usafiri. Kutokana na ukweli huo, sheria za Majiji hayo, zimetoa mwongozo na mamlaka kwa Majiji hayo kushughulikia baadhi ya masuala yenye athari za moja kwa moja kwa wananchi wa eneo husika ili kukabiliana na changamoto hizo. Kwa sababu hiyo, Mameya na Kamati zao wamepewa mamlaka makubwa ya kupanga na kutekeleza mipango ya maendeleo katika majiji wanayoyaongoza.

Mheshimiwa Spika, naomba tu hotuba yangu yote isipokuwa yale maeneo tuliyozungumza iingizwe kwenye *Hansard* kwa sababu muda siyo rafiki sana.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Usafiri Dar es Salaam *(UDA)* lilianzishwa mwezi Mei, 1974 chini ya Sheria ya Makampuni *(Companies Ordinance, Cap 212)* ikiwa na hisa zilizoidhinishwa *(Authorised Shares)* 15,000,000. Kati ya hisa hizo, hisa 7,119,697 zilizolipiwa *(allotted)* zilitolewa kwa Serikali kwa asilimia 100 na hisa zilizobaki 7,880,303 zilibaki kama hisa zisizogawiwa *(unalloted shares)* kwa shirika. Lengo kuu la kuanzisha shirika hilo lilikuwa ni kutoa huduma ya usafiri wa umma katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kutokana na *UDA* kushindwa kujiendesha, iliwekwa chini ya Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma *(PSRC)* mwaka 1997 kwa lengo la kuibinafsisha. Ili kutekeleza lengo hilo la kubinafsisha *UDA*, *PSRC* ilitangaza uuzaji wa asilimia 49 ya *UDA* kwa mwekezaji

aliyekuwa na nia ya kununua. Hatimaye, Kampuni ya *Simon Group Limited* ilinunua hisa hizo. Hata hivyo, hakukuwa na uwazi katika mchakato wa kuiuzia Kampuni ya *Simon Group* hisa hizo na pia mwanahisa mkubwa ambaye ni Msajili wa Hazina hakushirikishwa jambo ambalo lilizua mgogoro juu ya uhalali wa umiliki wa hisa za *UDA* na hasa ushiriki wa Kampuni ya *Simon Group*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na mchakato wa uuzaji wa hisa za *UDA* kwa Kampuni ya *Simon Group* kugubikwa na utata kwa kutozingatiwa kwa utaratibu wa uuzwaji wa hisa za Serikali na pia utata kuhusu uuzwaji wa hisa za Jiji, bado kuna haja ya wadau wa Jiji kukaa pamoja na kutafuta suluhu ya mgogoro huo. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri wadau wa *UDA* wakae na kuweka msimamo wa pamoja kutafuta suluhisho la sakata la *UDA* kwa manufaa ya Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, inafahamika duniani kuwa suala la usafiri ndani ya majiji husimamiwa na jiji husika na au kwa kushirikiana na sekta binafsi; na kwa kuwa, ilivyo sasa pamoja na makosa yaliyofanyika tayari *simon group* ndiyo kampuni pekee inayoendesha Shirika la *UDA* bila Halmashauri ya Jiji kuhusika katika kusimamia na kuendesha usafiri wa Dar es Salaam; na kwa kuwa hapa nchini vipo vitega uchumi vingi ambavyo vimebinafsishwa bila kuzingatia utaratibu; na kwa kuwa imetolewa kauli na Mheshimiwa Rais kutaka sehemu ya miliki ya hisa za Jiji kama suala la *UDA* halitapewa ufumbuzi; hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri kuwa wadau wa Dar es Salaam kwa maana ya Mameya, Madiwani wakubaliane masuala yafuatayo:-

Moja, kuwa Jiji lipewe hisa na haki ya kuwa sehemu ya kuendesha na kusimamia usafiri wa Dar es Salaam kama ilivyo katika majiji mengine duniani. *(Makofi)*

Pili, kuwa Halmashauri ya Jiji iwe na mamlaka ya kutoa leseni kwa mwekezaji mwingine ambaye atapewa kuwa sehemu ya kutoa huduma katika Jiji la Dar es Salaam

kuliko ilivyo sasa ambapo ni *Simon Group Limited* pekee wanaoendesha usafiri wa Jiji lote la Dar es Salaam, kwa zile *specified routes.*

Tatu, Serikali kuu ibaki na jukumu la kutoa miongozo ya kisera na kusimamia hisa zake katika vikao vya wanahisa na siyo kama ilivyo sasa ambapo kwa sasa *DART* ipo chini ya TAMISEMI ambayo ni Ofisi ya Rais.

Nne, kuwa kuisimamisha Kampuni ya *Simon Group* ambayo inajulikana kuwa ilipata hisa na miliki ya kuendesha usafiri wa Jiji bila kuzingatia utaratibu na njia zilizo wazi na pia ikijulikana kuwa tayari kampuni hiyo imeshakopa fedha kwa kutumia mali za Jiji na pia tayari kampuni hiyo ikiwa tayari inatoa huduma kwa wananchi wa Dar es Salaam, hautakuwa uamuzi wenye maslahi mapana kwa wananchi kuisimamisha kampuni ya *Simon Group*.

Mheshimiwa Spika, jambo muhimu hapa ni Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kuwa na *say* ama *stake* katika kupanga na kuendesha mradi wa usafiri wa umma kwa kuwa Halmashauri ya Jiji ndiyo wawakilishi wa wananchi. Kwa maneno mengine, mamlaka za kisheria za Jiji la Dar es Salaam za kupanga na kusimamia usafiri wa umma katika Jiji la Dar es Salaam kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) 1982 zilindwe na zitekelezwe.

Mheshimiwa Spika, wajibu wa Serikali katika bajeti ni kukusanya mapato na kutumia mapato hayo katika matumizi ya kawaida na maendeleo kwa kadiri itakavyokuwa imeidhinishwa na Bunge. Kwa maneno mengine, ni wajibu wa Serikali kutekeleza Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, licha ya Serikali kuwa na wajibu huo, kumeanza kuwa na utamaduni wa utekelezaji mbaya wa bajeti inayoidhinishwa na Bunge. Utekelezaji huu mbaya unatokana na kukosekana kwa umakini tangu Bajeti ya

Serikali inapoandaliwa na pia kuingiza matashi ya kisiasa katika Bajeti, jambo ambalo linaifanya bajeti yote kuwa *unrealistic.*

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri wa ukosefu wa umakini ni katika uandaaji wa Bajeti ya 2016/2017 inayomaliza muda wake, ambapo kulikuwa na tofauti kati ya takwimu zilizokuwa katika vitabu vya mapato na vile vya matumizi. Kwa mfano, wakati kitabu cha mapato ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaoanza tarehe 1 Julai, 2016 hadi tarehe 30 Julai, 2017 kinaonesha kuwa jumla ya mapato yote ya Serikali ni shilingi trilioni 22.063; vitabu vya matumizi ya kawaida na maendeleo vinaonyesha kuwa jumla ya matumizi yote ya Serikali katika kipindi hicho ni shilingi trilioni 23.847; kwa mchanganuo kwamba fedha za matumizi ya kawaida *(Volume II)* ni shilingi trilioni 13.3 na fedha za miradi ya maendeleo *(Volume IV)* ni shilingi trilioni 10.511.

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi ni kwamba kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali imepanga kukusanya jumla ya shilingi trilioni 22.063 ila ikapanga kutumia shilingi trilioni 23.847, kiasi ambacho ni zaidi ya mapato yake kwa shilingi trilioni 1.783. Swali hapa ni kwamba hii shilingi trilioni 1.783 iliyoongezeka kwenye matumizi itapatikana wapi wakati haipo katika kitabu cha mapato? Huku ni kukosekana kwa umakini na ndiyo chanzo cha utekelezaji mbaya wa Bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, chanzo kingine cha utekelezaji duni wa Bajeti ni kuingiza matashi au maslahi ya kisiasa katika uandaaji wa bajeti. Nasema hivi kwa sababu bajeti ya Serikali iliyopitishwa hapa Bungeni kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ililenga kupata umaarufu wa kisiasa na siyo kutatua kero za Watanzania. Hii ni kwa sababu ukisoma sura ya bajeti iliyowasilishwa katika hotuba ya Waziri wa Fedha na Mipango utaona kwamba jumla ya makusanyo yote yalitakiwa kuwa shilingi trilioni 29.539 na matumizi yote, shilingi trilioni 29.539 lakini takwimu zilizoandikwa kwenye vitabu vya mapato na matumizi ni tofauti kama nilivyoonyesha hapo juu. Hii ni kuwarubuni wananchi kwamba Serikali imekuja na bajeti

kubwa, hivyo wategemee unafuu katika huduma za kijamii kumbe ni usanii mtupu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mkanganyiko huo wa takwimu za Bajeti kwamba Serikali ingekusanya shilingi trilioni 29.5 na kutumia shilingi trilioni 29.5 wakati kwenye vitabu inaonekana ingekusanya trilioni 22.063 na kutumia trilioni 23.8, ndiyo kunaifanya Kambi Rasmi ya Upinzani kuiita Bajeti hiyo kuwa ina mwelekeo wa kuwa bajeti hewa na kwamba mkanganyiko huo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ni Kengele ya pili Mheshimiwa. Nakupa dakika mbili za ku-*wind up.*

**MHE. FREEMAN A. MBOWE – KIONGOZI WA KAMBI YA UPINZANI:** Mheshimiwa Spika, mchanganuo wa matumizi ya fedha za maendeleo katika baadhi ya Wizara zenye athari ya moja kwa moja kwenye uchumi ni kama ifuatavyo:-

(i) Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ilipewa shilingi bilioni 2.2 sawa na 2.2% ya shilingi milioni 110;

(ii) Wizara ya Viwanda na Biashara ilipewa sawa na 8% ya Bajeti yake ya Maendeleo;

(iii) Wizara ya Miundombinu ilipewa 58.71%. Uchukuzi wamepewa 30.%;

(iv) Wizara ya Nishati na Madini wamepewa 36%; na

(v) Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii wamepewa 25%.

Mheshimiwa Spika, kwa takwimu hizo, ni kwamba, Serikali imeshindwa kutekeleza bajeti ya maendeleo ya mwaka wa fedha 2016/2017 kwa takriban 70%. Kambi Rasmi

haioni muujiza unaoweza kufanyika ili hiyo 70% ya bajeti ambayo haijatekelezwa iweze kutekelezwa kabla ya mwaka huu wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utaratibu usio wazi wa matumizi ya shilingi bilioni 6.2 fedha za maafa ya wahanga wa tetemeko la ardhi, Kagera; hiyo nitaomba iingie moja kwa moja kwenye *Hansard.*

Mheshimiwa Spika, hoja ya bajeti ya kukuza demokrasia nchini vile vile naomba iingie kwenye *Hansard.* Naomba niende kwenye hitimisho.

Mheshimiwa Spika, wanazuoni wa Sayansi ya Siasa *(Political Science)* wanasema kwamba huwezi kutenganisha siasa na maendeleo. Uhusiano kati ya siasa na maendeleo ni sawa na uhusiano kati ya yai na kuku. Huwezi kuwa na kimoja bila uwepo wa kingine. Kwa sababu hiyo, ili Taifa liweze kuwa na maendeleo endelevu, ni lazima Taifa hilo liwe na mfumo mzuri wa siasa; siasa ambayo inaheshimu misingi ya Katiba na utawala wa sheria; siasa ambayo inaliunganisha Taifa na siyo kulisambaratisha kwa misingi ya tofauti za kiitikadi, kidini, kikabila na mambo yanayofanana na hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema hapo awali, ili maendeleo ya kiuchumi yaweze kumfikia kila mwananchi, ni lazima uchumi huo uwe shirikishi. Uchumi huo hauwezi kuwa shirikishi ikiwa tunabaguana kwa misingi ya tofauti za kisiasa au tofauti nyinginezo. Uchumi wa nchi yetu hauwezi kujengwa na kundi moja la jamii na kulibagua lingine.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika uchumi wa nchi yetu hautajengwa na chama kimoja cha siasa kwa kukibagua kingine au kuchochea migogoro ndani ya vyama vingine vya siasa. Mshikamano wa Kitaifa ni muhimu sana katika kujenga uchumi ulio imara. Ndoto ya kufikia uchumi wa viwanda haiwezi kufikiwa tukiwa na msigano wa namna hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wanazuoni wanasema: "kutofautiana kififikra ni afya ya akili." Ili ufumbuzi utokee, ni lazime kuwe na fikra mbadala *(alternative thinking).* Nilidhani kuwa Serikali na Chama cha Mapinduzi wangetambua kuwa uwepo wa watu wenye fikra mbadala katika Taifa hili ni tunu na zawadi kutoka kwa Mwenyezi Mungu, lakini badala yake Serikali wameona kuwa uwepo wa watu hao ni kama mwiba na kikwazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, nihitimishe kwa kuwashukuru Wabunge wote wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia kama kiongozi wao. Naishukuru sana Sekretariet ya KUB kwa namna wanavyokesha kufanya tafiti mbalimbali zinazosaidia uandaaji wa hotuba za Kambi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa nakushukuru wewe binafsi na Ofisi ya Katibu wa Bunge kwa ushirikiano vile vile ambao mnatupatia katika maeneo mengine ya kiutawala. Ahsante sana. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Freeman Mbowe, Kiongozi wa Upinzani Bungeni.

**HOTUBA YA KIONGOZI WA UPINZANI BUNGENI (KUB), MHE. FREEMAN AIKAELI MBOWE (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI.**

*Inatolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge,Toleo la Januari, 2016*

**UTANGULIZI**

**1. Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imepokea kwa masikitiko makubwa taarifa za kifo cha Mbunge mwenzetu Mhe. Dkt. Elly Macha (CHADEMA Viti Maalum) kilichotokea tarehe 30 Machi, 2017 huko nchini Uingereza alikokuwa matibabuni.

2. **Mheshimiwa Spika,** marehemu alikuwa kielelezo cha mtu jasiri, mwenye kujiamini na aliyekuwa mstari wa mbele kivitendo kujiendeleza na kuwapigania wengine; tena wasio na ulemavu licha ya yeye mwenyewe kuwa na ulemavu.

3. **Mheshimiwa Spika,** ni dhahiri, Taifa kwa ujumlalimempoteza mpiganaji madhubuti aliyeamini na kusimamia misingi ya haki na aliyependa kuona haki ikitamalaki na kutendeka katika makundi yote ya jamii.

4. **Mheshimiwa Spika,** nachukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi, Ofisi ya Katibu wa Bunge na Ubalozi wa Tanzania nchini Uingereza chini ya Balozi, Dr. Asha Rose Migiro kwa namna ambavyo mmekuwa wa msaada kwa njia mbalimbali kwa marehemu na Familia yake tangu wakati wa kuugua kwake hadi sasa wakati juhudi na mipango ikiendelea ya kuurejesha nchini kwa mazishi mwili wa marehemu Dr. Elly Macha.

5. **Mheshimiwa Spika,** tunatoa pole nyingi kwa wote walioguswa na msiba huu, na tunaiombea roho ya Marehemu mahali pema peponi. AMINA.

6. **Mheshimiwa Spika,** napenda kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kinilinda na kuniimarisha katika kuitenda kazi yake kwa njia ya siasa. Ni dhahiri, siasa sasa si salama tena kuifanya nchini mwetu kwani matukio kadhaa yanayotukumba wanasiasa na viongozi wa upinzani siyo ya kawaida na hayaakisi utamaduni wetu tuliouzoea kama Taifa.

7. **Mheshimiwa Spika,** kwa nchi na viongozi wanaoheshimu Demokrasia, huviona vyama vya siasa vya upinzani kama vyombo muhimu vya kuwasaidia katika kupata mawazo mbadala yaani "Free Consultancy". Hujipima mafanikio yaokwa kuchambua kwa makini maoni ya wapinzani na kujirekebisha pale inapobidi.

8. **Mheshimiwa Spika,** mwaka mmoja na nusu wa utawala wa awamu hii tumeshuhudia manyanyaso na uonevu kwa

baadhi ya viongozi na watendaji wetu kuuwawa au kupotea. Mfano aliyekuwa Mwenyekiti wetu wa Mkoa wa Geita Mhe. Alphonce Mawazo aliyeuwawa mchana kweupe na watu wakishuhudia na waliohusika wanajulikana. Msaidizi wangu Ben Rabiu Saanane kupotea baada ya kupokea vitisho kadhaa vyenye asili ya kisiasa na hadi sasa vyombo vya dola havijatoa maelezo ya kina ya Ben kapelekwa wapi!!

9. **Mheshimiwa Spika,** wabunge wetu nao hawajawa salama hata kidogo. Tumeshuhudia mbunge wetu Mhe.Peter Lijualikali kufungwa kwa uonevu mkubwa, Mbunge wetu mwingine Mhe. Godbless Lema kunyimwa dhamana kwa zaidi ya miezi minne kwa shtaka lenye dhamana na wengine wengi nikiwamo mimi mwenyewe na Mhe Tundu Lissu kukamatwa mara kwa mara na vyombo vya dola na kufunguliwa mashtaka mbalimbali yasiyo na nia njema wala afya kwa ujenzi wa demokrasia katika nchi yetu.

10. **Mheshimiwa Spika**, tunaamini mapito haya mazito ya kisiasa katika nchi yetu yanalenga kujaribu kufifisha ndoto ya Taifa - ndoto ya kuwa taifa huru linalosimamia misingi ya haki za binadamu, uhuru wa maoni ya kila raia, demokrasia ya kweli, - ndoto ya kuwa taifa linaloheshimu katiba ya nchi na ndoto ya kuwa taifa lenye uchumi unaomnufaisha kila mwananchi.

11. **Mheshimiwa Spika,**Mwenyezi Mungu ameendelea kuwa upande wetu, na hila hizo za baadhi ya wenye mamlaka hazijatuondoa kwenye lengo kubwa la kuwavusha wananchi wa Tanzania kuifikia ndoto hiyo ya Taifa; na kwa sababu hiyo tuna kila sababu ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kila jambo.

## UKIUKWAJI WA DEMOKRASIA NA UTAWALA WA SHERIA

**12. Mheshimiwa Spika,** Nchi yetu ya Tanzania imesifika duniani kote kwa tunu zake za amani, umoja na mshikamano kutokana na waasisi wa taifa hili kuheshimu na kuenzi misingi ya utawala wa sheria demokrasia na uhuru wa kupata habari.

**13. Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa ibara ya 20 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 ni kwamba: *"Kila mtu anao uhuru wa kukutana na watu wengine kwa hiari yake na kwa amani, kuchanganyika, kushirikiana na watu wengine na kwa ajili hiyo kutoa mawazo yake hadharani na kuanzisha na kujiunga na vyama au mashirika yaliyoanzishwa kwa madhumuni ya kuhifadhi au kuendeleza imani au maslahi yake au maslahi mengineyo".*

**14. Mheshimiwa Spika,** ibara ya 18 ya Katiba imeweka msingi wa uhuru wa maoni na uhuru wa kupata habari kwa kusema kwamba: *"Kila mtu anao uhuru wa kuwa na maoni na kueleza fikra zake; anayo haki ya kutafuta, kupokea na kutoa habari bila ya kujali mipaka ya nchi; anao uhuru wa kufanya mawasiliano na haki ya kutoingiliwa katika mawasiliano yake na anayo haki ya kupewa taarifa wakati wowote kuhusu matukio mbalimbali muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi na pia kuhusu masuala muhimu kwa jamii"*

**15. Mheshimiwa Spika,**tangu Serikali ya awamu ya tano imeingia madarakani, zimeonekana dalili za wazi za Serikali hiyo kuvunja Katiba ya Nchi kwa kutupilia mbali misingi ya utawala wa sheria, demokrasia na uhuru wa kupata habari jambo ambalo linaweza kuitumbukiza nchi yetu kwenye Dola la ki- dikteta.

**16. MheshimiwaSpika,** matukio mahsusi ya ukandamizaji wa haki na demokrasia yaliyofanywa na serikali kinyume cha katiba na sheria za nchi ni pamoja na haya yafuatayo.

**i. Kupiga Marufuku Mikutano ya Vyama vya Siasa: Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Waziri Mkuu na hatimaye Rais, imetangaza kwamba ni marufuku kwa vyama vya siasa kufanya mikutano ya kisiasa mpaka mwaka 2020 ili kuipa Serikali nafasi ya kufanya kazi. Huu ni uvunjaji wa Ibara ya 20 (1) ya Katiba kama ilivyonukuliwa hapo awali. Aidha, katazo la mikutano ya siasa linakiuka Sheria namba 5 ya Vyama vya siasa ya 1992 ambayo imetoa haki kwa vyama vya siasa kufanya kazi ya siasa.

**ii. Kupiga Marufuku Urushwaji wa moja kwa moja (live coverage) wa Mijadala ya Bunge:**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Waziri wa Habari, Utamaduni, Wasanii na Michezo ilipiga marufuku urushwaji wa moja kwa moja wa mijadala ya Bunge kupitia televisheni ya taifa na vyombo vingine vya habari. Katazo hilo ni kinyume na ibara ya 18 ya Katiba ambayo inatoa uhuru wa maoni na uhuru wa kupata habari kwa kila mwananchi. Aidha, kitendo kilichofanywa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Paul Makonda hivi karibuni cha kuvamia kituo cha habari cha Clouds akiwa na polisi wenye silaha za moto kwa malengo ya kushinikiza kituo hicho kurusha habari anazozitaka yeye sio tu kimekandamiza uhuru wa vyombo vya habari bali pia kimenajisi tasnia ya habari nchini.

**iii. Kudhibiti Wabunge wa Upinzani wawapo Bungeni:**

**Mheshimiwa Spika,** yamekuwapo matukio kadhaa yanayoashiria kutaka kuwadhibiti Wabunge wa Upinzani Bungeni kwa lengo la kuwanyamazisha wasiikosoe Serikali. Jambo hili limefanyika kwa namna mbali mbali ikiwa ni pamoja na kuwatengenezea kesi Wabunge wa Upinzani na kuwapeleka kwenye Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ambapo hukumu ya kuwaadhibu inakuwa imeshaandaliwa. Kwa hila hizo, wabunge wa Upinzani wamekuwa wakipewa adhabu za kufungiwa kuhudhuria kuanzia vikao kumi hadi mikutano miwili ya Bunge bila hata ya kusikilizwa jambo ambalo ni kinyume kabisa cha Kanuni za Bunge. Aidha, mara kadhaa wabunge wa Upinzani wamekamatwa kwa udhalili mkubwa na kusafirishwa umbali mrefu wanapokuwa wanahudhuria vikao vya Bunge.

***iv. Kuingilia Mhimili wa Mahakama:***

***Mheshimiwa Spika,*** *Serikali ya CCM kupitia Rais, kwa nyakati tofauti imeonekana kujaribu kuingilia uhuru wa Mahakama jambo ambalo ni hatari kwa utoaji wa haki nchini. Katika hotuba yake, wakati wa maadhimisho ya siku ya sheria duniani Rais alinukuliwa akisema kwamba Mahakama*

*iwahukumu harakaharaka watu waliokwepa kodi halafu atatumia asilimia fulani ya fedha ambazo zitakuwa zimepatikana kutokana na faini za wale walioshindwa kesi kuwapa Mahakama ili wafanye kazi vizuri ya kuendelea kuwahukumu na kuwafunga wakwepa kodi. Kauli kama hiyo inaweza kusababisha watuhumiwa wasisikilizwe na kutendewa haki. Aidha, kutoa ahadi ya kuipa Mahakama fedha ili ifanye kazi ya kuwahukumu wakwepa kodi wenye mgogoro na Serikali inatoa taswira ya rushwa.* **[*Maneno haya siyo sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge*]**

**v. Kupuuza Utawala wa Sheria:**

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 24 Juni, 2016; wakati wa uzinduzi wa siku ya usalama wa raia, Rais alinukuliwa akiwaruhusu polisi kuwaua majambazi bila kuwafikisha mahakamani ili sheria ichukue mkondo wake. Aidha aliuagiza uongozi wa Jeshi la Polisi kuwapandisha cheo watakaowauwa majambazi badala ya kuwashtaki mahakamani. Tafsiri ndogo ya Kauli ya Rais ni kwamba utawala wa sheria uwekwe kando na polisi sasa au wananchi wajichukulie sheria mkononi. Jambo hili litaiingiza nchi kwenye machafuko kwa kuwa utashi wa polisi sasa ndio utakaokuwa wa mwisho na wa kuaminika kuliko Mahakama. Watu wengi watauwawa kwa kisingizio kuwa ni majambazi kutokana na chuki binafsi tu na polisi. Nani ataamua haki katika mazingira hayo?

**vi. Uonevu unaofanywa na Vyombo vya Dola dhidi ya Wananchi wa Visiwa vya Unguja na Pemba:**

**Mheshimiwa Spika,**Wananchi wa Zanzibar waliukataa utawala wa CCM kupitia sanduku la kura katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2015. Serikali ya Muungano ikishirikiana na SMZ wakafanya hila kuupora ushindi wa Wazanzibari kwa kuufuta uchaguzi ule bila sababu za msingi na kuitisha uchaguzi mwingine haramu ambao ulisusiwa na Chama cha Wananchi - CUF, kilichokuwa kimeshinda uchaguzi uliofutwa. Kutokana na tukio hilo, Serikali ya Muungano ikishirikiana na SMZ imeamuru vyombo vya dola vikiwemo Jeshi la Polisi, JWTZ

na Usalama wa Taifa kuwaadhibu wananchi wa Zanzibar hususan wanaounga mkono Chama cha Wananchi – CUF kwa kuwavamia nyakati za usiku na kuwakamata, kuwapiga, kuwafungulia mashtaka bandia na kupora mali zao ikiwemo mifugo. Huu ni ukiukwaji mkubwa wa Haki za Binadamu unaopaswa kulaaniwa na watu wote.

## MCHAKATO WA KATIBA MPYA NA MUSTAKABALI WA TAIFA

**17. Mheshimiwa Spika,** kilio cha hitaji la Katiba Mpya ya Nchi yetu kilianza kusikika Tangu Mfumo wa Siasa ya Vyama vingi uanze hapa nchini miaka ishirini na tano iliyopita. Haina shaka kwamba vyama vya upinzani ndivyo vilivyoanza kutoridhishwa na mfumo wa uchaguzi, madaraka makubwa ya Rais, na mfumo mzima wa utawala na uendeshaji wa Serikali mambo yaliyoanzisha ajenda ya madai ya Katiba Mpya.

**18. Mheshimiwa Spika,** baada ya mapambano hayo ya kudai katiba mpya, hatimaye Serikali ilianzisha mchakato wa Katiba Mpya. Mchakato huo ulianza kwa Bunge kutunga Sheria ya Mabadiliko ya Katiba sura ya 83 mnamo mwezi Novemba, 2011 na baadaye kufanyiwa marekebisho mwaka 2012 na 2013. Aidha, Bunge lilitunga Sheria ya Kura ya Maoni mwaka 2013. Katika kipindi hicho hicho, Rais Mstaafu Jakaya Mrisho Kikwete aliunda Tume ya Mabadiliko ya Katiba ambayo ilifanya kazi kubwa ya kukusanya na kuyachambua maoni ya wananchi hadi kupata Rasimu ya kwanza ya Katiba mnamo tarehe 3 Juni, 2013.

**19. Mheshimiwa Spika,** rasimu hiyo ilipelekwa kwa wananchi kupitia Mabaraza ya Katiba kwa ajili ya maoni zaidi na hatimaye baada ya kuzingatia maoni ya wananchi ikatengenezwa rasimu ya pili ya Katiba ambayo ilikabidhiwa katika Bunge Maalum la Katiba kwa ajili ya kujadiliwa ili kupata Rasimu ya Katiba Pendekezwa.

**20. Mheshimiwa Spika,** yaliyotokea katika Bunge Maalum la Katiba yalikuwa ni fedheha na aibukubwa kwa Taifa kwani Chama Cha Mapinduzi kwa kutumia wingi wa wajumbe

wake katika Bunge hilo kiliuteka mchakato ule na kuyafuta kwa makusudi maoni ya wananchi yaliyokuwamo katika rasimu iliyowasilishwa katika Bunge Maalum na kuingiza sura na vifungu vipya kwa maslahi yao wenyewe.

**21. Mheshimiwa Spika,** itakumbukwa kuwa vyama vya Upinzani katika ushirikiano wa UKAWA, tuliondoka katika Bunge Maalum kwa kuwa hatukupenda kushiriki kunajisi mchakato wa kupata Katiba Mpya. Tangu vyama vya Upinzani tujitoe katika mchakato huo haramu, mchakato wa Katiba Mpya umekwama na mpaka sasa hakuna mwelekeo wowote kuhusu suala hilo.

**22. Mheshimiwa Spika,**kwa kuwa wananchi wa Tanzania bado wanahitaji mabadiliko makubwa ya kimuundo na kimfumo katika uendeshaji wa Serikali – mabadiliko ambayo msingi wake ni Katiba Mpya;

**Na kwa kuwa** Mgombea wa Urais kupitia CCM aliwaahidi wananchi kuleta mabadiliko hayo na kuongeza kuwa hatawaangusha;

**Hivyo basi,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Serikali kutekeleza ahadi hiyo kwa kurejesha tena mchakato wa Katiba Mpya. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kuwa mchakato wa Katiba Mpyaurudishwe nyuma katika ngazi ya Bunge Maalum ili kujadili maoni ya wananchi katika Rasimu ya Pili ya Katiba iliyowasilishwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba bila kuathiri maudhui ya maoni ya wananchi kuhusu Katiba Mpya.

## HALI YA UCHUMI KATIKA TAIFA

### Hali ngumu ya maisha

**23. Mheshimiwa Spika,** uchumi ndio msingi wa maisha ya binadamu. Hitilafu yoyote inayotokea katika ukuaji wa uchumi inakuwa na athari ya moja kwa moja kwa maisha ya mwananchi.

**24. Mheshimiwa Spika,** tangu Serikali hii ya awamu ya tano iingie madarakani imekuwa ikijigamba kuwa uchumi wa nchi unakuwa kwa kasi ikilinganishwa na serikali za awamu zilizotangulia, lakini kumekuwa na kilio kikuu kwa upande wa wananchi kuhusu hali ya maisha kuendelea kuwa ngumu kuliko wakati wowote katika historia ya nchi yetu.

**25. Mheshimiwa Spika,**kilio hiki cha wananchi kinamaanisha kwamba ukuaji wa uchumi unaohubiriwa na Serikali haujawafikia wananchi ambao ndio wadau wakubwa wanchi hii. Wanazuoni wa uchumi wanasema kwamba ***"Growth is inclusive when it takes place in the sectors in which the poor work (e.g. agriculture); occurs in places where the poor live (e.g. undeveloped areas with few resources); uses the factors of production that the poor possess (e.g. unskilled labour); and reduces the prices of consumption items that the poor consume (e.g. food, fuel and clothing)."***

**26. Mheshimiwa Spika,** kwa tafsiri isiyo rasmi ni kwamba ukuaji wa uchumi unakuwa shirikishi unapotokea kwenye sekta ambazo watu maskini wanafanya kazi kama vile kilimo; unatokea katika maeneo ambayo watu masikini wanaishi kwa mfano maeneo ambayo hayajaendelea na yasiyo na rasilimali; unatumia nyenzo za uzalishaji ambazo watu masikini wanazo kwa mfano nguvukazi isiyo ya kitaalamu; na unapunguza bei za bidhaa ambazo watu masikini wanatumia kwa mfano chakula, mafuta na nguo.

**27. Mheshimiwa Spika,** kwa muktadha huo, ukipima hali ya Tanzania utaona kwamba uchumi wetu sio shirikishi kwa kuwa ukuaji wake hautokei katika sekta ambazo watu masikini wanafanya kazi au maeneo ambayo watu masikini wanaishi. Aidha, ukuaji wa uchumi wetu hautumii nyenzo za uzalishaji ambazo watu masikini wanazo na pia ukuaji huo haujapunguza bei za bidhaa ambazo watu masikini wanatumia.

**Kukosekana Mkakati wa kuinua uchumi vijijini**

**28. Mheshimiwa Spika,** ukiangalia kwa makini vipaumbele vya Serikali ya awamu ya Tano, utagundua Serikali haina

mkakati wowote madhubuti wa kuinua uchumi wa wananchi waishio vijijini. (Rural Economy). Uchumi wa Vijijini unagusa kilimo, uvuvi na ufugaji na sekta hizi ndizo zenye uwezo mkubwa wa kuajiri watu na kupunguza umaskini. Tukumbuke asilimia zaidi ya 70 ya Watanzania wanaishi vijijini na wanategemea sekta hizi.

29. **Mheshimiwa Spika,** duniani kote, hakuna nchi iliyowahi kufanikiwa kuingia kwenye uchumi wa viwanda kabla ya kupitia mageuzi ya Kilimo. Nchi zote za Asia ambazo tunapenda kuiga economic model zao ziliendeleza kwanza kilimo na bado pamoja na kuingia kwenye uchumi wa viwanda, bado idadi kubwa ya watu wao wanaendelea na sekta hizi za rural economy.

30. **Mheshimiwa Spika,** kilicho dhahiri ni kuwa serikali ya awamu ya Tano haikujiandaa na sera hii na inakurupuka kufanya mambo mbalimbali bila kuwa na mpango mathubuti wenye matokeo yanayopimika yaani **"Integrated rural development plan".**Kwa miaka ya karibuni mchango wa Sekta ya kilimo unazidi kushuka na sasa ni pungufu ya 25.88% ya GDP.

31. **Mheshimiwa Spika,** Sekta hizi za Kilimo, Ufugaji na Uvuvi zilipewa asilimia 2.22 tu ya fedha zilizoidhinishwa kwa shughuli za maendeleo ambazo ni sawa na shilingi bilioni 2.2 ya shilingi bilioni 101.5 kwa fungu 43. Fungu 99, mifugo na uvuvi wametengewa bilioni 1.252 sawa na 7.9% ya shilingi bilioni 15.873 zilizotengwa kwenye bajeti ilhali zaidi ya bilioni 128 zimetumika kama malipo ya awali kununulia ndege za Air Tanzania, bila hata ya kuwepo Business Plan. Kwa Serikali hii, ndege zinazohudumia wananchi wasiozidi 10,000 ni muhimu na kipaumbele kuliko sekta inayogusa zaidi ya 70% ya wananchi wake."

**Hali ya Uwekezaji**

**32. Mheshimiwa Spika,**kwa mujibu wa tovuti ya Economic Freedom (http://www.heritage.org/index/country/tanzania) inayoonesha vigezo vya uhuru wa kuwekeza katika sekta za

uchumi, Tanzania ipo katika rangi nyekundu kwenye kigezo cha Uhuru wa kiuchumi ikishika nafasi ya 105, kati ya 180. Ikumbukwe kwamba uhuru wa kiuchumi ni kigezo kikubwa cha kimataifa cha kupima mwenendo wa uchumi. Nafasi ambayo Tanzania imeshika ni kiashiria kibaya kwamba uchumi wetu upo katika hatari ya kuporomoka vibaya.

**33. Mheshimiwa Spika,** uchambuzi uliofanywa na wataalamu wa uchumi inaonesha kwamba kwamba; uchumi wa Tanzania upo hatarini kuporomoka kutokana na mambo yafuatayo:

**i. Hali ya kisiasa ya nchi:**

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania bado iko katika hali tete ya kisiasa kufuatia uchaguzi wa 2015, ambapo suala la Zanzibar bado halijatatuliwa na kuendelea kukiukwa kwa misingi ya kidemokrasia, kubinywa kwa uhuru wa siasa za vyama vingi na uhuru wa vyombo vya habari. Jambo hili limeathairi uhuru wa kiuchumi na limewatia hofu wafanya biashara wa ndani na nje hivyo kupunguza kasi ya uwekezaji na ukuaji wa uchumi.

**ii. Ustawi wa Jamii na Utawala Bora:**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa taarifa ya Umoja wa Mataifa ya '*Human Development Indicator';*bado Tanzania inashika nafasi ya chini katika vigezo vya kimataifa vya ustawi wa jamii na utawala bora. Kwa mujibu wa taarifa hiyo, Tanzania inashika nafasi ya 151 kati ya 187. Aidha, kigezo cha ustawi kijinsia kinaishusha Tanzania kwenda kwenye nafasi ya chini zaidi yaani 129 kati ya nchi 159 - yaanini wa ishirini kutoka mkiani. (http://hdr.undp.org/sites/all/themes/hdr_theme/country-notes/TZA.pdf ukurasa wa 6)

**iii. Katiba ya Nchi:**

**Mheshimiwa Spika,** kukwama kwa mchakato wa Katiba mpya ya Wananchi kumesababisha kuwa na hali ya *'Constitutional Uncertainty'* jambo ambalo wachambuzi wa

masuala ya kiuchumi wanaliona kuwa na tishio au 'threat' kiuchumi. Hii ni kwa sababu nchi inapokuwa katika mkwamo wa kupata katiba inayoridhiwa na wananchi huweza kusababisha machafuko ya kisiasa (Political instability) na jambo hili huwatia hofu sana wafanyabiashara na wawekezaji wakubwa jambo ambalo huwafanya kuzuia mitaji yao mikubwa kwenda katika nchi yenye hali kama hiyo. Hili nalo limetuathiri kwa kiwango kikubwa na ndiyo maana kuna malalamiko miongoni mwa wananchi kwamba mzunguko wa fedha ni mdogo.

**iv. Mahusiano yasiyotabirika kati ya Serikali na Sekta Binafsi:**

**Mheshimiwa Spika,**kwa mujibu wa taarifa ya Formal Sector Employment and Earnings Survery ya 2015, ni kwamba 1/3 ya mapato ya kodi yanatokana na watumishi (waajiriwa) ambapo sekta binafsi ina waajiriwa 1,432,985 na sekta ya umma waajiriwa 708,366.Aidha, takriban 2/3 ya makusanyo ya TRA yanatoka katika sekta binafsi. Kwa takwimu hizo ni kwamba sekta binafsi ina mchango mkubwa katika mapato ya Serikali na hivyo katika uchumi wa nchi.

**Mheshimiwa Spika,** licha ya umuhimu huo wa sekta binafsi katia uchumi wa nchi yetu, Serikali imekuwa ikiweka mazingira magumu kwa sekta hii kukua.Sekta binafsi imekuwa ikilalamika kuwa mfumo wetu wa kodi sio rafiki kuikuza Sekta binafsi, pili mazingira ya kupata mikopo kutoka kwenye taasisi za fedha sio rafiki kwa biashara hasa zinazoanzishwa, kwani serikali inashindana na sekta binafsi katika kukopa kwenye taasisi za fedha. Haya mazingira yanapunguza kasi ya uanzishwaji wa biashara mpya kwani watu wanaogopa kuingia kwenye sekta binafsi.

**vi. Tishio la kuanguka kwa uchumi wa nchi:**
**Mheshimiwa Spika,** tayari Shirika la Fedha Duniani (IMF) limeionya Tanzania kuwa uchumi wake uko hatarini kuporomoka kutokana na kubana matumizi kulikopitiliza, kushuka kwa idadi ya mikopo, utekelezaji hafifu wa uwekezaji wa umma na kutotabirika kwa sera za serikali kuhusu sekta binafsi.

**Mheshimiwa Spika, IMF wanasema hivi kuhusu uchumi wa Tanzania:*"There are risks that could adversely affect economic growth going forward, arising from the currently tight stance of macroeconomic policies, the slow pace of credit growth that may become protracted, slow implementation of public investment, and private sector uncertainty about the government's new economic strategies"***

**Mheshimiwa Spika,** IMF wanapendekeza sera za fedha zilegezwe ili kuondoa tatizo la mzunguko mdogo wa fedha unaotokana na kubana matumizi pamoja na kuisadia sekta binafsi kupata mikopo***."Monetary policy should be eased to address the tight liquidity situation and support credit to the private sector"***Hii ni pamoja na kulipa wakandarasi mbalimbali wanaoidai Serikali kwani deni la ndani sasa linakaribia Trilioni 5.

**Mheshimiwa Spika,** angalizo hili la IMF limechangiwa na wabobezi wa Uchumi akiwemo Profesa Gabagambi wa Chuo Kikuu cha Mzumbe anayesema, nanukuu:***"...In fact right now, you could say we are in the stage of a recession and if we don't take heed of the IMF advice and act, the country may enter the stage of depression, which is worse"***

**Mheshimiwa Spika,** ushauri unaotolewa na mchumi huyu ni kwamba tutekeleze ushauri wa IMF - tusipotekeleza ushauri wa IMF, ni kwamba nchi itaingia kwenye anguko kuu la uchumi – economic depression.

**vii. Kutokuheshimu Mikataba na Uchumi kuendeshwa kwa kauli za Rais**

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na umuhimu wa kuhakikisha rasilimali za nchi zinainufaisha nchi yetu, ni muhimu kwa viongozi wetu kutambua "sensitivity" ya Multinational Corporations inapokuja kwenye suala la kubadilisha au kutokuheshimu mikataba.

**Mheshimiwa Spika**, pale ambapo Serikali inaona kuna mambo hayako sawa itake mazungumzo ya kurejea

mikataba kabla ya kutoa makatazo hadharani kama ilivyokuwa kwa katazo la kupeleka "mchanga wa Dhahabu" nje ya nchi kwa uchenjuaji linalohusu Kampuni ya Acacia inayochimba dhahabu nchini. Mambo haya yanahitaji muda na mipango na kamwe kukurupuka kutakuja kulisababishia Taifa hili ulipaji wa fidia kubwa sana na kibaya zaidi kuua kabisa imani ya wawekezaji wakubwa hususan wa kimataifa.

**34. Mheshimiwa Spika,** napenda kumalizia kipengele hiki cha uchumi kwa kusema kwamba, serikali isijifiche kwenye kivuli cha tarakimu kwamba uchumi wetu unakuwa kwa asilimia saba na kujidanganya kwamba Tanzania ni miongoni mwa nchi zenye uchumi unaokuwa kwa kasi duniani ilhali bado wananchi wake ni masikini wa kutupwa. Kwa mujibu taarifa ya Benki ya Dunia, Watanzania zaidi ya milioni 12 ni masikini wa kutupwa kwani wanaishi chini ya mstari wa kiwango cha umaskini (below poverty line). Hii ni dalili mbaya kwani inaashiria kwamba hakuna uhusiano katika ya ukuaji wa uchumi kwa asilimia 7 na kuboreka kwa maisha ya wananchi. Kwa maneno mengine ukuaji wa uchumi si shirikishi kama nilivyoeleza hapo awali na kwa maana hiyo unagusa kwa kiwango kidogo sana maisha ya mwananchi wa kawaida.

## Deni la Taifa na Athari zake kwa maendeleo ya Taifa

**35. Mheshimiwa Spika,** madeni ya Taifa hadi Desemba 2016 yamefikia zaidi ya dola za Kimarekani bilioni 20.7 yakiwemo ya ndani na nje ikiwa ni pamoja na mifuko ya hifadhi ya jamii.Kiwango hiki ni takriban shilingi za Kitanzania 46.66 trilion. Kasi ya kukua kwa deni hili inazidi kushika kasi kutokana na riba na adhabu mbalimbali zitokanazo na kuchelewa kulipa kwa wakati madeni yetu. Aidha kuongezeka huku kunachangiwa na Serikali kuendelea kukopa hususan kwenye vyanzo vya kibiashara ambapo riba zake ni kubwa.

36**. Mheshimiwa Spika,** deni la nje sasa hivi linaigharimu serikali karibu nusu ya makusanyo yake yatokanayo na kodi. Ukichanganya na mishahara, karibu asilimia 70 ya mapato

ya ndani yanatumika kulipia deni la nje na mishahara ya watumishi mbalimbali wa Serikali.

37. **Mheshimiwa Spika,** mara kadhaa watu wengi wametahadharisha kuhusu athari za kukopa kuliko uwezo wetu na Serikali imejitetea kwamba deni la nchi ni stahimilivu. Pamoja na ustahimilivu huo, sasa athari zake zinaanza kuwa na athari kubwa katika kutekeleza bajeti na hivyo mipango ya serikali ikiwepo miradi mbalimbali ya maendeleo.

**NAFASI YA TANZANIA KATIKA JUMUIYA YA KIMATAIFA**

**38. Mheshimiwa Spika,** nchi yetu ilijijengea heshima kubwa katika medani za kimataifa hasa kwenye masuala ya kupigania uhuru wa nchi nyingine barani Afrika, pamoja na kutetea nchi ambazo zilikuwa zinaonewa na mataifa mengine duniani.

**39. Mheshimiwa Spika,**Ushirikiano wa kimataifa kwa nchi inayoendelea kama Tanzania ni jambo la msingi sana kwani kuna mambo mengi ambayo tunahitaji kujifunza kutoka kwa mataifa mengine ili kuweza kuasili mabadiliko ya kisayansi, kiteknolojia, kiuchumi na kiutandawazi yanayoendelea kutokea kila siku duniani.

**40. Mheshimiwa Spika,** Licha ya umuhimu huo, serikali ya awamu ya tano imeonekana kufifisha ushirikiano wa kidiplomasia na mataifa mengine kwa kudhibiti safari za nje kwa kisingizio cha kubana matumizi. Ikumbukwe kwamba kudhibiti safari za nje kusiko kwa kimkakati ni kuliingiza taifa kwenye giza nene kwani safari hizo zilikuwa ni lango la fursa za biashara ya kimatafa (international trade) ambayo ndiyo msingi wa diplomasia ya ki-uchumi.

**41. Mheshimiwa Spika,** Ushirikiano wa kimataifa unaimarishwa pale ambapo wakuu wa nchi mbalimbali wanapokutana kujadili masuala mbalimbali kuhusu mustakabali wa nchi zao na namna ya kusaidiana kukabiliana na changamoto mbalimbali. Ni jambo la kustaajabisha kuona Rais wa nchi yetu akiwa na mwamko

mdogo wa kushiriki mikutano ya kimataifa kwa ajili ya kukuza ushirikano na mataifa mengine. Kitendo cha Rais kushindwa kuhudhuria Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN General Assembly) mwaka jana kimeiweka Tanzania nyuma katika uhusiano wa kimataifa.

**42. Mheshimiwa Spika,** Pamoja na kutambua kuwa Rais amekuwa akituma wawakilishi katika mikutano ya kimataifa, lakini viko vikao au mikutano ya kimkakati (strategic meetings) ambayo ni lazima Rais wa nchi kushiriki.

**43. Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa rai kwa Rais kuacha kukwepa kuhudhuria mikutano ya kimataifa na ya kikanda ambayo ni muhimu kwa ajili ya kujenga mustakabali wa diplomasia ya uchumi pamoja na uhusiano wa kimataifa kwa ujumla kama ambavyo umekuwa ni utamaduni wa taifa letu. Aidha, washauri wa Rais hasa wa masuala ya kimataifa wamshauri Rais juu ya umuhimu wa ushiriki wake katika vikao na mikutano hiyo pamoja na kuzingatia itifaki za kimataifa.

**44. Mheshimiwa Spika,** kuna udhaifu mkubwa sana katika Serikali hii wa kutozingatia itifaki za kimataifa. Wengi walishangazwa wakati Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa anakuja nchini na kupokelewa na Waziri wa Mambo ya njebila kupata fursa ya kuonana na Rais. Inaweza kuonekana kama ni kawaida tu Rais kutompokea Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa; lakini katika jicho la kidiplomasia kuna makosa makubwa sana ya kiitifaki yanayofanywa na Ofisi ya Rais.

**45. Mheshimiwa Spika,** uhusiano wa kimataifa unaweza kuathiriwa na namna sisi kama taifa tunavyowatendea raia wa nchi nyingine wanaoishi au kufanya kazi katika nchi yetu. Mataifa mengine huwa yanajali sana hali za raia wao wanaoishi au kufanya kazi katika mataifa mengine. Hivyo, mataifa hayo huwa yako tayari hata kupigana vita kwa ajili ya raia wao wanaonyanyaswa au kutendewa visivyo katika nchi nyingine.

**46. Mheshimiwa Spika,** kitendo cha hivi karibuni cha Rais wetu kuagiza pasi ya kusafiria ya mkandarasi kutoka India ambaye anajenga mradi wa maji wa Ngapa huko Lindi kutokana na makosa aliyoyafanya katika mradi huo unaweza kuingiza nchi yetu katika mgogoro wa kidiplomasia kwa sababu pasi ya kusafiria ni mali ya taifa ambalo limetoa pasi hiyo. Na katika pasi hiyo kuna tamko la Rais wa nchi husika linaloomba raia huyo apewe ulinzi na msaada wowote atakaohitaji katika nchi atakayokuwa ameingia kuishi au kufanya kazi.

**47. Mheshimiwa Spika,** ikumbukwe kuwa utamaduni duniani ni kuwa pasi ya kusafiria hutolewa na Rais wa nchi husika kwenda kwa mamlaka ya nchi ambayo mtu anasafiri kwa ajili kupata msaada wowote anaohitaji kulingana na malengo ya safari yake na taratibu za nchi aliyopo. Hata Sheria yetu inayosimamia utoaji wa pasi na nyaraka nyingine za kusafiri kifungu cha nne kinatamka kuwa pasi inatolewa na Rais kwa ajili ya kumtambulisha Mtanzania katika mamlaka ya nchi nyingine na kupatiwa msaada na usaidizi wowote atakaohitaji kwa mujibu wa taratibu za nchi husika. Hivyo, kuagiza pasi hiyo kushikiliwa ni kuidhalilisha mamlaka iliyotoa pasi hiyo kwa maana ya Rais wa nchi husika jambo ambalo linaiingiza nchi yetu katika mgogoro wa kidiplomasia moja kwa moja.

**48. Mheshimiwa Spika,** agizo la Rais la kushikilia *passport* ya mkandarasi huyo tayari limeripotiwa katika vyombo mbalimbali vya habari vya kimataifa ambavyo kwa vyovyote vile vinasomwa na watu mbalimbali duniani wakiwemo wawekezaji.

**49. Mheshimiwa Spika,** serikali ina vyombo vya ulinzi na usalama mpaka mipakani, kama mwekezaji au mkandarasi kutoka nje amepewa maelekezo ya kumaliza mradi kwa muda fulani, ni vema akapewa nafasi ya kufanya hivyo bila kuchukua pasi yake ya kusafiria. Mambo yote hayo yanafanyika kwa mujibu wa mikataba ambayo serikali imeingia na wawekezaji au wakandarasi na hivyo ni vema

mikataba ikazingatiwa na au maelekezo/makubaliano mengine kuliko kuanza kuchukua pasi za kusafiria za mataifa mengine.

**50. Mheshimiwa Spika,** athari za maamuzi au amri za Rais zinaweza zisionekane leo lakini kwa utafiti wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ni kuwa agizo la Rais la kuamuru pasi ya raia mwingine kuchukuliwa liliripotiwa katika vyombo vya habari vingi duniani pamoja na nchi ya India yenyewe. Jambo hili si tu linatia doa nchi yetu katika masuala ya uhusiano wa kimataifa lakini pia linaweza kuleta athari katika sekta ya uwekezaji.

**HALI YA UTUMISHI WA UMMA NCHINI**

**Utumbuaji Holela wa Watumishi Usiozingatia Sheria na Taratibu za Utumishi wa Umma.**

**51. Mheshimiwa Spika,** sekta ya utumishi wa umma imeghubikwa na hofu kubwa hivi sasa kutokana na utumbuaji holela wa watumishi usiozingatia sheria za nchi. Watu wachache wanaamini wao wanamamlaka ya kuamua vile wanavyoona inafaa wao kwa utashi wao bila kuzingatia sheria za nchi. Ifahamike kuwa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeti haipuuzi hata kidogo jitihada zinazofanywa na kila mmoja wetu katika kuhakikisha sekta ya umma inafanya kazi kwa weledi ili kuleta tija katika taifa. Lakini, jitihada hizi ni lazima zizingatie sheria na taratibu tulizojiwekea kama taifa ili kuepusha uonevu na matumizi mabaya ya madaraka kwa waliopewa dhamana.

**52. Mheshimiwa Spika,** ifahamike kuwa hakuna mtu yoyote ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliye juu ya sheria au mwenye mamlaka ya kutumia cheo chake kinyume na sheria. Nayasema haya kwa kuwa; kumeibuka tabia ya baadhi ya viongozi wa Serikali kutumia mamlaka yao kuwawajibisha watumishi wa umma bila kuzingatia sheria kwa kuwatumbua hadharani bila kupewa haki ya kusikilizwa na hata kutumia lugha za kejeli na udhalilishaji.Hii imechangiwa pia na 'umwamba' ambao kila mwenye

dhamana anataka kuuonyesha ili kufurahisha mamlaka zao za uteuzi au kwa hofu tu ya wao kutumbuliwa hata bila sababu za msingi.

**53. Mheshimiwa Spika,** Ikumbukwe kuwa katika Ibara ya 13 (6) (a) na (b)ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatao haki ya kupewa fursa ya kusikilizwa kwa ukamilifu,na pia haki ya kukata rufani au kupata nafuu nyingine ya sheria kutokana na maamuzi ya mahakama au chombo kinginecho kinachohusika, na katika kipengele (b) kinasema ni marufuku kwa mtu anayeshtakiwa kwa kosa la jinai kutendewa kama mtu mwenye kosa hilo mpaka itakapothibitika kuwa anayo hatia ya kutenda kosa hilo. Hivyo, basi Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kuacha mara moja tabia hii inayokiuka haki za watumishi wa umma, inayodhalilisha sekta ya umma na inayojenga hofu na itakayo iletea hasara kubwa serikali katika kulipa fidia.

**Uhakiki wa Vyeti na Watumishi Hewa**

**54. Mheshimiwa Spika,**Serikali inaendesha zoezi la uhakiki wa watumishi wa umma ikiwa ni pamoja na vyeti vya taaluma zao ili kukabiliana na tatizo la watumishi hewa pamoja na watumishi wasio na sifa.Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haina tatizo na zoezi la namna hiyo kwa kuwa linalenga kuokoa fedha za umma zinazopotea kutokana na watumishi hewa na kudhibiti ubora wa huduma zinazotolewa katika sekta ya umma kwa kuhakikisha watumishi wote wana taaluma au sifa stahiki katika kazi wanazozifanya.

**55. Mheshimiwa Spika,** Pamoja na dhamira hiyo njema ya serikali ni muhimu kazi hii ikafanywa kwa weledi bila kuathiri masharti ya Ibara ya 13 (1) ya Katiba ya nchi inayoonya ubaguzi wa aina yoyote kwa mtu yoyote bila kujali cheo chake,kabila lake, dini yake, elimu yake na hata jinsia yake.

**56. Mheshimiwa Spika,** wapo Watanzania wengi waliochukuliwa hatua baada ya kukutwa na vyeti feki lakini cha ajabu ni kuwa kitendo cha Mheshimiwa Rais kuendelea

kumkingia kifua Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Christian Makonda, ambaye anashutumiwa kutumia cheti ambacho sio chake na kushindwa hata kuamuru uchunguzi wa jambo hilo ufanyike, ni kitendo cha kufedhehesha sana kwani kinawagawa Watanzania. Ubaguzi wanamna hiyo unalifanya kundi fulani kujisikia wanyonge na hawana haki na kundi jingine kujisikia wao wana haki zaidi ya wengine. Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutenda haki katika zoezi hili la uhakiki kwani limeshaanza kuonyesha dalili za ubaguzi na upendeleo jambo ambalo linasababisha matabaka ya watu katika taifa.

**KAZI NA AJIRA KWA VIJANA**

**57. Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa taarifa ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu ya mwaka 2011 ni kwamba; asilimia 68 ya watanzania ni vijana wenye umri kati ya miaka 15 hadi 35. Nyaraka zinaonesha kuwa Tanzania inakadiriwa kuwa na nguvu kazi yawatu zaidi ya **22,152,320** na kati ya hao watu **19,783,648** hawana ajira iliyo rasmi. Kiwango cha ukosefu wa ajira kwa vijana kati ya umriwa miaka 15-34 ni asilimia 13.4.

**58. Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa tovuti "*youth employement*" *(www. youthemployementdecade.org)*, nguvu kazi mpya inayoingia kwenye soko la ajira kilamwaka ni zaidi ya watu **800,000** na kati ya hao ni vijana **40,000 tu** sawa na **asilimia 5.7** ndio wanaopata ajira katika sekta rasmi. Ikumbukwe kwamba takriban vijana 700,000 wanamaliza vyuo na shule katika ngazi mbalimbali kila mwaka na wengine 100,000 wanahamia mijini kutoka vijijini na wote hawa wanahitaji ajira.

**59. Mheshimiwa Spika,** ukosefu wa ajira hasa vijana ni janga la taifa na serikali isipochukua hatua za makusudi yamkini nchi hii inaweza kuja kuingia kwenye mgogoro mkubwa kutokana na hali ngumu ya maisha itakayokuwa imesababishwa na ukosefu wa ajira. Ili taifa lisifike huko, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri na kupendekeza

kwa serikali kwamba, itoe maagizo kwa wakurugenzi wote wa Halmashauri kutengeneza ajira angalau 20,000 kila mwaka katika miradi mbalimbali inayotekelezwa katika halmashauri zao, na taarifa ya utekelezaji wa agizo hilo iwe inatolewa kila mwaka kwenye Bunge la Bajeti wakati Waziri mwenye dhamana na TAMISEMA atakapokuwa anawasilisha bajeti ya wizara yake.

**60. Mheshimiwa Spika,** kukiwa na dhamira ya kutekeleza ushauri huu, tutapunguza kwa kiasi kikubwa tatizo la ajira nchini.

## SAKATA LA DAWA ZA KULEVYA

**61. Mheshimiwa Spika,** naomba nitumie fursa hii kutambua jitihada za Serikali,Waheshimiwa Wabunge na jamii kwa ujumla kwa kushirikiana kwa pamoja katika kupambana na biashara ya madawa ya kulevya pamoja na matumizi ya aina yoyote ya madawa ya kulevya. Sote tunatambua madhara makubwa ya madawa haya kwa kuwa tumepoteza ndugu, jamaa, marafiki na nguvu kazi ya taifa kutokana na matumizi ya dawa za kulevya.

**62. Mheshimiwa Spika,** kihistoria vita ya dawa ya kulevya nchini imeanza muda mrefu. Jitihada za kupambana na madawa haya zilizaa matunda yaliyopelekea kutungwa kwa Sheria ya madawa na Uzuiaji wa Usafirishaji wa Madawa Haramu tangu mwaka 1995 ambayo ilifutwa na baadaye kutungwa sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ya mwaka 2015. Aidha, iliundwa Tume ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Mfuko wa Udhibiti wa Dawa za Kulevya na uwepo wa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya kuzuia na kupambana na dawa za kulevya (DCEA) pamoja na kampeni mbalimbali zinazoendeshwa na serikali, taasisi binafsi, wanasiasa na hata viongozi wa dini katika kupambana na madawa hayo.

**63. Mheshimiwa Spika,** hivi karibuni harakati hizi zilichukua sura mpya baada ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam kuwataja hadharani watuhumiwa wa dawa za kulevya.

Jambo hili lilizua mtanzuko mkubwa kwa wanajamii huku kila mmoja akilipokea kwa namna yake.

**64. Mheshimiwa Spika,** Kitendo cha kuwataja watu hadharani bila kuwa na ushahidi wowote kilifanywa kibabe kwa kuwakejeli, kuwadhihaki na kwa uonevu mkubwa kwa kuwa hakukuwa na ushahidi wowote na pia mahakama haikuhusishwa katika hatua za awali. Hii ina maana kwamba Mkuu huyo wa Mkoa aliamua kuwa hakimu kwa kutumia cheo chake kuchafua majina ya watu na haiba walioitengeza kwa muda mrefu na gharama kubwa.

**65. Mheshimiwa Spika,** tabia ya viongozi wa namna hii wanaotumia madaraka yao vibaya kwa kuvunja sheria kwa makusudi ni lazima ipingwe kwa nguvu zote na hatua kali zichukuliwe dhidi yao bila kujali nafasi zao au vyeo vyao.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeshangazwa sana na kitendo cha Rais Magufuli kuendelea kumkingia kifua Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salam katika matukio tofauti tofauti huku ushahidi wa wazi ukionyesha matumazi mabaya ya madaraka pamoja na ukiukwaji wa haki za binadamu, umiliki wa mali ulio wa mashaka ikiwemo magari ya anasa ya wafanyabiashara aliowatuhumu kujihusisha na madawa ya kulevya, vitisho kwa vyombo vya habari , kuingilia uhuru wa habari nchini ,matumizi mabaya ya rasilimali za nchi ikiwa ni pamoja na kufanya tafrija ya kutimiza mwaka mmoja kazini kwa kivuli cha kampeni ya kutokomeza dawa za kulevya.

**66. Mheshimiwa Spika,** ni jambo la kusikitisha sana kuona Mheshimiwa Rais akimtoa kafara Waziri wake kwa gharama ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam.Tunajiuliza kuna jambo gani lililojificha baina ya Rais na Mkuu huyu wa Mkoa? Tatizo la madawa ya kulevya sio tatizo la mtu mmoja na wala halihitaji kufwanywa kama vita ya mtu binafsi.

**67. Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua Rais anamamlaka ya kuteua nakutengua uteuzi lakini hana mamlaka ya kumkingia kifua mtu yoyote pale anapovunja sheria za nchi hata kama Rais ndie aliyempa dhamana. Hivyo

basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inawataka viongozi wote waliopewa dhamana kuheshimu ‘utu’ na haki za kila raia. Ugomvi binafsi, kutofautiana kiitikadi,kiimani na hata kimtazamo kusimfanye yoyote mwenye dhamana kutumia mamlaka yake katika kumuonea mtu yoyote. Kama taifa tuna jukumu la kusimamia misingi ya utu na kuheshiminiana.

**68. Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inamtaka Mheshimiwa Rais kumchukulia mara moja hatua za kinidhamu Mkuu wa Mkoa Dar es Salaam. Aidha, Rais aache ubaguzi katika maamuzi ya kinidhamu kwa baadhi viongozi wa umma kwani hii ni kuwa na ***double standard***katika utekelezaji wa majukumu yake.

**MAMLAKA ZA KISHERIA ZA JIJI LA DAR ES SALAAM KATIKA KUSIMAMIA NA KUENDESHA USAFIRI WA UMMA**

**69. Mheshimiwa Spika,** majiji makubwa duniani yanakabiliwa na changamoto za kuongezeka kwa wakazi wake, jambo ambalo limepelekea kuwepo kwa mahitaji makubwa ya huduma za kijamii na za kiuchumi kama vile, afya, elimu, maji, huduma za uokozi, usalama wa raia na huduma za usafiri.Kutokana na ukweli huo, sheria za majiji hayo, zimetoa mwongozo na mamlaka kwa majiji hayo kushughulikia baadhi ya masuala yenye athari za moja kwa moja kwa wananchi wa eneo husika ili kukabiliana na changamoto hizo. Kwa sababu hiyo, Mameya na kamati zao wamepewa mamlaka makubwa ya kupanga na kutekeleza mipango ya maendeleo katika majiji wanayoyaongoza.

**Mamlaka ya Usimamizi wa Usafiri wa Umma Katika Majiji**

**70. Mheshimiwa Spika,** Ipo Mifumo tofauti ya umiliki na uendeshaji wa usafiri wa umma katika mabara ya Ulaya, Asia na Amerika ya Kaskazini. Katika Bara la Asia, nchi nyingi hutumia mfumo waushirika kati ya sekta ya umma na sekta binafsi – yaani PPP. Mfumo huo ni tofauti na ule unaotumika na nchi za Bara la Amerika ya Kaskazini ambapo umiliki na uendeshaji upo chini ya mamlaka za manispaa za miji husika. Nchi nyingi za bara la Ulaya huduma ya usafiri kwenye majiji

hutolewa na makampuni ya umma na makampuni machache ya watu binafsi.

**Mifano ya baadhi ya Majiji na Mamlaka ya Usimamizi na Uendeshaji wa Usafiri wa Umma.**

**71. Mheshimiwa Spika, Jiji la London: Jiji** hili limeanzisha mamlaka inayoitwa "Great London Authority." Mamlaka hii iko chini ya Meya wa London. Katika mamlaka hii ya Great London Authoriy, kuna idara maalumu inayoshughulikia usafiri wa wakazi wa London (Transport for Londoners). Kwa kifupi, mfumo mzima wa usafiri wa Umma katika Jiji la London, unaratibiwa na kusimamiwa na mamlaka ya jiji la London na msimamizi mkuu akiwa ni Meya wa Jiji la London.

**72. Mheshimiwa Spika,Jiji la Cape Town - Afrika ya Kusini:**katika Jiji hili, usafiri wa abiria upo chini ya Ofisi ya Meya. Mamlaka ya Jiji hili imeanzisha chombo kinachoitwa Transport for Cape Town, (TCT) ambacho kinasimamia na kuendesha mradi wa mabasi yaendayo kasi wa "My CiTi Bus Service".

Chombo hiki kina mamlaka ya kupanga, kusimamia, kudhibiti, kutoa mikataba kwa makampuni, na kukarabati miundo mbinu yote ya barabara katika Jiji la Capetown. *"The TCT has full mandate and autonomy over issues pertaining, planning, costing, contracting, regulating, monitoring, evaluating, communicating, managing and maintaining the city of Cape Town's Transport infrastructure, systems, operations, facilities and network."*

**73. Mheshimiwa Spika, Jiji la Johannesburg –Afrika ya Kusini:** Mamlaka ya jiji hili iliunda chombo kinachoitwa Rea-Vaya *"the City of Johannesburg's Revolutionary Bus Rapid Transit system. "REA VAYA, which means "we are going", offers fast, safe and affordable public transport on a network of bus routes across Johannesburg".* Rea-Vaya kwa sasa inaendeshwa kwa pamoja na ushirika wa wenye taxi ambao walikuwa ni wahanga baada ya mfumo huo kuanzishwa na Jiji hilo.

**UANZISHWAJI WA HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM NA MAMLAKA YAKE YA KISHERIA**

**75. Mheshimiwa Spika,** Jiji la Dar es salaam limeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji ) namba 8 kifungu cha 5 (1) na (4) ya mwaka 1982 ambapo Waziri mwenye mamlaka ya Serikali za Mitaa hutangaza kwenye gazeti la serikali kuanzisha Mamalaka ya Jiji.Majukumu ya Jiji yameainishwa katika kifungu cha 55 (1)(2) cha sheria namba 8 ya mwaka 1982 pamoja na majukumu mengine yaliyoainishwa kwenye jedwali la sheria kama ifuatavyo;

- Kuhakikisha barabara kuu zote ndani ya Jiji Zinakuwa katika hali ya usafi.

- Kusimamia matumizi ya usafiri wa umma kwenye masuala ya gharama za ukodishaji/ nauli, njia za magari hayo pamoja na maegesho.

- Mamalaka za Jiji kulingana na majukumu ya Jiji yameainishwa katika kifungu cha 59(h)(i)(l) kuwa kwa ruhusa ya Waziri mamlaka ya Jiji inaweza kuanzisha huduma ya usafiri, kutoza kodi kwenye huduma za Jiji na kuelekeza njia za magari/routes, mitaa ambayo magari yanayotoa usafiri wa umma yatapita bila kuathiri mwenendo mzima wa usafiri wa magari mengine.

**76. Mheshimiwa Spika,** majukumu mengine kwa mujibu wa jedwali la sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) ni kama ifuatavyo;

- ✓ kusimamia na kupanga makazi;

- ✓ kuanzisha na kuendesha masuala ya zimamoto kwenye Jiji;

- ✓ kuanzisha, kusimamia na kudhibiti mifumo ya taa katika maeneo ya umma ndani ya Jiji;
- ✓ **kuanzisha na kuendesha usafiri wa umma ndani ya Jiji;**
- ✓ kuanzisha na kuendesha usafiri wa feri au boti;
- ✓ kujihusisha na biashara au kuanzisha viwanda.

**MAMLAKA YA JIJI LA DAR ES SALAAM KATIKA KUMILIKI, KUENDESHA NA KUSIMAMIA SHIRIKA LA USAFIRI DAR ES SALAAM (UDA)**

**77. Mheshimiwa Spika,** Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA) lilianzishwa Mei 1974 chini ya Sheria ya Makampuni (Companies Ordinance, Cap 212) ikiwa na hisa zilizoidhinishwa (Authorised Shares) 15,000,000. Kati ya hiza hizo, hisa 7,119,697 zilizolipiwa (allotted) zilitolewa kwa Serikali kwa asilimia 100 na hisa zilizobaki 7,880,303 zilibaki kama hisa zisizogawiwa (unalloted shares) kwa shirika. Lengo kuu la kuanzisha shirika hilo lilikuwa ni kutoa huduma ya usafiri wa umma katika Jiji la Dar es Salaam.

**78. Mheshimiwa Spika,** Ili kuongeza tija na ufanisi wa uendeshaji wa shirika la UDA, mwaka 1985, Serikali iligawa hiza zake 3,631,046 zilizolipiwa sawa na asilimia 51 kwa jiji la Dar es Salaam na hivyo kubakia na hisa 3,488,651 sawa na asilimia 49. Hata hivyo, UDA ilishindwa kujiendesha kutokananaupungufu wa mtaji na udhaifu wa uendeshaji (management) uliochagizwa na ushindani wa kibiashara baada ya Serikali kuruhusu sekta binafsi kutoa huduma ya usafiri katika Jiji la Dar es Salaam.

**79. Mheshimiwa Spika,** kutokana na UDA kushindwa kujiendesha, iliwekwa chini ya Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma (PSRC) mwaka 1997 kwa lengo la kuibinafsisha. Ili kutekeleza lengo hilo la kubinafsisha UDA, PSRC ilitangaza uuzaji wa asilimia 49 ya UDA kwa mwekezaji aliyekuwa na nia ya kununua. Hatimaye, Kampuni ya Simon

Group Limited ilinunua hisa hizo. Hata hivyo hakukuwa na uwazi katika mchakato wa kuiuzia Kampuni ya SGL hisa hizo na pia mwanahisa mkubwa ambaye ni Msajili wa Hazinahakushirikishwa jambo ambalo lilizua mgogoro juu ya uhalali wa umiliki wa hisa za UDA na hasa ushiriki wa Kampuni ya SGL.

**80. Mheshimiwa Spika,** pamoja na mchakato wa uuzaji wa hisa za UDA kwa Kampuni ya Simon Group kugubikwa na utata kwa kutozingatiwa kwa utaratibu wa uuzwaji wa hisa za serikali, na pia utata kuhusu uuzwaji wa hisa za Jiji, bado kuna haja ya wadau wa Jiji kukaa pamoja kutafuta suluhu ya mgogoro huo. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinanzani Bungeni inashauri wadau wa UDA wakae na kuweka msimamo wa pamoja kutafuta suluhisho la sakata la UDA kwa manufaa ya Jiji la Dar es Salaam.

**81. Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa inafahamika duniani kuwa suala la usafiri ndani ya Majiji husimamiwa na Jiji husika na au kwa kushirikiana na sekta binafsi;

Na kwa kuwa ilivyo sasa pamoja na makosa yaliyofanyika tayari Simon Group ndiyo kampuni pekee inayoendesha shirika la UDA bila Halmashauri ya Jiji kuhusika katika kusimamia na kuendesha usafiri wa Dar es Salaam;

Na kwa kuwa hapa nchini vipo vitega uchumi vingi ambavyo vimebinafsishwa bila kuzingatia utaratibu;

Na kwa kuwa imetolewa kauli na Rais kupoka sehemu ya miliki ya hisa za Jiji kama suala la UDA halitapewa ufumbuzi; HIVYO BASI, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri kuwa wadau wa Dar es Salaam kwa maana ya Mameya, Madiwani wakubaliane masuala yafuatayo;

(i) Kuwa, Jiji lipewe hisa na haki ya kuwa sehemu ya kuendesha na kusimamia usafiri wa Dar es Salaam kama ilivyo katika majiji mengine duniani.

(ii) Kuwa, Halmashauri ya Jiji iwe na mamlaka ya kutoa leseni kwa mwekezaji mwingine ambaye atapewa kuwa sehemu ya kutoa huduma katika Jiji la Dar es Salaam kuliko ilivyo sasa ambapo ni Simon Group Limited pekee wanaoendesha usafiri wa Jiji lote la Dar es Salaam.

(iii) Serikali kuu ibaki na jukumu la kutoa miongozo ya kisera na kusimamia hisa zake katika vikao vya wanahisa na sio kama ilivyo sasa ambapo kwa sasa DART ipo chini ya TAMISEMI ambayo ni ofisi ya Rais.

(iv) Kuwa kuisimamisha kampuni ya Simon Group ambayo inajulikana kuwa ilipata hisa na miliki ya kuendesha usafiri wa Jiji bila kuzingatia utaratibu na njia zilizowazi, na pia ikijulikana kuwa tayari kampuni hiyo imeshakopa fedha kwa kutumia mali za Jiji na pia tayari kampuni hiyo ikiwa tayari inatoa huduma kwa wananchi wa Dar es Salaam, hautakuwa uamuzi wenye maslahi mapana kwa wananchi.

**82. Mheshimiwa Spika, jambo muhimu hapa ni** ni Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kuwa na say/stake katika kupanga na kuendesha mradi wa usafiri wa umma kwa kuwa Halmashauri ya Jiji ndio wawakilishi wa wananchi. Kwa maneno mengine, mamlaka za kisheria za Jiji la Dar es Salaam za kupanga na kusimamia usafiri wa umma katika jiji la Dar es Salaam kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) 1982 zilindwe na zitekelezwe.

**UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/17 NA UCHAMBUZI WA BAJETI INAYOPENDEKEZWA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/18**

**83. Mheshimiwa Spika,** wajibu wa Serikali katika bajeti ni kukusanya mapato na kutumia mapato hayo katika

matumizi ya kawaida na maendeleo kwa kadiri itakavyokuwa imeidhinishwa na Bunge. Kwa maneno mengine, ni wajibu wa Serikali kutekeleza Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge.

**84. Mheshimiwa Spika,** licha ya Serikali kuwa na wajibu huo, kumeanza kuwa na utamaduni wa utekelezaji mbaya wa bajeti inayoidhinishwa na Bunge. Utekelezaji huu mbaya unatokana na kukosekana kwa umakini tangu bajeti ya serikali inapoandaliwa na pia kuingiza matashi ya kisiasa katika bajeti, jambo ambalo linaifanya bajeti yote kuwa *'unrealistic'*.

**85. Mheshimiwa Spika,** mfano mzuri wa ukosefu wa umakini, ni katika uandaaji wa bajeti ya 2016/17 inayomaliza muda wake, ambapo kulikuwa na tofauti ya kati ya takwimu zilizokuwa katika vitabu vya mapato, na vile vya matumizi. Kwa mfano, wakati kitabu cha mapato ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaonza tarehe 1 Julai, 2016 hadi tarehe 30 Juni 2017 kinaonyesha kuwa jumla ya mapato yote ya Serikali ni shilingi trilioni 22.063; vitabu vya matumizi ya kawaida na maendeleo vinaonyesha kuwa jumla ya matumizi yote ya Serikali kwa kipindi hicho ni shilingi trilioni 23.847; kwa mchanganuo kwamba: Fedha za Matumizi ya Kawaida (Volume II) ni shilingi 13,336,042,030,510 na fedha za Miradi ya Maendeleo (Volume IV) ni shilingi 10,511,945,288,575.

**86. Mheshimiwa Spika,** kwa kifupi ni kwamba; kwa mwaka wa fedha 2016/17, Serikali imepanga kukusanya jumla ya **shilingi trilioni 22.063** ila ikapanga kutumia **shilingi trilioni 23.847,** kiasi ambacho ni zaidi ya mapato yake kwa **shilingi trilioni 1.783.** Swali hapa ni kwamba hii shilingi trilioni 1.783 iliyoongezeka kwenye matumizi itapatikana wapi wakati haipo katika kitabu cha mapato? Huku ni kukosekana kwa umakini na ndio chanzo cha utekelezaji mbaya wa bajeti.

**87. Mheshimiwa Spika,** chanzo kingine cha utekelezaji duni wa bajeti ni kuingiza matashi au maslahi ya kisiasa katika

uandaaji wa bajeti. Nasema hivi kwa sababu bajetiya Serikali iliyopitishwa hapa Bungeni kwa mwaka wa fedha 2016/17 ililenga kupata umaarufu wa kisiasa na sio kutatua kero za watanzania. Hii ni kwa sababu ukisoma sura ya bajeti iliyowasilishwa katika hotuba ya Waziri wa Fedha na Mipango utaona kwamba jumla ya makusanyo yote yalitakiwa kuwa shilingi trilioni 29.539 na matumizi yote shilingi trilioni 29.539 lakini takwimu zilizoandikwa kwenye vitabu vya mapato na matumizi ni tofauti kama nilivyoonyesha hapo juu. Hii ni kuwarubuni wananchi kwamba Serikali imekuja na bajeti kubwa hivyo wategemee unafuu katika huduma za kijamii kumbe ni usanii mtupu.

**88. Mheshimiwa Spika,** mkanganyiko huo wa takwimu za bajeti: kwamba; Serikali ingekusanya shilingi trilioni 29.5 na kutumia shilingi trilioni 29.5 wakati kwenye vitabu inaonekana ingekusanya trilioni 22.063 na kutumia trilioni 23.8 ndio kunaifanya Kambi Rasmi ya Upinzani kuiita bajeti hiyo kuwa ni ***'bajeti hewa'*** na kwamba mkanganyiko huo ndio kiashiria cha kwanza kikubwa; kwamba bajeti hiyo haikutekelezeka ipasavyo. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni iliita bajeti inayomaliza muda wake kuwa ni hewa kwa sababu iliainisha vyanzo hewa vya mapato. Kwa mfano, kuingiza malipo ya kiinua mgongo cha wabunge ambacho kinatakiwa kulipwa mwaka 2020 kwa mujibu wa sheria na kukifanya kuwa chanzo cha mapato katika mwaka huu wa fedha 2016/17, hakuna jina lingine la kukiita chanzo hicho cha mapato isipokuwa ni ***'chanzo hewa cha mapato'*** kwa kuwa fedha hiyo itapatika mwaka 2020 wakati wabunge watakapolipwa kiinua mgongo hicho.

**89. Mheshimiwa Spika,**kwa kuwa kumekuwa na vyanzo hewa vya mapato, ambavyo vimepelekea kuwa na bajeti hewa, basi hata utekelezaji wa miradi mingi ya maendeleo umekuwa hewa.

**90. Mheshimiwa Spika,** naomba nitoe takwimu za utaoji wa fedha kutoka hazina kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo katika wizara mbalmbali hadi kufikia mwezi Machi, 2017 ili kuthibitisha jambo hili. Hadi kufikia mwezi

March, 2017 serikali ilikuwa imetumia jumla ya **shilingi bilioni 4,168.009** sawa na**asilimia 35.26** ya bajeti nzima ya maendeleo ya **shilingi 11,820.503** iliyokuwa imeidhinishwa na Bunge.

**91. Mheshimiwa Spika,** mchanganuo wa matumizi ya fedha za maendeleo katika baadhi ya wizara zenye athari ya moja kwa moja kwenye uchumi ni kama ifuatavyo:

(i) Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ilipewa shilingi 2,251,881,250/= sawa na **asilimia 2.22** ya shilingi 101,527,497,000/= zilizoidhinishwa na Bunge.

(ii) Wizara ya Viwanda na Biashara ilipewa shilingi 7,200,000,000/= sawa na **asilimia 8** ya shilingi 40,000,000,000/= zilizoidhinishwa na Bunge.

(iii) Wizara ya Miundombinu ilipewa:

a) Ujenzi wamepewa jumla ya Tshs trillion 1.075 sawa na**asilimia 58.71** ya shilingi trilioni 2.176 zilizoidhinishwa na Bunge.

b) Uchukuzi wamepewa jumla ya shilingi bilioni 761.5 sawa na **asilimia 30.51** ya shilingi trilioni 2.496 zilizoidhinishwa na Bunge.

(iv) Wizara ya Nishati na Madini wamepewa shilingi bilioni 372.877 sawa na **asilimia 36** ya shilingi trilioni 1.056 zilizoidhinishwa na Bunge.

(v) Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii wamepewa shilingi 133,872,272,755/= sawa na **asilimia 25** ya shilingi bilioni 518.5/= zilizoidhinishwa na Bunge.

(vi) Wizara ya Elimu, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi wamepewa shilingi bilioni 500.452 sawa na asilimia 55.75 ya shilingi bilioni 897.658 zilizoidhinishwa na Bunge.

**92. Mheshimiwa Spika,** kwa takwimu hizo, ni kwamba, Serikali imeshindwa kutekeleza bajeti ya maendeleo ya mwaka wa

fedha 2016/17 kwa takriban asilimia 70. Kambi Rasmi haioni muujiza unaoweza kufanyika ili asilimia hiyo 70 ya bajeti ambayo haijatekelezwa iweze kutekelezwa kabla ya mwaka huu wa fedha haujaisha.

**93. Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani imebaini pia kwamba; Bajeti ya Serikali inayopendekezwa kwa mwaka 2017/18 haikuandaliwa kwa umakini. Hii ni kwa sababu kuna tofauti kati ya ukomo wa bajeti ulioainishwa kwenye Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka mitano na ukomo wa bajeti ulioainishwa katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2017/18.

**94. Mheshimiwa Spika,** Ukomo wa bajeti ulioainishwa katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa miaka mitano kwa mwaka wa fedha 2017/18 ni shilingi trilioni 30.4 wakati ukomo wa bajeti ulioanishwa katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2017/18 ni shilingi trilioni 31.6.

**95. Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuwa makini katika suala zima la uandaaji wa bajeti kwa kuwa, utekelezaji duni wa bajeti zilizotangulia unatokana kwa kiasi kikubwa na maadalizi dhaifu ya bajeti husika.

**URATIBU USIO WAZI WA MATUMIZI YA BILIONI 6.2 FEDHA ZA MAAFA YA WAHANGA WA TETEMEKO LA ARDHI – KAGERA**

**96. Mheshimiwa Spika,** Itakumbukwa kwamba tarehe 10 Septemba, 2016 kulitokea tetemeko la ardhi huko Mkoani Kagera – tetemeko ambalo lilisababisha maafa makubwa kwa wananchi wa Kagera.Kutokana na maafa hayo, wadau na wananchi mbalimbali walioguswa walijitoa kwa hali na mali kwa kuchanga fedha kwa ajili ya kuwasaidia wahanga wa maafa hayo.

**97. Mheshimiwa Spika,** Jambo la kushangaza ni kwamba Serikali ilikataza wadau kutoa michango ya moja kwa moja kwa wahanga na badala yake ikaunda kamati maalum ya

maafa ambapo ilielekeza watu waliotaka kutoa michango kwa ajili ya maafa hayo wachangie kupitia akaunti maalum ya maafa ya kamati hiyo.

**98. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeripoti kupitia randama ya Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Uratibu na Bunge, kwamba iliratibu upatikanaji wa shilingi bilioni 6.2 (6,235,930,095.04/=) kwa ajili ya maafa hayo ila haitoi maelezo yoyote juu ya namna fedha hizo zilivyotumika jambo linalozua hofu kuwa fedha hizo zilitumika tofauti na ilivyokusudiwa.

**99. Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa bado kuna wahanga wa tetemeko ambao bado hali zao ni mbaya kutokana na kukosa misaada; na kwa kuwa Serikali inakiri kuwa ilikusanya shilingi bilioni 6.2 kwa ajili ya maafa hayo, basi Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kumwagiza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi maalumu (Forensic Audit) wa matumizi ya fedha hizo, ili wahanga waweze kujuwa matumizi ya fedha za msaada kwa ajili yao.

**BAJETI YA KUKUZA DEMOKRASIA NCHINI**

**100. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2016/17, Tume ya Taifa ya Uchaguzi iliidhinishiwa na Bunge shilingi bilioni 1.6 (**1,684,723,167/=)** ikiwa ni fedha za Mradi wa Kukuza Demokrasia Nchini (Democratic Empowerment Project). Hata hivyo, fedha iliyotolewa na hazina hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2017 kwa ajili ya kutekeleza mradi huo ni shilingi **milioni 29** (29,085,278/=) sawa na **asilimia 2** tu ya bajeti yote iliyoidhinishwa.

**102. Mheshimiwa Spika,** kutotekelezwa kwa mradi huu ni uthibitisho kwamba Serikali ya awamu ya tano imedhamira kukandamiza demokrasia hapa nchini. Makatazo ya kufanya mikutano ya siasa, ukandamizaji wa uhuru wa vyombo vya habari, udhibiti wa watumiaji wa mitandao ya jamii kupitia Sheria kandamizi za Makosa ya Mitandao (Cyber Crime Act), Sheria ya Huduma za vyombo vya habari na Sheria ya Takwimu ni sehemu endelevu ya mkakati wa Serikali ya awamu ya tano inayovuta hisia za kuwepo mpango wa

kufuta mfumo wa vyama vingi vya upinzani hapa nchini, jambo ambalo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inalikemea kwa nguvu zote. Aidha, vitendo hivyo vyenye lengo la kukandamiza demokrasia vinakwenda kinyume na ibara ya 3(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayosema kwamba *"Jamhuri ya Muungano ni nchi ya kidemokrasia na ya kijamaa, isiyokuwa na dini, yenye kufuata mfumo wa vyama vingi vya siasa"*

**103. Mheshimiwa Spika,Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili imefanya jitihada zipi za kukuza demokrasia hapa nchini ikiwa imeshindwa kutekeleza bajeti iliyotengwa na bunge kwa ajili ya mradi wa kukuza demorasia hapa nchini?

**HITIMISHO**

**104. Mheshimiwa Spika,** wanazuoni wa Sayansi ya Siasa (Political Science) wanasema kwamba; huwezi kutenganisha siasa na maendeleo. Uhusiano kati ya siasa na maendeleo ni sawa na uhusiano kati ya yai na kuku. Huwezi kuwa na kimoja bila uwepo wa kingine. Kwa sababu hiyo, ili taifa liweze kuwa na maendeleo endelevu ni lazima taifa hilo liwe na mfumo mzuri wa siasa – siasa ambayo inaheshimu misingi ya katiba na utawala wa sheria, siasa ambayo inaliunganisha taifa na sio kulisambaratisha kwa misingi ya tofauti za kiitikadi, kidini, kikabila na mambo yanayofanana na hayo.

**105. Mheshimiwa Spika,** Kama nilivyoeleza hapo awali, ili maendeleo ya kiuchumi yaweze kumfikia kila mwananchi ni lazima uchumi huo uwe shirikishi. Uchumi huo hauwezi kuwa shirikishi ikiwa tunabaguana kwa misingi ya tofauti za kisiasa au tofauti nyinginezo. Uchumi wa nchi yetu hauwezi kujengwa na kundi moja la jamii na kulibagua lingine. Hali kadhalika uchumi wan chi yetu hautajengwa na chama kimoja cha siasa kwa kukibagua kingine au kuchochea migogoro ndani ya vyama vingine. Mshikamano wa kitaifa ni muhimu sana katika kujenga uchumi ulio imara. Ndoto ya kufikia uchumi wa viwanda haiwezi kufikiwa tukiwa na msigano wa namna hii.

106. **Mheshimiwa Spika,** wanazuoni wanasema: *"kutofautiana kifikra ni afya ya akili"***;** na ili uvumbuzi utokee lazime kuwe na *fikra mbadala - 'alternative thinking'.* Nilidhani kuwa Serikali na Chama cha Mapinduzi wangetambua kuwa uwepo wa watu wenye fikra mbadala katika taifa hili ni tunu na zawadi kutoka kwa mwenyezi Mungu; lakini badala yake Serikali wameona kuwa uwepo wa watu hao ni kama mwiba na kikwazo.

**107. Mheshimiwa Spika,** Nihitimishe kwa kuwashukuru Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani Bungeni kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia kama kiongozi wao. Naishukuru sana Sekretariat ya KUB kwa namna wanavyokesha kufanya tafiti mbalimbali zinazosaidia uandaaji wa hotuba za Kambi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha.

Freeman Aikaeli Mbowe (Mb)
**KIONGOZI WA UPINZANI BUNGENI NA**
**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI**
**KATIKA OFISI YA WAZIRI MKUU**
6 Aprili, 2017

**SPIKA:** Sasa Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na pande za wachangiaji. Sasa tukiwa tunaendelea...

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Muda wetu ni mdogo sana katika mambo haya. Kwa kifupi sana.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nasimama kwa kanuni ya 68(7), kuhusu suala lililotokea Bungeni kufuatia hotuba ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni na maneno ambayo ameambiwa ayatoe kwenye hotuba yake.

Mheshimiwa Spika, naomba ufafanuzi wako.

**SPIKA:** Hebu naomba ukae Mheshimiwa, maana yake unaturudisha kule kule. Maneno yale amekubali mwenyewe kuyatoa na ameyatoa. Kwa hiyo, sidhani kama mjadala wako utakuwa na afya. Unachofanya ni kumtaka sasa kiongozi wako tena arudishe vitu ambavyo ameshavitoa.

Kwa hiyo, tuokoe muda ili twende kwenye uchangiaji. Ushauri wangu ni kwamba tuna dakika kumi kumi Waheshimiwa kuanzia leo kwa siku kadhaa zijazo kwa ajili ya uchangaji wa hotuba hii muhimu ya Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Katika dakika hizo kumi, dakika kumi si kitu, ni kitu kidogo sana. Kwa hiyo, naomba wale wote watakaopata fursa za kuchangia, kwa kweli wajipange vizuri watumie dakika zao vizuri msije mkahisi kama meza inakatakata dakika zenu nakadhalika.

Meza nanyi mjitayarishe mkae vizuri, ni dakika kumi na siyo zaidi. Kwa mchangiaji mzuri mwenye uzoefu, dakika kumi ni hoja mbili au tatu. Ukienda na lingine; na lingine; hata ulichokiongea, hata ambacho hukuongea inakuwa hakieleweki. Huo ni ushauri wa jumla.

Kwa hiyo, tutaenda kwa uwiano ambapo tuna majina ya Wabunge kama nilivyoletewa na viongozi wa vyama husika au kambi husika. Kwa hiyo, ataanza Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi atafuatiwa na Edward France Mwalongo, atakuja Mheshimiwa Godbless Lema, Mheshimiwa Masood Abdalah Salum na atafuatia Amina Saleh Mollel kwa sasa. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Bwanausi uanze.

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kutoa shukrani kwa kupata fursa hii kama mchangiaji wa kwanza kwenye hotuba ya Waziri Mkuu. Nianze tu kwa kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, kwa kazi kubwa anayoifanya na kuonesha uzalendo wa hali ya juu katika kuhudumia Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, namshukuru sana mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa jinsi alivyotoa hotuba yake na jinsi alivyojaribu kuchambua maeneo mbalimbali yanayohusiana na shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, labda niende moja kwa moja, lakini pia bila kuwasahau Waziri anayeshughulikia Bunge, Ajira, Kazi, Vijana na Watu wenye Ulemavu, Mheshimiwa Jenista Mhagama pamoja na Naibu wake, ndugu yangu pale Mheshimiwa...

**SPIKA:** Mavunde!

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Mavunde kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende moja kwa moja kwenye kilimo na hasa kwenye ukurasa wa 23 wa kitabu cha hotuba ya Waziri Mkuu, alipozungumzia zaidi suala la stakabadhi ghalani. Nianze tu kwa kusema, kwa kweli Sheria ya Ushirika inabidi tuombe mamlaka zinazohusika zilete sheria ile tena, tuifanyie marekebisho kwa sababu sheria ya ushirika ina upungufu mwingi sana na kusababisha wananchi wetu kupata athari mbalimbali katika kupata haki zao katika mazao yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakubaliana kabisa na hoja ya Waziri Mkuu kwamba maeneo mengi, stakabadhi ghalani imeonekana moja kwa moja kuwa ndiyo ufumbuzi wa matatizo ya masoko katika mazao yetu mbalimbali, ikiwemo kahawa, chai, tumbaku, pareto, korosho na mengineyo. Nitolee mfano zao la korosho; tatizo kubwa lililojitokeza kufanya wakulima wetu wasipate haki vizuri ni tatizo la vyama vya msingi na vyama vikuu wakati mwingine kufanya kwa makusudi kabisa hujuma ya kuiba fedha za wakulima.

Mheshimiwa Spika, nikitolea mfano, wananchi walipeleka zao lao la korosho kwenye maghala tangu Septemba mwaka 2016, lakini ninavyosema hivi sasa, kwenye

Halmashauri yangu ya Wilaya ya Masasi kiasi cha zaidi ya sh. 1,200,000,000/= hazijalipwa kwa wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo hili linawakatisha tamaa wananchi na ndiyo maana nimesema ile Sheria ya Ushirika inabidi tuitazame upya, kwa sababu wenzetu wanaopata mamlaka kwenye vyama vya msingi na vyama vikuu wamegeuka kuwa miungu watu na kuona kwamba wao wana uhuru uliopitiliza kana kwamba wanaishi kwenye himaya tofauti na Watanzania wengine. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ombi langu kwa Ofisi ya Waziri Mkuu ni kwamba hebu iingilie kati kuona jinsi gani wananchi hawa wanavyoweza kupata haki zao, kwa sababu kwa kweli ni jambo ambalo wananchi hawalielewi, kwa sababu hakuna korosho zilizopo kwenye maghala lakini fedha zao hazionekani zipo wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende kwenye suala la tozo kama alivyozungumzia Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba Serikali mwaka huu imepania kuhakikisha kwamba inaondoa baadhi ya tozo kwenye mazao mbalimbali ya biashara yakiwemo tumbaku, chai, kahawa pamoja na korosho. Bahati nzuri mimi ni miongoni mwa wanaotoka kwenye maeneo yanayolima zao la korosho; Masasi ni Wilaya ya pili kwa uzalishaji ukiachia Tandahimba. Kwa kweli tunampongeza sana Rais pamoja na Waziri Mkuu kwa jinsi ambavyo wameshiriki katika kufanya zao la korosho kwa mwaka huu liweze kufikia kilo moja sh.3,800/=. Naamini kabisa Serikali ikiendelea kukaza uzi korosho zinaweza kuwa na uwezo wa kuuzwa sh. 5,000/= kwa kilo katika misimu ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sana katika tozo zile ambazo Mheshimiwa Waziri Mkuu amezisema, lakini napenda kwa mfano tozo ya magunia ambayo kwa kweli inatozwa kwa wakulima, nadhani iondolewe pamoja na zile nyingine ili kumfanya mkulima aweze kupata unafuu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningetaka niliseme, ni juu ya masuala ya umeme. Bahati nzuri ameelezea Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba yake kwamba Serikali ina nia nzuri ya kusambaza umeme, lakini napenda sana ieleweke kwamba wananchi wa Mikoa ya Mtwara na Lindi kwa sababu ambazo hata Mawaziri wanazijua kwamba maeneo haya yaliachwa kupewa huduma za umeme tangu mwanzo kwa sababu kulikuwa na tetesi kwamba Mkoa huu wa Mtwara na Lindi ulikuwa uhudumiwe na kampuni ambayo ilianza pale kusambaza gesi. Kwa hiyo, baadaye Serikali iliamua kusitisha makubliano yale na *TANESCO* kuendelea kuhudumia mikoa hii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tatizo ambalo lipo ni kwamba maeneo, vituo au Wilaya za Mkoa wa Mtwara na Lindi hazina magari. Hata magari yaliyoletwa hivi karibuni, hayakusambazwa tena katika mikoa hii vizuri na kufanya utendaji wa kazi katika Mkoa wa Mtwara na Lindi hasa Wilaya ya Masasi kuwa mgumu sana kiutendaji kwa sababu hawana usafiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba sana Serikali ione kwamba eneo hili linahitajika kutazamwa vizuri zaidi. Naipongeza suala la *REA* Awamu ya Tatu, kwamba linazinduliwa katika mikoa, lakini nataka tu nitoe angalizo kwa Serikali kwamba kama Mkoa wa Mtwara na Lindi haukutazamwa vizuri, unaweza ukajikuta maeneo mengine yote nchini yamemaliza vijiji vyake, lakini Mtwara na Lindi vikabaki kwa sababu kule hatukuwahi kupata ile *phase one* na wala zile fedha za *MCC* kwa ajili ya umeme hazikupatikana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukienda kwa uwiano ulio sawa, basi mikoa hii bado itabaki nyuma. Kwa hiyo, naomba sana hata katika usambazaji umeme, katika maeneo ambayo umeme ulipita muda mrefu, utakuta maeneo ya Mkoa wa Mtwara na Lindi bado maeneo mengi sana umeme umepita lakini wananchi hawajanufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la reli. Naomba sana hii reli ya kutoka Mtwara kwenda Mchuchuma na kama Mheshimiwa Nape alivyokuwa analalamika kwamba maeneo mengi yamewekwa 'x' lakini hatuoni zile juhudi za hasa za kuhakikisha kwamba kweli reli hii inataka ijengwe hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Jerome Bwanausi. Mheshimiwa Edward Mwalongo, tafadhali.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Nami nachukua fursa hii kwanza kabisa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake na Mawaziri wote waandamizi wenye Wizara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli napenda nianze kabisa na suala la kilimo. Sisi kule Jimbo la Njombe Mjini ni wakulima na hatuna shughuli nyingine zaidi ya kilimo. Katika suala la kilimo nianze kabisa kwanza kwa kuipongeza Serikali na Waziri Mkuu mwenyewe binafsi, kwa kazi kubwa iliyofanyika kudhibiti lumbesa. Leo hii wananchi wa Njombe wanafurahia kilimo chao cha viazi kwa sababu lumbesa imedhibitiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kiazi ni zao la msimu, naomba sana mikoa yote inayopokea viazi kutoka kwa wakulima wa viazi wa Mikoa ya Iringa, Njombe na Mbeya iendelee kudhibiti lumbesa katika masoko yao hasa hasa Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Ruvuma, Mtwara na kadhalika, ili tuweze kusaidia wakulima ambao wanalima zao hili la viazi. Leo hii wanafurahia bei ni nzuri na lumbesa imedhibitiwa naipongeza sana Serikali kwa jitihada hizo.

Mheshimiwa Spika, kilimo ndicho kinachoajiri Watanzania walio wengi. Naiomba Serikali, tunayo kazi

kubwa sana ya kufikiria namna gani tunaweza tukasaidia vijana wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuishauri Serikali sasa ianzishe makambi maalum ya kilimo kama mashamba darasa makubwa ambayo yataweza kusaidia kuwaweka vijana mahali ambapo pana miundombinu sahihi ya kilimo; kuna maji, makambi ya kuishi, mashine za kilimo ili vijijini vijana waende pale wafundishwe kilimo bora, walime wapate mitaji, halafu baada ya muda watakuwa wamefikia umri wa kuweza kujiendeleza. Warudi sehemu nyingine wakaendelee na shughuli za kilimo. Kuliko leo kuwahamasisha vijana waende wakalime. Vijana hawa kwenda kulima kwa jembe la mkono kwa maendeleo haya tuliyofikia, hawawezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaanzisha Vyuo vya *VETA* na katika bajeti iliyopita nilisema, vyuo hivi tunavyoanzisha maana yake nini? Tunahamisha vijana kutoka vijijini kupeleka mijini. Tukianzisha makambi maalum ya kilimo kwa vijana na tukawawekea miundombinu sahihi, tutawawezesha vijana hawa kubaki vijijini na kujishughulisha na kilimo katika mazingira yaliyoboreshwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naishauri Serikali sasa iangalie tunapojenga Vyuo vya *VETA* na tujenge makambi maalum ya kilimo yenye mashamba makubwa ili kusudi vijana waweze kufanya hizo kazi katika mazingira yaliyoboreshwa. Huo ndiyo ushauri ninaoweza kuutoa kwa Serikali juu ya suala la kilimo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine kwenye kilimo linalosumbua ni mbolea. Mbolea ni muhimu sana katika kilimo, lakini iko mbolea ya ruzuku. Naiomba sana Serikali iongeze kiwango cha ruzuku kwenye mbolea hii. Mbolea hii ina matatizo makubwa mawili; kwanza kiwango ni kidogo sana, lakini pili inafika kwa kuchelewa.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Njombe Mjini mbolea inafika mwezi wa kwanza. Sisi Njombe tunapanda

mwezi wa Kumi na Mbili mwanzoni. Sasa unapotuletea mbolea kupandia mwezi wa kwanza, maana yake sasa unasababisha hii mbolea iende katika mikono isiyo salama.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba sana Serikali iangalie, wataalam nafikiri wapo; ni nini kinachowashinda kujua kwamba mkoa fulani msimu wa kilimo ni huu; mkoa fulani msimu wa kilimo ni huu; matokeo yake wanakulazimisha ununue mbegu mwezi wa kwanza. Utapeleka wapi mbegu mwezi wa kwanza wakati wewe umeshapanda mwezi wa Kumi na Moja mwishoni? Kwa hiyo, naiomba sana Serikali iangalie itoe ruzuku ya kutosha na ihakikishe kwamba inaleta ruzuku hii katika muda ambao ndiyo muda wa kilimo kweli.

Mheshimiwa Spika, kingine ni suala la udhibiti wa mbegu. Mbegu za mazao zinahitajika kudhibitiwa. Pale Njombe kuna taasisi ya udhibiti wa mbegu, ina wataalam saba, ina gari moja inadhibiti mbegu kanda nzima; na hiyo kanda ni Mkoa wa Ruvuma, Njombe, Iringa, Mbeya, Rukwa; mikoa sita, gari moja; wataalam sita wanadhibiti mbegu. Ni jambo ambalo haliwezekani.

Mheshimiwa Spika, naiomba sana Serikali iangalie utaratibu mzuri wa kuhakikisha kwamba Kitengo hiki cha Udhibiti wa Mbegu na Ubora wa Mbegu kinapewa huduma inayotosha ili kusudi kiweza kutoa huduma.

Mheshimiwa Spika, vilevile hata sheria yake naomba iangaliwe, kwa sababu sheria ukikutwa na mbegu ambayo siyo mbegu halali, siyo mbegu safi, mbegu *fake*, faini yake ni ndogo sana. Kwa hiyo, mtu yuko tayari kuzalisha mbegu *fake* na kuuzia wakulima, kwa sababu anajua kwamba nikipigwa faini, itakuwa Shilingi bilioni 50 nami nimeshauza mbegu zaidi ya mabilioni ya pesa. Kwa hiyo, kwangu siyo tatizo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba sana Serikali iangalie Sheria ya Udhibiti wa Mbegu na ikiwezeshe kitengo hiki pale Njombe. Hawana hata maabara, wala *store* ya

kutunzia mbegu. Wametunza tu mbegu hovyo hovyo. Mbegu ikileta tatizo kwa mkulima ukirudi taasisi ya mbegu, ukichukua ile sampuli ya mbegu ambayo ililetwa na mzalishaji wa mbegu, ilishaliwa na panya. Kwa hiyo, hilo ni tatizo kubwa sana. Naiomba sana Serikali ikiangalie kwa jicho la pekee kile Kitengo cha Udhibiti wa Mbegu pale Njombe.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala lingine linalohusiana na mambo ya maliasili na hasa Kitengo hiki cha *TFS*. Sisi Njombe ni wazalishaji wakubwa sana wa mbao, miti, mijengo na makaa ya kupikia majumbani na kadhalika. Kitengo hiki hakijawa makini. Moja ya umakini ambao nauona unaleta tatizo kwa kitengo hiki ni kwamba, kinaeleza Sheria ile ya Udhibiti wa Misitu na hasa suala la mkaa, kama vile nchi nzima tunafanana katika mazingira yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi Njombe tuna mazao ya misitu ya kupanda; tunalo zao la mti mmoja unaoitwa uoto au mlingo au muwati. Miti hii inapandwa kwa muda wa miaka mitatu mpaka minne inavunwa. Mazao yanayotoka hapo kwenye huo mti ni maganda ambayo yanachukuliwa yanapelekwa viwandani kwa ajili ya ku-*process* mambo mengine huko viwandani. Vilevile matokeo mengine ni kuni, pia unaweza ukatengeneza mkaa. Sasa taasisi hii inasema kwamba mkaa sasa ni marufuku kuvuka Wilaya. Sisi Njombe milingo ni zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilidhani kwamba Tanzania *Forest Service* wanatakiwa waje Njombe walete nguvu za kutosha, wananchi wa Njombe wapande milingo mingi zaidi ili tufidie uzalishaji wa mkaa katika eneo lingine la nchi kusudi wananchi wengine waweze kupata mkaa. Huwezi kuzuia mkaa halafu hujaweka mbadala wa mkaa. Wananchi hawa watapikia nini; hasa wananchi kama wa miji mikubwa? Njombe kuna fursa ya kuzalisha hii miti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niombe *TFS* waje Njombe tushirikiane tuzalishe miti mingi, tuzalishe mkaa, wananchi katika nchi hii waendelee kutumia mkaa wakati tukiendelea kutafuta nguvu nyingine ya matumizi ya kupikia na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, vilevile wanaleta marufuku nyingine ambazo zinaleta kero kweli kwa wananchi. Wanasema ni marufuku kupakia mazao ya misitu kwenye pikipiki. Hivi hawa watu wa *TFS* wanaelewa maana ya mazao ya msitu? Maana yake kuna korosho humo ndani, ni marufuku kupakia korosho kwenye pikipiki. Kuna kuni, ni marufuku kupakia kuni kwenye pikipiki; kuna mkaa. Sisi hatuharibu sana mazingira kwa maana ya kwamba tunatumia miti ya asili.

Kwa hiyo, wanapotoa hizi sheria au maelekezo naomba sana Serikali iangalie hii taasisi iweze kutoa maelekezo ambayo hayasababishi kero kwa wananchi. Unapotoa maelekezo kama haya kwamba ni marufuku kupakia mkaa au kuni kwenye pikipiki matokeo yake ni kwamba anapokuja Afisa mwingine wa Serikali, yeye anasema hii ni sheria, huruhusiwi kupakia mkaa kwenye pikipiki.

Kwa hiyo, wananchi wananyanyasika kwa sababu tu hawa *TFS* wanatoa maelekezo ya jumla kwa nchi nzima. Mimi kama mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Njombe Mjini, siwezi kukubaliana kabisa na hili jambo, naiomba kabisa Serikali iweze kuwapa maelekezo ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, kingine, kuna kitu kinaitwa *TP (Transit Pass).* Naomba sana Serikali itusaidie sisi watu wa Njombe. Sisi ndio tunaozalisha mbao, miti, mijengo na kadhalika. Tukisafirisha mabanzi tu ndani ya Halmashauri ya Njombe, tunatozwa kitu kinaitwa *Transit Pass.* Sasa manufaa ya sisi kuwa na misitu ni nini? Tunapanda ile miti kwa jasho letu, tunazalisha miti kwa ajili ya wananchi wote, mbao na kadhalika; tukikutwa tu tumepakia kuni kwenye gari, *pickup* tani moja; *Tanzania Forest Service* wanataka tuwe na *TP.* Naomba Serikali iangalie tuweze kuondolewa *TP* wananchi wa Njombe ili kusudi tuendelee kuzalisha zaidi misitu, kwa sababu misitu tunayozalisha pale ndiyo inawasaidia wananchi wote.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja ya Waziri Mkuu, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Edward Mwalongo. Sasa tunahamia upande huu mwingine Mheshimiwa Godbless Lema atafuatiwa na Mheshimiwa Masood Abdallah Salum.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Ili kuepuka miongozo mingi naomba nianze na neno la Mungu kutoka kitabu cha Ufunuo mstari wa nane, inasema "bali waoga, na wasioamini na wachukizao na wauaji na wazinzi na wachawi na hao waabuduo sanamu na waongo wote sehemu yao ni katika lile ziwa liwakalo moto wa kiberiti." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watu waoga, Biblia imewafananisha na wazinzi; watu waoga biblia imewafananisha na wanaoabudu sanamu; watu waoga Biblia imewafananisha na waongo na biblia ikasema hawa hukumu yao ni ziwa la moto.

Mheshimiwa Spika, nilipokuwa Magereza nimekuombea sana, Mungu ni shahidi. Ili Bunge hili liweze kutenda haki, wale watu waliotajwa hapa kama wapo, wakatae kufanishwa na wazinzi na waabuduo sanamu.

Mheshimiwa Spika, nchi hii inapokwenda, kama leo Bungeni pasipokuwepo na uhuru wa majadiliano wananchi wataongelea wapi? Tukiongea nje, tunakaa ndani, tunanyimwa dhamana, tunapelekwa Magareza kwa miezi minne. Tukiongea Bungeni haturuhusiwi. Leo haturuhusiwi kuisema Ofisi ya Rais, mnafikiri mnamsaidia Rais! Ipo siku atatafuta watu makini. Huko mlikuwa wengi sana, wengine sasa hivi wako huku. Atatoka mmoja mmoja na wote mtakuja huku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namna ya kuisaidia nchi ni watu kutokuwa waoga. Ni watu kusema ukweli! Leo Taifa linayumba! Hakuna mtu ambaye hakuona Siku ya Sheria

Duniani, lakini hapa kila mtu anatetea chakula, anatetea mshahara kuliko utu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watoto na wajukuu wa Taifa hili wanaangalia kizazi cha Bunge hili kinatunga Sheria za aina gani? Maombi yangu ni kila Mbunge angalau apite jela kwa miezi minne ili mjue ninachokisema. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa!

**SPIKA:** Mheshimiwa Lema, upokee Taarifa.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nataka nimtaarifu Mheshimiwa Lema kwamba imeandikwa katika Biblia: "wanyenyekevu, watii, wapole, ndio watakaouona Ufalme wa Mungu. Bali wakorofi, wabishi, wajifanyao jasiri katika jeuri ya mioyo yao, hawatauona Ufalme wa Mungu." *(Makofi/Kicheko/Kelele)*

**SPIKA:** Jamani anayepewa taarifa ni Mheshimiwa Lema, hampewi ninyi. Sasa tumwachie Mheshimiwa Lema aliyepewa taarifa aipokee.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Spika, hakusema kitabu, lakini Biblia hiyo hiyo Mithali 16:12 inasema: "Wafalme wakitenda yasiyo haki, ni chukizo, maana kiti cha enzi huthibitika kwa haki." *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Waheshimiwa, mnageuza Bunge kuwa Kanisa sasa! Mtaacha watu waokoke hapa! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Lema, endelea!

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Spika, naomba nilindie sana muda wangu.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu gani? Waheshimiwa Wabunge tuisaidie nchi. Kuna siku mke wangu alikuwa anawaambia wanangu, nataka msome sana muwe kama profesa. Mtoto wangu mmoja akamwuliza, kama profesa nani? Mke wangu akasema ngoja ni-*google!*

Mheshimiwa Spika, tunataka Madaktari na Maprofesa walioko ndani ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi wawe mashuhuda wa kupigania haki ya Taifa hili. Leo msiporuhusu mijadala huru ambayo imeruhusiwa na Katiba hii kwa Wabunge, ndani ya Bunge, tunaenda kuongelea wapi mambo ya kulisaidia Taifa hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Hussein Mwinyi ni mtoto wa Mzee Mwinyi; baba yake leo ana faraja mtoto wake ni Waziri yuko Bungeni. Ben Saanane ni mtoto wa Mzee Focus; Ben Saanane amepotea, hajulikani alipo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imemtafuta Faru John kwa gharama zote; imemtafuta Faru John kwa nguvu zote; kuna mtoto anaitwa Ben Saanane, ana wazazi kama ambavyo Mzee Mwinyi ana mtoto anaitwa Hussein; kama ambavyo Mzee Maghembe ana mtoto wake, juzi tumemchagua kuwa Mbunge wa Bunge la Afrika Mashariki, akampa mkono akifurahi; leo kuna binadamu ana ndugu zake, ana wadogo zake anaitwa Ben Saanane; baba yake aliniambia maneno haya, "CHADEMA na Serikali nisaidieni kumtafuta mtoto wangu. Ben sio mbuzi wangu, Ben ni mtoto wangu." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imemtafuta Faru John. Leo nimeshangaa yaani wanyama wamekuwa na hadhi katika Taifa hili mpaka leo kuna mnyama anaitwa sijui Yusta na mnyama mwingine anaitwa Ndugai, wewe mwenyewe! Aisee! *I am wondering!* Yaani mpaka leo wanyama wanakuwa na thamani mpaka wanabatizwa majina ya binadamu na kuna mtu anapotea hapatikani.

Mheshimiwa Spika, Mawazo aliuawa, Geita. Mawazo ameuawa Geita, mahabusu wale wakalala barabarani wanasema Serikali ilete viongozi wakubwa tuwaambie watu

waliomuua Mawazo. Serikali haikuchukua hatua. Faru John ametafutwa kwa nguvu zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna maiti Ruvu, nilikuwa Magereza nasoma kwenye magazeti, saba; *DNA* yake haijapimwa, taarifa yake haijatolewa, lakini Faru John na Faru mwingine sijui Yusta sijui nani, ametafutwa kwa nguvu zote. Waheshimiwa Wabunge...

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, taarifa!

**SPIKA:** Taarifa upande gani? Endelea na Taarifa yako!

**TAARIFA**

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa kaka yangu Mheshimiwa Lema kuwa, suala la kupotea kwa Ben Saanane, kuna gazeti ambalo linamilikiwa na Mbunge wa CHADEMA liliwahi kuandika kuwa Ben Saanane amejificha kwa ajili ya mikakati ya kisiasa.

**SPIKA:** Taarifa hiyo, Mheshimiwa Lema.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Spika, naomba unilindie muda wangu sana. Nyie wenyewe mnamfahamu Mbunge wenu, kwa hiyo, mimi siwezi kuendelea naye sana. Nashukuru. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, haya mambo yanayoendelea mnakaa kimya; mnasikia mtu amepotea mnakaa kimya; mnasikia kuna damu imemwagika mnakaa kimya; mnafikiri hao sio watu; hii damu itanena. Hii damu itanena! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yaliyomkuta Mheshimiwa Nape juzi, yametukuta sisi siku za nyuma, yatamkuta kila mtu. Kama ambavyo wema ni mbegu, ubaya pia ni mbegu, kila mtu anavuna anachopanda. Wakati utafika, leo mko wengi, tulitarajia nyie ndio msaidie Taifa hili kwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo alikuwepo Mwalimu Mwakasege hapa, wakati tunasali tukawa tuko na Wabunge wa CCM wengi tu, nami nilikuwa karibu na Mheshimiwa Juliana Shonza. Nikafumbua macho kidogo nikaona Wabunge tunasali kwa pamoja. Nikasema hivi zile kura za hapana hawa hawakuwepo! Nikasema hawa kwenye kura za hapana hawakuwepo! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi hii isipoacha usiasa ndani ya Bunge, upande huu na upande huu, tusipoacha siasa za vyama ndani ya Bunge, Taifa hili tunalipasua! Leo inaonekana Vyombo vya Dola vina nguvu, leo inaonekana mna majeshi. Tumeongea habari ya Mahakama hapa mkasema tusiingilie Mahakama.

Mheshimiwa Spika, mimi nilishawahi kupewa mdhamana na ikasainiwa *remand order*. Nimekaa jela miezi minne, nina dhamana lakini sina masharti ya dhamana. Hakimu aliyefungwa mikono kuninyima masharti ya dhamana, alifunguliwa mikono kutoa masharti ya dhamana. Tunapokuja kuongea habari ya Mahakama, hamwezi kujua vizuri mpaka mwende jela.

Mheshimiwa Spika, nimetoka jela, kuna mtu yuko jela mwaka wa tatu kwa kesi ya bangi ambayo akienda aka-*plead guilty* Mahakama Kuu faini yake ni 18,500/=. Kuna Mwanasheria, Mheshimiwa Mwakyembe anamjua, amekaa jela anaanza mwaka wa saba, kesi yake ni *money laundering.* Miaka saba! Hiyo kesi akikutwa na hatia pengine ni miaka minne jela. Kuna watu wanaozea jela. Ofisi ya *DPP* inatumika vibaya, tumetunga kesi mbaya. Nenda Keko, zimejaa watu kesi za *money laundering. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna hasira inakusanyika kwenye mioyo ya watu. Hamuwaoni watu wanaandamana barabarani, watu wanaandamana ndani ya mioyo. Ipo siku watatoka barabarani bila sauti ya CHADEMA! Iko siku watatoka barabarani bila sauti ya *CUF!* Iko siku mtawakuta barabarani!

Mheshimiwa Spika, Taifa hili litapasuka vipande viwili! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huu uonevu mnaotufanyia, hatufanyi mikutano ya hadhara leo. Leo mkutano wa hadhara nchi hii tumekatazwa...

**SPIKA:** Mheshimiwa Lema, muda hauko upande wako. Muda, muda, umekwisha.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Spika, nina dakika zangu mbili, nilikuwa naangalia hapa. Dakika zangu mbili.

Mheshimiwa Spika, leo tumezuiwa kufanya mikutano ya hadhara. Tunaambiwa tufanye mikutano ya hadhara 2020. Ni sawa na kuliambia Kanisa lifanye Ibada *Christmass.* Ni sawa na kuuambia Msikiti ufanye Ibada Siku ya Idd! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nyie mnafikiri ni kwetu, wakishamaliza kutushughulikia sisi, meno yale yale, msumeno ule ule, utakuja upande wenu. Ngoja watumalize kwanza, utakuja upande wenu. Nawaambia, kila mbegu mnayopanda mtavuna na tuko kushuhudia haya na Mungu ni shahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Lema. Kabla sijamwita Mheshimiwa Masudi, nifafanue jambo moja tu. Hawa wanyama wanaoitwa faru... *(Kicheko)*

Ni vizuri nikasema maana wakati mwingine Taifa letu, wanaweza wasijue kwa nini kuna faru huko Ngorongoro anaitwa Faru Ndugai. Siyo kwa sababu ya zawadi nyingine yoyote ile; siyo kwa sababu ya Uspika; siyo kwa sababu ya Ubunge wa Kongwa; ni kwa sababu, katika maisha yangu ya ujana wangu niliyatumia kwa kiasi kikubwa katika hifadhi

za wanyama. Kwa hiyo, ukienda katika hifadhi kuu tatu za nchi hii, mimi nimekuwa mmoja wa Viongozi Wakuu wa hifadhi hizo. *(Makofi)*

Hifadhi ya Selous, ambayo ukubwa wake ni sawa sawa na Rwanda na Burundi kwa pamoja; nimekanyaga kwa mguu kilometa kwa kilometa mimi mwenyewe. Kwa magari, kwa nini, kwa kila kitu! Hifadhi ya Serengeti yenye kilometa za mraba 14,000 naifahamu kama mkono wangu huu; na nyingine zinazozunguka pale *Serengeti... system* yote, iwe Grumet, iwe Ikorongo, iwe Maswa.

Mheshimiwa Spika, ukija Ngorongoro yenyewe yenye kilometa za mraba 8,200 pale ndiyo penyewe! Kwa hiyo, katika *circles* hizo mchango wangu ni mkubwa sana. Kwa hiyo, zawadi peke yake niliyopewa ni ya faru mmojawapo anaitwa Ndugai, basi! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru nami kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyo mbele yetu. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu Subhanah-Wataallah aliyetujalia uzima na afya njema katika miezi hii mitukufu tunayoendanayo; na wale wanaofunga inshallah Mwenyezi Mungu awabariki na funga zao azikubali.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kuwapongeza wananchi wangu wa Jimbo la Mtambile kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya, lakini hasa pale ambapo Katibu Mkuu, kipenzi chetu, Maalim Seif Shariff Hamad ambaye alikuwa akipita katika ziara zake za kuongoza chama chetu. Hongera wananchi wa Jimbo la Mtambile, hongera Katibu Mkuu Mstahiki Maalim Seif Shariff Hamad, wewe ni kiboko ya viboko, tuendelee na kazi, hakuna Katibu Mkuu mwingine mpya. Ni wewe tuliyekuchagua katika Mkutano Mkuu mwaka 2014, hakuna Mkutano mwingine Mkuu uliofanyika. Chapa kazi Katibu Mkuu Maalim Seif Shariff Hamad, songa mbele, *aluta kontinua*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili. Naomba niendelee. Kwenye ukurasa wa 10 wa Kitabu cha Mheshimiwa Waziri Mkuu alikipongeza Chama cha Mapinduzi kwa kupata viti 19 vya Udiwani katika chaguzi zilizopita.

Mheshimiwa Spika, naomba nimkumbushe Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba Chama cha Mapinduzi kilipata pigo, kilishindwa vibaya katika uchaguzi wa marudio wa Lindi Mjini; mitaa yote saba Chama cha Wananchi – *CUF* kilishinda. Naomba, hawa ni jirani zako, CCM ilipata kipigo kitakatifu; CCM ilishindwa vibaya na wananchi walisema hiyo rasha rasha tu, 2020 ndiyo muziki hasa. Hawa jirani zako lazima ilikuwa uwakumbuke kwamba CCM ilipigwa vibaya Lindi Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwapongeze mitaa ambayo ilishinda katika Mitaa ya Mnubi, Migombani, Ndolo Juu, Mnazi Mmoja, Nachingwea, Tulieni na Runyu. Mitaa yote saba hii ilichukuliwa na Chama cha Wananachi – *CUF* kama taasisi. Hongera sana wananchi wa Lindi Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mambo ambayo tunakwenda nayo naomba niseme kwamba, Serikali kwa wakati huu haioneshi wazi kwamba ina dhamira ya kuleta maendeleo. Kwa sababu, hata pale ambapo bajeti imepangwa itekelezwe, basi imekuwa ni kizungumkuti.

Mheshimiwa Spika, ni aibu na fedheha iliyotosha kwamba hadi hivi sasa bajeti ya maendeleo ambayo imeletwa ni 34% tu, hii ni aibu. Tena na bajeti hiyo, kinachosikitisha ni kwamba ilikuwa ni bajeti ya shilingi trilioni 29, mara hii Serikali imeleta bajeti ya trilioni 31, miezi iliyobakia ni mitatu wanasema kwamba fedha zilizobakia eti wataweza kuzileta. Hiyo miujiza itatoka wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ikiwa miezi tisa Serikali haikuweza kukamilisha fedha za 100%, eti miezi hii iliyobakia mitatu watakamilisha bajeti ya 66%. Ni aibu na fedheha kwa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba, katika hili, jambo ambalo linatushangaza hata bajeti yako ya Bunge, bajeti ya maendeleo 2016/2017 ilikuwa ni bilioni saba, hadi leo ninavyojua, labda wameweka fedha jana au mchana huu, wametoa shilingi milioni 200 tu. Aibu na fedheha iliyotosha.

Mheshimiwa Spika, ni aibu kubwa kwamba Serikali haina dhamira iliyo wazi; ukiangalia Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali bajeti iliyopita alitengewa fedha za maendeleo shilingi bilioni 10, lakini amepata shilingi bilioni 2.4 tu. Tena asilimia 90 ya fedha hizi, ni fedha za wafadhili. Ni aibu kwa Serikali inayosema hapa kazi na mwendokasi. Kasi iko wapi? Kutakuwa na kasi kweli mwaka huu hapa! Hii ni fedheha na aibu kubwa kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, ni imani yangu kwamba wakati sisi Wabunge tunapitisha bajeti za maendeleo Serikali iwe makini kuangalia ni jinsi gani ambavyo fedha za maendeleo zitatolewa kwa wakati, vinginevyo ni aibu na fedheha kwamba tunapitisha bajeti za maendeleo, lakini Serikali inaendelea kutumia fedha za maendeleo kwa mambo ambayo Wabunge hatukupitisha. Ni jambo baya sana.

Mheshimiwa Spika, nini athari yake kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali? Ni kwamba hapewi fursa iliyo nzuri kuangalia miradi mbalimbali ili kuanika uozo na uovu ambao unaonekana kwenye Serikali. Huu ni mkakati maalum wa Serikali kwamba mnamdhibiti asifanye kazi zake vizuri kwa sababu mnajua kuwa kwenye Serikali kuna maovu yaliyo mengi. Hii ni aibu na fedheha kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaiomba Serikali ikubali ushauri kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali apewe fedha inayostahiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aibu nyingine na aibu iliyoje, katika miaka kadhaa iliyopita sisi vyama vya siasa tumekuwa tukilelewa na mtu anayejulikana kama Msajili wa Vyama vya Siasa. Leo Msajili wa Vyama Vya Siasa amethubutu na kutoa

ruzuku shilingi milioni 369 kwa akaunti isiyostahiki. Mbaya zaidi imekwenda mbali zaidi, huu ni ufisadi wa hali ya juu, fedha hizi kwenda katika benki isiyostahiki, *NMB,* baadaye fedha hizi kuhamishwa kupelekwa kwa mtu binafsi, fedha hizi zikatumika isivyo. Hii ni kama *Escrow*! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ni aibu kubwa na fedheha. Kama taasisi naiomba Serikali iangalie sasa fedha za Msajili wa Vyama vya Siasa zinatumikaje? Hii ni aibu na fedheha kwamba fedha unazipeleka katika akaunti isiyostahili, baadaye fedha zinachukuliwa zinapelekwa kwenye akaunti ya mtu binafsi; zinachukuliwa zinatumika visivyo na bado Serikali ipo inachekacheka tu! Tatizo nini kwa Serikali? Aibu kwa Serikali inayosema Hapa Kazi na Mwendokasi. Kama kasi ndiyo hii, aibu kubwa! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, aibu nyingine ambayo inakuja, Serikali inasema tuko katika mkakati wa uchumi wa viwanda, lakini siyo muda mrefu Kiongozi wetu Mheshimiwa Freeman Mbowe amesema hapa jinsi gani ambavyo fedha za viwanda zilivyotolewa asilimia ngapi ya fedha za Wizara ya Viwanda. Kama kweli tuna nia nzuri, inakuwaje hadi leo unaendelea kutoa 8% ya fedha za viwanda? Serikali ambayo inasema tunaelekea katika uchumi wa viwanda! Hiyo ni aibu nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee kwa kusema kwamba ndani ya uchumi wa viwanda tuna sababu gani ya msingi, baadhi ya viwanda vilivyopo, baadhi ya wafanyabiashara bado wanaagiza baadhi ya bidhaa kama ngano kutoka nje? Leo viwanda hapa vipo. Kuna kiwanda cha ngano cha Bakhresa, lakini 90% Bakhresa anaagiza kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, hapa Serikali kazi yake ni kuchukua mikasi kukata utepe, ati mnazindua viwanda. Kazi gani! Njombe ngano inastawi, Iringa ngano inastawi, maeneo mengine ngano inastawi, lakini 90% ya ngano ya Bakhresa inatoka nje. Sisi kazi yetu ni kutembea na mikasi tu, tunazindua viwanda. Si aibu hiyo! Aibu kubwa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo naliona, tunazungumza habari ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA); tumeshuhudia kwamba wakati wa ukame Serikali ina mpango wa kudhibiti na kuweka chakula kwenye ghala la chakula – *NFRA.*

Mheshimiwa Spika, ni kwa nini tunaona mifugo yetu inakufa kwa kukosa majani au nyasi wakati tungeweza kuweka mkakati wa udhibiti katika maeneo mbalimbali ili hawa ng'ombe wetu wapate nyasi za kutosha? Hivi jamani hata hilo linahitaji mshauri mwelekezi kutoka nje?

Mheshimiwa Spika, ukienda katika mapori mbalimbali wakati wa ukame, unaona jinsi gani ambavyo ng'ombe wamekufa, lakini kumbe tuna nyasi za kutosha katika mikoa mbalimbali. Hili ni jambo ambalo Serikali ni lazima mliangalie. Sasa huo mkakati wa kupunguza umaskini uko wapi kama wafugaji wameachwa ng'ombe wao wanakufa, lakini nyasi kumbe zipo?

Mheshimiwa Spika, nchi nyingine duniani wanafanya hivyo, wanavuna nyasi, wanavuna yale majani wanayaweka kwa wakati maalum na wakati ukifika ule wa ukame ng'ombe wanapatiwa majani na wanakula, hawafi. Binadamu Tanzania wana njaa, ng'ombe wana njaa; shida kweli! Hapa kazi kweli mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije kwa Walimu. Walimu mara nyingi wamekuwa na malalamiko yao na mara nyingi Walimu wamekuwa wakipuuzwa.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba Walimu madeni yao yanayostahili hawalipwi kwa wakati, ndio maana Walimu wanakuwa ni maskini. Walimu wana malalamiko mengi, lakini kwa sababu inaonekana labda watu hawaelewi maana ya Ualimu; Mheshimiwa Simbachawene herufi 'U' maana yake ni uvumilivu. Kwanza

ni usumbufu; "A" maana yake ni adha wanayopata walimu; 'L" ni lawama wanazopata walimu. Inda, mahangaiko, mwisho ni uvumilivu na umaskini...

*(Hapa kengele ilila kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Spika, naomba walimu wapewe stahiki zao zinazostahili. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Masoud nakushukuru sana, ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Amina Salehe Mollel na atafuatiwa na Mheshimiwa Balozi Diodorus Kamala na Mheshimiwa Julius Masele ajiandae. Mheshimiwa Mollel.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutukutanisha tena katika Bunge hili la bajeti.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa pole kwako wewe kwa kuondokewa na mwenzetu Mheshimiwa Dkt. Elly Macha lakini vile vile nitoe pole kwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni na Wabunge wote.

Mheshimiwa Spika, kwetu sisi kama Wawakilishi wa Watu Wenye Ulemavu ni pigo kubwa kwa sababu ni miongoni mwa mwenzetu ambaye tulikuwa tukitoa mchango mkubwa katika kuhakikisha kwamba haki za watu wenye ulemavu na kuhakikisha kwamba yale masuala ya watu wenye ulemavu basi yanazungumzwa hapa Bungeni.

Nawaomba tu Waheshimiwa Wabunge pamoja na viongozi na Mawaziri kuhakikisha kwamba tunamuenzi Dkt. Elly Macha kwa kuyatimiza yale aliyokuwa akiyapigania humu Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nichukue nafasi hii kwa kuipongeza Serikali pamoja na Mawaziri wote

kwa kazi kubwa wanayofanya kwa Serikali hii ya Awamu ya Tano. Pia natoa pongezi za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Rais kwa kutambua na kuthamini mchango wa Watu Wenye Ulemavu na kuchukua uamuzi wa kuwapa nafasi katika nyanja mbalimbali na hii inaonesha kwamba kuwa na ulemavu siyo kulemaa. Hongera sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nijikite tu kwa kutoa ushauri kwa Serikali na hasa nianze kwa suala zima la elimu. Napenda kuishauri Serikali kwamba kwa sababu Serikali imetoa elimu bure kwa elimu ya msingi mpaka sekondari; na hii imekuwa ni faraja kwa sababu miongoni mwa watu ambao walinyimwa elimu kutokana na mila na tamaduni za jamii za kiafrika na hasa sisi wenyewe.

Mfano mzuri tu, hata katika jamii ninayotoka. Kwa maana hiyo basi, mpango huu wa elimu bure, umesaidia sana kuhakikisha kwamba jamii inawapeleka watoto wenye ulemavu kupata elimu. Katika shule mbalimbali hivi sasa watoto wenye ulemavu wengi wanatambua na wanapata elimu. Kwa hiyo, naipongeza Serikali kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, naishauri pia Serikali kuhakikisha kwamba inatimiza wajibu wake kwa kupeleka fedha kwa wakati unaotakiwa ili kuepusha usumbufu na kuhakikisha kwamba hata ile mianya yote ambayo wamekuwa wakitumia baadhi ya watu wasio waadilifu wanaosababisha fedha hizi kupotea katika njia zisizoeleweka, basi Serikali iwabane na kuweza kuwafikisha katika vyombo vya sheria.

Mheshimiwa Spika, naungana na Serikali na naipongeza pia kwa kutambua haki ya msingi ya kikatiba kwa Watu Wenye Ulemavu kupata haki ya msingi ya kupata taarifa. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ameeleza dhahiri kwamba Serikali imevitaka vyombo vya habari vihakikishe kwamba vinaajiri Wakalimani ili wenzetu nao waweze kupata taarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali na naviomba tu vyombo vya habari kuhakikisha kwamba vinatimiza agizo hili la Serikali kuhakikisha kwamba linaajiri. Namwomba Waziri mwenye dhamana Mheshimiwa George Mwakyembe, ahakikishe kwamba vyombo vya habari vinatimiza wajibu kuajiri wakalimani ili basi viziwi nao waweze kupata taarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuishauri Serikali katika Mfuko wa Watu Wenye Ulemavu; katika bajeti ya mwaka 2016/2017 mfuko wa watu wenye ulemavu haukutengewa fedha.

Mheshimiwa Spika, kama mnavyofahamu, hii ni haki ambayo nchi imeridhia Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watu Wenye Ulemavu na nchi yetu imeridhia mkataba huo ambao baada ya kuridhia ni kuhakikisha zile haki za watu wenye ulemavu zinatimizwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mfuko huu katika bajeti iliyopita inayoishia katika Bunge hili haukuweza kutengewa fedha, kwa hiyo, naishauri tu Serikali kuhakikisha kwamba mwaka huu fedha hizo zinafanya kazi, kwa sababu mfuko huu utakapotengewa fedha ni kwamba Baraza la Watu wenye Ulemavu litaweza kufanya kazi na litakuwa ni msaada mkubwa katika kuishauri Serikali katika nyanja mbalimbali na hasa masuala mbalimbali yanayowahusu Watu Wenye Ulemavu.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu Serikali ya Awamu ya Tano ina nia ya dhati kabisa katika kuhakikisha kwamba inashughulika na masuala ya watu wenye ulemavu, kwa hiyo, nisisitize tu kwa kusema kwamba, hili ni jambo jema, lakini tuhakikishe kwamba linaendana na fedha ili basi Baraza hili liweze kufanya kazi na kushughulikia changamoto mbalimbali zinazowakabili watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa kuendelea kutoa huduma kwa watu wenye ulemavu na katika hotuba

ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imeelezea ni jinsi gani basi ambavyo inatambua na itaendelea kutoa huduma kwa watu wenye ulemavu. Pamoja na kauli hii, kumekuwa na changamoto mbalimbali ambazo zimekuwa zikiwakabili watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Serikali imekuwa na utaratibu mzuri tu kwa watoto wasioona, zipo shule maalum ambazo zimetengwa na shule hizo wamekuwa wakienda hawa watoto kupata elimu na wamekuwa wakilipiwa gharama mbalimbali na hasa nauli kwa sababu jamii haitambui mchango wa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikiwapa nauli na kuwapeleka katika shule zilizotengwa. Mfano Shule ya Uhuru Mchanganyiko, lakini kuna shule nyingine ipo Iringa.

Mheshimiwa Spika, tatizo lililopo hivi sasa wale watoto wanapokwenda na inapofika wakati wa likizo hawawezi kwenda nyumbani na matokeo yake wanabaki mwaka mzima huko huko. Kwa sababu wazazi wengi hawatambui hilo na tayari walikuwa wamezoeshwa hivyo, kwa hiyo, wale watoto wanakuwa hawana tena nafasi ya kurudi majumbani.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ije na majibu kwamba je, ni kweli wao ndio wametoa agizo hilo kwamba hakuna fedha kwa ajili ya watoto hawa au ni baadhi ya Walimu wa hizi shule ambao wamekuwa wakijichukulia madaraka wao wenyewe na kuamua maamuzi kwamba watoto hawa wasirudi nyumbani?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nitamwomba sana Mheshimiwa Waziri wakati wa kuhitimisha bajeti hii basi aweze kutoa hizo taarifa ili tuweze kujua ni jinsi gani tunaweza kuwasaidia watoto hawa ili na wao pia waweze kupata elimu; na kama mnavyofahamu elimu ndio ufunguo wa maisha.

Mheshimiwa Spika, unapomsaidia mtoto mwenye ulemavu akapata elimu, umemwokoa na mambo mengi. Mara nyingi nimekuwa nikitoa mfano kwamba sisi tusingesoma hizi nafasi hapa tusingeweza kupata. Kwa hiyo, ili tuweze kujikomboa sisi wenyewe elimu ndiyo msingi na elimu ndiyo silaha yetu ili tuweze kujisaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo, nisemee suala la Mahakama. Katika suala la Mahakama tuhakikishe tu kwamba zile kesi ambazo walikuwa wamehukumiwa wale watu au kesi ambazo zinaendelea katika Mahakama mbalimbali nipate tu takwimu ni wangapi wamehukumiwa? Wangapi ambao bado kesi zao zinaendelea? Vile vile tujue kama kumekuwa na taarifa nyingine za mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Amina Mollel kwa kutumia muda wako vizuri. Ahsante sana.

Mheshimiwa Balozi Dkt. Diodorus Kamala, atafuatiwa na Mheshimiwa Ahmed Mabkhut Shabiby na Mheshimiwa Stephen Masele ajiandae.

**MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia hii fursa ya kuwa mchangiaji katika hoja muhimu iliyo mbele yetu. Naomba niseme awali kabisa kwamba naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia ukurasa wa 26 kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu; huduma za kiuchumi; amebainisha kwamba Serikali iko kwenye mchakato wa kuanzisha mfumo unganishi; mfumo wa kuweka kumbukumbu za ardhi, mfumo funganishi wa kuhifadhi kumbukumbu za ardhi na tayari wameshaanza kujenga.

Mheshimiwa Spika, jambo hili ni zuri na nitaomba liharakishwe na liweze kukamilika kwa wakati kwa sababu litatusaidia sana katika kuondoa migogoro ya mara kwa mara ya ardhi ambayo kwa kiasi kikubwa ukiangalia inachangiwa na kutokuwa na utaratibu mzuri wa kuweka kumbukumbu za ardhi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nyote mnafahamu kuna mgogoro mkubwa kule Misenye uliochukua muda mrefu, lakini ukiuangalia ule mgogoro kwa nini umechukua muda mrefu, sababu kubwa ni kutokuwepo kwa mfumo wa kuweka kumbukumbu za ardhi; na hasa kutokuwa na kumbukumbu za kielektroniki. Nitaeleza hoja tano kwa nini nasema kutokuwa na mfumo huu kumechangia sana kuleta migogoro ambayo ingeweza kuepukika?

Mheshimiwa Spika, la kwanza, ramani inayotumiwa na *NARCO* kwa mfano, ramani inayotumiwa na *NARCO* na iliyotumika katika kugawa *blocks* kule Misenyi. Ramani hiyo kwanza inatumika kwa siri kubwa, lakini ramani yenyewe ukiwauliza *NARCO* wenyewe kwamba iko wapi hawawezi kukupa ramani ambayo inatumika; kila mtu anatumia ramani yake kulingana na anavyoona inafaa.

Mheshimiwa Spika, siku moja nilisikitika sana nilipoelezwa na mtaalam mmoja kwamba ramani waliyonayo iliyoanzisha *Misenyi Ranch,* mpaka ukishavuka Mto Kagera kwenda mpaka Uganda yote ni *Misenyi Ranch.* Sasa maana yake, mwenye ramani ile na anayetumia ramani ile anakuwa hatambui na anapuuza ukweli kwamba katika eneo hilo kuna Vijiji, Kata na watu wanaishi. Pia ukiangalia hata *blocks* zenyewe zilizotengwa katika Misenye *Ranch,* migogoro iliyopo kati ya *blocks* na vijiji inasahau ukweli kwamba vijiji vilikuwepo kabla *Ranch* haijaanzishwa. Kwa hiyo, hii imekuwa ikileta mgogoro.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nasema tukiwa na kumbukumbu za vijiji, maana vijiji vinapimwa, vinakuwa na

hati, ziwe kwenye mfumo mmoja ili mtu asitoe hati juu ya hati. Maana kwa kufanya hivyo, matokeo yake inakuwa ni kuleta vurugu.

Mheshimiwa Spika, pia ukiangalia ni kwamba mipaka ya *blocks* zile zilizotengwa inabadilishwa kila kukicha na tuliowapa hizi *blocks* wana mamlaka siku hizi wanabadilisha *blocks* kadiri wanavyoona inafaa. Akiamka asubuhi anaanza kutembea anaweka mipaka na leo kwa mfano nimeletewa taarifa zaidi ya kaya 3,000, sasa ni *displaced persons* ni watu ambao wapo ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini hawana sehemu ya kuishi, wameondolewa katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, sababu nyingine ambayo inatokana na kutokuwepo na mfumo wa kuweka kumbukumbu, sote tunafahamu kwamba vijiji katika Misenye *Ranch* vilikuwepo kabla ya *ranch* na mipaka inajulikana kwamba ni Mto Kyaka, Kuru na Kigoroga lakini historia hii imepotoshwa, hakuna anayejua historia hii na kumbukumbu hazipo.

Mheshimiwa Spika, tuna tatizo lingine kubwa ambalo sote tunalijua ni kati ya misitu. Kwa mfano kule Minziro ukiangalia migogoro inayojitokeza kule Kata ya Minziro ni mipaka kati ya Minziro kama Kata na Vijiji vilivyo ndani ya Kata ile na Msitu wa Minziro.

Mheshimiwa Spika, sasa nasema ndiyo maana nimefurahia sana huu utaratibu wa kuanzisha mfumo unganishi wa kuweka kumbukumbu za kieletroniki ukianzishwa na taarifa zinaonesha unaanza itatusaidia sana. Hilo ni jambo la kwanza, ndiyo maana nimesema naunga mkono hoja hii kwa sababu inakuja na utaratibu ambao unaweza kutusaidia.

Mheshimiwa Spika, pia migogoro mingi ya ardhi tuliyonayo; iliundwa tume hapa ya kusaidia kutafuta ufumbuzi

na Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati anaunda tume ile alitoa hadidu za rejea na akasema jambo moja kubwa kwamba tuwe na subira. Akatuomba viongozi tuwe na subira, tusubiri hiyo tume imalize kazi yake.

Mheshimiwa Spika, matarajio yangu tume hiyo ikimaliza kazi yake Wabunge watapewa fursa ya kupokea ripoti hiyo na kushirikishwa kama tulivyoahidiwa; lakini subira hii naona Mheshimiwa Waziri Mkuu iko kwa wanasiasa tu, lakini kwa viongozi wengine kule Kagera, wao hawana subira yoyote. Hawasubiri cha tume, wala nini, wanaendelea kila mtu anafanya anavyoona anataka.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa ninapozungumza imetolewa *ultimatum* ya miezi minne watu wote kuondoka na kwenda kule watakapoona inafaa; jambo ambalo mimi kama mwakilishi wao silikubali, kwa sababu limetolewa kabla hata Tume yenyewe iliyoundwa kufuatilia suala hili haijatoa taarifa yake.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri wakati wanasiasa tunaombwa kuwa na subira, basi hawa Waheshimiwa wengine nao niombe pia na wao wawe na subira. Subira ikiombwa kwa upande mmoja tu, hiyo siyo subira; sote ni viongozi lengo letu ni moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi waliniomba kule wakasema Mheshimiwa inaonekana sasa ng'ombe wanapendwa kuliko watu, nikawaambia hapana watu kwanza, ng'ombe baadaye. Wakaniomba wakasema Mheshimiwa sasa uturuhusu tushike fimbo tuweze kupambana; nikasema hapana, siwezi kuwaruhusu kwa sasa kwa sababu tuliombwa tuwe na subira. Kama ukifika wakati huo, basi mimi nitakuwa wa kwanza kuongoza mapambano hayo lakini kwa sasa tuwe na subira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Nakushukuru sana Mheshimiwa Balozi Diodorus Kamala. Mheshimiwa Ahmed Mabkhut Shabiby, atafuatiwa na Mheshimiwa Stephen Julius Masele.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake ambayo imegusa kila sekta na kila kona ya nchi yetu.

Vile vile namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na wasaidizi wake kwa kuwezesha vijana zaidi ya 1,000 kupata ajira katika Kiwanda cha Nguo cha Morogoro wakiwepo vijana wa Wilaya yangu. Nawashukuru kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo nitaanza na pombe ya viroba. Najua wengi watashangaa, watasema huyu jamaa Muislam; na najua wale watu wanaopenda kuweka maneno kwenye midomo ya watu wengine, wataweka maneno mengi. Siyo kwamba naunga mkono watu wanywe viroba, napinga na viroba visiwepo kwa sababu vinaathiri hali za watu na hata sasa hivi watu wananenepa baada ya viroba kuacha kuwepo mitaani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashauri kitu kimoja; kwa sababu katika bajeti ya mwaka 2016 wakati tunaweka kodi katika vinywaji na katika bajeti yetu na mapato yetu, hata viroba navyo tulivihesabu na vilikuwepo kihalali.

Mheshimiwa Spika, ni kweli pombe hii inadhuru watu, lakini naomba au nashauri kwa wakati mwingine utaratibu utakaotumika kuzuia vitu kama hivi, basi uchukuliwe kwa umakini sana. Waanze kuzuia kwenye *production* ili huku zinakouzwa, basi ziishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ni mfanyabiashara sikuingia hapa kama nachunga ng'ombe wala kama mkulima au nani, nimeingia kama mfanyabiashara.

**MBUNGE FULANI:** Hata ng'ombe ni biashara.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni lazima nizungumze habari ya biashara na kama sisi Wabunge wa vyama vyote hapa tusipozungumza wenyewe basi tujue biashara kwenye nchi hii itakufa. Kwa sababu mtu amenunua mali ya shilingi bilioni moja, shilingi milioni 300 halafu amenunua kisheria, ana risiti zote za *TRA* na amelipa kodi leo unakuja unamwambia kuanzia sasa hivi hii mali ni haramu. Tayari ameshaingia kwenye matatizo amekopa katika mabenki huko na biashara yake imeshafungwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba mnielewe vizuri, siungi mkono unywaji wa viroba lakini utaratibu uliotumika naomba usirudiwe tena. Kwa sababu leo anaweza akaja mtu hapa akasema tena kitu kingine kikaleta madhara. Kwa hiyo, tuangalie utaratibu mzuri wa kufanya mambo haya. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, wewe mwenyewe Spika ni shahidi kwa sababu kati ya watu wanaoathirika na jambo hili ni mimi na wewe. Wakulima wetu ambao wanalima katika upande wa Wilaya ya Kiteto wamekuwa wananyanyaswa kupita kiasi hasa na vyombo vya dola ambavyo viko pale wilayani na mkoani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Mbuga ya Murtangos wanasema ile ni hifadhi. Hawawazuii watu kulima wakati wanakwenda kulima, wanangoja mahindi yameshafika labda mwezi mmoja, wanakuja ng'ombe wanachungia mule wakienda wale wakulima kushtaki na wao wanawekwa ndani. Mpaka sasa hivi ninavyozungumza wapo watu wa Pandambili ambayo ni wilaya yako na wapo watu wa Gairo wapo ndani mpaka sasa hivi na wale Wamasai ambao

wanachungia kwenye ile mbuga wapo nje, hao jamii ya kifugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama mnataka kuzuia, hatukatai kuzuia, kwa nini msizuie wakati wanalima mnakuja kuzuia wakati mahindi yameshakuwa makubwa? Kama hiyo ni hifadhi, hifadhi gani ambayo ng'ombe wanachungwa lakini wakulima hawaruhusiwi, hiyo ni hifadhi ya aina gani? Naomba viongozi wetu na Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu ambaye ni mtiifu na msikivu akienda pale asisikilize masuala ya wilayani wala mkoani, aangalie tu yeye mwenyewe atume watu wake wachunguze atapata jibu ambalo lipo sahihi. Akitaka na majina nitampa ya wakulima wetu ambapo zaidi ya heka 3,000 watu wamechungia na wako nje halafu tunasema zaidi ya asilimia 80 ya wananchi ni wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hizi pesa, watu wanasema tu, pesa zimepotea, hamko kwenye mzunguko wa kibiashara, ukiujua vizuri mzunguko wa kibiashara pesa imepotea kwa sababu wakulima wa mwaka jana hawajapata mazao. Hawa wakulima wadogowadogo wangeweza kuvuna mwaka jana kila mtu hapa angefanya biashara na mzunguko wa pesa ungekuwa mkubwa. Tunasema tu aah Magufuli kazuia pesa, Magufuli kafanya nini, Serikali imezuia pesa, wakulima hawakuvuna mwaka jana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ni mfanyabiashara sasa hivi nina zaidi ya miaka 25, najua mwaka wowote mkulima mdogo anayelima heka mbili au tatu akipata mazao atakwenda kwa fundi cherehani atanunua sare, atakwenda kwa huyu atanunua maji, atakwenda kwa huyu atanunua hiki, ndiyo mzunguko. Yule naye biashara yake ikitoka atapanda basi, ataenda Dar es Salaam, kwa hiyo kila mtu atafanya biashara. Wakulima hawa wasipopata pesa ina maana mzunguko haupo, kila kitu kitakuwa kibaya tu, tutalalamika tu. Hata ukiachiwa hizo pesa za benki, unasema mkopo hakuna, hata ukiachiwa, *security* zenyewe unazo? Maana yake mabenki siyo rafiki wa mtu maskini, huo ndio ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna jambo lingine la matrekta. Tunashukuru matrekta 1,860 yale ya SUMA JKT yamekuja na waliwakopesha wananchi kwa kulipa asilimia 30. Hata kwangu Gairo pale nimepata matatizo makubwa sana maana niliambiwa Mbunge weka dhamana, nimeweka dhamana nyingine badala ya kuandika jina la niliyemkopea limeandikwa jina Ahmed Shabiby ndiyo kakopa. Sawa watu wangu nawajua najua tu yatalipwa lakini wakati SUMA JKT anapewa auze matrekta hajui hata sheria za kuuza, kwanza na yeye mwenyewe akatafuta tena dalali mwingine ndio amuuzie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halafu baada ya hapo haya matrekta hata ukilipa hupewi kadi wala halina namba, kwa hiyo, linatembea tu kama mkokoteni wa ng'ombe. Tafuteni watu wote wenye matrekta haya, waliopewa kadi hawazidi 300. Mkulima akiomba kadi anaambiwa hebu soma *engine number,* wewe angalia namba yoyote bandika, sasa anabandika namba ipi, atakataje *insurance?* Kwa hiyo, matrekta yale hayana namba sasa sijui ni utaratibu gani. Halafu leo tena mnakwenda mnakamata, mnafanya kuangalia rangi, lile la bluu wanakimbiza wanakamata yamejaa pale, hii ni dhuluma? Mkulima anataka umpe kadi yake akumalizie deni humpi, kwa sababu ameshaambiwa na wenzake waliomaliza madeni kwamba hatupati kadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa matrekta yote ya Manyara, Tabora na Tanzania nzima kwa ujumla yamekamatwa halafu watu tunasifia tunasema hawa wameshindwa kulipa madeni, wameshindwa nini, jamani tusiwaangushe hawa wakulima wetu tuwaombee tena yaje matrekta mengine wakope, tuangalie kosa liko wapi. Naomba Waziri anayehusika aende akachunguze kama SUMA JKT wanazo *registration cards* za haya matrekta. Hakuna namba, hata *insurance* atakataje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni maji. Leo maji nimeamua kuzungumzia chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Toka mwaka 2007, Gairo imepewa Sh.6,600,000,000, lakini

kilichofanyika wamekwenda kuchimba visima vile vya maji tisa vinatoa maji lakini yale maji hata akinywa ndege anatapika.

**MBUNGE FULANI:** Duh!

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Haijawahi kutokea. Wamekwenda kupima kwa Mkemia hayafai. Nimewapa ushauri wa kila aina hawajafuata ule ushauri, sasa miaka 10 na mimi Mbunge nakwenda hiki kipindi cha tatu, kwa hiyo, hata wale wananchi wangu kwa sababu wengine hawana uelewa wanasema Mbunge amekula pesa alipewa yeye hela za mradi kafanyia biashara zake sasa maji hakuna.

**MBUNGE FULANI:** Kanunua mabasi.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Nimewaambia basi huu mradi kama mmefeli hizi pesa zilizobakia kuna chanzo cha maji kiko pale karibu tu, kilometa kama 25, nunueni basi mabomba tupate maji ya mserereko lakini imekuwa hadithi. Ukiongea hapa unajibiwa hiki lakini hakuna linalofanyika. Tunakwenda kwenye uchaguzi hiyo miaka ijayo, pesa zipo lakini hazitumiki, ndiyo maana leo nimeamua kumwachia Mheshimiwa Waziri Mkuu alifuatilie suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu niende naye Gairo, hapa na Gairo saa moja tu, aende akashuhudie matenki yamejengwa, mitandao ya matenki ipo lakini kuvuta tu maji kupeleka pale sasa hivi mwaka wa kumi hakuna kinachofanyika...

**MBUNGE FULANI:** Na pesa ipo.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Ndiyo na pesa ipo. Kila siku ukiwaambia kaleteni maji ya mserereko hakuna kinachofanyika. Wamekuja watu ambao wameletwa na Wizara ya Maji wamechora ramani wamefanya kila kitu lakini bado hatupati maji. Kila nikiongea na Mheshimiwa Waziri anasema subiri kidogo safari hii tayari wewe maji umepata,

sasa maji nimepata yako wapi, haya maji nitasema mpaka lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama unavyojua Jimbo la Gairo watu wanalima sana, wanapata sana mazao lakini tatizo maji yake chini ya ardhi yako mbali na hasa pale Gairo Mjini huwezi kupata maji matamu hata ufanye nini, utapata tu haya maji ya chumvi. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu safari hii angalau aje Gairo pale kwa sababu yeye kidogo wakimwona na akifahamu maendeleo ya pale ya miaka kumi na asilimia iliyofikiwa mpaka sasa hivi kwa kuona kwa macho itasaidia. Ndiyo maana leo hili suala la maji nimeona naweza nikakosa nafasi kwenye Wizara ya Maji nimuachie Waziri Mkuu ili siku nyingine mwakani kama hakuna maji mimi nitachangia tena Wizara hii hii nimuulize Waziri Mkuu imekuwa vipi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ahmed Mabkhut Shabiby. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Stephen Masele atafuatiwa na Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala. Mheshimiwa Mbunge wa Shinyanga Mjini, karibu.

**MHE. STEPHEN J. MASELE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi pia ya kuchangia bajeti hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, nami nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake ambayo inatoa dira ya mipango ya maendeleo ya Serikali. Nitumie nafasi hii pia kuwapongeza Mawaziri, Mheshimiwa Jenista Mhagama, kwa kazi nzuri na anaonesha kweli akinamama wanaweza. Nimpongeze pia Naibu Waziri kijana, Mheshimiwa Anthony Mavunde kwanza kwa kazi kubwa ambayo anaifanya ya kuwaunganisha vijana wa Tanzania lakini pia kwa programu ile ya mafunzo ya vijana ambayo anaifanya. Nimwombe tu programu hiyo pia ifike Shinyanga kwa sababu kuna vijana wengi wanahitaji programu kama hiyo na kusema kweli kama vijana wenzako hujatuangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee sana kwa niaba ya wananchi wa Shinyanga nataka nimshukuru sana Mheshimiwa Rais. Alipofanya ziara Shinyanga alitoa maelekezo kwa Mamlaka na Wizara ya Maji kushughulikia tatizo la bei ya maji Shinyanga. Kama Mheshimiwa Shabiby alivyosema, leo nazungumzia kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu kwa sababu bado hatujaona jitihada za Waziri wa Maji kushughulikia tatizo la uendeshaji wa Mamlaka ya Maji Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, maji ni huduma ya msingi, maji sio anasa. Shinyanga na mikoa ya Kanda ya Ziwa ni mikoa michache ambayo ina chanzo cha maji cha uhakika cha Ziwa Victoria. Serikali imetumia shilingi bilioni 250 kujenga Mradi wa Maji wa Ihelele, kodi za Watanzania, leo Wizara haiweki msisitizo wa kutunza mitambo ile. Shilingi bilioni 250 hazijamaliza hata miaka 10, Serikali haipeleki pesa za kutunza mitambo ile. Ni asilimia 25 tu ya mitambo ile ndiyo inafanya kazi, asilimia 75 haifanyi kazi. Ipo mikoa mingine kama Arusha wanahangaika vyanzo vya maji, Gairo huku amezungumza Mheshimiwa Shabiby wanahangaika na vyanzo vya maji, lakini sisi tuna chanzo cha maji cha uhakika lakini hatukitunzi, tumeweka shilingi bilioni 250 hatutunzi.

Mheshimiwa Spika, wiki iliyopita Shinyanga, Kahama, Ngudu, Igunga ambayo yote yapo kwenye Mradi huu wa Ihelele yanatakiwa yapelekewe maji lakini hayajapelekwa. Mradi ule umekatiwa umeme, siku nne wakazi wa Shinyanga hawana maji kwa sababu Serikali haijapeleka mchango wake wa asilimia 60 wa kuendesha mradi ule. Sasa wananchi wanapata adhabu ambapo wamelipia bili zao za maji wanastahili wapate huduma wanaikosa huduma kwa uzembe wa watu wengine, hii inasikitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mradi ule hauwezi kuharibika kwa uzembe wa watu wachache. Nimwombe Waziri, namheshimu, ni rafiki yangu, akae na Wabunge wa Kanda ya Ziwa ambao wanahusika na ule mradi wa maji tushauri namna bora ya uendeshaji wa mradi ule. Mradi ule ukiweza kuwafikia watumiaji wengi, kwa mfano wa Ngudu, Kwimba,

Igunga, Nzega, Tabora, Sikonge na kwa *capacity* ya mradi ule unaweza kuleta maji mpaka Mkoa wa Dodoma. Pampu zile nane zikifunguliwa zote Dodoma inaweza kupata maji ya Ziwa Victoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, andiko la mradi ule linaweza kuhudumia watu milioni 10. Leo ni wakazi wa Manispaa ya Shinyanga ambao hawafiki 200,000 na wakazi wa Mji Mdogo wa Kahama ambao hawafiki 200,000 ndiyo wanahudumia gharama za uendeshaji za mradi wa shilingi bilioni 250. Naomba Serikali iangalie kwa upana mradi huu. Naomba pia Serikali iongeze bidii za kusambaza haya maji kwenye vijiji vile vinavyohusika, zile kilometa tano vijiji vile vipate maji.

Mheshimiwa Spika, lakini yapo mambo ambayo tunaweza kumshauri Waziri, kwa mfano, mamlaka hizo zote mfano *SHUWASA* na mamlaka nyingine, kwenye vifaa vya mabomba kwa mfano vya kuunganisha maji, vimewekewa kodi, kuna *SDL* iko pale, kuna *VAT* iko pale. Vitu kama hivi vikiondolewa kwa sababu maji ni huduma, gharama za uendeshaji wa mamlaka hizi zitakuwa chini na hatimaye wananchi watapata huduma ya maji kwa gharama nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia madeni hayalipwi. Sasa taasisi muhimu kama Mamlaka za Maji zinakatiwa huduma, nilikuwa naangalia *television,* Kigoma pale wananchi wanagombania maji kwa sababu mamlaka imekatiwa maji. Shinyanga pale tumekatiwa maji siku nne, tuna viwanda pale vya maji, kuna viwanda vya soda, wananchi wanakosa maji eti kwa sababu bili ya *KASHUWASA* haijalipwa na huyo *KASHUWASA* hiyo pesa anayotakiwa atoe inatakiwa itolewe upande wa Serikali. Sasa sisi wananchi tumelipa bili tunataka huduma tu. Tunapata adhabu kwa sababu ya watu wengine. Hospitali haina maji, *imagine* hospitali ya mkoa inayopokea wagonjwa zaidi ya 200 inakatiwa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimezungumza hili kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu kule nyumbani wananchi wamenituma wamesema tunataka

nizungumzie suala la maji. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu suala hili ulisimamie kwa karibu kwa sababu pale tumeweka pesa nyingi za walipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Manispaa ya Shinyanga imejengewa mtandao wa maji safi lakini hakuna mtandao wa majitaka, majitaka yote yanayonyonywa hakuna pa kuyapeleka. Naomba Serikali itenge fedha kwenye bajeti hasa ya Waziri wa Maji, tujenge mtandao wa maji taka kwa sababu ulikuwepo kwenye andiko la mradi huu kwamba lazima na mitandao ya majitaka pia ijengwe. Leo majitaka pale Shinyanga hakuna pa kuyapeleka, mbaya zaidi hata vifaa vinavyokuja vyote ikiwemo na mita zinakuja mita feki, bili za wananchi zinachakachuliwa, wananchi wanapigwa bili kubwa kwa mita feki zinazokuja.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri asimamie hizi mamlaka kwa karibu, aangalie hata hizo mita zinazoagizwa, huyo mtu aliyepewa tenda ya kuagiza mita ziwe zina ubora unaostahili sio kuwaibia wananchi kwa kuleta mita ambazo ni feki, zinaongeza gharama za uendeshaji, zinaongeza bili ya maji kwa wananchi. Wananchi wangu bado hawana uwezo mkubwa wa kubeba mzigo wa gharama za kuhudumia maji ambayo kimsingi Serikali ilitakiwa isaidie ruzuku ili kuweza kuhakikisha mradi huu unawafikia watumiaji wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukiongeza *foot print* ya mradi huu gharama zile tutagawana wote, maji yale yafike mpaka Tabora, Sikonge, Ngudu, Sumve, Igunga, Singida na Malya, wote wapate yale maji ili tuweze kugawana gharama za uendeshaji. Tusipofanya hivyo tutaendelea kubeba msalaba huu sisi peke yetu na mradi ule utakufa kwa sababu hatuna uwezo wa kuuhudumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Stephen Julius Masele. Nilikuwa nafikiria kwa rafiki yangu Mheshimiwa Shabiby, kuchukua maji umbali wa kilometa 25 mbali sana

kwa nini usichukue pale Majawanga kilometa hata nane hazifiki maji Gairo yalishajaa. Majawanga ni kwangu Kongwa lakini tuna maji mengi tunakupa tu. *(Makofi/Kicheko)*

Pia hili la kwamba maji yapo, mitambo ipo halafu *TANESCO* inakuwa tatizo, kwa mfano Kongwa *TANESCO* wameweka LUKU kwenye mitambo ya umeme. LUKU maana yake ni kwamba lazima ulipe *front,* wakati Idara ya Maji lazima watu watumie maji ili ikusanye ndiyo ipeleke *TANESCO.* Sasa hilo jambo linakwenda kinyume, utapata wapi hela za kulipa kabla hujatumia wakati lazima watumiaji kwanza watumie ndio upate hela ndio uwalipe *TANESCO.* Kwa hiyo, LUKU kwenye mitambo ya maji ni jambo ambalo linajikanyaga lenyewe. Ningeomba Wizara ya Nishati na Madini waliangalie hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala!

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii na mimi kuweza kuchangia hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, nami nianze na suala zima la maji. Suala hili limekuwa ni changamoto kubwa sana kwa Watanzania wa nchi hii. Nitazungumzia suala la maji kwa Manispaa ya Dodoma, lakini pia nitazungumzia suala la maji kwa Wilaya ya Chemba.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Chemba tuna Mradi wa Maji Ntomoko. Mradi huu umeanza mwaka 2014 na ulikuwa una gharama ya shilingi bilioni 2.8. Mradi huu ulitakiwa kuhudumia vijiji 18 lakini ni kwa bahati mbaya sana katika vijiji 18 vijiji nane vikaondolewa vikabaki vijiji 10. Kati ya hivyo vijiji 10 hivi ninavyoongea hakuna kijiji hata kimoja ambacho kimepata maji kutokana na mradi huo na mpaka sasa mkandarasi ameshalipwa shilingi bilioni 2.4, maji hakuna.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji Ntomoko ulidhamiria kupeleka maji kwenye kituo cha afya ambacho kinatumika kama Hospitali ya Wilaya ya Chemba. Hospitali

ile haina maji, miundombinu ya maji imeshaharibika. Mwanamke mjamzito anapokwenda hospitalini kupata huduma ya kujifungua sharti ndugu zake waende na ndoo ya maji kichwani ili mwanamke yule aweze kupata huduma ya maji. Kama ndugu zake wakishindwa kwenda na maji mwanamke yule atapata huduma ya kujifungua, atafungashiwa uchafu wake atakwenda nao nyumbani kwake kwenda kupata huduma ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la maji ni kero katika Taifa letu, ni shida katika nchi hii. Tatizo la maji katika Taifa hili siyo suala la upatikanaji wa vyanzo vya maji kwani tunavyo vya kutosha sana. Shida ya Taifa hili ni mfumo wa namna ya kuyasambaza maji hayo kuwafikishia Watanzania kwenye maeneo yao, vyanzo vya maji vipo vya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maji ya Ntomoko ninayokwambia siyo maji unayokwenda kuyachimba bali ni maporomoko ya maji unakwenda kuyatega wananchi wanapata maji, imekuwa ni shida kweli kweli. Shilingi bilioni mbili watu wamelamba, wamekaa kimya, Watanzania wanapata shida na suala la maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi niseme ule mradi kwa kuwa ulikuwa ukamilike mwezi wa Pili mwaka huu umeshindikana na hakuna sababu zozote za msingi ambazo Watanzania wa Wilaya ya Chemba wanapewa, tunaomba huo mradi uondolewe kwetu ili tutafutiwe mradi mwingine mbadala utakaoweza kuleta tija na utakaofanya wananchi wetu waweze kupata maji. Nimeamua kulisemea hili kwa Waziri Mkuu ili na yeye aweze kuona kwa jicho la pekee sana hususani kwenye ile hospitali ambayo watu wanakwenda kupata huduma pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwenye suala zima la maafa. Mfuko wa maafa uko kwenye ofisi ya Waziri Mkuu. Kama unavyojua nchi yetu imekumbwa na ukame na hali ya chakula katika Taifa letu siyo nzuri kwenye maeneo kadhaa na hususan katika Mkoa wangu wa Dodoma hali ya chakula ni mbaya sana. Nilisema hapa siku ya Jumatatu

kwenye *briefing* kwamba Watanzania wa Mkoa wa Dodoma kuna njaa ya kutosha na imekithiri.

Mheshimiwa Spika, hapa ninapoongea, debe la mahindi Dodoma Mjini hapa sokoni pale Mwembeni na Majengo ni Sh.23,000, kilo ya mahindi wanapima Sh.1,250. Kondoa debe ni Sh.25,000, Chemba ni Sh.27,000, Kongwa kwako pale Kibaigwa ni Sh.22,500. Sijaona kwenye kitabu cha Waziri Mkuu akituambia suala la ukame katika Taifa hili katika yale maeneo ambayo yana changamoto ya bei kubwa za mazao ni nini amekifanya au anatarajia kufanya kitu gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii si sawa, hatuwatendei haki hawa Watanzania wetu. Watu wanakufa, watu wanajiua, wanaume Wilaya ya Kondoa wawili wameamua kujiua kwa sababu familia zao zimekosa chakula kwa muda wa siku tatu. Wanaume wanakimbia familia zao, wanawake ndiyo wanaobaki kwenye majumba na watoto wao lakini mwanamke huyo naye mvua Dodoma safari hii haijanyesha ya kutosha. Hata vibarua mwanamke aende akalime apate fedha ya kununua kilo ya mahindi hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningetaka kujua ni lini Serikali itatuletea chakula watu wa Dodoma. Tunahitaji chakula watu wa Dododma na naamini hata wewe unahitaji chakula kwa ajili ya watu wa Kongwa. Mheshimiwa Waziri Mkuu watu wa Dodoma tunaomba yale mahindi yanayooza Shinyanga tani 8,000 tunazihitaji watu wa Dodoma tuna shida na chakula, acheni kuozesha chakula wakati watu wanakufa kwa njaa. Kama ninyi upande wa pili hamuwezi kusema sisi tuacheni tuseme, tuko hapa kwa ajili ya kuwasemea Watanzania. Hatuko hapa kwa ajili ya kuona nafsi zetu ziko salama lakini kesho tutakuwa huko na sisi mitaani maana yake kazi hii siyo ya kudumu. Niombe nipate ufafanuzi kwenye suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwenye suala la Mahakama. Mahakama zetu zimekuwa ni changamoto kubwa sana hususani kwenye upande wa watumishi, lakini

pia kwenye suala zima la miundombinu kwa maana ya majengo yako. Wilaya yangu ya Chemba haina hata hiyo Mahakama ya Wilaya tu.

Mheshimiwa Spika, pili, Mahakama hizi za Mwanzo ambazo ziko kwenye Kata zetu kule chini ziko kwenye nyumba za watu ambao wamejitolea, lakini hata hao wahudumu unakuta kuna Karani mmoja na Hakimu mmoja anayeweza kuzunguka kwenye Kata zaidi ya nane, ameenda Kata chache sana ni Kata tano. Tuone ni namna gani tunaongeza Watumishi kwenye sekta hii ama kwenye Wizara hii ya Mahakama ili wananchi wetu waweze kupata huduma hii kwa urahisi lakini pili kwa uharaka ili waweze kuendelea na shughuli zingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni migogoro ya ardhi. Kaka yangu Mheshimiwa Shabiby amezungumzia tu mgogoro wa kwako kule pamoja na kwake. Kuna mgogoro kama huo wa Kiteto, mgogoro uliko baina ya Wilaya ya Chemba pamoja na Wilaya ya Kiteto ukiwa unahusisha hifadhi ya *WMA*-Makame. Wananchi wanakufa kule, hakuna vyombo vya habari vinavyoweza kuwamulika watu kwa namna gani wanavyokufa.

Mheshimiwa Spika, hayo matrekta yamechomwa moto hivi ninavyoongea, watu wameshapigwa, kuna watu 18 wameshafungwa jela, Mahakama ya Kiteto lakini kuna watu 27 wapo *lock up* Kiteto mpaka leo. Kwa hiyo, suala hili la migogoro tungeomba sana lishughulikiwe. Wabunge tuliambiwa tuorodheshe migogoro iliyoko katika maeneo yetu, tumeorodhesha migogoro hii kwa nchi nzima lakini hatupewi ripoti migogoro hiyo imesuluhishwa kwa namna gani na imeishia wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu aweze kuona suala la migogoro ya ardhi ndiyo itakayokwenda kutuletea vita ya wenyewe kwa wenyewe. Bila kumaliza migogoro ya ardhi ndoto za kufikia Tanzania ya Viwanda ni hadithi za Abunuwasi. Haitakuwepo kwa sababu

ardhi hiyo ndiyo tunayoitarajia Watanzania wetu waweze kutafuta malighafi mbalimbali ili tuweze kuendesha hivyo viwanda ambavyo tunavisema leo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niombe sana mgogoro wa Kiteto pamoja na Chemba ambao unahusisha pia Makame-*WMA* ambayo iko Kiteto ambayo hifadhi ile inawanufaisha watu wa Kiteto basi ufanyiwe kazi kwa haraka ili wananchi wale waweze kupata maeneo yao ya kuweza kulima na waweze kujijengea uchumi wa familia zao lakini na Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa muda ulioweza kunipatia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala. Mheshimiwa Nkamia fungua macho. Mheshimiwa Godfrey William Mgimwa atafuatiwa na Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene. *(Kicheko)*

**MHE. GODFREY W. MGIMWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukru sana kwa kunipa nafasi. Awali ya yote, kwanza nipende kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri lakini vilevile niweze kumshukuru Mheshimiwa Jenista Mhagama na msaidizi wake Mheshimiwa Anthony Mavunde kwa kazi nzuri ambazo wameendelea kuzifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jioni ya leo napenda kuzungumza machache kuhusu hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Tunazungumza kuhusu masuala mazima ya kuhamia Dodoma. Suala la kuhamia Dodoma kama lilivyoelezwa kwenye hotuba ni suala jema na lazima tuipongeze Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi kwa maamuzi haya ambayo yamefikiwa. Ingawa Serikali zilizopita zilijitahidi kufanya hivi lazima tupongeze hatua zilizofikiwa na Serikali ya Awamu ya Tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nigusie kidogo kuhusu suala la wanawake na vijana. Mheshimiwa Mavunde amejitahidi sana

kufanya kazi na vijana. Katika utaratibu ambao ameuanzisha wa kuhakikisha kwamba vijana Tanzania nzima wanawezeshwa, napenda sana utaratibu huu Mheshimiwa Mavunde uendelee nao na mimi kama kijana nakuunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunazungumza uwezeshwaji wa vijana na akinamama lakini tunapofanya uwezeshaji huu tuhakikishe kwamba ajira inakwenda sambamba na uwezeshwaji wa mambo haya yaliyozungumzwa katika hotuba. Tunavyozungumza kuhusu uwiano wa ajira na namna ambavyo Wizara husika inafanya kazi kuinua uchumi wa akinamama na vijana tuangalie Kanda ya Afrika Mashariki namna gani ambavyo wenzetu wamefanikiwa au wameshindwa.

Mheshimiwa Spika, katika uwiano wa ajira Tanzania tuko kwenye asilimia 10.3 lakini vijana wako kwenye uwiano wa asilimia 13 tuko vizuri ukilinganisha na nchi ya Kenya ambao wao uwiano wa ajira kwa upande wa vijana ni mkubwa zaidi hata mara tatu ya Tanzania. Kwa sababu hiyo niipongeze sana Serikali na Mawaziri husika kwa kazi ambazo wanaendelea kuzifanya. Namwalika Mheshimiwa Mavunde kuja pale Kalenga kuwahakikishia vijana wenzangu kwamba nao wananufaika na utaratibu huu ulioanzisha.

Mheshimiwa Spika, naomba nijikite sasa kwenye suala maji. Maji ni tatizo kubwa sana katika nchi yetu ya Tanzania na hususan katika Jimbo langu la Kalenga. Nina miradi mbalimbali ambayo bado haijakamilika ambayo nimezungumza sasa zaidi ya miaka miwili na kwa sababu ipo kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu lazima niizungumze.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Kalenga lina wananchi wengi ambao wanaiona miradi yao lakini haijakamilika. Nina mradi wa maji ambao unatoka Isupilo, Magunga na Itengulinyi ambapo jumla ya shilingi bilioni mbili ziliwekwa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba mradi huu wa maji unatekelezeka na wananchi katika vijiji hivi wananufaika.

Leo ni miaka miwili mkandarasi aliyekuwa pale *site* ameondoka ingawa amelipwa zaidi ya shilingi bilioni 1.2, hakuna malipo yoyote yanayofanyika na hivyo basi kufanya wananchi waweze kuleta mkanganyiko na kutokuwa na makubaliano kati ya Mbunge, wananchi, viongozi na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, napenda sana kuona kwamba Serikali inakuja na mkakati maalum wa kuhakikisha kwamba mkandarasi huyu analipwa ili maji yaweze kutoka katika vijiji hivi vitatu. Tutakapofanikiwa kupata maji katika vijiji hivi vitatu nina uhakika tunaweza kusaidia vijiji vingine kwa sababu mtandao utakuwa umeshasogea katika vijiji vya jirani. Sasa kupoteza shilingi bilioni 1.2 na kumuacha mkandarasi aende ni hasara kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, mkandarasi huyu ameishtaki Halmashauri ya Wilaya yangu, anadai riba ya zaidi ya shilingi milioni 250 kwa sababu ya mradi ambao haujakamilika. Nashangaa wakati mwingine kwa nini Serikali inaweza ikaruhusu vitu vya namna hii kutokea katika Majimbo yetu na mwisho wa siku fedha zinapotea, wananchi wanaendelea kulalamika maji na vilevile hata baada ya kuongea sana bado maji yanakuwa hayatoki. Huo ni mradi wa kwanza.

Mheshimiwa Spika, mradi wa pili ni wa maji wa Nyamulenge ambao nilizungumza hata katika bajeti iliyopita nikasema mradi huu unaweza ukahudumia zaidi ya vijiji 18 katika Jimbo la Kalenga na hata vijiji vingine katika upande wa pili wa Mheshimiwa Mwamoto katika Jimbo la Kilolo. Mradi huu unahitaji shilingi milioni 49 na nilipeleka dokezo kwa Mheshimiwa Naibu Waziri akanieleza kwamba tatizo hili tutalitatua. Leo hii bado hatujaweza kupata majibu, wananchi wanaendelea kupiga makelele na tuliwaahidi katika kampeni zetu tutawaletea maji lakini mpaka leo hii hakuna dalili za maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nisisitize zaidi na zaidi kwamba tunavyozungumzia maji tunazungumza uhai wa wananchi wetu waliotupa kura zetu. Tutakuja kudaiwa baadaye kipindi tutakapokuja kuomba kura. Ni kumbukumbu ambazo

napenda kuzitoa kwa sababu tulipita tukiwaomba kura kwa vigezo hivi. Leo hii unazungumza na mkandarasi anakwambia sijalipwa, unazungumza na Mhandisi wa Halmashauri anasema nimepeleka *certificate* kwenye Wizara. Ukiongea na Wizara wanasema hapana hatujapokea *certificate*, sasa sijui nani tumtafute hapa?

Mheshimiwa Spika, ni jambo ambalo linasikitisha sana, lakini napenda kuona kwamba maeneo mbalimbali siyo Jimbo la Kalenga tu, Wabunge wengi wamepiga kelele kuhusu maji, uwekwe mkakati maalum ambapo tutaweza kuona kwamba maji yanawafikia wananchi wetu kwa ukaribu na katika namna ambayo ni ya kipekee. Tumefanikiwa katika umeme kwa nini tushindwe kwenye maji? Naomba hayo yaweze kuwekwa kwenye kumbukumbu.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile Jimbo la Kalenga lina Hospitali ya Ipamba nimeomba gari la wagonjwa sasa miaka miwili na nusu. Jimbo la Kalenga ambalo ndilo linabeba hospitali ile ambayo inahudumia Majimbo mawili ya Wilaya nzima leo hii hakuna gari la wagonjwa. Narudia tena, Wilaya ya Iringa Vijijini ina Hospitali ya Ipamba ambayo haina gari la wagonjwa yaani nimeongea mpaka sasa naona kichwa kinaniuma.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iweze kuiangalia hospitali hii inayohudumia zaidi ya wananchi ya 300,000 wa Jimbo la Isimani na Jimbo la Kalenga na hata Iringa Mjini kama Manispaa lakini bado tunaendela kuomba. Kuna mambo ambayo tunatakiwa tuyaangalie tu kwa haraka haraka tukaona hawa ni wananchi wetu, hawa ni akinamama wanaokwenda kuhudumiwa katika huduma hizi ambazo ni za msingi. Kwa hiyo, napenda sana Serikali iweze kuliangalia suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine niipongeze sana Serikali na Wizara kwa ujumla kwa namna ambavyo wameweza kuliangalia suala la UKIMWI. Nimesoma katika kitabu nimeona kwamba kuna shilingi milioni 347 ambazo

tumechangia kama harambee, niipongeze sana Serikali kwa hilo lakini vilevile kuna shilingi bilioni 5.6 ambazo zimetengwa. Tatizo hili ni kubwa, tunaomba zile fedha ziweze kutengwa kwa watu hawa ambao kwa namna moja au nyingine wamenyanyasika kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, katika kitabu hiki jambo moja ambalo limenisikitisha kuna neno moja limetumiwa linaitwa WAVIU, WAVIU ni watu gani hawa? Watu wenye virusi vya UKIMWI ni watu gani? Watu hawa tukiwatafutia maneno ya *stereotype* tukasema kuna hawa wenye UKIMWI, hawa wenye hivi tutashindwa kufikia majibu yetu. Haya ni maneno ambayo tunayaweka wenyewe na tunakuja kufika wakati ambapo tunashindwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Godfrey.

**MHE. GODFREY W. MGIMWA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Godfrey William Mgimwa. Kama nilivyosema mwanzoni Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene anafuata.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Nami nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri iliyosheheni masuala mengi ya maendeleo ya Taifa letu. Pia nampongeza Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri wote walioko chini ya idara zake zote nikiamini kuwa ushirikiano wao mzuri unaleta maendeleo mengi tunayoyaona sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kuanza kwa kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kuendelea kuinua na kukuza uchumi wetu kwa asilimia saba kwa takribani miaka karibu 10 sasa. Nataka kuiomba Serikali yangu sasa iangalie jinsi ya kutafsiri ukuaji huu wa uchumi kwa wananchi wengi

walioko chini. Naomba Serikali yetu sasa hivi mikakati yake yote ijielekeze zaidi kwa wananchi katika maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, tunazungumzia kilimo lakini bado hatujakipa umuhimu unaotakiwa. Watu wengi wanapata ajira zao, wanapata uchumi wao kifedha kupitia kilimo, ufugaji, uvuvi na shughuli zilizoko vijijini lakini mpaka sasa hivi dhana ya kilimo inaachiwa wananchi wenyewe kuhangaika peke yao. Sikatai Serikali imeingiza nguvu sana kwenye masuala ya pembejeo na vilevile mafunzo kidogo ya ugani lakini haujawa ni mkakati wa kitaifa ambao unaenea kila mahali na kuhakikisha kuwa kila mtu anayelima, anayefuga au anayevua anafikiwa. Tuna mifano ya mikakati ya kitaifa ambayo imefanywa na ikafanikiwa kama *REA*. Kwa nini tusifanye mambo hayohayo katika masuala ya uzalishaji ili sasa ule ukuaji wa uchumi ukaonekane katika ukuaji wa uchumi wa wananchi mmoja mmoja vijijni.

Mheshimiwa Spika, napenda sana kuhamasisha hili suala kwa sababu najua ukombozi wetu utatokana na wananchi wetu kuweza kuzalisha kwa tija, kuuza kwa tija na kuweza kumudu maisha yao. Nataka kuhamasisha uwezekano wa kuwa na mikakati ya kutoa mafunzo mahsusi kwa vikundi vya wanawake, wanaume na vijana wanaofanya kazi za kilimo. Isiwe ni programu au mradi mmoja mmoja unaokwenda kule kwa ufadhili mmoja au mwingine lakini uwe ni mkakati wa Kitaifa. Mataifa yote yaliyofaidika na *green revolution* ulikuwa ni mkakati wa kitaifa. Naomba sana iangaliwe jinsi ambavyo kutakuwa na mkakati wa kuhakikisha kuwa uzalishaji unakuwa wa tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi wengine tunakotoka kilimo ndiyo kazi kubwa ya wananchi wengi na wengine tunatoka maeneo mazuri sana kwa kilimo lakini tumekwama miundombinu inayounganisha wakulima na masoko. Sasa hatuwezi kuzungumzia kilimo cha tija bila kuwa na miundombinu bora ya usafirishaji, maghala, maji na masuala kama hayo. Tunazungumzia vitu kimoja kimoja bila kuviunganisha, lile suala la mnyororo mzima wa uzalishaji

naomba sana lizingatiwe. Mwaka juzi tulizungumzia sana masuala ya maghala pamoja na stakabadhi ya mazao ghalani. Sijausikia sana lakini napenda uendelee kwa sababu hata kule ambako umefanyika umekuwa wa tija sana na wakulima wengi wananufaika na inawasaidia kuondokana na yale masuala ya kulanguliwa.

Mheshimiwa Spika, nataka kuzungumzia suala zima la Maafisa Ugani. Hata kama hatuwezi kuwapata wale wataalam waliosomea *degree* lakini tufundishe watu vijijini, vijana wasomi ambao wamekaa bure wawe wanafanya hizi kazi za kuraghibisha masuala haya vijijini kwetu ili tuweze kuwa na watu ambao wanatoa taaluma japo kwa kiasi fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nazungumzia masuala ya maendeleo. Kwa kweli nchi yetu ni kubwa sana na kweli sio rahisi kila mahali kukua kwa wakati mmoja. Hata hivyo, kwa miaka hamsini hii kuna maeneo ambayo yamekua sana na kuna maeneo ambayo bado yako nyuma sana. Naomba sana Waziri Mkuu na Serikali kwa ujumla, hebu waangalie na yale maeneo ya pembezoni ambayo yana tija na yana wananchi ambao ni wachapakazi lakini wanakosa zile huduma muhimu kama miundombinu na taaluma mbalimbali za kuwawezesha kukuza uchumi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi natokea Jimbo la Ileje, lina mvua nyingi sana, lina udongo mzuri sana, lina misitu lakini tuko nyuma kiuchumi kwa sababu ni Jimbo ambalo halina miundombinu hata kidogo yaani Ileje ni kama kijiji kikubwa. Umeme tunamshukuru Mungu sasa *REA* inakwenda lakini hakuna barabara ya lami hata moja, maji ni mengi sana lakini haina miundombinu ya kuyapeleka kwa wananchi. Tuna maeneo mazuri ya kulima lakini wananchi watalima wayapeleke wapi mazao yao wakati hakuna barabara wala masoko? Kwa hiyo, haya ni mambo ambayo tunataka kuomba sasa Serikali hebu katika kuangalia maendeleo tujikite na kule pembezoni nako ili wananchi wa Tanzania wa kule waone kuwa na wao tunapowapa hizi *data* za kukua kwa uchumi nao waone kweli wanakua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kuja kwenye suala lingine la maji. Kama hatuwezi kuzungumzia maji na kuhakikisha kuwa maji yanapatikana kwa kweli tunapoteza muda wetu. Tunazungumzia uchumi wa viwanda, tunazungumzia masuala ya usindikaji, tunazungumzia masuala ya kufuga kwa tija, tunazungumzia umwagiliaji, tutafanyaje bila kuwa na uhakika na maji?

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo ambayo yana maji mengi, kuna maeneo ambayo hayana maji kabisa lakini utakuta *treatment* ni ile ile moja, haiwezekani! Sehemu ambayo ina maji mengi *treatment* yake au utaratibu wa kuhakikisha hayo maji yanapatikana unakuwa tofauti na kule ambako hakuna maji kabisa. Kwa hiyo, ionekane kabisa hiyo tofauti lakini kama kila mahali watu wanazungumzia visima hata mahali ambapo kuna maji mengi, haiwezekani! Mimi kwangu sihitaji visima, nahitaji miundombinu ya kunipelekea maji kwa wananchi. Kwa hiyo, hayo nayo yatofautishwe wakati wa kuweka mikakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niende kwenye suala la *VICOBA, SACCOS* na Vyama vya Ushirika. Kwa kweli hili ndilo kimbilio la wananchi wengi kwa sababu mabenki hatuwezi kuyategemea, tumeshaona. Hata hivyo, *SACCOS, VICOBA* vinajiendesha vyenyewe havina mkakati wa Serikali wa kusema sasa tunatoa mafunzo ya aina hii. Wanaachiwa *NGO's,* wanaachiwa taasisi zenyewe kujianzishia vitu vyao, kunakuwa hakuna mfumo ambao unalingana nchi nzima wa *VICOBA, SACCOS* ambavyo vinaweza vikategemewa hata kuwa ndio njia bora ya kupata mikopo.

Mheshimiwa Spika, najua Mheshimiwa Jenista ananisikia na amekuwa akilifanyia kazi sana ili tusaidie kuwe na mfumo mzuri wa *VICOBA na SACCOS* nchi nzima, hata kama ni kuwekea utaratibu wa sheria au kanuni ambazo zitatumika kila mahali ili mwisho wa yote hizi *SACCOS* na *VICOBA* ndio zije zitengeneze benki za vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ajira kwa vijana. Ajira kwa vijana ingekuwa ni jambo rahisi sana kulifanya kama tungekuwa

tuna njia ya kuhakikisha kuwa tunawaweka hawa vijana pamoja na kuwawezesha. Kwenda kuwaambia tu vijana, 'mkalime, mkajiajiri' bila kuwaonesha wakajiajiri vipi au waende wapi ndiyo watapata nini au kuwawekea mitaji au mafunzo, wataendelea kucheza *pool,* kunywa viroba, kuvuta bangi na kufanya uhalifu wa kila aina. Tuwe na *system* ya kuwawekea vikosi vya kazi. Mwaka wa kwanza, wa pili na wa tatu tuwawezeshe, mwisho wa yote hawa watakuja kuwa *responsible.* Kule ambako tunawawezesha mbona wanafanya kazi nzuri sana, sidhani kama vijana ni wakorofi kiasi hicho lakini hawana njia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Janet, ahsante sana

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene. Tunaendelea na Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi atafuatiwa na Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha na Mheshimiwa Hussein Bashe ajiandae. Mheshimiwa Kapufi!

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza kabisa naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kwa namna ya pekee pamoja na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na watendaji wote, nijikite katika kulifikisha hili mbele yenu kwa maana ya hotuba ya Waziri Mkuu ukurasa ule wa kumi na moja na kwa afya ya kikao hiki naomba nipasome hapa.

*"Ili kuendelea kuboresha demokrasia hapa nchini, hatuna budi kujenga jamii inayoheshimu na kuzingatia sharia, kanuni na taratibu za nchi pamoja na kuwa na uvumilivu wa kisiasa. Ninatoa rai kwa wadau wa siasa wote nchini kujenga*

*utamaduni wa masikilizano na kuendesha siasa za maendeleo badala ya siasa za malumbano; siasa za kuunganisha watu watu wetu badala ya kuwagawa; na siasa za uwajibikaji badala ya siasa za mazoea. Serikali itaendelea kulinda na kuheshimu misingi ya siasa zinazolenga kuleta ustawi wa wananchi na zinazotanguliza maslahi ya nchi na wananchi".*

Mheshimiwa Spika, hili limebeba ujumbe wote ambao nilikuwa nakusudia kuusema. Pia nimejaribu kufuatilia hotuba ya Kambi ya Upinzani nikakutana na kauli moja na mimi niliiona sio mbaya, ambayo wanasema kwamba:-

*"Wanazuoni wanasema kutofautiana kifikra ni afya ya akili na ili uvumbuzi utokee lazima kuwe na fikra mbadala."*

Mheshimiwa Spika, mimi naona niende mbele zaidi na ili twende mbele tusipinge kila kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, eneo la kwangu kwa maana ya Katavi nikizingatia sekta ya utalii ambayo imeongelewa vizuri katika hotuba ya Waziri Mkuu, naiona sekta ya utalii na usafiri wa anga kama watoto pacha. Utakapoboresha usafiri wa anga unaboresha eneo la sekta ya utalii. Kwa misingi hiyo, hata nilipokutana na habari ya nchi kununua ndege, mara ya mwisho katika kutafuta habari nilikutana na nchi moja ya Ethiopia, uchumi wake mkuu umejikita katika maeneo yafuatayo, ukiacha kilimo, kuna suala la usafiri wa anga, wamekuwa wakifanya vizuri na kuibua fursa nyingine kwa kupitia usafiri wa anga. Leo tunapotamani hata kiongozi wa nchi atoke akaiangalie dunia anakwendaje huko kwingine? Ni lazima atakwenda kwa kutumia usafiri wa anga. Kwa hiyo, ninapoona nchi yangu inakwenda kuzungumzia habari za usafiri wa anga suala hilo naliunga mkono na kupanga ni kuchagua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mtu mmoja hakujenga nyumba, hakufanya kitu kingine, yeye alianza kwa kununua mziki. Kwa kupitia mziki ilimletea utulivu wa fikra akaweza kujipanga akaibua fursa mbalimbali na baadaye akajenga

nyumba na vitu vingine vyote vikaendelea. Kwa hiyo, kupanga ni kuchagua. Kila mmoja anaweza akaamua anaanza na kitu gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikizungumzia suala hilo la utalii kwa maana ya Katavi, nimeshukuru katika hotuba ya Waziri Mkuu amezungumzia habari ya kupanua wigo. Eneo lile ni kweli tuna mbuga nzuri ya Katavi lakini pamoja na kuwa na uwanja mzuri, ukiuliza ni kwa nini uwanja ule wa Katavi haufanyi kazi tunaambiwa tatizo hakuna ndege zinazokwenda kule. Mimi niombe, kwa maana ya ndege hizi ambazo zipo, zianzishiwe safari ya kwenda Katavi ili kuibua fursa hiyo ya utalii. Kama kuna tatizo linalotokana na suala la mafuta au kutokuwepo kwa gari la zimamoto, naiomba Serikali yangu sikivu iangalie suala hilo kwa sababu upande ule tukifanya vizuri inakuwa sio kwa ajili ya wana Katavi tu ni kwa ajili ya maslahi mapana ya nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikitoka hapo naomba nije upande wa sekta ya madini. Nilifarijika nilipokutana na habari ya kutenga maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo wadogo. Najua fursa hiyo ya uchimbaji madini na hasa tunapoelekeza kwa wachimbaji wadogo, baadaye watakuja kuchangia pato la Taifa. Kule kwangu kuna maeneo ya Dirif na Kapanda, niombe isiishie kwenye kuandika kwenye vitabu hivi kwamba maeneo hayo yatatengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo, twende kwenye hatua ya mbele zaidi ya kuhakikisha kweli maeneo hayo wanapatiwa hao wachimbaji wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna suala zima la kuongeza thamani kwa maana ya madini lakini hata kama tutaongeza thamani naomba twende mbali zaidi na suala la masoko pia. Watu hawa tunaweza tukawahamasisha wakachimba, wakaongeza thamani lakini inapokuwa hakuna soko naona kama ni tatizo pia.

Mheshimiwa Spika, nikitoka kwenye sekta hiyo naomba niende kwenye sekta ya afya. Eneo la sekta ya afya nimeliona likizungumziwa humu kwa maana ya afya ya

mama na mtoto mimi naomba niende mbali zaidi. Tunapozungumzia habari ya afya ya mama na mtoto naomba sana ilenge pia kwenye kupiga vita mimba za utotoni na hili naliona ni tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kule kwangu Katavi taarifa zinatuambia 45% ya mimba za utotoni zinatoka kwetu Katavi, naliona hili ni tatizo. Kwa hiyo, naomba kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, mazingira yaendelee kutengenezwa, namna ya kuirudisha jamii hii kulitambua hili kwamba ni tatizo, inapokuwa mama yeye mwenyewe ni mtoto halafu anakuwa na mtoto hata mipango mingine ya kitaifa hatutaifikia, kwa sababu mama mwenyewe anakuwa hajitambui na huyo mtoto atakuwa katika mazingira magumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kulisema hilo, naomba pia niende katika suala la elimu. Nafarijika kusikia habari ya Kusoma, Kuandika na Kuhesabu lakini naomba twende mbali zaidi. Katika eneo hili hili la elimu, fursa ambayo nimekuwa nikiiona na wakati huo Watanzania hatufanyii kazi fursa hii kwa maana ya lugha adimu ambayo ni Kiswahili, mimi napata tabu. Huko duniani watu wengine wanaajiriwa kwa kupitia Kiswahili tu. Kuna nchi moja watu wake wengi wanarudisha pato katika nchi yake kwa kupitia wasomi mbalimbali kwenda katika maeneo mbalimbali duniani wanakusanya fedha na kuzirudisha kwenye nchi yao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Watanzania wenzangu katika eneo hili hili la elimu, Kiswahili tusikibeze. Kiswahili kitatoa ajira, kitatoa fursa kwa watu wetu, suala ni kujipanga vizuri. Tunapoambiwa kama ni wazungumzaji wazuri wa Kiswahili lakini unakuta nchi nyingine ndiyo wanafanya kazi na wanakuwa mbele wakati Watanzania tuko nyuma mimi hapo nakuwa sijisikii vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa suala la michezo. Michezo ni afya lakini shida moja ambayo naiona kwa sisi Watanzania, muda umekuwa ni mrefu tunakuwa kama kichwa cha mwendawazimu na sababu ni nini? Ni mipango

yetu kuwa ya muda mfupi, mara nyingi tunakwenda na mipango ya zima moto. Naomba turudi kwenye mipango endelevu, tuwekeze katika eneo hili. Akina Bayi wa miaka hiyo wako wapi? Tunatamani kuwaona watu hao katika maeneo yote iwe ni riadha au mpira wa miguu. Nimefarijika kuona kwamba tutarudi kuendeleza michezo huko mashuleni na kwenye shule za msingi lakini tuendelee kuwekeza na ukitaka fedha, tumia fedha.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naendelea kusema naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi. Nilikuwa nimesema kwamba Mheshimiwa Maryam Msabaha atafuatia, atafuatiwa na Mheshimiwa Hussein Bashe na Mheshimiwa Anna Lupembe ajiandae.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kunijalia uhai na uzima na mimi kusimama mbele yako kwenye Bunge lako Tukufu na kuchangia Wizara ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, naipongeza hotuba ya Kambi ya Upinzani iliyowasilishwa na kiongozi wetu wa Kambi ya Upinzani. Naishauri Serikali, yale yote mazuri yaliyozungumzwa kwenye hotuba ya Kambi ya Upinzani myachukue na myafanyie kazi kwa mustakabali wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba ya Waziri Mkuu nitachangia ukurasa wa 11 kuhusu mambo ya Muungano. Kweli kuna mambo mengi ya Muungano, kero zimetatuliwa na nyingine mpaka leo hazijapata ufumbuzi na sio vibaya pia kuuliza ni zipi zilizopata ufumbuzi na zipi ambazo hazijapata ufumbuzi. Nakumbuka kuna Tume ya Pamoja ilianzishwa miaka mitano ya nyuma kwa ajili ya masuala ya kifedha na Akaunti ya Pamoja kwa pande zote mbili, kwa upande wa Zanzibar na Tanzania Bara lakini mpaka sasa hivi hii Tume sijui imeingiziwa kiasi gani cha fedha. Ukitazama hata fedha wanazozipata ni za kulipana tu mishahara,

ukiangalia majengo wanayoyatumia ni ya kukodi. Nataka niulize Serikali ni kiasi gani cha fedha kimeingizwa katika Akaunti hii ya Pamoja ya masuala ya Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Akaunti hii ya Pamoja inashughulikia mambo mengi lakini sasa kuna kizungumkuti, hatujui kinachoingizwa. Nadhani ni vizuri wananchi kwa pande zote mbili tujue pande hii ya Zanzibar wanachangia kiasi gani na Tanzania Bara wanachangia kiasi gani ili wananchi wajue faida za Muungano na hasara za Muungano.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali zile kero za Muungano ambazo zimekuwa ni kero sugu na kama zimepatiwa ufumbuzi wa kudumu ziwe zinatolewa kwenye magazeti ya Zanzibar Leo au magazeti ya Serikali ili wananchi na vyombo vya habari mbalimbali wapate kufuatilia kero hizi za Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikiondoka kwenye masuala ya Muungano bado nimo kwenye kitabu cha Waziri Mkuu kwenye ukurasa wa 10 kuhusu masuala ya siasa. Siasa ni maendeleo, tukiwa na siasa safi lazima tutakuwa na maendeleo. Tukiwa na utawala bora lazima tutakuwa na maendeleo. Tukiwa na utawala ambao unaheshimu haki za binadamu, haki za sheria na kufuata misingi ya demokrasia ni lazima maendeleo na uchumi wa Taifa utakua kwa kasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo vyama vya siasa vimezuiliwa kufanya mikutano, vyama vya siasa mtaji wao uko kwa wananchi na chama cha siasa bila kufanya mikutano, bila kutangaza sera za chama chao hamwezi kuingiza wanachama na hawawezi kujua sera za chama ni nini. Nashauri Ofisi ya Rais iangalie suala hili, Waziri Mkuu aangalie suala hili kwa mustakabali wa Taifa hili tusiingize migogoro isiyokuwa ya lazima, vyama vya siasa viruhusiwe kufanya mikutano. Vyama vya siasa vyote vyenye usajili wa kudumu vina haki ya kufanya mikutano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuangalie pia katika Marais wote waliopita, Zanzibar lazima kulikuwa na changamoto zake. Pia niwapongeze kwa dhati ya moyo wangu Marais waliothubutu kukaa na upande wa Zanzibar kuangalia zile changamoto na matatizo ya kisiasa na hata wakakaa wakapata muafaka.

Mheshimiwa Spika, niombe haya yaliyotokea sio mambo mazuri kwa Tanzania hii tuliyokuwa nayo. Turudi tukae mezani tuzungumze kwa kina tuangalie mustakabali wa nchi kwanza na maslahi ya wananchi kwa pande zote za Muungano ili tupate maendeleo, tupate muafaka wa kisiasa. Tusifanye siasa za kuburuzana, chuki na ubabe. Ndiyo maana nimetangulia kusema tukiwa na siasa safi lazima tutapata maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nimwombe Mheshimiwa Rais aangalie kisiwa cha Zanzibar na Pemba kama ambavyo Marais waliotangulia wa Muungano walikaa meza moja wakaangalia mustakabali wa Zanzibar, wakaangalia mustakabali wa Pemba na Muungano ili tupate muafaka tusonge mbele tujenge Tanzania yetu, utaifa kwanza. *(Makafi)*

Mheshimiwa Spika, hakuna kitu kizuri kama masikilizano, hakuna kitu kizuri kama kufahamiana na mkifahamiana na mkisikilizana Mwenyezi Mungu huleta baraka, neema na kila lenye heri kwa wanaosikilizana lakini kukiwa na mfarakano mkawa hamsikilizani baraka pia inaondoka. Namshauri Mheshimiwa Rais asiogope arudi meza moja wakae na Maalim Seif, wakae na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar waangalie mustakabali wa Zanzibar na Muungano unakokwenda tupate kujenga nchi kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hayo kwa nini? Kuna wengi wanaogopa kumshauri Rais, lakini mimi namshauri Rais wangu namwambia rudi Zanzibar tunakupenda, wakae meza moja watafute mustakabali wa Taifa hili. Hatuwezi kwenda na siasa za chuki, hatuwezi kwenda na utawala usiokuwa na mantiki na Tanzania hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nirudi kwenye masuala ya vyombo vya ulinzi na usalama. Suala hili ni mtambuka, nimeshangaa sana na namshauri Mheshimiwa Rais kama wengine mnaogopa kumshauri, tangu enzi ya Mwalimu Nyerere vikosi vya jeshi havijawahi kulipa umeme wala havijawahi kuwekewa LUKU. Majeshi ni kitu muhimu katika nchi yetu, vyombo vya ulinzi ni kitu muhimu katika nchi yetu, maslahi ya vyombo vya ulinzi na usalama yatazamwe kwa jicho pana, yatazamwe kwa uangalifu, yatazamwe kwa maslahi ya nchi. Leo tusiingize migogoro isiyokuwa na sababu katika vikosi vya ulinzi na usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii nchi ni yetu sote, hakuna nchi ya CHADEMA, CCM, *CUF, ACT* wala ya *NCCR*-Mageuzi, tukae tusikilizane, tusibaguane. Leo mimi huwezi kuniambia nisiende kwa mtoto wa Ali Hassan Mwinyi kumsalimia, utakuwa umenikwaza au nisiende sijui kwa ndugu yangu Mheshimiwa Nahodha pale kumsalimia utakuwa umenikwaza, tukae tusikilizane. Tushauriane tuangalie nchi inakwenda wapi na wao watanishauri wataniambia Bi. Maryam unavyokwenda sivyo nitapokea ushauri wao kama kaka zangu, tuondoshe chuki za kisiasa, tujenge Tanzania yetu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Mungu ibariki Tanzania. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Bi. Maryam Msabaha. Kabla ya Mheshimiwa Hussein Bashe nitoe tangazo moja nisije nikasahau, kama mnavyojua kesho ni *Karume Day* si ndiyo jamani...

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**SPIKA:** Kwa hiyo, ni siku ya mapumziko lakini kwa wale wanachama wa *APNAC* mnaarifiwa kwamba saa tatu asubuhi itaanza semina inayohusu masuala ya rushwa na utawala bora ambayo itafanyika *African Dreams Conference Center, Area D,* hapa Dodoma. Tangazo hili limeletwa na Mwenyekiti wa *APNAC,* Kapteni Mstaafu Mheshimiwa George Mkuchika. Wale wajumbe wa *APNAC* kesho *African Dreams,*

hapa Dodoma tunasema kuna mambo mswano kule, kwa hiyo, muwahi kule kesho saa tatu. Mheshimiwa Hussein Bashe.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE**: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa. Kwanza nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia sote kufika hapa kwa ajili ya kutimiza wajibu wetu. Vilevile nitumie fursa hii kukupa pole wewe kwa kuondokewa na mmoja kati ya sisi, Mbunge wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo, Mheshimiwa Dkt. Macha ambaye alikuwa Mjumbe mwenzangu wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii. Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi.

**WABUNGE FULANI:** Ameen.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE**: Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nampongeza kwa jambo moja kubwa sana, *humbleness.* Kwa kipindi cha mwaka mmoja ambao amekuwa Waziri Mkuu wetu ame-*portray* kuwa kiongozi mtulivu, mwadilifu na msikivu. Simpongezi kwa sababu labda ya unafiki au kuna kitu nataka, *this is the naked truth.* Ni Waziri Mkuu mpole, msikivu na anayesimamia kile ambacho anakiamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia viongozi wa ngazi mbalimbali na Wabunge wamekuwa wakisema katika *levels* mbalimbali za wilaya na mikoa viongozi wengi kukosa sifa aliyonayo Mheshimiwa Kassim Majaliwa. Hiki ni kipaji ambacho Mwenyezi Mungu amempa na hatuna budi kumpongeza kwa kuonesha hilo. Nadhani viongozi wengine katika nchi wana wajibu wa kujifunza jambo hili alilonalo Mheshimiwa Majaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende kwenye kuchangia. Kwanza niipongeze Ofisi ya Waziri Mkuu, ukiangalia kwenye maelezo ya hotuba yake na Kamati, bajeti ya maendeleo wamepata asilimia 44, ndicho walichokipata. Hii ni taswira inayoonesha kwamba Serikali katika Wizara mbalimbali suala la upelekaji wa fedha limekuwa tatizo. Kwa hiyo, ningeshauri kwenye *cabinet* kabla ya bajeti ya Serikali Kuu haijaja ingawa

katika Kamati tumeona wote, mimi kwenye Kamati niliyopo nimeona utekelezaji wa bajeti ulivyo tatizo hasa fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Waziri Mkuu ukiangalia ukurasa wa 16, anapoongelea suala la Serikali kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana imetoa mikopo ya 1. 5 *billion shillings* kwa vikundi 297 lakini ameongelea Mamlaka ya Serikali za Mitaa kutoa 4.6 *billion* lakini tulioshiriki kwenye mchakato huu, mimi nimeenda na Mkoa wangu Serikali za Mitaa kuona ni kiwango gani fedha kutoka *Central Government* zinavyoathiri upatikanaji wa asilimia tano na asilimia 10.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano katika Halmashauri ya Mji wa Nzega, *OC* iliyokuwa *budgeted* kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ilikuwa ni shilingi milioni 606, tulichokipokea ni asilimia 27 peke yake. *Development budget* ilikuwa ni 5.7 *billion* tulichokipokea ni asilimia 24. Maana yake ni kwamba fedha tulizokusanya katika mapato ya ndani zote zitaenda kusukuma shughuli za uendeshaji wa ofisi, asilimia tano ya akinamama na asilimia tano ya vijana haiwezi kuwa *attained.* Kwa hiyo, tafsiri ni moja tu, ni lazima tupange *realistic budget.* Sio vibaya kuwa na uhakika kuliko kujenga matumaini makubwa kwa watu wetu ambayo hayapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pale Ofisini kwa Waziri Mkuu na mimi nimpongeze kuanzisha hiki kitengo cha ku- *track* ahadi za Rais, nampongeza sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu ningekuomba uende hatua ya mbele zaidi, ile ofisi yako inayo-*track* ahadi za Rais kwa mfumo wa kidigitali na utekelezaji wake katika kila Wizara tungeomba angalau kila miezi sita Wabunge tugawiwe, kwa sababu sisi ndio tuliokuwepo kwenye majimbo wakati Rais anatoa hizi ahadi. Zipo ahadi za Ilani na zipo ahadi ambazo Rais alitoa pale pale hadharani. Kwa mfano, katika Jimbo langu Rais aliahidi ujenzi wa daraja la Nhobola na sisi katika Halmashauri

tukaamua kutoa fedha imefanyika *feasibility study* na kila kitu tume-*submit* Wizara ya Ujenzi, kwa sababu uwezo wa TAMISEMI kujenga haupo.

Mheshimiwa Spika, aAhadi ile tuliahidiwa itatekelezwa mwaka huu mpaka leo hatuoni dhamira pamoja na kukutana na Mawaziri katika *corridor*. Wakati Rais anakwenda Chato Desemba alifanya mkutano Nzega na kwenye *podium* akasema kwamba jambo hili linashughulikiwa mwaka huu wa fedha, hakuna, wananchi wanaishi kwa matumaini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye hotuba hii ya Waziri Mkuu amezungumzia suala la kukua kwa uchumi kwa asilimia saba na nimemsikia dada yangu Mheshimiwa Janet Mbene amezungumza suala hili. *Economic growth* na *economic development* ni vitu viwili tofauti. Tunapozungumzia *growth* ya uchumi bila kuzungumzia kubadilika kwa maisha ya watu tutakuwa tunajidanganya kwenye takwimu na tatizo liko wapi? Tatizo la kwanza ndugu zangu nimeangalia alichoki-*present* Waziri wa Fedha hapa hakuna *inclusion,* kwenye mpango wetu tunaokuja kuupitisha wa 2017/2018 ni ule ule hauna tofauti na 2016/2017. Hakuna *focus* kwenye *agro-sector*.

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kuondoa matatizo ya watu wetu kama hatuwekezi kwenye kilimo. Ni hatari kweli! Mimi nataka niseme, kama hatutokuwa makini kutatua changamoto ya umaskini wa watu wetu kwa kuangalia *sector* zinazokua, zinazogusa maisha ya watu, *it is just a time bomb,* iko siku watu watatafuta haki yao mitaani na hii itahatarisha usalama wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, angalia sekta zilizo-*contribute* asilimia saba kutokana na hotuba ya Waziri Mkuu, madini, usafiri, mawasiliano, *financial institution.* Madini ni yapi? Ni *GGM* na *Acaccia*. Ripoti ya Kamati ya Bomani ambayo iliundwa na Serikali ya Awamu ya Nne mpaka leo utekelezaji wa mapendekezo yake *its only* 30%. Kamati ya Bomani

ilipendekeza mrahaba wa 3% - 15% hiyo ndiyo *range*. *Revenue sharing plan* hatujafanya, matokeo yake tumefanya nini? Ndiyo hii tunafanya zima moto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunayo mipango, tuna Sera ya Madini ya nchi, tuna mapendekezo ya ripoti ya Bomani hayajatekelezwa, tunafanya hizi kazi za zima moto. Ningeomba Mheshimiwa Waziri Mkuu niishauri Serikali kwa heshima kabisa, kule kwangu Nzega wanaamini yale makontena yaliyoko pale bandarini ndani yana dhahabu yaani kuna zile *gold bar*. Tunaomba mrekodi hili tukio la uchunguzi mtuoneshe kwenye *TV* kilichomo ndani ya zile kontena.

Mheshimiwa Spika, mimi ni mmoja wa watu ambao naamini uwekezaji wa migodi mikubwa haujasaidia nchi yetu. Haujasaidia kabisa na mimi ni muathirika natoka Nzega. Yule *Resolute* kaondoka na 10 *billion shillings* ya *service levy,* nimesema humu, *TMA* wamefanya, nimeandika barua na kwa taarifa yako Mheshimiwa Spika, mwezi wa Sita anapewa *certificate* na Serikali *ya* ku-*close* mradi na kuondoka. Anaondoka na bilioni kumi ya Watanzania na ya wananchi wa Nzega, *it is very painful*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niishukuru Serikali kwa kugawa maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo, mimi kwangu wameanza kupata. Hata hivyo, naiomba Wizara ya Nishati na Madini, nimpongeze Waziri na Naibu Waziri kwenye hili wamekuwa *supportive.* Wale mnaowapa leseni wakija kwenye Halmashauri zetu angalau mhusishe jamii kwa sababu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Bashe, muda hauko upande wako.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE**: Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Anna Lupembe atafuatiwa na Mheshimiwa Zuberi Kuchauka na Mheshimiwa Joseph Kakunda ajiandae. Mheshimiwa Anna Lupembe.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwanza kabisa, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupa uzima na uhai leo tuko katika Bunge hili tukichangia bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze sana Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoifanya katika nchi yetu ya Tanzania. Waziri Mkuu unajituma sana, hongera sana na kote ulikopita kuna mafanikio makubwa sana. Naomba tukupongeze sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Waziri Mheshimiwa Jenista pamoja na Naibu wake kwa kazi kubwa waliyoifanya. Kama safari hii sisi mmetupa nafasi ya kuwasha mwenge katika Mkoa wetu wa Katavi, tumepata manufaa na mafanikio makubwa, naomba niwapongeze sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwapongeze Mawaziri, mnyonge, mnyongeni lakini haki yake mpeni. Mawaziri wetu mnafanya kazi kubwa sana, mnatembea usiku na mchana kwa ajili ya nchi yenu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba nijielekeze kwenye elimu ya msingi. Serikali imefanya jitihada kubwa, imeondoa kero ya Watanzania na watoto wetu wanasoma bure. Vilevile kulikuwa kuna changamoto ndani ya shule zetu za misingi tulikuwa hatuna madawati lakini Serikali ilifanya jitihada kubwa kutafuta madawati pamoja na wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na wananchi, wote kwa ujumla wakachangia, sasa shule zetu zina madawati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini bado tuna tatizo moja kubwa sana ndani ya shule zetu za misingi la vyumba vya

madarasa. Sasa hivi kutokana na elimu bure, wazazi wengi wanaenda kuandikisha watoto ili waweze kusoma na kupata elimu ya msingi. Unakuta takibani watoto 1,000 darasa la kwanza hawana sehemu ya kusomea, sehemu nyingine watoto wamepangiwa madawati nje wanasoma. Maeneo yetu kama Mkoa wa Katavi ni ya mvua, mvua ikinyesha wale watoto hawapati elimu, inabidi watawanywe warudi nyumbani.

Mheshimiwa Spika, kwa vile hii ni changamoto, tunaomba Serikali ipange mpango mkakati kuhakikisha tatizo hili linashughulikiwa. Wananchi wanajitoa kwa hali na mali kuchangia elimu. Unaenda unakuta wananchi wamejenga madarasa, wengine wamemaliza wengine uwezo wao wanafika kwenye lenta. Tunaomba Serikali ipange mkakati mpana kwa ajili ya kuongeza madarasa katika shule zetu. Tunapongeza kwa jitihada kubwa wanazofanya lakini inabidi mpango mkakati uwe mpana zaidi ili watoto waweze kupata sehemu ya kusomea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende kwenye elimu ya sekondari. Katika hotuba ya Waziri Mkuu ameelekeza wananchi wahamasishwe ili watoto waweze kusoma sayansi. Ni kweli, shule zetu nyingi za sekondari walimu wa sayansi hatuna, wako wachache sana. Unakuta shule ya sekondari ina mwalimu mmoja wa sayansi au hakuna kabisa, watoto wengi wanajielekeza kwenye masomo ya biashara. Tunaomba Serikali iwaajiri walimu wa sayansi ili waweze kwenda kwenye shule zetu za kata kwa sababu ndizo wananchi wengi watoto wao wameenda kusoma huko ili tuweze kuibua walimu wa sayansi na vipaji vipya. Kuna shule baadhi kama kwetu Shule ya Usevya ina walimu wachache sana wa sayansi lakini wamesaidia kuibua wale watoto wa *Form V* au *Form VI* wanatoka wanaenda kusaidia kufundisha wanafunzi sehemu nyingine.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee maji vijijini. Hakuna Mbunge atakayesimama hapa asizungumzie maji kwa sababu tunavyoenda huko vijijini tunaona hali halisi. Serikali ilifanya jitihada kubwa ya kuchimba visima virefu na

vifupi. Hata hivyo, kuna sehemu nyingine watalaam walienda kuangalia wakaona kabisa hapa pana maji lakini walipochimba yale maji yakapotea kutokana na hali halisi sasa hivi Watanzania wengi wanakata miti, wanaharibu sehemu nyingi ambazo maji yanatokea, unakuta kunakuwa kuna ukame mwingi. Naomba Serikali ijipange vizuri upande wa maji. Vijijini wananchi hawana maji kabisa. Unakuta kijiji hakuna hata kisima kimoja. Mwananchi anatoka maeneo husika anaelekea maili 20 au 30 kwa ajili ya kutafuta maji. Tunaomba Serikali ipange mkakati mpana kwa ajili ya maji vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile tunaipongeza Serikali kwa ajili ya maji mijini. Mamlaka za Maji Mijini zinajitahidi, miradi mbalimbali inaelekezwa huko. Tunaomba Serikali, kuna miradi ambayo ipo lakini bado wale wakandarasi hawajaweza kulipwa pesa zile wanazodai. Tunaomba wawalipe wakandarasi ili waweze kutimiza miradi ile ambayo iko kwenye Mamlaka ya Maji Mijini.

Mheshimiwa Spika, Hospitali yetu ya Wilaya ya Mpanda ilikuwa haina duka la dawa lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu alivyofika alielekeza na leo hii tunajivunia Mkoa wa Katavi, Wilaya ya Mpanda tuna duka la dawa, tunapongeza sana. Hata hivyo, kuna tatizo kidogo, dawa zinakuja chache. Tunaomba dawa na vifaa tiba viongezeke ili wananchi waweze kupata huduma safi na salama kwa ukaribu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nipongeze kwa Kituo cha Afya Kalema kupata gari na sasa hivi tumepata chumba cha upasuaji, akinamama pale wanazaa kwa uzazi salama zaidi. Pia Tarafa ya Mishamo tuna Kituo cha Afya ambacho upasuaji unafanyika na vilevile tumepewa gari. Bado tarafa nyingine tunahitaji mtufikirie tuweze kupata vyumba vya upasuaji na vilevile tuweze kupata magari ya afya kwa sababu kutoka kwenye tarafa mpaka mjini ni mbali.

Mheshimiwa Spika, naomba niipongeze Serikali, najua Wabunge wa Katavi wengi wanasema hili, sisi Mkoa

wetu wa Katavi tuna uwanja mzuri sana Serikali mlitujengea. Naomba tuipongeze Serikali kwa kutujengea ule ule uwanja. Tuna ndege ambazo tumenunua ndani ya Serikali yetu ya Awamu ya Tano. Tunaomba basi na sisi Mkoa wa Katavi tuweze kupata huduma hiyo ya ndege hata moja, katika *route* yoyote ile inayoenda Tabora au Kigoma ili wananchi wa Katavi nao waweze kufurahia matunda ya Serikali yao ya Awamu ya Tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna Ziwa Tanganyika ambalo linapita Ikola na Kalema. Kuna hii meli ya *MV Liemba* ina miaka 110...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Spika, tunaomba Serikali ijenge meli hii kwa sababu sisi wa Mkoa wa Katavi inatuhusu kupitia Ikola na Kalema. Tunaona meli nyingi zinajengwa...

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Anna Lupembe.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Zuberi Kuchauka atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kakunda.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi jioni hii ya leo ili na mimi niweze kuchangia hotuba hii ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo ada, naomba nijielekeze moja kwa moja kwenye hotuba hii nikilenga kwanza hii Taasisi ya Uvunaji wa Misitu (*TFS).* Kama ambavyo unafahamu 60% ya Wilaya ya Liwale inazungukwa na misitu,

kwa hiyo, uchumi mkubwa wa watu wa Liwale unategemea sana maliasili za misitu pamoja na wanyama. Kwa hiyo, naomba moja kwa moja nianzie huko.

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri Mkuu au Wizara inayohusika walete hapa marekebisho ya Sheria ya *TFS. TFS* kutupatia sisi Halmashauri 5% ya uvunaji wa mazao ya misitu kwa kweli ni kutokututendea haki. Ukienda kuangalia Liwale jinsi magogo yanavyovunwa pale, miti inavyohama na faida wanayoipata Wanaliwale wale kwa 5%, tena hiyo 5% yenyewe namna ya kuipata ni kwa shida kwelikweli. Naomba hii sheria iletwe hapa irekebishwe, 5% ni ndogo sana.

Mheshimiwa Spika, vilevile naomba niuelekeze mgogoro wa Hifadhi ya Selou pamoja na Wanakijiji wa Kikulyungu kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwa nini nauelekeza mgogoro huu kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu? Ni kwa sababu kwenye Wizara husika naona mgogoro huu umeshindikana. Kwa hiyo, naomba moja kwa moja kwa nafasi hii niuelekeze mgogoro huu kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu pengine tukapata msaada ili wale wananchi wa Kikulyungu wakaepukana na adha wanayoipata leo hii ya kupigwa vibaya na Askari wa Wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo naomba nijielekeze kwenye upande wa takwimu. Sensa ya mwaka 2012 kwa kweli sisi Wilaya ya Liwale imetuathiri sana. Imetuathiri kwa maana ya kwamba, imeonesha wakazi wa Wilaya ile ni kidogo sana. Nitoe mfano ufuatao. Wilaya ya Liwale kwenye *Basket Fund* tunapata Sh.8,000,000/=, Wilaya ya Nachingwea Sh.18,000,000/=, Wilaya Kilwa Sh.17,000,000/=, Wilaya ya Ruangwa Sh.21,000,000/=. *Basket Fund,* Liwale 350, Ruangwa bilioni 1, Kilwa milioni 600, Nachingwea milioni 800 lakini sisi hii idadi tuliyonayo sio kweli kwamba Wilaya ya Liwale yenye Kata 20 ina watu 92, siyo kweli, hii takwimu sio sahihi.

Mheshimiwa Spika, nashindwa kuwaelewa hawa watu wanaosimamia hizi takwimu. Katika Mkoa wa Lindi,

Hospitali pekee inayoona wagonjwa wengi kwa mwezi ni Hospitali ya Wilaya ya Liwale lakini ndio hospitali pekee inayopata mgawo mdogo. Naomba nilielekeze hili kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu ili liweze kupatiwa ufumbuzi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, kuna taarifa.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Spika, nataka nimpe taarifa mzungumzaji anayeendelea kuzungumza kwamba mwaka 2012 tulipokuwa tunafanya sensa tulipata matatizo makubwa ya baadhi ya watu kutokupenda kuhesabiwa na hii ndiyo imetusababisha kuwa na takwimu ambayo haiko sawasawa. Sasa fursa nyingine ya kufanya hivyo ni mpaka itakapofika. Kwa sasa takwimu zinazojulikana na kuaminika na Serikali ni hizo zilizochukuliwa mwaka 2012 wakati wa Sensa ya Taifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka, taarifa yako hiyo.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napokea taarifa yake kwani haijapingana na nilichokieleza lakini bado narejea palepale, kama takwimu za hospitali zinaletwa kila mwezi kwamba katika Mkoa wa Lindi hospitali inayoona wagonjwa wengi ni ya Wilaya ya Liwale. Sasa ni mwenye akili gani timamu hiyo hospitali inayoona wagonjwa wengi akaipa mgawo kidogo? Napata wasiwasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nijielekeze kwenye upande wa hiyohiyo takwimu inatuathiri vilevile kwenye mgawo wa wafanyakazi kwa maana ya ikama ya wafanyakazi. Ikama ya wafanyakazi kwa upande wa elimu, ikama ya wafanyakazi kwa upande wa afya, tuna matatizo sana. Mpaka leo hii ninavyoongea kwenye Bunge hili Tukufu, Liwale hatuna daktari bingwa, tuna uhaba wa madaktari, tuna uhaba wa walimu wa sekondari, lakini ukiuliza unaambiwa kwamba wale waliopo ndio wanafanana na

idadi ya watu walioko kule wakati sio kweli. Naomba hizi takwimu zirekebishwe, kama ripoti unaletewa ya idadi ya wanafunzi iweje sasa ushindwe kuitumia ripoti hiyo uende mwaka 2012? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naingia kwenye vyama vya ushirika. Vyama vya ushirika naomba iletwe sheria hapa ili tufanye marekebisho, vyama vya ushirika wawekewe masharti namna ya kuajiri wahasibu. Tumepata matatizo sana mwaka huu, kwenye Chama Kikuu cha Lunali hawajawahi kupatiwa fedha kama mwaka huu lakini wamevurunda mpaka sasa hivi vyama vya ushirika wameshamaliza pesa lakini wakulima hawajapata hela. Sawa, wale viongozi wa vyama vya msingi tutawapeleka Mahakamani watafungwa au watafilisiwa lakini bado mkulima aliyepeleka korosho yake mwezi wa 10 mwaka jana mpaka leo hajapata hela. Kufungwa au kupelekwa Mahakamani kwa huyu mtu mkulima yule imemsaidia nini?

Mheshimiwa Spika, leo hii mwezi wa Nne tunaandaa mashamba lakini mtu amepeleka korosho mwezi wa 10 mpaka leo hajapata pesa. Ombi langu ni kwamba, Sheria ya Vyama vya Ushirika iletwe hapa, tuwaundie sheria ili ajira za vyama vya ushirika ziendane na taaluma. Kwa sababu tatizo kubwa tulilolipata safari hii ni watu hawana taaluma ya uhasibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nijielekeze kwenye Sera ya Wazee. Sera ya Wazee imetungwa nafikiri tangu mwaka 2003 lakini mpaka leo Sheria ya Wazee haijawahi kuletwa kwenye Bunge hili, sijui mmekwama wapi? Naomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge hapa ndani sisi wote hapa ni wazee watarajiwa. Tunapolichelewesha hili tunajichelewesha sisi wenyewe na waathirika wakubwa ni sisi, leo vijana, kesho ni wazee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza sana wenzetu Zanzibar pamoja na uchumi wao kuwa hafifu lakini wamewakumbuka wazee angalau hata kuwapa Sh.200/=. Leo hii Tanzania Bara tumenyamaza, hata hiyo Sh.10,000/=

tuliyoambiwa watapewa mpaka leo haijulikani, tutafikaje huko hata sheria yenyewe haijaletwa hapa? Naomba sana Sheria hii ya Wazee iletwe hapa ili tuone wazee sisi watarajiwa huko mbele tumejiwekea akiba gani?

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa napenda nizungumzie kuhusu bajeti. Watu wengi sana wamezungumzia kuhusu upelekaji wa fedha kwenye miradi ya maendeleo, kwenye *OC,* siyo mzuri. Jamani, hapa tatizo siyo upelekaji, hela hakuna! Mimi sidhani kama Serikali wana pesa halafu hawapeleki! Tuseme kweli kwamba pesa hizo hazipo, makusanyo hayo hayapo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri wa Fedha anieleze pengine mimi kwa sababu ya elimu yangu ndogo sielewi. Hizi *figure* hizi zinazokuja hapa kila mwaka ambazo hata 50% tunashindwa kuzifikisha zina maana gani? Kuna tofauti gani leo hii tukasema kwamba hii bajeti yetu ni ya shilingi trilioni 18 badala ya kuweka 30? Shilingi trilioni 18 tunaweza tukaifikia! Kwa nini tunaweka shilingi trilioni 31 ambayo mwisho wa siku hata shilingi trilioni 20 hatufiki! Kuna sababu gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Waziri mwenye dhamana anisaidie ili na mimi nipate uelewa ili siku nyingine nisije nikasimama tena hapa nikauliza kuhusu jambo hilihili. Kwa nini tunaletewa hizi *figures* kubwa kubwa ambazo hazina mwisho?

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa naomba niongelee walimu. Kuna tatizo kubwa sana la matokeo. Matokeo ya elimu mwaka huu, kwa mfano kama Mkoa wa Mtwara, Mheshimiwa Spika shahidi, Mkuu wa Mkoa ametimua watu, amepunguza watu lakini mimi nasema hii siyo *solution, solution* ni kuangalia maisha ya walimu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, walimu wetu tumewasahau na kama tumesahau walimu na elimu nayo tunaisahau. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kuchauka. Tupelekee salamu kule Liwale Mjini pale Makunjiganga, Nangano, Kimambi unapoelekea Kilwa, Kikulyungu unapoelekea Nachingwea, Mtawatao kwenye mpunga, Ndapata unapopakana na Selou, Barikiwa. Liwale sio ya kwako peke yako bwana. Mheshimiwa Kakunda. *(Kicheko)*

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwanza nianze kwa kupongeza kwa dhati kabisa Serikali kwa mambo manne makuu yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza, Serikali kutekeleza uamuzi wa miongo minne iliyopita wa kuhamia Dodoma, naipongeza sana. La pili, viongozi wa sekta za muungano na zisizo za muungano kuendeleza mashauriano chanya yenye nia ya kudumisha Muungano. Tatu, Serikali kukamilisha Kituo cha Kuhifadhi Taarifa na Takwimu za Serikali *(Government Data Centre)* ili kuhakikisha uhakika wa upatikanaji wa taarifa za Serikali. Hii ni pamoja na program ya kielektroniki ya kufuatilia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi na ahadi za Rais na viongozi wakuu wengine wa Kitaifa. La mwisho, hatua za kuboresha usimamizi kwenye sekta za mazao ya biashara ya korosho, pamba na tumbaku. Hili nampongeza kwa dhati sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kauli mbiu ya HAPA KAZI TU inaendelea kuthibitika, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina mchango katika maeneo machache, nikianza na afya. Uamuzi wa Serikali wa kila kijiji kiwe na zahanati na kila kata iwe na kituo cha afya ni wa takribani miaka 10 iliyopita. Kwenye hotuba ya Waziri Mkuu haijasisitizwa wito huo wa kila kijiji kiwe na zahanati na kila kata iwe na kituo cha afya. Nilitegemea Serikali ije na mkakati wa makusudi wa kusaidia Halmashauri angalau vijiji vitano kila mwaka viwe na zahanati na angalau kata tatu kila mwaka zipate kituo cha afya. Angalau hiyo inaweza ikaonesha utekelezaji lakini naamini hata kwenye bajeti ya

Wizara ya Afya mkakati huo haupo. Naomba sana kama uwezekano upo wa kurekebisha hapo, tuweze kufanya marekebisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, sekta ya kilimo. Sisi kule Sikonge tunalima sana tumbaku. Kitu ambacho nataka niongelee hapa pekee ni kiwanda cha kuchakata tumbaku cha Morogoro. Kiwanda hiki kilibinafsishwa na waliopewa kiwanda hiki na Serikali ni *TLTC* na *Alliance One* ambao kwa bahati mbaya sana hao nao ni wanunuzi wa tumbaku. Kwa hiyo, huwezi kupata *good governance* na *fair competition* ambapo wanunuzi hawa wawili wanamiliki kiwanda halafu kuna kipengele cha sheria ambacho kinawalazimisha wanunuzi wote, wao wenyewe pamoja na wengine kwamba hawaruhusiwi kusafirisha nje tumbaku hadi ipelekwe pale kwenye kiwanda cha Morogoro kuchakatwa. Kwa hiyo, ina maana kwamba, hiyo inazuia *fair competition* kwa wanunuzi wengine ambao sio wamiliki wa hicho kiwanda kwa sababu kuna uwezekano wakapewa *rate* ambazo ni tofauti na zile ambazo wanazitumia wao wenyewe ambao ni wamiliki wa kiwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suluhisho hapo kwa Serikali ni moja tu, aidha kukitaifisha kile kiwanda kirudi mikononi mwa Serikali au apatikane mtu mwingine akinunue tena kile kiwanda ambaye sio mnunuzi wa tumbaku au kufuta kile kipengele cha sheria ambacho kinalazimisha wanunuzi wote kuchakata tumbaku pale ili wengine wapate sehemu nyingine ya kupeleka kuchakata tumbaku badala ya pale. Hapo ndiyo wanunuzi wengi wa tumbaku watakuja Tanzania hapa na mkulima atanufaika kwa kuongeza ushindani kwenye zao la tumbaku, huo ni ushauri wa pili.

Mheshimiwa Spika, wa tatu ni kwenye eneo la utawala. Wilaya yangu ya Sikonge ina eneo kubwa sana. Kuna watu kule Matagata ili aweze kufika Sikonge Makao Makuu ya Wilaya analazimika kutembea kilometa 400. Ile Tarafa ya Kitunda ina wakazi 85,000 na wako mbali kwelikweli na Makao Makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, mimi nilisoma Marekani, niliwauliza Abraham Lincoln alitumia kigezo gani kikubwa kuanzisha *county* ambayo ni sawasawa na wilaya zetu hapa? Alitumia uwezekano wa mtu kutembea na chombo cha usafiri cha kawaida cha wakati ule, farasi, atoke nyumbani kwake saa 12.00 asubuhi, aende Makao Makuu ya Wilaya amalize shida zake arudi nyumbani kabla jua halijatua, ndiyo kigezo ambacho alitumia.

Mheshimiwa Spika, kama usafiri wetu wa kawaida ni baiskeli, tunamtegemea na mwananchi wa Matagata atoke Matagata aende kwa Mkuu wa Wilaya akamalize shughuli zake arudi nyumbani kabla jua halijatua. Ingawa kigezo kile hatuwezi kukifikia basi tumpunguzie mzigo huyu mwananchi. Kwa hiyo, ombi letu litakapokuja kwa Waziri Mkuu la kuanzisha Wilaya Mpya kwenye Tarafa ya Kitunda naomba lipate *support* ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la nne ambalo napenda nilizungumzie ni elimu. Tunaomba Serikali ichukue hatua za haraka kuhakikisha tunakuwa na usawa wa uwiano wa walimu na wanafunzi katika nchi nzima. Ipo mikoa hapa Tanzania ina ziada ya walimu, ipo mikoa kama Tabora ina upungufu mkubwa sana wa walimu. Kule ambako kuna ziada inatakiwa isawazishwe na kule ambako kuna upungufu ili ule uwiano wa 1:40 upatikane kwa mikoa yote badala ya mikoa mingine kuwa na walimu wengi mpaka na wa ziada ambao hawana kazi, wanasukana nywele tu kwenye shule na mikoa mingine ina upungufu mkubwa wa walimu. Naomba sana hili lisimamiwe na Waziri Mkuu, maana Wizara ya Elimu wameshindwa kulitatua kwa miaka 10 iliyopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka nilizungumzie ni eneo la barabara. Sisi kule kwetu tuna barabara mbili za kiwango cha changarawe ambazo ni muhimu sana. Barabara ya Ipole–Rungwa kilometa 182 na Sikonge–Mibono–Kipili kilometa 280. Barabara ya Ipole–Rungwa ilitengenezwa tu pale ambapo Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete alipokuja Sikonge akatembelea Kitunda, tarehe 10/3/2010. Akatoa amri, nataka hii barabara

itengenezwe kwa vyovyote vile. Wewe *Regional Manager* hakikisha unapata hela za kutengeneza hii barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaomba basi Rais apange safari ya kuja Sikonge ili aende Kipili ili na hiyo barabara ya Sikonge – Kipili nayo itengenezwe. Maana hao watu wa Wizara ya Ujenzi wanatwambia hakuna hela. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kakunda muda wako umekwisha.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, naomba niishie hapo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Nakushukuru sana Mheshimiwa Kakunda, dakika 10 ni chache, lakini umejitahidi kuwasilisha hoja zako. Jioni hii tumeweza kufanikiwa kupata wachangiaji 18, si haba kwa kuanzia na wengine tutaendelea nao wakati utakaofuata.

Kwa kuwa, muda wetu hauruhusu tena kuendelea na kazi zilizopangwa hapa Mezani kwa siku ya leo zote zimekamilika, nachukua nafasi hii moja kwa moja kuahirisha shughuli za Bunge hadi Jumatatu, saa tatu kamili asubuhi. Nawatakia *long weekend* njema.

*(Saa 1.45 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu, Tarehe 9 Aprili, 2017, Saa Tatu Asubuhi)*